**13 MEI, 2026**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TATU

**Kikao cha Ishirini na Nane - Tarehe 13 Mei, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka 2026/2027.

**MHE. ENG. JOHNSTON J. MUTASINGWA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, ufuataο ni Mwongozo wa Spika ulioombwa na Mheshimiwa Ado Shaibu Ado kuhusu kukinzana kwa majibu ya Serikali kwenye maswali yaliyoulizwa kuhusu ujenzi wa Kituo cha Afya cha Nampungu.

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 7 Mei, 2026, katika Kikao cha Ishirini na Nne cha Mkutano wa Tatu wa Bunge la Kumi na Tatu, Mheshimiwa Ado Shaibu Ado, Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kaskazini, kwa kutumia Kanuni ya 79 ya Kanuni za Kudumu za Bunge 2025, alisimama na kuomba Mwongozo wa Spika.

Katika maombi hayo, Mheshimiwa Ado alieleza kuwa majibu ya Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, Mbunge, na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Elimu), kwa swali la nyongeza la Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo yanakinzana na majibu yaliyotolewa na swali la nyongeza la Mheshimiwa Ado la tarehe 14 Aprili, 2026.

Wabunge hao wote waliuliza, "ni lini Serikali itatoa fedha ili kukamilisha Kituo cha Afya cha Nampungu kilichopo katika Wilaya ya Tunduru?"

Waheshimiwa Wabunge, Kiti kilijitahidi kupitia *Hansard* ili kujiridhisha kuhusu maswali na majibu yaliyotolewa na kisha kutoa mwongozo. Nimepitia *Hansard* ya tarehe 14 Aprili, 2026 na vilevile *Hansard* ya tarehe 7 Mei, 2026. *Hansard* ya tarehe 14 Aprili, 2026 inaonesha kuwa, Mheshimiwa Ado aliuliza swali la nyongeza kwa swali la msingi Na. 74 kama ifuatavyo: -

"Tarafa ya Nampungu haina Kituo cha Afya na haijapata bajeti ya kutosha katika ukamilishaji wa ujenzi wa kituo hicho. Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya Nampungu?"

Tarehe hiyo *Hansard* inaonesha kuwa, wapo Wabunge wengine waliopata fursa ya kuuliza maswali ya nyongeza kuhusu ujenzi wa vituo vya afya kwa maeneo yao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Festo Sanga, Mbunge aliuliza, "mara kadhaa nimesimama hapa kuomba ujenzi wa Kituo cha Afya Matamba, Je, ni lini Serikali watajenga kituo kipya cha afya kama ambavyo wameahidi kwenye hotuba mara kwa mara?"

Mheshimiwa Joseph Tama aliuliza, "Je, ni lini Serikali itatoa fedha za ujenzi Kituo cha Afya Igwisi katika Jimbo la Kaliua?" Mheshimiwa Jonas Mbunda aliuliza, "Serikali ilitoa shilingi 250,000,000 kujenga kituo cha afya kilichopo Kata ya Mnyanganyanga ambacho yalijengwa kwa majengo mawili tu. Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kumaliza ujenzi huo?"

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 14 Aprili, 2026, kwa niaba ya Serikali, majibu yalitolewa na Mheshimiwa Dkt. Jafar Rajab Seif, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuwa Serikali imewasilisha andiko la kuomba fedha Hazina kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa vituo vya afya vya kimkakati kwenye majimbo yenye uhitaji. Alifafanua zaidi kwamba tayari Hazina wamepitisha andiko hilo ambapo fedha hizo zikiingia, Serikali itakamilisha ujenzi wa vituo hivi.

Waheshimiwa Wabunge, *Hansard* ya tarehe 7 Mei, 2026 inaonesha kwamba suala hilo liliibuka tena, Mheshimiwa Sikudhani Chikambo, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Ruvuma aliuliza swali la nyongeza katika swali la msingi Na. 269. Swali hilo lilitaka kujua, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa kituo cha afya cha Nampungu? Mheshimiwa Sikudhani alidokeza kuwa kituo hicho kilitengewa shilingi 500,000,000 lakini zimepelekwa shilingi 250,000,000 tu, hivyo kusababisha ujenzi kusimama.

Waheshimiwa Wabunge, siku hiyo kwa niaba ya Serikali Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa alijibu kama ifuatavyo:-

"Ni kweli kwamba, vipo vituo vya afya ambavyo vilipelekewa fedha kwa awamu mbili, shilingi 500,000,000 na shilingi 250,000,000. Kauli ya Serikali ilikuwa, kwanza, Wakurugenzi wa Halmashauri kote nchini ambao walipokea fedha kwa kujenga vituo vya afya ambavyo havijakamilika, wawasilishe taarifa hiyo Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Pili, watenge fedha za mapato ya ndani kwa uwezo wao angalau huduma za wagonjwa wa nje *(OPD)* zianze kwenye vituo hivi wakati tunaendelea na hatua ya ukamilishaji wa miundombinu iliyosalia."

Waheshimiwa Wabunge, kupitia majibu hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri alisisitiza kuwa Serikali inatambua kuwa vipo vituo vya afya ambavyo havijakamilika, hivyo alielekeza Wakurugenzi wa Halmashauri nchini wawasilishe taarifa Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Halikadhalika, aliwataka Wakurugenzi hao kutenga fedha za mapato ya ndani ili kuwezesha vituo vya afya kutoa huduma kwa wagonjwa wa nje *(OPD)* wakati Serikali inaendelea na hatua za ukamilishaji wa miundombinu iliyosalia.

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na majibu ya Mheshimiwa Dkt. Dugange, Mheshimiwa Ado alitumia Kanuni ya 79 kuomba Mwongozo wa Spika, kwa jambo lililotokea mapema siku hiyo ya tarehe 7 Mei, 2026. Mheshimiwa Ado aliomba Mwongozo kutaka kujua, iwapo inaruhusiwa kwa Serikali kutoa majibu yanayokinzana kwa maswali mawili yaliyoulizwa kuhusu ujenzi na ukamilishaji Kituo cha Afya Nampungu.

Mheshimiwa Ado Shaibu alioanisha jibu la swali Na. 269 na alieleza kuwa fedha zipo, jibu hilo lilikinzana na jibu la Serikali iliyotoa mapema siku ya tarehe 7 Mei, 2026 lililotaka Wakurugenzi kutenga bajeti kwa ajili ya vituo hivyo vya afya.

Waheshimiwa Wabunge, katika kutafakari maombi ya Mwongozo na baada ya kupitia *Hansard* kuhusu maswali ya

nyongeza ya Waheshimiwa Wabunge na majibu ya Manaibu Waziri, nimejiuliza swali, je, majibu yaliyotolewa kwenye maswali ya nyongeza kuhusu Kituo cha Nampungu yanakinzana au hayakinzani?

Waheshimiwa Wabunge, kumbukumbu za Bunge zimeonesha kuwa tarehe 14 Aprili, 2026 Mheshimiwa Festo Sanga, Mheshimiwa Joseph Tama, Mheshimiwa Jonas Mbunda na Mheshimiwa Ado S. Ado; na tarehe 7 Mei, Mheshimiwa Sikudhani Chikambo waliuliza maswali yanayofanana.

Waheshimiwa Wabunge, kupitia maswali hayo, Waheshimiwa hao walionesha kuwa vituo vilivyotajwa havijakamilika, hivyo ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa vituo vya afya. Mheshimiwa Ado na Mheshimiwa Sikudhani, japokuwa ilikuwa siku tofauti, wote walitaka kujua lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya cha Nampungu kilichopo Wilayani Tunduru?

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 12 Aprili, 2026, Mheshimiwa Dkt. Jafar Rajab Seif, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI (Afya) alimjibu Mheshimiwa Ado kuwa, Serikali imewasilisha maombi ya fedha Hazina kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa kituo cha afya cha kimkakati.

Kwa upande mwingine, tarehe 7 Mei, 2026, suala hilo liliulizwa na Mheshimiwa Sikudhani, ambaye alijibiwa na Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri, TAMISEMI, (Elimu), Mheshimiwa Naibu Waziri, aliwaelekeza Wakurugenzi wa Halmashauri kuwasilisha taarifa katika Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI pia kutenga fedha za mapato ya ndani ili kupata fedha za ukamilishaji wa Kituo cha Afya cha Nampungu.

Waheshimiwa Wabunge, majibu yaliyotolea na Mheshimiwa Dkt. Jafar Seif, tarehe 14 Aprili, 2026 na majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, tarehe 07 Mei, 2026, yanakinzana. Wakati tarehe 14 Aprili, 2026 ilielezwa kuwa, fedha za kukamilisha Kituo cha Afya Nampungu zitatoka Hazina na kuwa andiko la maombi ya fedha limekubaliwa; na kupitia jibu la

tarehe 7 Mei, 2026, Bunge lilifahamishwa kuwa, Wakurugenzi wanatakiwa kutenga fedha kutoka vyanzo vya mapato ya ndani.

Waheshimiwa Wabunge, majibu haya yanaleta mkanganyiko ambao ufafanuzi zaidi unatakiwa kutolewa na Serikali ili kujua hatma ya vituo hivi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 56 inamtaka Waziri kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge kikamilifu. Kanuni hiyo ya 56(3) inaeleza ifuatavyo: "Iwapo Spika ataridhika kuwa swali la msingi au la nyongeza halijapata majibu ya kuridhisha, ataagiza lijibiwe kwa ufasaha zaidi katika Kikao kingine cha Bunge."

Waheshimiwa Wabunge, suala la ukamilishaji wa ujenzi wa vituo vya afya lina maslahi mapana kwa wananchi. Maswali yaliyoelezwa hapo juu, yanataka kujua ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati ikiwemo cha Nampungu. Msimamo wa Serikali kuhusu maswali hayo bado haujajulikana, kwa kuwa majibu yaliyotolewa yanakinzana. Hivyo ninaona ipo haja ya Serikali kuweka suala hilo sawa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuhitimisha, kwa mujibu wa Kanuni ya 56(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge 2025, ninaielekeza Serikali kwa wakati muafaka ilete majibu ili kufafanua suala hili. Majibu hayo yatatolewa kabla ya kumalizika kwa Mkutano huu.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo Mwongozo wa Spika, umetolewa leo tarehe 13 Mei, 2026. *(Makofi)*

Waheshimiwa, sasa ninamwita Mwenyekiti aje kuendelea na ratiba inayofuata. *(Makofi)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Katibu, tuendelee.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Mheshimiwa Christina Solomon Mndeme, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 322

**Hitaji la Watumishi wa Afya – Tabora**

**MHE. CHRISTINA S. MNDEME** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza Watumishi wa Afya katika Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati za Mkoa wa Tabora?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Christina Solomon Mndeme, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Tabora kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutenga bajeti na kuajiri watumishi wa kada mbalimbali za afya nchini. Katika kipindi cha mwaka 2020/2021 hadi kufikia 2025/2026 jumla ya watumishi wa kada za afya 37,921 wameajiriwa na kupangiwa vituo vya kazi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Tabora una mahitaji ya wataalam wa afya 8,121. Waliopo ni 3,467 sawa na 43%, upungufu ni 4,654 sawa na 57%. Kati ya mwaka 2024/2025 na 2025/2026 Serikali imeajiri na kuwapangia vituo watumishi wa kada za afya 856 katika Halmashauri za Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Tabora umeandaa mikakati ya kupunguza changamoto ya upungufu wa watumishi

ambapo katika mwaka wa fedha 2026/2027 Halmashauri Nane za Mkoa wa Tabora kwa kupitia mapato ya ndani zimetenga jumla ya shilingi milioni 413.8 kwa ajili ya kuajiri kwa mkataba watumishi wapatao 87 wa kada mbalimbali za Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Christina Solomon Mndeme.

**MHE. CHRISTINA S. MNDEME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru sana Serikali kwa majibu mazuri, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Serikali imekuwa ikifanya vizuri sana kuajiri watumishi, na tumesikia hapa katika jibu la msingi watumishi 856 wameajiriwa ndani ya Mkoa wa Tabora, tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea watumishi hawa, lakini pia amepanga kuajiri kwa mkataba watumishi 87; na kwa kuwa, bado kuna upungufu mkubwa wa watumishi takribani 4,654 sawa na 57%, na katika upungufu huu waathirika wakubwa ni wanawake na watoto waliopo vijijini, je, Serikali ina mkakati gani wa kufanya msawazo wa watumishi ili sasa kujaza nafasi zilizopo vijijini ili kuchukua hatua za dharura, kwa sababu mjini wako wengi angalau wapelekwe vijijini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa, Serikali imekuwa ikiajiri watumishi wa maabara katika hospitali zetu, vituo vya afya na zahanati; na kwa kuwa, watumishi hawa wanastahili kufanya kazi kwa saa 24 kulingana na *nature* ya kazi zao, je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa kipaumbele cha kuajiri na kuongeza idadi ya watumishi wa maabara katika Mkoa wa Tabora? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Chistina

Solomon Mndeme, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Tabora, kwa kuuliza maswali madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu msawazo Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, tunaendelea kufanya msawazo; na tumeitisha taarifa kutoka katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma ili kuendelea kufanya msawazo ili mama zetu kule vijijini waendelee kupata huduma hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika zile ajira mpya 5,000 ambazo Mheshimiwa Rais aliridhia vibali na zilikuwa ahadi zake, Mkoa wa Tabora walipata jumla ya watumishi 357. Kwa hiyo, Serikali inatambua upungufu uliopo, na inaendelea kuajiri watumishi. Ndiyo maana kuna maelekezo ya kuendelea kutoa ajira za mkataba, hasa katika yale maeneo ambayo yana changamoto zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, swali la pili ambalo ameulizia suala la maabara, nimwelekeze tu Mkurugenzi wa Jiji waendelee kuwapanga watumishi hawa kulingana na uhitaji wa maeneo hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Edward Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Hospitali ya Wilaya ya Kiteto ina mtaalam wa *X-Ray* mmoja tu wilaya nzima, lakini Kituo cha Afya cha Engusero, Sunya, Mwanya, na Kijungu wana daktari mmoja mmoja wa upasuaji na wataalam wa maabara. Je, ni lini watatuletea wataalamu hawa muhimu kwa haraka sana?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Olelekaita kuhusu upungufu wa watumishi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto. Kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge. Tulipofanya ziara katika Halmashauri ya Kiteto kwenye

mwendelezo wa ziara za Mheshimiwa Waziri Mkuu tulizunguza kuhusu mambo haya ya watumishi. Tulichukua maombi haya maalum kwa ajili ya kuweza kuongeza watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwahidi Mheshimiwa Mbunge na Wanakiteto kwamba tutaendelea kuajiri watumishi kadiri tunavyowapokea kutoka Ofisi ya Rais, Menagementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili kuendelea kutoa huduma katika maeneo yetu hasa yale ya vijijini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anne Malecela.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mazingira magumu ya sehemu za kufanyia kazi ambazo watumishi wengi wanakuwa wanazihofu, kama vile sisi ambao tuna maeneo ambayo ni ya milimani sana, unakuta 80% ya jimbo ni milima. Je, Serikali haioni kwamba ni vyema ikaweka utaratibu maalum wa kutoa *incentives* za muhimu sana wanapopeleka wafanyakazi sehemu ambazo zina maisha magumu sana?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kusisitiza suala la *incentives,* na tumekuwa tukipokea michango ya aina hii ya Waheshimiwa Wabunge. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengine kwamba Serikali iko tayari, na itaendelea kutoa *incentives* hasa kwa wale watumishi ambao wanafanya katika mazingira magumu. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Wilaya yetu ya Kilolo ina upungufu wa wafanyakazi katika sekta ya afya takribani 865, na ina vituo vya afya na inafanya upasuaji wa dharura. Pia zahanati nyingi sana hazina watumishi. Je, kuna

mkakati gani wa haraka kuhakikisha kwamba wananchi wa Kilolo hawateseki kwa upungufu wa wafanyakazi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimwelekeze Mkurugenzi kuendelea kufanya msawazo katika halmashauri hii ili watumishi wetu waende kutoa huduma kwenye zahanati ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaendelea kuvuta taarifa kutoka kwenye halmashauri zote ili kuona upungufu uliopo na tuchukue hatua za dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninaendelea kuwaelekeza Wakurugenzi kuendelea kutoa ajira za mikataba, kama ambavyo Mkoa wa Tabora wamejipanga kuendelea kutoa ajira za mikataba hasa kwenye maeneo yale yenye upungufu mkubwa na uhitaji mkubwa. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi.

Na. 323

**Ujenzi wa Kituo cha Kuegesha Malori**
**Nyakahura – Biharamulo**

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha kuegesha Maroli Nyakahura Wilayani Biharamulo, kama alivyoelekeza Mheshimiwa Waziri Mkuu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Jimbo la Biharamulo Magharibi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Maegesho ya Malori Nyakahura katika Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo unaendelea katika hatua mbalimbali, ambapo hadi Machi, 2026, jumla ya shilingi milioni 71.12 zimetolewa na kutumika kutekeleza kazi mbalimbali za kutwaa eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 11,689.25 katika Kijiji cha Ngarambe katika Kata ya Nyakahura kwa ajili ya ujenzi wa maegesho hayo. Usawazishaji wa eneo la ujenzi, ujazaji wa kifusi na ujenzi wa makalavati mawili umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa choo matundu manne upo katika hatua za ukamilishaji, na kuvuta maji na umeme pamoja na kusawazisha eneo la maegesho. Makadirio ya gharama ya ujenzi mpaka kukamilika ni shilingi bilioni 2.05.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa maegesho ya malori katika eneo la Nyakahura ambapo katika mwaka wa fedha 2025/2026 imetenga shilingi milioni 40 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa mradi huu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa nafasi nyingine ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pia ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niweke *clarification* kidogo. Tarehe 21 Septemba, 2021 Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya ziara Mkoa wa Kagera akakagua Kituo cha Maegesho ya Malori Nyakanazi, wakati huo ndiyo kilikuwa kinajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipofika Nyakahura tukiwa tunaelekea Ngara, *issue* kubwa ilikuwa malori ni mengi sana pale

Nyakahura, kwa sababu ujenzi wa barabara inayotoka Rusahunga kwenda Rusumo ulikuwa haujaanza, akaelekeza kwamba mtafute eneo, na eneo litakalopatikana uanzwe mchakato ikiwa ni pamoja na kuleta maombi huku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu tayari Serikali imeshaanza ujenzi wa barabara ile kwa takribani shilingi bilioni 165 kutoka Rusahunga kwenda Rusumo, barabara itakapokamilika, kitendo cha kuendelea kupaki malori barabarani, barabara ile itaharibika. Ndiyo maana tunaomba, kwa sababu ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tupate fedha kutoka Serikali Kuu ili iweze kufanya haya mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivi? Hiki kilichofanyika ni sisi halmashauri kuondoa malori barabarani kwa sababu ujenzi unaendelea, ndiyo maana tumeamua tuweke hiki kitu kama halmashauri; kwa sababu kama ujenzi ni shilingi bilioni mbili, leo imetengwa shilingi milioni 40, itachukua miaka mingine kumaliza hiyo *project*. Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba kauli ya Serikali. Je, ni lini tutapata fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi huu kama ahadi ya Waziri Mkuu ilivyokuwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa tunapojenga barabara mpya na maeneo mengi, malori yakiegeshwa barabarani yanaharibu barabara; kuna *moving weight* na *stationary weight;* magari yanapotengenezwa yakiwa yanatembea *it is fine,* barabara zinaweza zikahimili, lakini malori yanapopaki mengi sehemu moja barabara zinatitia na matokeo yake thamani ya barabara iliyowekwa na Serikali kwa muda mrefu inaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina kauli gani ili siku nyingine tunapokuwa tunajenga barabara mpya tuweke na maegesho ya malori kabisa kwenye maeneo ambayo yanapaki ili tuweze kuokoa hizi barabara ambazo zinajengwa kwa gharama kubwa zaidi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya maswali hayo mawili.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa *Engineer*. Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi. Ninafahamu kwamba amelifuatilia mara kadhaa suala la ujenzi wa *parking* ya malori katika eneo la Nyakahura, na ni kweli kwamba mwaka 2021 Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya ziara katika Jimbo la Biharamulo, na alitoa maelekezo kwamba Serikali itafute fedha kwa ajili ya kuwaunga mkono wananchi wa Biharamulo kujenga stendi au maegesho ya malori katika eneo la Nyakahura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, ahadi za viongozi wa Kitaifa ni kipaumbele chetu namba moja. Tumeendelea kushirikiana na Halmashauri ya Baharamulo na Mkoa wa Kagera kuhakikisha kwamba tunaandaa utaratibu wa kibajeti, kwanza kupata eneo, ambapo tayari tumeshapata eneo lenye ukubwa zaidi ya *square metre* 11,000; pili kuanza kuandaa miundobinu, ujenzi wa vyoo, na kuweka *level* eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hizo zinaendelea kufanyika. Vilevile tutaendelea kutenga fedha kuhakikisha kwamba sasa tunajenga maegesho hayo ili yaweze kutimiza mahitaji ya malori katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili ninaomba nisisitize kwamba fedha ya Serikali ni pamoja na fedha ya mapato ya ndani ya halmashauri pamoja na fedha ya Serikali kuu; zote ni fedha ya Serikali. Ilimradi fedha ya halmashauri inaweza kuingia ifanye kazi, lakini wakati huo Serikali inaendelea na utaratibu wa kupata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huu, miradi yote ya ujenzi wa stendi au masoko na kadhalika ambayo ni ya kimkakati, halmashauri wanawajibika kuandika andiko maalum la kimkakati la kuomba fedha Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa ombi la Mheshimiwa Mbunge kwamba tuone namna ambavyo Serikali Kuu itachangia

nguvu hizo, nitumie nafasi hii kumwelekeza Mkurugenzi wa Biharamulo waandike andiko la kimkakati na kuwasilisha kwa utaratibu uliopo ili tuweze kuona namna ambavyo Serikali kuu itaunga mkono juhudi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni kweli kwamba tunazo barabara ambazo wakati mwingine malori yanahitaji kuegeshwa. Ni muhimu kuwa na maeneo ya maegesho ya malori. Ninafahamu kuwa suala hili limekuwa likifanyika katika barabara zetu, kunakuwa na michepuko ambayo malori yanaweza yakaegeshwa katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeichukua hoja hiyo kuendelea kushirikiana sisi kama *TARURA* na wenzetu wa *TANROAD* kuona namna nzuri ambayo tutaweka maeneo mazuri ya kupaki malori hasa maeneo ambayo yana mtiririko mkubwa zaidi wa magari makubwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi,

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kata ya Temeke iliyobeba Jina la Wilaya ya Temeke haina kabisa kituo cha afya na wala zahanati. Pale wananchi wa Temeke wanapougua, inabidi waende kwenye kituo cha afya au zahanati ya Vituka na maeneo mengine kwa sababu hawawezi kwenda kwenye hospitali ya mkoa. Je, ni lini Serikali itajenga kituo cha afya au zahanati katika Kata ya Temeke?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi hilo swali halifanani na swali la msingi. Itabidi ulilete kwenye swali la msingi. Mheshimiwa Waziri ninakushukuru sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Mheshimiwa Mattar Ali Salum, Mbunge wa Shaurimoyo aulize swali lake.

**MHE. MATTAR A. SALUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Shauri Moyo ninaomba swali langu 325 lipatiwe majibu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Mattar, kuna swali la Mheshimiwa Benjamin Lukubha Ngayiwa, Mbunge wa Kahama Mjini.

Sasa Mheshimiwa Benjamin Lukubha Ngayiwa, Mbunge wa Kahama Mjini, aulize swali lake. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Cecilia Paresso.

Na. 324

**Kuboresha Miundombinu ya Barabara Kahama**

**MHE. CECILIA D. PARESSO K.n.y. MHE. BENJAMIN L. NGAYIWA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha miundombinu ya Barabara za Mitaa na Kata za pembezoni mwa Manispaa ya Kahama?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Benjamin Lukubha Ngayiwa, Mbunge wa Jimbo la Kahama Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka mipango mbalimbali na imeanza utekekelezaji wa kuboresha miundombinu ya barabara za mitaa na kata za pembezoni mwa Manispaa ya Kahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024 na 2024/2025 Manispaa ya Kahama kupitia mradi wa uboreshaji Miji *(TACTIC)* chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia inatekeleza ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa kilometa 16.58 kwa gharama

ya shilingi bilioni 22.31, barabara za mitaa ya Mjini kilometa 15.21 na kata ya pembezoni kilometa 3.08.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2026/2027 *TARURA* imepanga kujenga barabara za mitaa ya Kahama Mjini na kata za pembezoni zenye kilometa 62.5 kwa kiwango cha changarawe kwa gharama ya shilingi milioni 855.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya uboreshaji wa barabara za Mitaa na Kata za pembezoni mwa Manispaa ya Kahama ili ziweze kupitika kwa wakati wote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Pamoja na kazi kubwa ambayo inafanyika katika Mji wa Kahama, lakini tuna uhitaji wa ujenzi wa mitaro, kwa maana ya kwamba barabara zijengwe pamoja na mitaro. Je, hilo pia linazingatiwa katika ujenzi wa barabara hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa Mkoa wa Arusha unaenda kwenye maandalizi makubwa ya *AFCON,* na ni kweli kwamba barabara zetu nyingine, ukiacha hizo ambazo zitahudumiwa na *TANROADS,* zile za *TARURA* bado siyo nzuri na siyo rafiki hasa ukizingatia tunapata ugeni mkubwa. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuendelea kuongeza fedha za kutosha ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na barabara nzuri?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa dada yangu Mheshimiwa Cecilia Paresso kwa namna ambavyo amekuwa msemaji madhubuti sana wa wananchi wa Mkoa wa Arusha na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakishie tu kwamba, katika *design* zetu za miradi ya barabara, jambo la msingi ambalo tumelipa msisitizo mkubwa ni kuhakikisha kwamba barabara zetu zinakuwa na mitaro au mifereji ya kutiririsha maji ili kuepusha maji kupita katikati ya barabara na kuathiri barabara zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika mradi huu wa Kahama wa *TACTIC*, pia na miradi mingine yote ya *TARURA* tunaendelea kuhakikisha kwamba mifereji inajengwa kwa ubora ili kuziwezesha zile barabara kudumu kwa muda mrefu zaidi. Jambo hili tutaendelea kulitekeleza katika ujenzi wa barabara kote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali la pili, ni kweli kwamba tunatarajia mwakani tutakuwa na michuano ya *AFCON* katika nchi yetu, na ni shughuli muhimu sana, tunatarajiwa kuwa na miundobinu muhimu ya barabara katika Jiji la Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Serikali imeshaweka wakandarasi kwenye barabara kadhaa kupitia *TARURA* katika Jiji la Arusha. Kupitia mfuko wa kawaida na bajeti za dharura za *TARURA* tutaendelea kuboresha barabara zote muhimu katika eneo la Jiji la Arusha, na pia katika eneo la kuzunguka uwanja ule ambao unatarajiwa kutumika ili kuhakikisha usafiri na usafirishaji wakati wa michuano ya *AFCON* mwakani inakwenda kwa uthabiti unaotakiwa.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo kwa Waheshimiwa Wabunge kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Mattar Ali Salum, Mbunge wa Shaurimoyo aulize swali lake.

Na. 325

**Kupandisha Hadhi *NEMC* kuwa Mamlaka**

**MHE. MATTAR ALI SALUM** aliuliza: -

Je, kwa nini Serikali haipandishi hadhi *NEMC* kuwa Mamlaka ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mattar Ali Salum, Mbunge wa Shaurimoyo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na mchakato wa mabadiliko ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191 ambapo miongoni mwa masuala muhimu yaliyozingatiwa ni pamoja na kuimarisha Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* kuwa chombo Madhubuti; na taasisi mahiri ya usimamizi wa mazingira nchini, kwa kulipandisha hadhi Baraza kuwa Mamlaka ili liweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mattar.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

*(Hapa kipaza sauti kilizimika)*

**MWENYEKITI:** Angalia *mic* nyingine ambayo inafanya kazi.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimshukuru sana Mheshimiwa waziri kwa majibu yake mazuri ambayo ameyatoa, lakini nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa suala la *NEMC* ni *sensitive* sana, ni la muhimu sana katika nchi yetu. Ninaomba *commitment* ya Serikali. Je, ni lini mchakato huu utakamilika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge Mattar Ali Salum, Mbunge wa Shaurimoyo, kwa umakini wake na ufuatiliaji wa karibu wa mambo yote yanayohusu masuala ya Muungano na masuala ya mazingira na hususan suala hili la *NEMC*. Vilevile ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa uzoefu, yupo Bungeni tangu mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala hili tayari Serikali inaendelea na ukamilishaji wa taratibu za kulileta jambo hili la kuifanya *NEMC* kuwa mamlaka kamili hapa Bungeni. Tumewashirikisha wadau wote ndani na nje ya Serikali katika maandalizi ya awali. Wizara yetu iliyopo chini ya Makamu wa Rais, inafanya kazi kwa ukaribu sana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuhakikisha kwamba maandalizi ya Muswada utakaokuja Bungeni yawe yamezingatia vitu vyote vya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe saba Mei tulilipeleka suala hili kwenye kikao kazi *IMTC;* kikao cha wataalamu ndani ya Serikali ili kuwajengea uelewa wa pamoja wa jambo hili na kuwawezesha wao kuweka maoni yao. Kwa sasa tumeshapata idhini ya kuanza maandalizi ya mapendekezo ya waraka utakaokwenda kwenye Baraza la Mawaziri. Kesho tarehe 14 Mei tunakamilisha mapendekezo haya, tayari kwa ajili ya kwenda kushauri kikao hicho cha mamlaka ya juu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, jambo hili la *NEMC* kuwa mamlaka kamili lilizungumzwa vizuri au lilifafanuliwa vizuri wakati tunapitisha bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ninashukuru kwa majibu hayo.

Tunaendelea sasa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Mheshimiwa Jesca John Magufuli, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake. Mheshimiwa Agnes Hokororo kwa niaba yake.

Na. 326

**Athari za Vijana Kujiingiza Kwenye Migogoro ya Kimataifa**

**MHE. AGNES E. HOKORORO K.n.y. MHE. JESCA J. MAGUFULI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga utashi kwa vijana kuhusu athari za kujiingiza katika migogoro ya Kimataifa kama vile vita ya Ukraine na Urusi?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (MHE. DKT. NGWARU J. MAGHEMBE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa mbele, ninaomba nichukue dakika moja kutoa neno la shukurani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai, rehema na baraka tele, ambazo anatupa sisi wote Wabunge humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuniteua mimi kuwa, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Ni imani kubwa sana ambayo amenipa mimi kijana wa huko milimani Upareni. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninapenda kukishukuru Chama changu CCM, kunilea tangu mdogo mpaka hivi juzi kuniteua kuwa mgombea wa Jimbo la Mwanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, ninapenda sana kuwashukuru wapiga kura wangu, Wajumbe wangu, na wananchi wa Wilaya ya Mwanga. Bila upendo wao

na imani yao, nisingekuwepo hapa leo. Ninawashukuru sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hilo neno fupi la shukrani, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Jesca John Magufuli, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya Kimataifa, ikiwemo vita baina ya Ukraine na Urusi, ina athari kiuchumi, kijamii na kiusalama na kwa namna moja au nyingine inawagusa vijana wetu. Hivi karibuni kumekuwepo na mwenendo kwa baadhi vijana, hususan kutoka Bara la Afrika, kuhamasishwa kujiunga na majeshi ya nchi mbalimbali zenye migogoro ya kivita, ili kushiriki katika vita kwa lengo la kujipatia kipato, kutokana na changamoto za kiuchumi na upatikanaji mdogo wa fursa za ajira katika nchi zao za asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na hali hiyo, Serikali kwa kuzingatia miongozo mbalimbali, ikiwemo Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001, Toleo la Mwaka 2024 na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050, imeendelea kutoa elimu ya uraia na uelewa kwa vijana kuhusu athari za kujiingiza katika migogoro ya Kimataifa, kwa kuwa kufanya hivyo ni kunyume na sheria za nchi na sheria za Kimataifa, na kwamba kunaweza kugharimu maisha yao ikiwemo vifo na kupata ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara, imeendelea kuratibu upatikanaji wa fursa za ajira nje ya nchi kwa kusaini mikataba inayotekelezwa kupitia ushirikiano uwili, kikanda na Kimataifa, katika nchi zenye mazingira salama ya kazi. Mathalani, Serikali katika mwaka huu wa fedha, imefanikisha upatikanaji wa nafasi 1,500 za ajira, katika fani ya udereva kwa vijana wa Kitanzania nchini Qatar, pamoja na nafasi 300 za ajira, kada ya wauguzi nchini *Saudi Arabia*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imeendelea kutekeleza programu mbalimbali za kuwawezesha vijana, ikiwemo kutenga shilingi bilioni 200 kwa ajili ya kutoa mikopo,

sambamba na kutekeleza programu maalum za kisekta, zinazolenga kuongeza ushiriki wao katika shughuli za kiuchumi. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnes Hokororo.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa kumekuwepo na mawakala ambao wamekuwa wakiwachukua vijana, na kuwaahidi kupata ajira nje ya nchi yetu, je, Serikali ina ithibati gani zinazowapatia mawakala hao, ili kuhakikisha changamoto zilizojibiwa kwenye jibu la msingi zisitokee? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa, kwenye jibu la msingi Naibu Waziri amesema uelewa umekuwa ukijengwa kwa vijana, je, ni programu zipi mahususi, ukiacha mikopo inayotolewa kwa vijana, ili kuhakikisha sasa vijana hawashawishiki kwenda nje ya nchi ili wasikumbane na athari ambazo amezijibu kwenye swali lako la msingi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (MHE. DKT. NGWARU J. MAGHEMBE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kwanza kumshukuru Mheshimiwa Jesca John Magufuli kwa kuuliza hili swali, anajali sana vijana. Ninapenda pia kumshukuru Mheshimiwa Agnes Hokororo kwa haya maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza kuhusu hawa mawakala wa ajira, msimamo wa Serikali kwanza kabisa ni kwamba sisi hatufungamani na upande wowote kwenye hii migogoro ambayo ipo huko nje ya nchi. Kwa sababu hiyo, tumekuwa tukichukua hatua za kidiplomasia, lakini za kimya kimya kupambana na hawa mawakala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kwanza, Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Ajira na Kazi, wamekuwa wakifanya *vetting* ya

hawa mawakala wote. Pia, vyombo vyetu vya ulinzi na usalama, vimekuwa vikiendelea kuchunguza hawa mawakala kuhakikisha kwamba wale ambao wanaahidi vijana wetu *things which are too good to be true,* (wanaahidi mishahara mikubwa ambayo haiwezekaniki na kadhalika) wote wanafungiwa. Hilo ni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Ofisi ya Waziri Mkuu, kupitia Wizara ya Kazi na Ajira, wana mawakala ambao wameshafanyiwa *vetting* na wamesajiliwa. Tunawasihi vijana wetu wawatumie wakala hao kutafuta kazi nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Wizara yetu ya Mambo ya Nje, pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu, tumekuwa tukisisitiza kwamba, vijana wetu wakitaka kazi za ajira za nje ya nchi, watumie tovuti *(official website)* ya Serikali, ambayo ni tovuti ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo ni *www.kazi.go.tz* kwa sababu, zile kazi zote ambazo zimetangazwa pale ni rasmi, ambazo zimeshafanyiwa *vetting*. Hilo ni swali la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali la pili, in tena Mheshimiwa Agnes kwa swali zuri. Tangu Mheshimiwa Rais aingie madarakani mwaka 2025 kwenda mbele, amechukua hatua za makusudi kuhakikisha kwamba, vijana wetu wanapata fursa. Kwanza kabisa, Mheshimiwa Rais ameanzisha Wizara mpya ya vijana, kuondoa ukiritimba kwenye fursa za vijana ambazo zinatoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya kutoa shilingi bilioni 200 kwa vijana ambayo tayari ameshaitekeleza, na mpaka sasa vijana 10,000 wameshaingia kwenye mfumo huo wa kupata mkopo, na wamepata mkopo vijana 10,000, ambao una thamani ya shilingi bilioni 48 mpaka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kama unavyojua, tumekuwa na hii mikopo yetu ya halmashauri ambayo inatolewa na halmashauri. Mpaka sasa mwaka 2025 - 2026, mikopo imetolewa ya shilingi bilioni 52 kwa vijana na wakina mama. Pia, Serikali kupitia Wizara yetu, tukiratibu, imeanzisha kituo cha mauzo ya nje

na programu za kidijitali. Machi mwaka huu 2026 Serikali ilizindua kituo cha mauzo haya kwa vijana kwa lengo la kuunganisha vijana 100,000 na masoko ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo.

Waheshimiwa Wabunge kulingana na muda wetu, tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria. Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 327

**Marekebisho ya Kipengele cha 13 cha Sheria ya Ndoa ya 1971**

**MHE. TASKA R. MBOGO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itarekebisha kipengele cha 13 cha Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, ambacho kinaruhusu mtoto wa kike kuolewa na umri wa miaka 15?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ndoa, Sura ya 29 wakati inatungwa mwaka 1971, ilitanguliwa na ukusanyaji wa maoni kwa jamii kwa njia ya *white paper,* ambapo Watanzania wote walishirikishwa. Aidha, tangu sheria hii itungwe, imeshafanyiwa marekebisho mara nne, mwaka 1972, 1980, 1996 na 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilikusanya maoni katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Mtwara, Lindi, Arusha, Dodoma na Mara kuhusu Sheria ya Ndoa, Sura ya 29. Hata hivyo, baada ya uchambuzi wa maoni yaliyokusanywa, imeonekana kuna hitaji la kukusanya maoni zaidi katika mikoa iliyosalia, zoezi ambalo limepangwa kuanza katika mwaka wa fedha wa 2026/2027. Mara

baada ya kukamilika kwa zoezi hilo, Serikali itawasilisha Bungeni Muswada huo ukiwa umezingatia maoni ya wananchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Serikali, ninayo maswali ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa Sheria ya Ndoa ya mwaka 1977 inakinzana na sheria nyingine ambazo tunazo nchini Tanzania ikiwemo Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, kipengele cha pili ambacho kinasema kwamba, umri wa mtu mzima ni miaka 18. Sheria hii ya Ndoa, pia inakinzana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kipengele cha 12 ambacho kimeainisha haki za mtu. Kipengele hiki kinasema, binadamu wote huzaliwa huru na wote ni sawa. Kipengele cha pili kinasema kwamba, kila mtu anastahili heshima, kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele cha tatu, kinasema kwamba, watu wote ni sawa mbele ya sheria, wanayo haki bila ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria. Je, Serikali, kuwepo kwa kipengele hiki cha Kifungu hiki cha 13 kwenye Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, ambayo inaweka tofauti ya kuoa ya mtoto wa kiume na mtoto wa kike; mtoto wa kiume anaruhusiwa kuoa akiwa na miaka 18, na mtoto wa kike anaozeshwa akiwa na miaka 15; ni lini Serikali itaharakisha huo mchakato wa kukusanya maoni ili uweze kubadilisha sheria hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya uongozi madhubuti wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imekuwa ikijenga shule nyingi nchini Tanzania. Imejenga shule kila mkoa kwa ajili ya masomo ya sayansi kwa watoto wa kike. Watoto hawa, wamekuwa wengine wakiozeshwa wakishindwa kwenda kusoma, na kufubaza ile nia ya Serikali ya Mheshimiwa Rais ya kujenga hizo shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuwaozesha watoto wakiwa na miaka 15 kumesababisha kuwa na ndoa nyingi za utotoni nchini Tanzania, lakini na vifo vya mama na mtoto wakati wa kujifungua, kwa sababu ya umri mdogo. Je, ni lini Serikali itakuja na mkakati madhubuti na kutoa muda wa kubadilisha Kifungu cha 13 cha Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, kinachowabagua watoto wa kike? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Taska Mbogo, kwa maswali yake yanayolenga kufuatilia maslahi mapana ya watoto wa kike, na hasa kuhakikisha pia wanapata haki zao nyingine za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye majibu ya msingi kwamba, tangu Serikali imepokea suala hili la marekebisho ya sheria ya ndoa, Serikali tayari imechukua hatua mbalimbali, ikiwemo kukusanya maoni kwa wanajamii, kwa sababu sheria yoyote inayotungwa, inayowahusu wanadamu, ni lazima itungwe na jamii husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge limekuwa likifanya kazi hiyo, kuwakilisha wananchi kutunga sheria mbalimbali. Serikali imeona umuhimu mkubwa sana wa kukusanya maoni kutoka kwa wanajamii ili Sheria hii iwe inaakisi mahitaji ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali tayari imepita katika mikoa saba kwa ajili ya kukusanya maoni ya wanajamii, na bado itaendelea na kazi hiyo katika mikoa 19 iliyosalia. Katika mwaka wa bajeti 2026/2027, Serikali itaendelea na kazi hiyo. Mwisho wa siku tunataka tuwe tuna sheria ambayo inaakisi na inazingatia maoni ya wananchi. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tumesikia jinsi anavyopaza sauti kuhusiana na marekebisho ya sheria hii, na Serikali itaendelea na hizi jitihada mbalimbali nilizozitaja hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali la pili la Mheshimiwa Mbunge, ni kweli kabisa Serikali, ikiwemo Serikali ya Awamu ya Sita inafanya uwekezaji mkubwa sana, wa kuhakikisha kwamba inalinda maslahi ya watoto wote, wakiwemo watoto wa kike. Ni kweli, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, Serikali inafanya uwekezaji katika miundombinu ya shule, lakini inaimarisha upatikanaji wa elimu, ikiwemo pia kulipia ada, ili watoto wasome bila ada kuanzia darasa la kwanza mpaka wanapofika katika shule za sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa watoto wetu wa kike kupata haya maslahi mapana. Ndiyo maana ninaendelea kusisitiza, Serikali itaendelea na hizi jitihada katika mchakato huu kuhakikisha maoni ya wananchi yanapatikana, na sheria inarekebishwa kwa kuzingatia mahitaji ya jamii yetu, na maoni ya wananchi wetu. Kwa hiyo, ninaomba nikuhakikishie, Serikali itaendelea na jitihada hizo.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Mbunge. Tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera, Mbunge wa Musoma Mjini, aulize swali lake.

Na. 328

**Uboreshaji wa Bandari ya Musoma**

**MHE. MGORE M. KIGERA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza uboreshaji wa Bandari ya Musoma ili meli ya *New MV Mwanza* ianze safari zake kuelekea Musoma Mjini - Kisumu hadi Jinja?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera, Mbunge wa Musoma Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TPA* imetenga kiasi cha shilingi bilioni moja za Kitanzania kwa ajili ya kuratibu upembuzi yakinifu kwa bandari zote za maziwa, likiwemo Ziwa Victoria, ambapo Bandari ya Musoma ipo, ili kubaini mahitaji halisi na uwezekano wa kuendeleza Bandari zote kwa awamu. Aidha, baada ya ukamilikaji wa zoezi hilo, *TPA* itakuwa kwenye nafasi ya kuelewa namna bora, na lini Bandari ya Musoma itaendelezwa kutokana na matarajio ya shehena na abiria, na kuwezesha safari za meli za shehena na abiria kama MV Mwanza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera.

**MHE. MGORE M. KIGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninapenda nishukuru majibu mazuri ya Serikali ya kuonesha dhamira ya dhati ya kufanya maboresho katika Bandari ya Musoma. Ninaomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Musoma, ndiyo Bandari pekee katika Ziwa Victoria iliyopakana na nchi mbili, ambayo ni Kenya pamoja na Uganda. Ukizingatia dhamira ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais kwa matarajio yake, anatarajia kufikia 2030, Reli ya kutoka Tanga - Arusha mpaka Musoma iweze kuwa imekamilika na iweze kufanya kazi. Reli hiyo itaenda ku-*connect* Bahari ya Hindi pamoja na Ziwa Victoria. Je, Serikali haioni ni muhimu kuipa umuhimu wa kipekee Bandari hii ya Musoma, na kuifanyia upembuzi yakinifu kwa uharaka na kufanya uboreshaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kupitia Wizara yetu ya Uchukuzi, katika Sekta ya Anga tunacho Kiwanja chetu cha Ndege cha Musoma. Mheshimiwa Naibu Waziri aliwahi kutoa majibu hapa hapa, kwamba watafanya *first test* haraka iwezekanavyo itakapofika mwezi Machi. Leo ni mwezi Mei na uwanja huu bado hiyo *first flight* haijafanyika. Nini kauli ya Serikali

kuhusu Uwanja wa Ndege wa Musoma Mjini kuweza kuanza kufanya kazi haraka iwezekanavyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mgore kwa anavyofuatilia kwa ukaribu maendeleo ya wananchi wa Musoma. Ninakubaliana naye pia kwamba ni kweli kabisa ipo haja ya kuitazama Bandari ya Musoma kwa upekee wake, na hii ni kutokana na kwamba Ilani ya CCM 2025/2030, maelekezo ya Mheshimiwa Rais na Dira yetu ya 2050 vyote kwa pamoja vinaeleza umuhimu wa Taifa letu la kujenga reli ya Kaskazini, na maandalizi yameshaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapoboresha Bandari ya Tanga, unapeleka shilingi bilioni 429; maana yake ni maandalizi. Tumeshamaliza usanifu, na sasa tunakwenda kwenye hatua pengine ya kuhuisha kwa upande wa reli ya Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua itakayofuata sasa tutakwenda kujenga Bandari ya Musoma kama alivyosema na sote tunakubaliana, Ziwa Victoria lilikuwa ni ziwa ambalo ni ajira kwa muda mrefu na Mheshimiwa Dkt. Samia kutokana na umuhimu wake, kama ni ziwa kubwa duniani ambalo kimsingi nchi yetu ndiyo inamiliki 51%, ameamua kuligeuza liweze kuwa uchumi, kuwa sehemu ya kusafirishia bidhaa kwenda kwenye nchi ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninakubaliana naye tumepokea ushauri wake wa kuendelea kuipa umuhimu Bandari ya Musoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuhusiana na uwanja wa ndege wa Musoma, kwanza, ninampongeza Mheshimiwa Mbunge, ana moyo wa shukrani wa kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuwa iliamua kutokana na umuhimu wake mkubwa wa uwanja wa Musoma kwanza, kwenye madini, pili kwenye utalii na kwenye mifugo na kwenye uvuvi, kaamua kujenga uwanja wa Musoma, na shilingi bilioni 35 zilielekezwa

kwenye uwanja huo ambapo tayari mkandarasi yupo *site* amemaliza kujenga *runway* kwa maana ya njia ya kutua na kushuka ndege pamoja na maegesho na vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichobaki sasa ni kumalizia vitu vilivyobakia ili ndege iweze kuanza kutua. Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge avumilie, tunamalizia vitu vichache vilivyobakia na mara baada ya hapo, ndege itaanza kutua kwa sababu tumeshavuka zaidi ya 60% ya ujenzi wa uwanja huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine nitoe maelekezo pia kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa kwamba wenzetu wa *ATCL* waendelee na mchakato wao wakishirikiana na *TCAA* ili mara tu taratibu zitakapokamilika, basi ndege hiyo iweze kuanza kutua.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba nisisitize maswali mafupi ya nyongeza. Hata mwuliza swali akiwa na maswali ya nyongeza anatakiwa aulize maswali mafupi na Mawaziri wanatakiwa wajibu kwa ufupi na kwa kueleweka. Tukiendelea kuhutubia na kujenga hoja katika maswali, watu wengine hawatapata fursa ya kuuliza maswali.

Tunaendelea na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero, aulize swali lake.

Na. 329

**Kupunguza Bei za Nauli ya Mabasi Kilombero**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itasimamia kupunguza nauli za Mabasi na Vyombo vya Usafiri kutoka Ifakara, Mang’ula hadi Mkamba Kidatu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Uchukuzi, kupitia *LATRA*, hupanga nauli za mabasi yanayotoa huduma za usafiri wa umma nchini kwa madaraja ya kawaida *(ordinary)* na daraja la kati yaani *(semi-luxury)*. Nauli hizi hupangwa kwa kuzingatia hali zote za kiuchumi na kijamii na pia huzingatia umbali pamoja na hali ya barabara. Baada ya kukamilisha upangaji wa nauli kwa kilomita, *LATRA* huandaa majedwali ya nauli kulingana na urefu wa safari kwa kila njia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, *LATRA* hufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara na kutoa ufafanuzi wa nauli kupitia namba zake za bure ikiwemo 0800110019 kuwawezesha watumiaji huduma kutoa taarifa za ukiukaji wa sheria au huduma zisizokidhi viwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara inatambua kuwepo kwa changamoto za ukiukwaji wa taratibu za sheria katika maeneo ya kutoka Mikumi kuelekea Ifakara, Mang'ula, Kilombero hadi Malinyi ambapo *LATRA* huchukua hatua kali dhidi ya watoa huduma wanaokiuka masharti ya leseni zao ikiwemo kutoza nauli inayozidi kikomo kilichoidhinishwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri kwa kuwa umekiri kwamba Barabara ya Ifakara kwenda Mikumi kuna changamoto za watu kuongeza nauli. Ni barabara ya lami, ina kilometa 67 tu, lakini wananchi wamekuwa wakitozwa labda zaidi ya shilingi 6,000, tofauti na Moshi (kwa mfano) ambapo Moshi - Arusha ni karibu kilomita 100 watu wanatozwa nauli hiyo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kwamba ni muhimu kuilekeza *LATRA* kuweka timu maalum katika Halmashauri ya Mji wa Ifakara ili ku-*deal* na watu hawa

wanaonyonya wananchi wetu ambao wana hali ngumu ya kiuchumi na uchumi ni kigezo kimojawapo cha upangaji wa nauli?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Asenga kwa jinsi anavyopigania maendeleo ya wananchi wake, lakini na kushughulikia changamoto zinazowakabili ikiwa ni pamoja na watu wachache wanaoweza pengine kukiuka masharti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, ninawaelekeza *LATRA* waendelee kuweka mkazo katika eneo hilo na wale wote wanaobainika kukiuka, waweze kuchukuliwa hatua. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ninakushukuru sana kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Mbunge. Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Timida Mpoki Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 330

**Ufanisi wa Mageuzi ya Mitaala na Elimu ya Amali kwa Vijana**

**MHE. TIMIDA M. FYANDOMO** aliuliza: -

Je, vigezo gani vinatumika kupima ufanisi wa mageuzi ya Mitaala baada ya kusisitiza Elimu ya Amali ili kupunguza pengo la Elimu na soko la ajira kwa Vijana?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, ninaomba kujibu swali la namba

330 la Mheshimiwa Timida Mpoki Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hupima ufanisi wa mitaala ili kubaini kama unakidhi mahitaji ya soko la ajira, malengo ya ujifunzaji yanafikiwa, na changamoto zilizopo katika utekelezaji wake. Tathmini za sasa zinaonesha kuwa shule zinazotekeleza mkondo wa amali zinatoa ujuzi unaohitajika katika soko la ajira kutokana na ulinganifu wa maudhui ya mitaala na mahitaji halisi ya ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya upimaji endelevu wa Kitaifa, hususan Mitihani ya Kidato cha Pili mwaka 2025, yameonesha wanafunzi wamefikia malengo yaliyokusudiwa ya ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, kuongezeka kwa hamasa ya wanafunzi kujiunga na mkondo wa amali pia kunaashiria kuimarika kwa imani ya jamii katika mfumo huo, ambapo shule zinazotekeleza mkondo huo zimeongezeka kutoka 35 mwaka 2024 hadi shule 119 mwaka 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutumia tafiti za ufuatiliaji wa wahitimu *(tracer studies)*, tathmini za umahiri wa vitendo, na ushirikiano kati ya taasisi za elimu na sekta binafsi ili kuhakikisha wahitimu wanapata ujuzi unaokidhi mahitaji ya soko la ajira.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Timida Mpoki Fyandomo.

**MHE. TIMIDA M. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Je, Serikali imeweka utaratibu gani wa kuwashirikisha sekta binafsi, viwanda, waajiri katika tathmini ya mitaala hii. Ili kuhakikisha ujuzi unaotolewa unaendana moja kwa moja na mahitaji ya soko la ajira ili kufikia malengo ya Ilani Chama cha Mapinduzi ya kutoa ajira milioni 8...

*(Hapa kipaza sauti kiizimika)*

**MWENYEKITI:** Zima, halafu washa tena.

**MHE. TIMIDA M. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya kuhakikisha sekta binafsi inachangia 70%?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, je, Serikali ipo tayari kuweka mfumo wa kufuatilia matokeo na maendeleo ya vijana hawa wanaohitimu ili kupima ufanisi halisi wa mageuzi haya ya mitaala? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Fyandomo kwa ufuatiliaji wake. Ninajua anawakilisha vijana. Kwa hiyo, ndiyo maana anawasemea vijana kuona kwamba mafunzo wanayopata yanakidhi soko la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka utaratibu wa kushirikisha sekta binafsi, viwanda na waajiri katika kuandaa, kutathmini na kupitia mitaala ambayo inahakikisha ujuzi unatolewa unaendana na mahitaji ya soko la ajira. Hili hufanyika kupitia vikao vya wadau, warsha za tathmini, tafiti za soko la ajira lakini pia mafunzo kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyofafanua juzi kwenye bajeti kwamba tarehe 9 Februari, 2026 Serikali iliingia katika makubaliano na waajiri sekta binafsi na wenye viwanda kuhakikisha kwamba masomo yanayotolewa katika vyuo vyetu yanaendana na *gaps* ambazo zipo katika soko la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali imekuwa ikifanya hivi na hivi sasa waajiri sekta binafsi na viwanda wanazungumza lugha moja na vyuo ambavyo vinatoa mafunzo kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kama nilivyojibu katika swali langu la msingi kwamba Serikali itaendelea kutumia tafiti za ufuatiliaji wa wahitimu *(tracer studies)*, tathmini za umahiri wa vitendo, na ushirikiano kati ya taasisi na sekta binafsi ili kuhakikisha

wahitimu wanapata ujuzi unaokidhi mahitaji ya soko la ajira. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ninakushukuru sana kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Mbunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maji Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Missenyi aulize swali lake.

Na. 331

**Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria**

**MHE. FLORENT L. KYOMBO** aliuliza: -

Je, lini Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Kata ya Kashenye, Kanyizo na Bwanjai utakamilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Jimbo la Missenyi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi wa maji wa kutumia chanzo cha Ziwa Victoria kwenda Kata ya Kashenye iliyopo katika Wilaya ya Missenyi Mkoani Kagera kwa gharama ya zaidi ya Shilingi bilioni 1.8. Mradi huo kwa sasa unahudumia wananchi wapatao 4,630 waishio katika vijiji vitatu vya Kashenye, Bukwali na Bushago.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kiasi cha zaidi ya shilingi bilioni sita kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi huo unaolenga kunufaisha zaidi ya wananchi 17,433 waishio katika vijiji 10 vilivyopo katika kata mbili za Kanyigo na Banjwai.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipongeze sana juhudi za Serikali kwa sababu tangu kuumbwa kwa dunia, kata hizo ambazo zipo kando mwa Ziwa Victoria zilikuwa hazina majisafi na salama, lakini mbele ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amevunja rekodi kwa kuhakikisha sasa mradi huo wa Ziwa Victoria unakamilika katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ulikuwa na Awamu ya Kwanza na ya Pili kama ambavyo imejibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri. Katika Awamu ya Kwanza ilikuwa ni kuhakikisha vijiji vitatu vya Kata ya Kashenye ambavyo ni Bukwali, Bushago na Kashenye yenyewe lakini na vijiji vinne vya Kata ya Kanyigo ambavyo ni Kitarama, Weyunge, Kikukwe pamoja na Bugombe vinapata majisafi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mradi huu sasa umekamilika na mkandarasi kwa kusimamiwa na Ofisi ya *RUWASA* Mkoa na Wilaya wame-*test* maji yanatoka, je, sasa ni lini wananchi katika vijiji hivyo vya Kata hizo mbili, Kashenye na Kanyigo watasambaziwa maji na kuhakikisha kwamba vijiji vyote wamepata maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Mradi huu wa Awamu ya Pili ilikuwa ni kujenga miundombinu ya maji kwenda Kata ya Bwanjai. Kata ya Bwanjai ni kata muhimu kwa kuwa ina Kituo cha Hija ambacho wananchi kutoka Tanzania, Rwanda, Burundi na Kenya huwa tunajumuika kwa mwaka mara moja kwa ajili ya hija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika vijiji hivyo sita vya Kata ya Bwanjai ambavyo ni Rwamashonga, Buhekela, Buhangaruti, Bukabuye pamoja Nyabihokwe na Bukabuye na Buhekela wananchi hawa hawana majisafi na salama. Ni lini sasa Serikali kwa kuwa imeshafanya kazi nzuri itatoa kibali ili awamu ya pili itangazwe mradi huu uanze kujengwa katika vijiji sita vya Kata ya Bwanjai? Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza kaka yangu kwa kazi kubwa anayoifanya kuwatetea wananchi wa Missenyi na kwa kuhakikisha kwamba Serikali inaendelea kumtua mama ndoo kichwani. Pia ninampongeza sana kwa ufuatiliaji wa karibu wa miradi yote hii ambayo inaendelea kutekelezwa. Nimpongeze sana kwani wakati anaingia madarakani Mheshimiwa Mbunge, upatikanaji wa maji katika Jimbo la Missenyi ulikuwa 56% na sasa ni 78%. Ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kufanya kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mradi huu wa Awamu ya Kwanza kati ya Kashenye, Bukwali pamoja na Kanyigo, mradi huo sasa upo 95% na kama ambavyo amesema, kazi iliyobaki ni kusambaza na kufikisha kwa wananchi. Kwa hiyo, iliyofikiwa mpaka sasa, tunaamini mpaka ikifika Oktoba, 2026 mradi huo utakuwa umekamilika na wananchi wataanza kupata huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali la pili, ni kweli kabisa awamu ya pili ambayo tumeiweka kwenye bajeti yetu ya 2026/2027 na tunaamini na kushukuru pia kwa kushiriki kupitisha bajeti hii, nitumie fursa hii kwa niaba ya Waziri wa Maji kumwelekeza *DG* wa *RUWASA* atoe kibali mara moja ili iweze kutangazwa *tender* na mradi huu uanze mara moja bila kuchelewa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo ya Maji, Mheshimiwa Martha Festo Mariki, Mbunge Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 332

**Maji ya Ziwa Tanganyika Kuhudumia Mikoa Jirani**

**MHE. MARTHA F. MARIKI** aliuliza: -

Je, mpango wa kuyapeleka maji ya Ziwa Tanganyika katika maeneo jirani kama vile Mpanda, Katavi umefikia wapi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, jibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Festo Mariki, Mbunge Viti Maalum, Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali ni kuhakikisha inatekeleza miradi ya maji kwa kutumia vyanzo vya maji vya uhakika ikiwemo Ziwa Tanganyika ikiwa ni uelekeo wa kujenga Gridi ya Taifa ya Maji. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali imeanza kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kupitia Mtaalam Mshauri kwa ajili ya kuyatoa maji ya Ziwa Tanganyika kwenda mikoa ya Kigoma, Rukwa pamoja na Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hiyo imeanza mwezi Machi, 2026 na inatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 18. Kukamilika kwa kazi hiyo kutaiwezesha Serikali kuanza kutafuta fedha za utekelezaji wa mradi huo kulingana na mahitaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Martha Mariki.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na kwa kuwa mradi huu utanufaisha pia wananchi wa Wilaya ya Tanganyika katika vijiji vya Ikola, Karema, Kapalamsenga, Kabungu pamoja Sibwesa, je, Serikali haioni ipo haja ya kuharakisha mradi huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa chujio la maji katika Kata ya Mamba ili wananchi wa kata hizo waweze kupata majisafi na salama hususan wakina mama ambao wamekuwa wakitembea umbali mrefu sana kwenda kutafuta majisafi na salama? Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Martha Festo Mariki, Mbunge mahiri kabisa kutoka Mkoa wa Katavi na kwa kazi kubwa ya kuwasemea akina mama wa Mkoa mzima wa Katavi na kwa kuendelea kushirikiana nasi, kuendelea kubainisha maeneo ambayo yana changamoto ili tuweze kuchukua hatua stahiki ili wakina mama waendelee kupata huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haja ya Serikali kuharakisha mradi huu. Mradi huu wa ujenzi wa Gridi ya Taifa ya Maji ni mkubwa, lakini tunafahamu kwamba iwapo mradi huu utajengwa, tutahitaji kuwa na ukubwa wa mtandao wa zaidi ya kilomita 6,200. Pia mtandao wa mabomba peke yake utakuwa zaidi ya kilomita 5,000, lakini kutakuwa na mitaro ambayo ni zaidi ya kilomita 1,200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni uwekezaji mkubwa sana ambao umewahi kutokea katika Serikali yetu. Tumpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuchukua maamuzi haya. Maamuzi haya ni mwarobaini kwa changamoto ya maji katika Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba Mheshimiwa Rais tayari ameshatoa shilingi bilioni sita kuhakikisha kwamba Mtaalamu Mshauri analipwa na ndani ya miezi 18 usanifu wa kina na upembuzi yakini utakuwa umekamilika, na baada ya hapo tutajua gharama gani ambayo itakwenda kutekeleza mradi huo ili Serikali ianze mchakato wa kupata hizo fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Bwawa la Mamba Majimoto ni bwawa ambalo lipo kwa Mheshimiwa Laurent Luswetula. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Martha Mariki kwa kuibua hili jambo, lakini mradi huu wa chujio ambalo lipo Mamba una gharama ya shilingi bilioni 4.4, na katika bajeti hii, tayari tumeweka fedha kwa mpango huo na tayari Serikali imetenga zaidi ya shilingi milioni 344 ya kuanza nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini kwamba mradi ukishaanza, kila pale ambapo mkandarasi atakuwa anakamilisha hatua mojawapo na kuwasilisha hati za madai atakuwa analipwa ili kuhakikisha kwamba mradi huu unakamilika kwa ajili ya kutibu maji na wananchi wapate huduma ya majisafi na yaliyo salama na endelevu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ninakushukuru sana kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Mbunge. Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa aulize swali lake.

Na. 333

**Fidia kwa Wananchi wa Kitongoji cha Isela Ndolezi**

**MHE. JAPHET N. HASUNGA** aliuliza:-

Je, upi mpango wa Serikali kuwalipa fidia Wananchi wa Kitongoji cha Isela Ndolezi ili kupisha upanuzi wa eneo la Kimondo na kuleta wanyamapori?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mbunge wa Vwawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1967 Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Idara ya Malikale ilitangaza Kimondo cha Mbozi kuwa eneo la Urithi wa Taifa kwa Tangazo la Serikali Na. 90. Aidha, Wizara ilikasimisha rasmi Kituo cha Kimondo kwa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kupitia Tangazo la Serikali Na. 631 la tarehe 14/08/2020 ili kuimarisha usimamizi, uendeshaji na uendelezaji wa eneo hilo kwa lengo la kukuza uhifadhi na utalii wa mikoa ya ukanda wa kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya uchambuzi wa kina wa eneo lililopo sasa, Serikali iliona ni busara kuliendeleza eneo hilo ili kuona tija yake kabla ya kuwa na mipango ya kutwaa maeneo ya jirani. Hivyo, kwa sasa Serikali haina mpango wa kupanua eneo hilo wala kuanzisha shughuli nyingine tofauti na zile zinazoendelea kwenye eneo hilo kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Isela - Ndolezi wanaombwa waendelee na shughuli zao katika maeneo yao na kushirikiana na Serikali katika uendelezaji wa utalii katika eneo hilo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba tuzungumze kwa sauti ya chini ili tuweze kusikilizana.

Mheshimiwa Japhet Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa hii nafasi. Ninaomba nichukue nafasi hii kumpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla kwa majibu mazuri sana na yenye faraja, kwa kweli tunashukuru sana. Sasa ninayo maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wananchi wa eneo hili tulifanya vikao kadhaa wakati tunataka kutoa lile eneo kiasi kwamba wakakosa amani, sasa ni lini Serikali itaenda pale ili ikawatangazie rasmi kwamba mradi ule sasa haupo, waendelee kula maisha katika lile eneo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa kila mwaka siku ya vimondo duniani tulikuwa tunafanya sherehe pale kwenye eneo la Kimondo kwa muda wa siku tatu kwa ajili ya kukitangaza na kutangaza utalii, lakini huduma hii ilisitishwa karibu miaka mitatu, minne iliyopita, je, ni lini Serikali sasa itarudisha utaratibu ule wa kusherehekea Siku ya Vimondo Duniani ili kuweza kutangaza utalii wa kusini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu, ninaomba uniruhusu nimpongeze sana, kwa namna alivyokuwa anafuatilia suala hili la fidia pale Mbozi, tena kwa hekima na busara ya hali ya juu. Hongera sana Mheshimiwa Hasunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara tu baada ya Mkutano huu wa Bunge, nitaambatana na Mheshimiwa Mbunge twende kutoa taarifa rasmi kwa wananchi wetu kwamba eneo hili sasa ni halali kutumia, lile ambalo wamezuiliwa na tuwe pamoja katika kuendeleza urithi wetu ule wa kimondo kile pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kweli, alichosema Mheshimiwa Mbunge kwamba tulikuwa na maadhimisho ya kila mwaka, mara nyingi ni tarehe 30 Juni. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala lile la maadhimisho litaendelea na mwaka huu wa fedha tarehe 30 mwezi wa Sita, mimi na yeye na wananchi. Ninaomba awaambie wananchi wenzetu kwamba tutakuwepo huko kwa ajili ya maadhimisho hayo.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Mbunge.

Tunamalizia Wizara ya Ujenzi. Mheshimiwa Moses Charles, Bujaga, Mbunge wa Sumve, aulize swali lake.

Na. 334

**Ujenzi wa Barabara ya Ndugu – Malya (Kilometa 24 – *Package II*)**

**MHE. MOSES C. BUJAGA** aliuliza:-

Je, lini Barabara ya Ngudu – Malya (kilometa 24 – *Package II)* itakamilika kwa kiwango cha lami ili kuimarisha usafiri kati ya Majimbo ya Sumve na Kwimba?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Moses Charles Bujaga, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa Barabara ya Ngudu – Malya kwa kiwango cha lami. Mara baada ya kukamilika kwa usanifu na gharama za mradi kujulikana, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Moses Charles Bujaga.

**MHE. MOSES C. BUJAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Hungumalwa - Ngudu kwenda Magu imezungumzwa kwa muda mrefu na mwaka 2025 mwezi Mei wakati wa ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri alipokea maelekezo kutoka kwa Mheshimiwa Rais kwamba kipande cha barabara kutokea njia panda ya Nyambiti kwenda Nkalalo kijengwe kwa kiwango cha lami. Sasa tulitaka kujua ni lini wananchi wa Jimbo la Sumve watapata lami? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Barabara ya Fulo - Nyambiti kwenda Malya inafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Ni lini kazi hii itakamilika ili mkandarasi apatikane kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishe Mheshimiwa Bujaga kwamba maelekezo aliyotoa Mheshimiwa Rais na pia akiwepo Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi ni maelekezo ambayo yako kwenye mipango yetu na yatatekelezwa kama yalivyokuwa yameelekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Barabara ya Hungumalwa, Ngudu hadi Magu tutaijenga barabara kwa awamu ambapo tumeahidi kuanza kuijenga kwa kilometa 10 na mkandarasi alishapatikana. Mkandarasi anatakiwa kuendelea tu akishalipwa fedha ya awali, tutaanza kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara ya pili ambayo ameitaja ya kutoka Fulo - Sumve kwenda Nyambiti, barabara hii iko kwenye usanifu, na tunavyoongea sasa hivi, iko karibu 60% ili iweze kukamilika kusanifiwa, na baada ya hapo sasa tutajua gharama na tutakuwa tayari kuijenga kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Chamazi, aulize swali lake.

Na. 335

**Ujenzi wa Barabara ya Mbande – Kisewe Hadi Msongola**

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Mbande – Kisewe hadi Msongola utakamilika kwa kuzingatia umuhimu wake?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Chamanzi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Barabara ya Mbande – Kisewe hadi Msongola yenye urefu kilometa 3.8 unaendelea ambapo kwa sasa jumla ya kilometa 1.6 zimewekwa tabaka la lami, kilometa 1.1 zipo kwenye tabaka la kokoto na kilometa 1.1 zipo kwenye hatua za matabaka ya udongo. Ujenzi wa barabara hii unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2026.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Chaurembo.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mkandarasi aliyepewa kazi hii amekuwa akisuasua sana, je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kuongozana na mimi kufika *site* na kutoa maelekezo mahsusi yatakayowezesha mpaka kufikia mwezi Juni kuwa barabara hiyo imekamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Je, Serikali ina mpango gani wa kupanua Barabara ya kutoka Rangi Tatu mpaka Mbande ili kuja kuunganisha na barabara hii tunayoizungumzia?

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Abdallah kwa maswali mafupi ya Kibunge. Waziri, Mheshimiwa Ulega, majibu.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaomba nitumie fursa hii kumpongeza Naibu Waziri Mheshimiwa *Engineer* Msongwe Kasekenya kwa majibu mazuri ya msingi aliyoyatoa. Pili, ninaomba nimpongeze sana Mbunge wa Jimbo la Chamazi, Mheshimiwa Abdallah Chaurembo kwa swali hili zuri. Maswali yake yote mawili yanayohusu Barabara ya Msongola – Mbande, na hili ni kwamba mkandarasi huyu tulishafanya utaratibu wa muda mrefu wa kuhakikisha kwamba tunamtoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana *engineer* wa Mkoa wa Dar es Salaam, amefanya ubunifu kwa maana ya kumtoa ni jambo moja, lakini kumsaidia kuhakikisha kwamba anakamilisha kazi ya wananchi ni jambo la pili, na ndilo muhimu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, alichokifanya *engineer* ni kuhakikisha kwamba ana *subcontract,* yule mkandarasi apate *supplier* wa lami na vifaa vya ujenzi kulingana na hesabu zake kuwa ziko chini ya uwezo na hivi sasa *subcontract* ambaye wamekubaliana amekuwa akim-*supply* ni sababu ya mvua. Mvua sasa Dar es Salaam inakwenda kukoma na *inshallah* wataenda kukamilisha eneo lote mpaka lile la Mbande kazi ile ya wananchi wa Barabara hii ya Rangi Tatu – Mbande - Chanika mpaka Mvuti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni barabara ya kutoka Rangi Tatu mpaka Chamazi - Mbande. Jambo hili ni muhimu sana kwa sababu barabara hii inahudumia watu wengi sana na kwa hivyo kwa sasa hivi tumekubaliana barabara hiyo tutakwenda kuitanua iwe barabara nne, kwa sababu ni barabara muhimu na yenye *population* kubwa sana ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari *TANROADS,* Mkoa wa Dar es Salaam wameshaanza utaratibu wa kufanya *compensation*. Liko eneo la mwanzo; Rangi Tatu - Kona halina shida. Tayari wananchi wamekubaliana na *TANROADS* kwamba mpaka kufika mwezi wa Tano au wa Sita wafanyabiashara wenye maduka wa eneo lile watakuwa wao wenyewe wameondoka na sehemu iliyobaki tunaendelea na majadiliano ili wenye haki wapate haki yao na wale ambao walishapata haki waweze kutupisha tufanye utanuzi wa barabara ile inayokwenda katika Kiwanja cha Azam, kiwanja ambacho tunayo matumaini kitatumika kwa ajili ya mazoezi wakati wa *AFCON*. Ninaomba kuwasilisha, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri wa Wizara ya Ujenzi kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Mbunge.

Swali letu la mwisho itaulizwa na Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Mbunge wa Karagwe.

Na. 336

**Ujenzi wa Barabara ya Nyakahanga – Benako**

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha ili kukamilisha ujenzi wa Barabara ya Nyakahanga – Benako?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Mbunge wa Karagwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Nyakahanga – Benako ni Sehemu ya barabara ya Bugene – Kasulo (Benako) yenye urefu wa kilometa 128.5. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imeanza ujenzi kwa kwango cha lami wa barabara hii kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha kwa kuanza na sehemu ya Bugene – Burigi Chato yenye urefu wa kilometa 60 ambapo utekelezaji unaendelea. Kwa sehemu zilizobaki, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, kipande hiki ambacho amekisema cha kilometa 60 kuanzia Nyakahanga – Bisheshe – Nyashozi - Chanyamisa mpaka Kijiji cha Muungano barabara imeharibika kwa sababu ya mvua na mkandarasi haendelei na kazi kwa sababu anadai shilingi bilioni 9.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Ulega alishatembelea hizi barabara. Je, ni lini mkandarasi huyu atalipwa hizi fedha shilingi bilioni 9.2 ili kuweza kuendelea na ujenzi na kutoa adha kwa wananchi? Barabara hii sasa hivi haipitiki kwa sababu ya mvua kubwa ambazo zimenyesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, rafiki yangu, kaka yangu Mheshimiwa Ulega, tulitembelea barabara ya kutoka pale Karagwe – Kayanga – Omugakorongo – Kituntu – Rwambaizi – Igurwa - Businde mpaka Murongo. Ni barabara muhimu sana kwa Mkoa wa Kagera pamoja na nchi yetu kwa maana inaunganisha Nchi za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, manunuzi yamekuwepo muda mrefu, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, ndugu yangu, rafiki yangu, toka nimetoka kwenye hii Wizara tuko kwenye hatua ya manunuzi, je, ni lini manunuzi haya yatakamilika? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba mkandarasi ameshawasilisha hati za malipo Wizarani na sisi kama Wizara tumeshawasilisha hayo madai yake Wizara ya Fedha ili aweze kulipwa hiyo fedha ambayo anaidai na mkandarasi yuko karibu 48% ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mvua zilikuwa zinanyesha na Mheshimiwa Mbunge atakubaliana na mimi eneo hilo la Karagwe mvua ni nyingi sana, na sasa imeanza kupungua, nimwelekeze tu Meneja wa Mkoa aweze kumsimamia mkandarasi huyo, kwa sababu ana wajibu wa kuhakikisha kwamba hiyo barabara inapitika aweze kumsisitiza ili aweze kuwa barabarani na wananchi waweze kuitumia hiyo barabara ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala lake la pili la barabara ya Mrongo - Rwambaizi kuja Omugakorongo, tayari hiyo barabara imegawanywa kwenye *lot* mbili. *Lot* ya kwanza ambayo tunaanza kuijenga tumeshakamilisha hatua za manunuzi zote. Tunachosubiri sasa ni ku-*sign* ili kazi iweze kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge, tunatambua umuhimu wa hizo barabara kwa sababu ndiyo zinazounganisha wenzetu wa Uganda kwa maana wakitokea Murongo ama Mtukula na wenzetu wa Rwanda na Burundi. Kwa hiyo, ni barabara ambazo kama Serikali inaziangalia kwa upekee wake kwa sababu inakuwa ni njia ya mkato sana mtu akitoka Burundi ama Rwanda - Benako - Nyakahanga anaweza kwenda Murongo ama Mtukula.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Mbunge.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umekwisha, na maswali ya leo tumemaliza. Sasa hivi ni wakati wa kuwatangaza wageni.

Tuna wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Kwanza tuna wageni wa Mheshimiwa Spika: *Members of the Forum of Parliaments (FP-ICGLR): Honorable Sergio Leonardo Vaz, Head of Delegation and Member of Parliament from Angolan Parliament; Honorable Suzana Augusta de Melo, Member of Parliament From Angolan Parliament; Ambassador Deo Mwapinga, Secretary General of the Forum of Parliaments Of ICGLR; Ambassador Dominingos de Almeida da Silva Coelho, The Angolan Ambassador Accredited in Tanzania; Julcimara Dominique Viriato Cordoso Joaquim, First Secretary Angola Embassy; Maria Graciana Jaime, Staff Angola Embassy; Isaura Vicente, Program Manager from the Forum of Parliaments of ICGLR; Antonio Pinto, Staff Angolan Parliament. You are most welcome our members from ICGLR. (Makofi)*

Wageni wengine ambao wamekaa kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika ni wageni wa Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, Waziri wa Uchukuzi; hao ni Profesa Godius Kahyarara, Katibu Mkuu; Balozi Ernest Jumbe, Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania; Ndugu Jaffer Machano, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Reli; Ndugu Juma Fimbo, Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania; *Captain* Mussa Mandia, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania; Profesa Ame Ahmed Ame, Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini *(LATRA)*; na Ndugu Khamisi Mwinyimvua, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurungezi ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania; *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu George Kavenuke, Mwenyekiti CCM wa Wilaya ya Mufindi, Dkt. Linda Salekwa, Mkuu wa Wilaya wa Mufindi; Ndugu Reuben Chongolo, Katibu Tawala wa Wilaya ya Mufindi; Ndugu Castory Masangula, Mwenyekiti wa Halmashauri Wilaya ya Mufindi; Ndugu Regina Kivinge, Mwenyekiti wa

Halmashauri Mafinga Mji; na Ndugu Mashaka Mfaume, Mkurugenzi wa Wilaya ya Mafinga. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Fidelica Myovella, Mkurugenzi Mafinga Mji; Ndugu Clemence Nakuli, Katibu wa CCM, Mufindi; *CPA*. Dkt. Habibu Suluhu, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Udhibiti na Usafiri wa Ardhini; Ndugu Mohamed Salum, Mkurugenzi wa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania; Ndugu Plasduce Mbossa, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania; Ndugu Masanja Machibya, Mkurugenzi Mkuu Shirika la Reli Tanzania; Dkt. Jabiri Kuwe, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania; Ndugu Mzee Kilele, Mkurugenzi wa Biashara wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania; na Mhandisi Peter Ulanga, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Ndege Tanzania. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Patrick Mwanry, Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Ndege ya *Precision*; Ndugu Luo Yeping, Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Zijing; Ndugu Fortunatus Magambo, Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma; Ndugu Esther Mangenya, Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Azania; Ndugu Maseke Mabiki, Mkurugenzi wa Sera na Mipango ya Wizara ya Uchukuzi; na Ndugu Lucas Kambelenje, Mkurugenzi wa Utawala na Menejimenti ya Rasilimali Watu Wizara ya Uchukuzi. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Paul Chiganga, Mkurugenzi wa Huduma za Uchukuzi Wizara ya Uchukuzi; Ndugu Shomari Shomari, Mkurugenzi wa Miundombinu Wizara ya Uchukuzi; Ndugu Stella Katondo, Mkurugenzi wa Usalama na Mazingira Wizara ya Uchukuzi; na Ndugu Silvanus Kapandila, Mhasibu Mkuu wa Wizara. Karibuni sana wageni wetu kutoka Wizarani. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Profesa Mbarawa ni watumishi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (*TAA)*. Kuna *Cabin Crew* wa Shirika la Reli Tanzania na marubani na *Cabin Crew* wa Shirika la Ndege Tanzania. Karibuni sana marubani na *Cabin Crew* wa Shirika la Ndege *Precision*. *Cabin Crew* wa Baraza la Usafirishaji Njia ya Maji, *TASAA*. *(Makofi)*

Wapo wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Tuna wageni 77 wa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, Mbunge na Waziri wa Maliasili na Utalii. Hawa ni wanafunzi na walimu wa Shule ya *Kondoa Islamic* ya Mkoa wa Dodoma. Karibuni sana wanafunzi wetu kutoka hapa Dodoma. *(Makofi)*

Yupo Mgeni wa Mheshimiwa David Ernest Silinde, Naibu Waziri wetu wa Kilimo. Huyu ni rafiki yake Dkt. Peter Dalali Kafumu, Mbunge Mstaafu wa Igunga. *(Makofi)*

Mwingine ni mgeni wa Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagula ambaye ni Ndugu Paschal Itambula, ni mtoto wake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Devota Mathew Minja, ambaye ni Ndugu Ibrahim Hamis kutoka Moshi Mkoani Kilimanjaro. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Yohana Stephen Msita wa Jukwaa la *Central Zone Awards* kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava. Hawa ni viongozi wa Kwaya ya Safina KKT, Mombo, Mkoani Tanga, Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, ambaye ni Mwenyekiti wa Mtaa wa Mivinjeni, Ndugu Fadiga Legele, kutoka Jijini Dar es Salaam.  Karibu sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Amour Seif Abdalla ambaye ni Ndugu Edwin Maturu, ni Mkurugenzi wa *Agriculture Group Limited* kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wengine ni wageni watatu wa Mheshimiwa Asma Ali Mwinyi ambaye ni familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia, wapo wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Tunaye Ndugu Tatu Nassoro kutoka Manyoni, Mkoani Singida, na Ndugu Yesaya Japhet kutoka Tukuyu Mkoani Mbeya. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 71 na walimu saba wa Shule ya Msingi Mkapa ya Jijini Dodoma, karibuni sana wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Vilevile, wapo wanafunzi wengine 83 na walimu 10 wa Shule ya Sekondari Ula kutoka Wilaya ya Kondoa, Mkoani Dodoma. Karibuni sana wageni wetu wote katika Bunge letu. *(Makofi)*

Pia, yupo Ndugu Japhet Shirima, Makamu wa Rais wa *Red Cross Tanzania.* Karibuni sana wageni wetu wote katika Bunge letu. *(Makofi)*

Katibu, tuendelee.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa ninamwita Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, ili awasilishe Mpango na Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kutoka Wizara ya Uchukuzi. Karibu sana.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia Taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ambayo imechambua Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kuidhinisha

Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kutujalia, kutuwezesha kukutana hapa leo tukiwa na afya njema. Ninaomba Mwenyezi Mungu atuongoze vyema katika kujadili hotuba hii ya Wizara ya Uchukuzi na Bajeti ya Serikali kwa ujumla, ili kufikia malengo ya Dira 2050 katika kuwaletea Watanzania maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee ninaomba kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa ushindi alioupata katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 29 Oktoba, 2025. Ushindi huu unaonesha imani kubwa ambayo Watanzania wameendelea kuwa nayo kwa uongozi wake wenye maono, na unawaletea wananchi maendeleo. Aidha, ninapenda kumpongeza kwa dhati kwa hatua madhubuti alizozichukua katika kutekeleza ahadi alizozitoa kwa wananchi ndani ya siku 100 za mwanzo katika kipindi chake cha awamu ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji huo umeonesha dhamira ya kweli ya kuhakikisha kuwa, Serikali inatekeleza ahadi zilizotolewa na kuleta matokeo chanya kwa sekta mbalimbali nchini. Tunamtakia Mheshimiwa Rais afya njema, umri mrefu, hekima na mafanikio zaidi katika kuiongoza nchi yetu ili kufikia malengo ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mchango wake mkubwa wa kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu ya Serikali. Aidha, ameendelea kusimamia kikamilifu masuala ya Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na kuthibitishwa kwa kishindo na Bunge hili Tukufu kuwa Waziri

Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wote ni mashahidi kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameonesha umahiri mkubwa katika kusimamia shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mussa Azan Zungu kwa kuchaguliwa kwa kishindo na Waheshimiwa Wabunge kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninampongeza pia Mheshimiwa Daniel Sillo kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge hili Tukufu. Aidha, ninatumia fursa hii kuwapongeza Wenyeviti wa Bunge, kwanza wewe Mheshimiwa Najma Giga na Mheshimiwa Philip Mwanyika, kwa kuendelea kuaminiwa kuwa Wenyeviti wa Bunge. Kwa namna ya kipekee ninampongeza Mheshimiwa Cecilia Paresso kwa kuchaguliwa pia kuwa Mwenyekiti wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru na kuipongeza sana Kamati ya Kudumu ya Miundobinu inayoongozwa na Mwenyekiti Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso, ambaye amechaguliwa kwa mara nyingine tena kuiongoza kamati hii. Ninapenda pia kuishukuru Kamati hii kwa uchambuzi ilioufanya kwenye Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninamshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa kwa kuendelea kuniamini na kuniteua katika nafasi hii kwa mara nyingine kuwa Waziri wa Uchukuzi. Ninapenda kumhakikishia kuwa, kwa kushirikiana na Naibu Waziri, Mheshimiwa David Kihenzile, tutatekeleza majukumu aliyotukabidhi kwa kufuata miongozo anayotupatia pamoja na miongozo mingine ya nchi yetu. Pia, tutaendelea kutekeleza shughuli za Wizara ili kuweza kufikia malengo mahususi ya kuendeleza Sekta ya Uchukuzi na kuwa na mchango mkubwa katika kuchochea ukuaji wa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri walioaminiwa na kuteuliwa, ili kuongoza Wizara mbalimbali. Ninatumia nafasi hii ya leo kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa na

waliochaguliwa kuwakilisha wananchi katika Bunge hili Tukufu la Kumi na Tatu. Ninawahakikishia kuwa Wizara iko tayari kupokea ushauri na maoni ya Watanzania, kupitia kwenu, ili kuendelea kutatua kero na changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa, ninatoa pole kwa Bunge lako Tukufu, familia na Watanzania wote kufuatia kifo cha Mheshimiwa Jenista Mhagama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho, kilichotokea tarehe 11 Disemba mwaka 2025, Mheshimiwa Halima Idd Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, kilichotokea tarehe 18 Januari mwaka 2026 na Mheshimiwa William Lukuvi aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Isimani na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu kilichotokea tarehe 25 Machi mwaka 2026. Hakika tunaendelea kuthamini na kuenzi michango yao katika Bunge hili na Taifa kwa ujumla. Tunamwomba Mwenyezi Mungu awapumzishe mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuendelea na uwasilishaji wangu, ninawashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa hotuba zao ambazo zimefafanua utendaji wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Mwelekeo wa Mwak mwaka wa fedha 2026/2027. Vilevile ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote waliowasilisha hotuba zao kabla yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, sasa ninaomba uniruhusu niwasilishe Taarifa ya Mapitio ya Mchango wa Sekta ya Uchukuzi katika kukuza uchumi wa Taifa, Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2025/2026 hadi kufikia Mwezi Machi mwaka 2026, na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninahitimisha kwa kuomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Bajeti kwa ajili ya Utekelezaji wa Shughuli na Miradi ya Wizara ya Uchukuzi, Fungu – 52 kwa Mwaka

wa Fedha 2026/2027 na Mchango wa Sekta ya Uchukuzi katika kukuza uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uchukuzi imeendelea kutoa mchango mkubwa katika kuchochea shughuli za uzalishaji na utoaji huduma katika sekta mbalimbali hapa nchini. Kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa ya mwaka 2024, Sekta ya Uchukuzi imekua kwa 4.2% na kuchangia pato la Taifa kwa 7.5% ambapo, ilikuwa ni ya tano katika sekta kubwa 17 katika kuchangia pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uchukuzi imeendelea kuchangia zaidi katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali yanayotokana na huduma za bandari. Mathalani, kati ya mwaka wa fedha 2020/2021 hadi mwaka wa fedha 2024/2025 mapato yanayotokana na kodi ya forodha za kibandari yamechangia wastani wa 40% ya mapato yote yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Aidha, mapato haya yataendelea kuongezeka siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Sekta ya Uchukuzi imeendelea kuchangia katika upatikanaji wa fedha za kigeni kupitia mauzo ya huduma za uchukuzi, usafirishaji na za kibandari. Taarifa ya Benki Kuu ya Tanzania ya Mwaka 2025 inaonesha kuwa, Sekta ya Uchukuzi imechangia mauzo ya kiasi cha Dola za Kimarekani bilioni 2.79 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani bilioni 2.35 zilizochangiwa mwaka 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukuza upatikanaji wa ajira nchini, Sekta ya Uchukuzi imeendelea kutoa ajira 198,480 wakati wa ujenzi wa miradi mbalimbali, pamoja na utoaji wa huduma za uchukuzi. Maelezo ya kina kuhusu mchango wa Sekta ya Uchukuzi katika kukuza uchumi wa Taifa yameainishwa katika Kitabu changu cha Hotuba ya Bajeti kuanzia aya ya 14 hadi aya ya 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026: Wizara ya Uchukuzi Fungu – 52 iliidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 2.746, kwa ajili ya matumizi ya kawaida na

utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 125.43 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, sawa na asilimia nne nukta tano saba na shilingi trilioni 1.621 zilikuwa, kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na 95.43%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Machi mwaka 2026, jumla ya shilingi trilioni 1.37 zilikuwa zimetolewa. Kiasi hiki ni sawa na 66.75% ya shilingi trilioni 2.059 zilizotakiwa kutolewa katika kipindi hicho. Kati ya fedha hizo zilizotolewa, shilingi bilioni 99.682 ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 1.275 ni fedha za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupokea fedha hizo, Wizara ya Uchukuzi imeendelea kutekeleza majukumu yake katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo: Kwanza, udhibiti na utoaji wa huduma za uchukuzi, udhibiti wa huduma za usafiri wa anga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu ya udhibiti wa usafiri wa anga, Serikali kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania *(TCAA)* imeendelea kusimamia ubora wa viwanja vya ndege nchini. Aidha, Shirika la Usafiri wa Anga Duniani limeendelea kuikasimisha Tanzania jukumu la uongozaji ndege zinazoruka na kupita urefu wa futi 25,000 juu ya anga la nchi ya Burundi. Sambamba na jukumu hilo, katika kipindi cha Julai mwaka 2025 hadi Machi mwaka 2026 jumla ya ndege 189 zimefanyiwa ukaguzi na kupewa vyeti vya ubora na kuendelea kufanya kazi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai mwaka 2025 hadi Machi mwaka 2026, abiria waliotumia usafiri wa anga wameongozeka na kufikia milioni 6.81 ikilinganishwa na abiria milioni 6.037 katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2024/2025 sawa na ongezeko la 12.63%. Kwa upande wa mizigo katika kipindi hicho, jumla ya tani 34,750.2 zimesafirishwa ndani na nje ya nchi ikilinganishwa na tani 33,112.5 zilizosafirishwa ndani na nje ya nchi katika kipindi kama hicho mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita, kupitia *TCAA*, imeendelea

na ujenzi wa Chuo cha Usafiri wa Anga, Jijini Dar es Salaam, ambapo utekelezaji wake umefika 11.3%. Maelezo ya kina kuhusu udhibiti wa utoaji wa huduma za anga kupitia *TCAA* yameainishwa katika Kitabu changu cha Hotuba ya Bajeti kuanzia aya ya 24 hadi 36.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara, kupitia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini yaani *LATRA,* imeendelea kutekeleza majukumu ya kusimamia udhibiti wa usafiri ardhini katika maeneo matatu; usafiri wa barabara, reli, na waya. Katika kutekeleza majukumu hayo. *LATRA* katika kipindi cha kuanzia Julai mwaka 2025 hadi Machi mwaka 2026 imetoa leseni 388,715 za usafirishaji, ongezeko la 55% kutoka mwaka uliopita. Leseni hizo zimehusisha mabasi ya abiria, magari ya mizigo na ya kukodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia kupitia *LATRA,* imeendelea kudhibiti nauli na ubora wa huduma huku ikihamasisha matumizi ya nishati mbadala, ikiwemo magari ya umeme hapa nchini. Mabasi 13,843 yameunganishwa kwenye mfumo wa ufuatiliaji wa *VTS* na madereva 12,699 wamesajiliwa kwa ajili ya kuongeza usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mfumo wa tiketi-mtandao umeendelea kutumika, ambapo mabasi 8,126 yameunganishwa na zaidi ya abiria milioni 21 wametumia mfumo wa tiketi-mtandao kununua tiketi zao hadi mwezi Machi mwaka 2026. Maelezo ya kina kuhusu udhibiti wa usafiri wa ardhini, kupitia *LATRA* yameoneshwa katika Kitabu changu cha Hotuba ya Bajeti kuanzia aya ya 39 hadi 57.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kusimamia udhibiti wa usafiri wa majini, Serikali kupitia Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania *(TASAC)* imeendelea kusimamia usalama wa vyombo vya usafiri majini, udhibiti wa uchafuzi wa mazingira unaotokana na shughuli za meli katika eneo la Tanzania Bara na kutoa huduma ya ugomboaji na uondoshaji wa shehena kwa bidhaa mahususi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa watoa huduma za usafiri majini. Katika kipindi cha Julai, mwaka 2025 hadi Machi

mwaka 2026, jumla ya watoa huduma 1,794 walisajiliwa na kupewa leseni, ikilinganishwa na watoa huduma 1,556 waliosajiliwa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha usalama wa usafiri katika Ziwa Victoria, Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Uganda zimeendelea kutekeleza mradi wa Kikanda wa kuboresha mawasiliano na uchukuzi katika Ziwa hilo. Mradi huo unajumuisha ujenzi wa kituo kikuu cha uratibu wa utafutaji na uokoaji na ununuzi wa boti mbili za ufuatiliaji na uokoaji pamoja na boti moja ya matibabu ambazo zimeanza kutoa huduma katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali imenunua boti nyingine mbili za kisasa za utafutaji na uokoaji ambazo zimeanza kutoa huduma katika Ziwa Tanganyika na katika Ukanda wa Bahari ya Hindi eneo la Mkoa wa Tanga. Maelezo ya kina kuhusu udhibiti wa usafiri majini kupitia *TASAC* yameoneshwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia aya ya 55 hadi 69.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania *(TMA)* imeendelea na utoaji wa udhibiti wa huduma za hali hewa nchini. Katika kuboresha huduma za hali ya hewa zinazotolewa kwa sekta ndogo ya usafiri wa anga, *TMA* imekamilisha ufungaji wa mitambo miwili ya uangazi wa hali ya hewa katika viwanja vya ndege vya Mpanda na Pemba. Aidha, *TMA* imeendelea na ujenzi wa miundombinu ya hali ya hewa ikiwemo maabara ya uhakiki wa vifaa vya hali ya hewa *(calibration center)* hapo Dar es Salaam ambayo ujenzi wake umefikia 46%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu udhibiti wa utoaji wa huduma ya hewa kupitia *TMA* yameonyeshwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia aya ya 70 hadi 83.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)* imeendelea kusimamia bandari za mwambao wa Bahari ya Hindi na Maziwa Makuu kwa

kuendeleza miundombinu na utoaji wa huduma za kibandari kwa viwango vinavyokubalika kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha kuanzia Julai mwaka 2025 hadi Machi mwaka 2026 *TPA* ilihudumia jumla ya tani milioni 29.66 za shehena ikilinganishwa na tani milioni 23.18 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2024/2025 sawa na ongezeko la 27.96%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, shehena iliyosafirishwa kwenda nchi za jirani imeongezeka hadi kufikia milioni 10.93 ikilinganishwa na tani milioni 8.29 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2024/2025, sawa na ongezeko la 32.64%. Ongezeko hilo limetokana na uboreshaji wa miundombinu na ushirikishwaji wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu kupata uhuru, nchi yetu imekuwa na changamoto ya kuhifadhi mafuta, Serikali ya Awamu ya Sita imeamua kulifanyia kazi suala hili kwa vitendo, ambapo *TPA* imeanza ujenzi wa miundombinu ya kupokea na kuhifadhi mafuta unaohusisha ujenzi wa matanki 15 ya mafuta yenye uwezo wa kuhifadhia mita za ujazo 378,000 ambapo utekelezaji wake umefikia 42% na unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, mwaka 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 imeainisha umuhimu wa kujenga Bandari ya Bagamoyo. Ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali kupitia *TPA* imekamilisha maandalizi ya kuanza utekelezaji wa mradi huu wa kimkakati. Bandari hiyo itahusisha ujenzi wa gati lenye urefu wa kilometa 1.32 pamoja na miundombinu wezeshi ya kuhudumia meli kubwa za kisasa ya aina ya *Megamax* ambazo haziwezi kuhudumiwa katika Bandari ya Dar es Salaam kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji awamu ya kwanza ya mradi huu, tayari miundombinu kwa ajili ya uchimbaji wa kina cha maji imepatikana na kazi hiyo inatarajiwa kuanza rasmi katika mwaka wa fedha ujao 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupunguza msongamano katika Bandari ya Dar es Salaam, Serikali imeendelea kuhimiza matumizi ya bandari kavu nchini ikiwemo bandari kavu ya Kwala iliyopo Mkoa wa Pwani ambayo imeendelea kutoa huduma, ambapo hadi kufikia mwezi Machi mwaka 2026 bandari hiyo ilihudumia makasha 14,460. Katika hatua nyingine mwezi Machi, mwaka 2026 *TRC* ilianza usafirishaji wa shehena kwenda katika Bandari Kavu ya Isaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea na uboreshaji wa bandari katika Maziwa Makuu nchini ambapo hadi kufikia mwezi Machi, mwaka 2026 uboreshaji wa Bandari za Bukoba na Kemondo umekamilika, na uboreshaji wa Bandari ya *Mwanza North* umefikia 75%. Serikali inaendelea na mradi wa uboreshaji wa Bandari ya Kigoma ambao umefikia 13% kwa upande wa Bandari ya *Mbamba Bay* umefikia 49%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikishwaji wa sekta binafsi katika shughuli za uendelezaji na uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam. Kama inavyokumbukwa mwaka 2023 Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilifanya uamuzi wa kimkakati wa kushirikisha sekta binafsi katika shughuli za uendelezaji na uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam kwa lengo la kuongeza ufanisi, ushindani na tija katika utoaji wa huduma za kibandari nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uamuzi huo, Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi iliingia mikataba na waendeshaji mahiri wa bandari wenye uzoefu mkubwa Kimataifa. Hatua hiyo imeendelea kuzaa matokeo chanya na manufaa makubwa kwa Taifa ikidhihirisha dira sahihi ya Serikali katika kuimarisha Uchumi wa Buluu na nafasi ya Tanzania kama lango kuu la biashara kwa ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Kuongezeka kwa shehena inayohudumiwa katika Bandari ya Dar es Salaam kutoka tani milioni 16.2 mwaka wa

fedha 2020/2021 hadi kufikia tani milioni 27.76 mwaka wa fedha 2024/2025, sawa na ongezeko la 70.62%.

(ii) Kuongezeka kwa wastani wa shehena ya makasha yanayohudumiwa kwa mwezi, kutoka makasha 61,000 hadi makasha 102,000 sawa na ongezeko la 67.21%.

(iii) Kupunguza kwa gharama za uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam kutoka shilingi bilioni 652.83 mwaka 2023/2024 hadi kufikia shilingi bilioni 308.95 mwaka 2025.

(iv) Kuongezeka kwa makusanyo ya mapato ya *TPA* yatokanayo na ada za huduma za kibandari kutoka shilingi bilioni 896.95 mwaka 2020/2021 hadi kufikia shilingi trilioni 1.3 mwaka 2024/2025.

(v) Kupungua kwa muda wa kuhudumia meli za makasha gatini kutoka wastani wa siku 10 hadi siku tatu; na;

(vi) Kupungua kwa muda wa meli kusubiri nangani kutoka wastani wa siku 46 hadi hadi wastani wa siku saba kwa meli za mizigo za mchanganyiko na za kichele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua za Serikali ya kukabiliana na ongezeko la shehena katika Bandari ya Dar es Salaam. Kutokana na kuongezeka kwa ufanisi wa Bandari ya Dar es Salaam pamoja na kuimarika kwa imani ya watumiaji wa bandari hiyo ndani na nje ya nchi, kumekuwepo na ongezeko kubwa la shehena ya mizigo inayohudumiwa bandarini. Ili kuhakikisha bandari hii inaendelea kutoa huduma kwa ufanisi, ushindani na viwango vinavyokidhi mahitaji na matamanio ya watumiaji wetu, Serikali inaendelea kutekeleza hatua mbalimbali za kimkakati kama ifuatavyo:-

(i) Kukamilisha ujenzi wa njia ya reli ya kisasa *SGR* inayoingia moja kwa moja bandarini *(port link)* ambapo utekelezaji wake umefikia 99.7% na majaribio ya usafirishaji wa mizigo kwa reli hiyo yameanza na yanaendelea kwa muda. Sambamba na hilo, *TRC* inaendelea kujenga eneo maalum,

*loading platform* ya kupakia mizigo kwenye treni ya *SGR* ndani ya eneo la bandari kwa lengo la kuongeza kasi na ufanisi katika utoaji wa mizigo bandarini.

(ii) Kuendelea na upanuzi wa eneo la Kurasini lenye ukubwa wa mita za mraba 220,000 kwa ajili ya kuhudumia makasha 700,000 kwa mwaka. Awamu ya kwanza ya mradi huu inatarajiwa kukamilika mwezi Juni mwaka 2026 na huduma ya makasha kwa huduma ya makasha 150,000 kwa mwaka, huku awamu ya pili ikitarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2027.

(iii) Kujenga kituo cha kisasa cha mizigo katika Stesheni ya *SGR* Morogoro chenye ukubwa wa mita za mraba 68,000 na uwezo wa kuhudumia makasha 600 kwa siku kwa ajili ya kuhudumia mizigo inayosafirishwa kwa njia ya barabara kuelekea mikoa mbalimbali na nchi za jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu huduma za bandari yameainishwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia aya ya 84 hadi 110. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za usafiri wa reli kupitia reli ya *MGR* na *SGR*, Wizara imeishukuru Serikali kwa kuchukua hatua za kuboresha Shirika la Reli Tanzania, zoezi lililoanza mwaka 2017. Tangu kuanzishwa kwa shirika hilo, Serikali imekuwa ikitoa ruzuku ya mishahara. Ninaomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika mwaka wa fedha 2026/2027 *TRC* haitatengewa tena ruzuku kwa ajili ya mishahara kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TRC* imeendelea na ujenzi na uendeshaji wa reli ya kisasa *SGR* pamoja na kuboresha mtandao wa reli ya *MGR* yenye urefu wa takribani kilometa 2,707. Ujenzi wa reli ya *SGR* unatekelezwa kwa awamu mbili, ikihusisha kilometa 1,219 za njia kuu kwa awamu ya kwanza kutoka Dar es Salaam – Mwanza na kilomita 1,590 za awamu ya pili ikihusisha vipande vya Tabora – Kigoma na Uvinza – Msongati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa awamu hizi mbili za treni ya *SGR* kutaifanya Tanzania kuwa na mtandao mkubwa wenye jumla ya kilometa 2,809 za reli ya *SGR*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji na uendeshaji wa reli ya kisasa ya *SGR*. Serikali kupitia *TRC* imeendelea na ujenzi wa reli ya *SGR* ambapo hadi kufikia mwezi Machi mwaka 2026 ujenzi wa kipande cha kwanza cha Dar es Salaam mpaka Morogoro na kipande cha pili Morogoro – Makutupora umekamilika kwa sehemu kubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, *TRC* inaendelea na utoaji wa huduma za usafiri wa treni kwa vipande husika. Kwa kipande cha Mwanza – Isaka ujenzi unaendelea na umefikia 68.77%. Hadi kufikia mwezi Machi mwaka 2026 ujenzi wa *SGR* katika kipande cha tatu Makutupora – Tabora na kipande cha nne cha Tabora – Isaka unaendelea ambapo kazi mbalimbali zinaendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, ujenzi wa vipande hivi umekuwa na changamoto kwa muda mrefu ambazo zilisababisha utekelezaji wake kuwa na kasi ndogo. Hata hivyo, Serikali imepata suluhisho la kukamilisha ujenzi wake kwa kupata mkopo wenye masharti nafuu wa thamani ya dola za Kimarekani bilioni 1.277 sawa na takribani shilingi trilioni 3.32.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafirishaji wa abiria na mizigo kwa reli ya *SGR* na *MGR*. Serikali kupitia *TRC* imeendelea na usafirishaji wa abiria kati ya Dar es Salaam na Dodoma kupitia reli ya *SGR*. Usafirishaji kupitia reli hiyo umezidi kuimarika ambapo katika kipindi cha Julai mwaka 2024/2025 hadi Machi mwaka 2026 jumla ya abiria milioni 2.51 walisafirishwa ikilinganishwa na abiria milioni 2.05 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2024/2025 sawa na ongezeko la 22.40%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi kufikia mwezi Machi, 2026, *TRC* ilisafirisha jumla ya tani 102,452 za mizigo ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Serikali ya kuanza usafirishaji wa mizigo kupitia reli ya *SGR*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua za kuunganisha miundombinu ya reli ya *SGR* na *MGR* Serikali imeendelea na uunganishaji wa reli hizo katika eneo la Ruvu ili kuwezesha usafirishaji wa mizigo kutoka Bandari za Dar es Salaam na Tanga, ambapo utekelezaji wake umefika 85%. Aidha, ujenzi wa kuunganisha reli ya *MGR* na *SGR* unaendelea katika eneo la Bahi kwa lengo la kuwezesha uhamishaji wa mizigo *(transshipment)* kati ya reli hizo mbili na unaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuboresha Reli ya *MGR* kwa kubadilisha reli nyepesi na kuweka reli nzito pamoja na kuongeza uwezo wa madaraja. Ukarabati huo unaendelea kupitia mfuko wa reli ambapo hadi kufikia mwezi Machi mwaka 2026 kipande cha Kaliua – Mpanda kilikuwa kimekamilika kwa 32.72%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukabiliana na mafuriko yanayoathiri reli ya *MGR* katika eneo la Kilosa – Kidete – Igandu, Serikali imekamilisha ujenzi wa njia ya reli yenye urefu wa kilometa 6.2 na daraja katika eneo la Godegode – Gulwe ambalo ujenzi wake umefikia 99%. Aidha, Serikali kupitia mradi wa *TIRP II* wa Wizara ya Uchukuzi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea na maandalizi ya ujenzi wa mabwawa sita katika Mto wa Kinyasungwe. Mabwawa hayo yatapunguza mafuriko na kuboresha uendeshaji wa reli mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Tanzania na Zambia zimeendelea kushirikiana katika kusafirisha mizigo na abiria kwa kutumia Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia *(TAZARA)*. Hata hivyo, kwa muda mrefu reli hii imekuwa na ufanisi mdogo kutokana na uchakavu wa miundombinu na uhaba wa vitendeakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika hotuba yake wakati wa kufungua rasmi Bunge la Kumi na Tatu, tarehe 14 Novemba mwaka 2025, aliliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali yake kwa kushirikiana na

nchi mwanahisa Zambia, imeanza mkakati mahsusi wa kufanya maboresho makubwa ya reli ya *TAZARA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, uzinduzi wa mradi wa kukufua reli ya *TAZARA* ulifanyika mwaka 2026 tarehe 20 Novemba, Jijini Lusaka huko Zambia. Uzinduzi huo ulifanyika kufuatia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Zambia mnamo tarehe 29 Septemba mwaka 2025 kusaini mkataba wa uendeshaji *(Concession Agreement)* na Kampuni ya *CCECC* kutoka China kwa ajili ya kuboresha reli ya *TAZARA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni hii itawekeza jumla ya Dola za Marekani bilioni 1.4, ambayo ni sawa na takribani shilingi trilioni 3.6. Maboresho ya reli hii ya *TAZARA* yanatarajiwa kuongeza uwezo wa kusafirisha mizigo 2,400,000 kwa mwaka na kuzalisha ajira takribani 100,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu huduma za usafiri wa reli na utekelezaji wa miradi ya miundombinu ya reli kupitia *TRC* na *TAZARA* yameoneshwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia aya ya 111 hadi 145.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za uchukuzi katika bahari na maziwa makuu. Huduma za usafiri na usafirishaji katika maziwa makuu. Serikali kupitia *(TASHICO)* imeendelea kusimamia ujenzi wa meli mpya na ukabarati wa meli zilizopo ili kuimarisha usafiri wa abiria na usafirishaji wa mizigo. Kwa kipindi cha Julai mwaka 2025 hadi Machi mwaka 2026 *(TASHICO)* ilisafirisha abiria 128,191 na tani za mzigo 71,796.25 ikiwa ni sawa na ongezeko la 22.51% ikilinganishwa na kipindi kama hicho cha mwaka uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha ujenzi wa meli ya *MV New* Mwanza katika Ziwa Victoria. Serikali pia inaendelea na ukarabati wa meli katika Ziwa Victoria ambapo ukarabati wa Meli ya Uokozi ya MT. Ukerewe imefikia 79%. Vilevile Serikali kupitia *(TASHICO)* imeanza maandalizi ya ujenzi wa meli yenye uwezo wa kubeba tani 3,000 za mizigo katika ziwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa kutumia fursa zilizopo ukanda wa Ziwa Tanganyika. Kutokana na umuhimu wa ukanda wa Ziwa Tanganyika, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo, kwanza ujenzi wa meli nne za mizigo katika Ziwa Tanganyika zilizojengwa na *TPA* kwa kushirikiana na sekta binafsi ambazo kila meli ina uwezo wa kubeba tani 2,000 za mizigo na kwa sasa meli hizi zimekamilika; kuanza ujenzi wa meli mpya ya abiria; kuanza ujenzi wa karakani ya ujenzi wa meli; kuanza ujenzi wa magati mawili ya kisasa katika Bandari ya Kigoma ambapo hadi kufikia mwezi Machi mwaka 2026 utekelezaji wake umefikia 13%; na kuendelea na ukarabati wa meli ya *MV* Liemba ambapo ukarabati wake umefikia 64%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu huduma za uchukuzi katika Bahari na Maziwa Makuu kupitia *(TASHICO)* yameoneshwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 146 hadi 156.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za viwanja vya ndege. Katika uendelezaji na uendeshaji wa miundombinu ya viwanja vya ndege, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania *(TAA)* imeendelea kusimamia na kuendeleza viwanja vya ndege vya Serikali. Katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025, Serikali imeahidi kukipandisha hadhi Kiwanja cha Ndege cha Mwanza kuwa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na *TAA*, tayari imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mradi wa ujenzi wa jengo jipya la abiria litakalokuwa na uwezo wa kuhudumia abiria milioni 2.5 kwa wakati mmoja, pamoja na miundombinu wezeshi. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kufanyika kwa ushirikiano kati ya *TAA* na Mfuko wa Hifadhi wa Jamii *(NSSF)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Machi mwaka 2026, Wizara kupitia *TAA* imeendelea na uboreshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Arusha, ambapo ufungaji wa mfumo wa taa za

kuongozea ndege umefikia 65% na ujenzi wa tabaka la juu la lami la barabara ya kurukia na kutua ndege katika kiwanja hicho inaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza viwanja vya ndege vya mikoa, Wizara kupitia *TAA* imeendelea na uboreshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Musoma na Kiwanja cha Ndege cha Moshi. Pia, kwa upande wa mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mkoa wa Kagera, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TAA* imeendelea na utekelezaji wa maboresho ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro ikiwemo ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, ufungaji wa mfumo wa taa za kuongozea ndege, na ujenzi wa eneo la kuhifadhia mizigo mikavu, ambapo ujenzi wake umefikia asilimia tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, wakandarasi wa ujenzi wa jengo jipya la watu mashuhuri *(New VIP Terminal)* wamepatikana na maandalizi ya ujenzi yanaendelea. Maendeleo ya kina kuhusu huduma za viwanja vya ndege kupitia *TAA* yameonyeshwa katika kitabu cha hotuba yangu ya bajeti kuanzia aya ya 157 hadi 167.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa huduma za usafiri wa anga, tangu mwaka 2025 Serikali imeendelea kuifufua Kampuni ya Ndege ya Tanzania *(ATCL)*, ambapo idadi ya ndege imeongezeka kutoka ndege moja mwaka 2016 hadi ndege 16 mwaka 2026. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na ongezeko la abiria kutoka 107,016 mwaka 2016/2017 hadi abiria 1,178,025 mwaka 2024/2025; mapato kuongezeka kutoka shilingi bilioni 23 hadi kufikia shilingi biioni 595.7, pamoja na mapato ya fedha za kigeni kupanda kutoka Dola za Kimarekani milioni 9.85 hadi kufikia Dola za Kimarekani milioni 157.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai mwaka 2025 hadi Machi mwaka 2026, *ATCL* ilisafirisha abiria milioni 1.07, sawa na ongezeko la 22.38%, ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka uliopita, huku tani 4,129.72 za mizigo zilisafirishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya mafanikio hayo, kampuni bado inakabiliwa na changamoto ya mtaji mdogo na mfumo wa umiliki wa ndege unaoathiri mizania ya kifedha. Serikali ipo katika hatua za mwisho za kuboresha mfumo huu ili kuimarisha ufanisi na mizania ya kihesabu ya Shirika la Ndege la *Air Tanzania*. Maelezo ya kina kuhusu huduma za usafiri wa anga kupitia *ATCL* yameoneshwa katika kitabu cha hotuba yangu ya bajeti kuanzia aya ya 168 hadi 150.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu vyuo vya mafunzo vya sekta na masuala mtambuka. Wizara ya uchukuzi inasimamia uendeshaji wa vyuo vya mafunzo vya kisekta vilivyo chini yake ili kuhakikisha sekta ya usafirishaji na usafiri nchini inakuwa na wataalamu wa ndani wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji na Chuo cha Baharia Dar es Salaam *(DMI)*. Katika kuendelea kukijengea uwezo Chuo cha Taifa cha Usafirishaji na *DMI,* Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya kuboresha miundombinu na vifaa vya kufundishia. Hii imeongeza udahili wa kozi mbalimbali kwa kiasi kikubwa kama inavyoonyeshwa kwenye kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia aya ya 181 hadi 205.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio, changamoto na hatua zilizochukuliwa. Ninaomba niainishe kwa muhtasari mafanikio makubwa yaliyopatikana katika mwaka wa fedha 2025/2026 hadi kufikia mwezi Machi mwaka 2026 kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kuendelea na ujenzi wa Reli ya *SGR* kwa awamu zote mbili. Serikali imeendelea na ujenzi wa Reli ya *SGR* kwa awamu zote mbili, na utekelezaji wake uko katika hatua mbalimbali kama ilivyoainishwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuendelea kwa ufanisi wa usafirishaji wa abiria kupitia Reli ya *SGR*. Sote ni mashuhuda kuwa, usafirishaji wa abiria na mizigo kupitia Reli ya *SGR* umeendelea kuimarika kati ya Dar es Salaam na Dodoma, ambapo takribani wastani wa abiria 280,000 husafirishwa kwa mwezi, sawa na abiria

9,300 kwa siku. Kwa mwenendo huu, inakadiriwa kuwa, zaidi ya abiria milioni tatu watakuwa wamesafirishwa kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2025/2026, ikilinganishwa na wastani wa abiria 400,000 wanaosafirishwa kwa Reli ya *MGR* kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uendeshaji huo, katika kipindi cha kuanzia Julai mwaka 2025 hadi Machi mwaka 2026, jumla ya shilingi bilioni 82.77 zimekusanywa. Aidha, takwimu hizo zinaifanya Serikali kuwa imekusanya jumla ya shilingi bilioni 169.37 tangu kuanza safari za *SGR* hapa nchini kuanzia mwezi Juni mwaka 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kuanza kwa usafirishaji wa mizigo kwa reli ya *SGR*. Katika hotuba yangu ya mwaka 2025/2026 niliahidi kuanza huduma za usafirishaji wa mizigo kupitia Reli ya *SGR*. Ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, mwezi Juni mwaka 2025 *TRC* ilianza rasmi usafirishaji wa mizigo kupitia reli ya *SGR* kati ya Dar es Salaam na Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, *TRC* kuanza kujiendesha bila ruzuku kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali. Ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kuanzia Januari kwaka 2026 *TRC* imefanikiwa kuanza kujitegemea kwa upande wa mishahara na matumizi mengineyo bila uwezeshaji kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa kipindi cha takribani miaka 10, kiasi cha shilingi bilioni 12.92 kila mwaka kilikuwa kinatolewa na Serikali kwa *TRC* kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, kuongeza uwezo wa Bandari ya Dar es Salaam kuhusu shehena. Ili kuendelea kuiongezea uwezo Bandari ya Dar es Salaam katika kuhudumia shehena, Serikali imeendelea na upanuzi wa eneo la Kurasini *(Kurasini Port Extension)*, lenye ukubwa wa meta za mraba 220,000 kwa ajili ya kuhudumia makasha 700,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, ufanisi wa ushiriki wa sekta binafsi katika Bandari ya Dar es Salaam na kuongezeka kwa shehena kwa bandari zote nchini. Kutokana na kuendelea kwa utaratibu wa kushirikisha sekta binafsi katika uendeshaji wa

bandari hapa nchini, hususan Bandari ya Dar es Salaam kwa kipindi cha kuanzia Julai mwaka 2025 hadi Machi mwaka 2026, shehena iliyohudumiwa katika Bandari ya Dar es Salaam ilifikia tani milioni 27.83, ikilinganishwa na tani milioni 19.31 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2024/2025, sawa na ongezeko la 29.83%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, inatarajiwa kuwa, shehena ya mizigo itakayohudumiwa na bandari hii itaongezeka hadi kufikia wastani wa tani milioni 40.839, na kwa bandari zote nchini shehena ya mizigo inategemewa kufikia tani milioni 59.768 kwa mwaka 2030/2031.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba, kuimarisha usafiri katika Maziwa Makuu. Serikali imekamilisha ujenzi wa Meli ya *MV New Mwanza* katika *Ziwa Victoria*. Aidha, ukarabati wa meli ya *MT Sangara* umekamilika na sasa imeanza kutoa huduma. Vilevile, Serikali kupitia *TPA* kwa kushirikiana na sekta binafsi imekamilisha ujenzi wa meli nne za mizigo katika Ziwa Tanganyika zenye uwezo wa kusafirisha tani 8,000 za mizigo kwa meli zote nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nane, kuongezeka kwa mtandao wa vituo vya safari za anga vinavyohudumiwa na *ATCL*. Kutokana na juhudi za Serikali katika kuimarisha utendaji, Kampuni ya *ATCL* imeongeza vituo vya huduma vya usafiri wa anga, ambapo hadi kufikia mwezi Machi mwaka 2026 ina vituo 32 ikilinganishwa na vituo 23 vilivyokuwepo mwaka 2020/2021. Kati ya vituo hivyo, vituo 16 ni vya ndani ya nchi, vituo 14 ni vya kikanda, na vituo vitatu ni vya nje ya Bara la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tisa, kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato yanayotokana na huduma za usafiri wa anga kupitia *ATCL*. Kampuni ya *ATCL* kwa mwaka 2024/2025 ilikusanya mapato ya shilingi bilioni 626.5, ikilinganishwa na shilingi bilioni 175.69 zilizokusanywa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumi, kuimarika kwa huduma ya viwanja vya ndege. Katika kuimarisha huduma za usafiri wa anga nchini, Serikali imekamilisha ukarabati wa Viwanja vya Ndege vya

Sumbawanga, Songea, Shinyanga, na Tabora. Aidha, ukarabati mkubwa wa jengo la kuhifadhia mizigo inayoharibika haraka katika Kiwanja cha Ndege cha *KIA* umekamilika, na hivyo kuchochea kuimarika kwa mnyororo wa usafirishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumi na moja, kuanza kutolewa kwa mafunzo ya urubani nchini. Kama nilivyoahidi katika hotuba yangu ya mwaka 2025/2026 kuwa Serikali itaanza rasmi kutoa mafunzo ya urubani katika Chuo cha Taifa cha Usafirishaji. Ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali kupitia Chuo cha *NIT* imeanza rasmi kutoa mafunzo ya urubani mwezi Julai mwaka 2026, ambapo wanafunzi 22 wamedahiliwa na wanaendelea na masomo yao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio hayo yamewezesha kupunguza gharama za masomo nje ya nchi kwa kozi ya urubani. Kuanza kutolewa kwa mafunzo hayo ni utekelezaji wa maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuimarisha usafiri wa anga. Maelezo ya kina kuhusu mafaniko yaliyopatikana hadi kufikia mwezi Machi mwaka 2026 yanaonyeshwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia aya ya 223 hadi 252.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto na hatua zilizochukuliwa. Wizara ya Uchukuzi imekabiliwa au ilikabiliwa na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Changamoto hizo na mikakati ya kuzitatua zimeonyeshwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia aya ya 253 hadi 254.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027; katika Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara imezingatia Dira 2050, Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2025, Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano, Mpango wa Taifa wa Mwaka 2026/2027, Mpango Mkakati wa Wizara ya Uchukuzi wa Miaka Mitano, pamoja na maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Wizara ina vipaumbele mbalimbali kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kuendelea na ujenzi na uendeshaji wa reli ya kisasa ya *SGR*; pili, kuendelea na ukarabati na uboreshaji wa reli ya *MGR* na *TAZARA*; tatu, uboreshaji wa miundombinu na huduma katika bandari; nne, kuendelea na uboreshaji wa usafiri wa anga; tano, kuendelea na ujenzi na ukarabati wa meli; sita, kuendelea kuboresha huduma za hali ya hewa; saba, kuboresha udhibiti ubora na usalama wa huduma za uchukuzi; na nane, kuendelea na uboreshaji wa vyuo vya mafunzo hapa nchini vya sekta ya uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara ya Uchukuzi Fungu 62 imetengewa jumla ya shilingi trilioni 2.872, ambapo kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 126.04 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, sawa na asilimia nne nukta tatu nane ya bajeti, na shilingi trilioni 2.746 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, sawa na 95.62%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, shilingi bilioni 1.135 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi, na shilingi bilioni 25.906 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)* kwa Wizara na taasisi zinazopokea ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, shilingi trilioni 2.452 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 294.18 ni fedha za nje. Vipaumbele na bajeti iliyotengwa katika mwaka wa fedha 2026/2027 vimeainishwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia aya 255 hadi 259.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya maendeleo itakayotekelezwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027, miradi ya kielelezo na kimkakati itakayotekelezwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni eneo la miradi ya uboreshaji wa miundombinu ya bandari na huduma za usafiri majini. Miradi itakayotekelezwa katika eneo hili ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni Mradi wa Uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam. Miradi mingine itakayotekelezwa ya uboreshaji wa bandari itatekelezwa kupitia mapato ya ndani ya *TPA*, ikiwemo uboreshaji wa Bandari za Mwambao wa Bahari ya Hindi ambazo ni Bandari ya Bagamoyo, Bandari ya Mtwara (Kisiwa Mgao), na Bandari ya Maziwa Makuu ambapo ni Bandari ya *Mwanza North*, Bandari ya *Mbamba Bay*, na mradi wa uboreshaji wa Bandari ya Kigoma, na mradi wa ujenzi na ukarabati wa meli katika Maziwa Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Bandari ya Dar es Salaam kupitia sekta binafsi, *DP World* itaendelea na mpango mkubwa wa utekelezaji katika vifaa vya kisasa vya kuhudumia mizigo, lengo ikiwa ni kuongeza ufanisi, kasi, na ushindani wa huduma za bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufikia mwaka 2025/2026 kampuni tayari imevuka zaidi ya nusu ya lengo la uwekezaji za Dola za Kimarekani milioni 250, sawa na shilingi bilioni 650 ndani ya miaka mitano, ikiwa ni mafanikio makubwa ndani ya miaka miwili ya kwanza ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2027, maboresho yataendelea kupitia upanuzi wa miundombinu, uboreshaji wa mifumo ya utendaji, na kuimarisha uwezo wa huduma za mizigo kwa viwango vya kisasa. Miongoni mwa mipango hiyo ni upanuzi wa mitambo ya kisasa ya upakiajia na upakuaji *(cranes)*, ujenzi wa mageti mawili yanayounganisha bandari na Barabara ya Nelson Mandela, pamoja na uwekezaji katika mitambo ya kushushia shehena za kichele *(dry bulk)* utakaoongeza uwezo kwa 65% hadi kufikia takribani tani milioni 5.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, uwezo wa kuhudumia mizigo mchanganyiko, utaongezeka kwa 25%, huku sekta ya usafirishaji wa magari ikitarajiwa kukua kwa 30% kutokana na maboresho ya sera na miundombinu. Hatua hizi pia zitaongeza ufanisi wa Bandari ya Tanga na Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla ifikamo mwaka 2028 sekta ya bandari inatarajiwa kuwa imepiga hatua kubwa ya mageuzi ikiwa na uwezo wa juu zaidi wa kuhudumia mizigo, kasi ya huduma na ushindani wa Kimataifa. Hivyo, kuifanya Tanzania kuwa kitovu muhimu cha biashara katika ukanda mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya kuboresha usafiri wa anga na hali ya hewa. Miradi hiyo ni pamoja na ununuzi wa ndege na uimarishaji wa Kampuni ya Ndege ya *ATCL*, ujenzi wa Chuo cha Usafirishaji, ujenzi, ukarabati na uboreshaji wa viwanja vya ndege vya Mwanza, Arusha, Mtwara, Serengeti, Kagera, Kilimanjaro, na Julius Nyerere, pamoja na viwanja vya ndege vya mikoa ambavyo ni Kiwanja cha Moshi, Lindi, Njombe, Musoma, na Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa miradi ya uendelezaji wa miundombinu ya reli, miradi itakayotekelezwa kwenye eneo hili ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni ujenzi wa Reli ya *SGR* na ukarabati na uboreshaji wa *reli* za *MGR* na reli ya *TAZARA;* pili, ujenzi wa reli ya treni ya mjini katika Jiji la Dar es Salaam, ambapo upembuzi yakinifu utafanyika mwaka 2026/2027; na mwisho ujenzi wa Kituo cha Kisasa cha Mafunzo ya Reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya uboreshaji wa vyuo vya mafunzo vya kisekta, miradi itakayotekelezwa katika eneo hili ni pamoja na ujenzi wa miundombinu na ununuzi wa vifaa vya kufundishia katika Chuo cha Taifa cha Usafirishaji. Pili, mradi wa uanzishwaji wa *Campus* ya Lindi katika sekta ya usafiri majini, mafuta, na gesi, na mradi wa *East Africa Skills for Transformation and Regional Integration*. Maelezo ya kina kuhusu miradi itakayotekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 na

fedha zilizotengwa kwa kila mradi yameainishwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti, kuanzia aya 260 hadi 286.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli nyingine zitakazotekelezwa na Wizara katika mwaka wa fedha 2026/2027, kupitia mapato ya ndani ya taasisi zilizo chini ya Wizara katika udhibiti utoaji wa huduma za uchukuzi na masuala ya kisekta na mtambuka, zimeainishwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia aya 287 hadi 314.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani. Utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026 umeleta mafanikio makubwa. Mafaniko ambayo Wizara imeyapata yasingeliwezekana kutokea bila ya ushauri na usimamizi wa Bunge lako Tukufu. Kutokana na mafanikio hayo, ninaomba nitoe shukrani kwako wewe, kwa Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa ushauri na michango yao ambayo imewezesha Wizara kufikia mafanikio haya makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninawashukuru wananchi na wadau wengine kwa kuendelea kutoa michango ya hali na mali katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, pamoja na kuendelea kushirikiana na Serikali katika kulinda miundombinu ya usafiri na usafirishaji, ambayo Serikali imewekeza kiasi kikubwa cha fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuwapongeza na kutambua michango iliyotolewa na viongozi wanaonisaidia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa kuanzia na Naibu Waziri, Mheshimiwa David Kihenzile, na Katibu Mkuu, Profesa Kahyarara. Vilevile niishukuru Menejimenti ya Wizara, Wakuu wa Taasisi za Wizara, pamoja na watumishi wote wa Wizara na Taasisi kwa juhudi zao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, nizishukuru taasisi na Mashirika ya Kitaifa na ya Kimataifa ambayo yameshirikiana na Wizara katika uendelezaji wa Sekta ya Uchukuzi

hapa nchini. Ninaomba kutaja baadhi ya mashirikika ya Kitaifa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya *NSSF* na *PSSSF*; Taasisi za Kifedha za *CRDB, NMB, AZANIA BANK, NBC* na *TCB;* na asasi mbalimbali za kiraia. Aidha, mashirika ya Kimataifa na wadau wa maendeleo wanaoendelea kushirikiana na Wizara ambao ni pamoja na *TradeMark Africa*, Shirika la Bahari Duniani, Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga, Shirika la Hali ya Hewa Duniani, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Dunia, Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japani *(JICA)*, na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Korea Kusini *(KOICA)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni *Foreign Commonwealth and Development Office*, Shirika la Maendeleo la Ufaransa, Shirika la Nchi zinazouza Mafuta ya Petroli Nje ya Nchi zao *(OPEC)*, Jumuiya ya Umoja wa Ulaya, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya, Shirika la Chakula Duniani, na Shirika la Biashara na Maendeleo la Marekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia inashukuru ushirikiano kutoka nchi za kikanda kupitia Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)*. Vilevile, kutoka Nchi za Urusi, Umoja wa Falme za Kiarabu, Uingereza, China, Sweden, Denmark, Korea Kusini, Jamhuri ya Czech na Uturuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho siyo kwa umuhimu, ninaishukuru Sekta Binafsi, hususan wafanyabiashara na watoa huduma wote wa Sekta ya Uchukuzi kwa kuendelea kutoa huduma bora za uchukuzi hapa nchini. Maelezo ya kina ya shukurani yameainishwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia aya ya 315 hadi 319.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhtasari wa maombi ya fedha ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka Wa Fedha 2026/2027. Katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Uchukuzi inaliomba Bunge lako Tukufu kuidhinisha bajeti ya jumla ya shilingi 2,872,738,082,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 126,041,236,000 ni kwa ajili ya Matumizi

ya Kawaida na shilingi 2,746,696,846,000 ni fedha za Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba hii, nimeambatisha majedwali mbalimbali yenye taarifa na takwimu kwa ajili ya kutoa uelewa zaidi kwa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kuhusu Sekta ya Uchukuzi. Ninaomba majedwali hayo ambayo yameainishwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 198 hadi ukurasa wa 247 yachukuliwe kama sehemu ya hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ambayo ni *www.uchukuzi.go.tz*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa, ninaomba kutoa hoja.

**HOTUBA YA WAZIRI WA UCHUKUZI MHESHIMIWA PROF. MAKAME MNYAA MBARAWA (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**A. UTANGULIZI**

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, ambayo imechambua utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2025/26 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/27, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kuidhinisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2026/27.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na kutuwezesha kukutana tena siku ya leo kujadili maendeleo ya Sekta ya Uchukuzi, hususan katika shughuli zinazosimamiwa na Wizara ya

Uchukuzi. Wizara hii imeendelea kutekeleza majukumu yake kulingana na Hati Idhini za Mgawanyo wa Majukumu ya Serikali kupitia Tangazo la Serikali Na. 685 la tarehe 19 Desemba, 2025. Ninamuomba Mwenyezi Mungu atuongoze vyema katika kujadili Hotuba hii ya Wizara ya Uchukuzi na Bajeti ya Serikali kwa ujumla ili kufikia malengo ya Dira 2050 katika kuwaletea Watanzania maendeleo.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee naomba kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushindi alioupata katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 29 Oktoba, 2025. Ushindi huu unaonesha imani kubwa ambayo Watanzania wameendelea kuwa nayo kwa Uongozi wake wenye maono na unaowaletea wananchi maendeleo. Aidha, napenda kumpongeza kwa dhati kwa hatua madhubuti alizochukua katika kutekeleza ahadi alizotoa kwa wananchi ndani ya siku 100 za mwanzo katika kipindi chake cha awamu ya pili. Utekelezaji huo umeonesha dhamira ya kweli ya kuhakikisha kuwa Serikali inatekeleza ahadi zilizotolewa na kuleta matokeo chanya katika sekta mbalimbali nchini.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa ahadi hizo umeimarisha imani ya wananchi kwa Serikali yao na umeweka msingi imara wa kuendelea kuijenga Tanzania yenye ustawi, umoja, amani na maendeleo kwa wote. Tunamtakia Mheshimiwa Rais afya njema, umri mrefu, hekima na mafanikio zaidi katika kuiongoza nchi yetu ili kufikia malengo ya maendeleo ya Taifa letu.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutumia fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mchango wake mkubwa wa kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu ya Serikali. Mheshimiwa Makamu wa Rais ameendelea kutoa ushirikiano mkubwa katika juhudi na mikakati ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kufikia malengo ya kuwatumikia Watanzania. Aidha, ameendelea kusimamia kikamilifu Masuala ya Muungano na Mazingira.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** nimpongeze pia Mheshimiwa. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na kuthibitishwa kwa kishindo na Bunge hili Tukufu kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wote ni mashahidi kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu ameonesha umahiri mkubwa katika kusimamia shughuli za Serikali kwa ajili ya kuliwezesha Taifa letu kusonga mbele pamoja na kuimarisha utendaji wa Serikali kwa ujumla.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwa kishindo na Waheshimiwa Wabunge kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Uzoefu na umahiri wako uliouonesha katika nafasi ya Naibu Spika katika Bunge lililopita umewezesha Waheshimiwa Wabunge kukuchagua na kukupa jukumu la kusimamia Bunge hili ambalo limeendelea kuishauri na kuisimamia Serikali katika kutekeleza majukumu yake. Nimpongeze pia Mheshimiwa Daniel Barran Sillo (Mb.), kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge hili Tukufu. Aidha, nitumie fursa hii kuwapongeza Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb.) na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika (Mb.) kwa kuendelea kuaminiwa kuwa Wenyeviti wa Bunge. Kwa namna ya kipekee nimpongeze Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso (Mb.) kwa kuchaguliwa pia kuwa Mwenyekiti wa Bunge.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** naishukuru na kuipongeza sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu inayoongozwa na Mwenyekiti Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso (Mb.) ambaye amechaguliwa kwa mara nyingine tena kuiongoza Kamati hiyo. Aidha, nimpongeze Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga (Mb.) kwa kuchaguliwa katika nafasi hiyo. Sambamba na viongozi hao wa Kamati, niwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Kamati hii imeendelea kutoa ushauri na kuisimamia Wizara katika utekelezaji wa shughuli na miradi ya maendeleo. Ushauri unaotolewa na Kamati hii umeendelea kuwa na tija katika utendaji wa Wizara na kuimarisha huduma za usafiri na usafirishaji nchini. Napenda pia kuishukuru Kamati hii kwa uchambuzi iliyoufanya kwenye Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti

kwa mwaka wa fedha 2025/26 na Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa fedha 2026/27. Maoni na ushauri wa Kamati uliotolewa umeiwezesha Wizara kukamilisha kwa ufanisi maandalizi ya Mpango wa makadirio ya mapato na matumizi tunaouwasilisha siku ya leo mbele ya Bunge lako Tukufu.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, namshukuru kwa dhati Mheshimiwa. Rais, kwa kuendelea kuniamini na kuniteua katika nafasi hii kwa mara nyingine ya kuongoza Wizara ya Uchukuzi. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais kuwa, kwa kushirikiana na Naibu Waziri Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile (Mb.), nitatekeleza majukumu aliyotukabidhi kwa kufuata miongozo anayotupatia pamoja na miongozo mingine ya nchi yetu. Pia, tutaendelea kutekeleza shughuli za Wizara ili kuweza kufikia malengo mahsusi ya kuendeleza Sekta ya Uchukuzi na kuwa na mchango mkubwa katika kuchochea ukuaji wa Uchumi wa Taifa kwa manufaa mapana ya Watanzania. Vilevile, niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri walioaminiwa na kuteuliwa ili kuongoza Wizara mbalimbali.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie siku ya leo kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa na waliochaguliwa kuwawakilisha wananchi katika Bunge hili Tukufu la 13. Ni wazi kuwa, Watanzania wametuamini na kututuma ili tuwatumikie katika kutatua kero zao na kushirikiana kwa karibu katika kutafuta suluhu ya changamoto zinazowakabili. Niwahakikishie kuwa, Wizara yangu iko tayari kupokea ushauri na maoni ya Watanzania kupitia kwenu ili kuendelea kutatua kero na changamoto zilizopo.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa masikitiko makubwa nitoe pole kwa Bunge lako Tukufu, familia na Watanzania wote kufuatia kifo cha aliyekuwa Spika Mstaafu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hayati **Job Yustino Ndugai** kilichotokea tarehe 06 Agosti 2025, hakika alitoa mchango mkubwa katika kulitumikia Bunge na Taifa kwa ujumla. Aidha, nitoe pole kwa Bunge lako Tukufu kufuatia vifo vya Waheshimiwa Wabunge: **Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho kilichotokea tarehe 11 Desemba, 2025; **Mheshimiwa Halima Iddi Nassor** aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum

kilichotokea tarehe 18 Januari, 2026; na **Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Isimani na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu kilichotokea tarehe 25 Machi, 2026. Hakika tutaendelea kuthamini na kuenzi michango yao katika Bunge hili na Taifa kwa ujumla. Tunamwomba Mwenyezi Mungu awapumzishe mahali pema peponi, Amina.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** kabla ya kuendelea na uwasilishaji wangu, niwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji kwa hotuba zao ambazo zimefafanua utendaji wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/26 na mwelekeo kwa mwaka wa fedha 2026/27. Vilevile, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote waliowasilisha hotuba zao kabla yangu.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya utangulizi huo, naomba sasa uniruhusu niwasilishe Taarifa ya Mapitio ya Mchango wa Sekta ya Uchukuzi katika kukuza uchumi wa Taifa; Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2025/26 hadi kufikia Machi, 2026; na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/27. Aidha, nitahitimisha kwa kuomba Bunge lako Tukufu liidhinishe bajeti kwa ajili ya kutekeleza shughuli na miradi ya Wizara ya Uchukuzi (Fungu 62) kwa mwaka wa fedha 2026/27.

## B. MCHANGO WA SEKTA YA UCHUKUZI KATIKA KUKUZA UCHUMI WA TAIFA

14. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Uchukuzi imeendelea kutoa mchango mkubwa katika kuchochea shughuli za uzalishaji na utoaji huduma, na hatimaye kukuza ukuaji wa uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Mchango huo umewezesha kuendelea kukua kwa sekta nyingine za uzalishaji zikiwemo sekta za Kilimo, Uvuvi, Madini, Utalii, Viwanda na Biashara. Kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2024 iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Sekta

ya Uchukuzi ilikua kwa asilimia 4.2 na kuchangia katika Pato la Taifa kwa asilimia 7.5, ambapo imekuwa ya tano (5) kati ya sekta kubwa 17 katika kuchangia Pato la Taifa na hivyo kuendelea kutoa mchango stahiki katika ukuaji wa uchumi.

15. ***Mheshimiwa Spika,*** mchango huo wa Sekta ya Uchukuzi umetokana na hatua mbalimbali zilizochukuliwa katika uendelezaji na uboreshaji wa miradi mikubwa ya kielelezo na kimkakati katika sekta ndogo za reli, anga, bandari, viwanja vya ndege, huduma za hali ya hewa pamoja na maboresho ya miongozo mbalimbali ya kisera na kisheria. Miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na: maboresho yaliyofanyika katika Bandari za Dar es Salaam, Tanga, Mtwara pamoja na bandari za Maziwa Makuu; ujenzi na uboreshaji wa viwanja vya ndege nchini; kuendelea kwa uendeshaji wa huduma za reli ikiwemo reli ya SGR; kushirikisha Sekta Binafsi katika uendelezaji na uendeshaji wa shughuli za Sekta ya Uchukuzi; ujenzi na ukarabati wa meli; ununuzi wa ndege; kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA; kuendelea kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa; na kuendelea kuimarisha udhibiti wa huduma mbalimbali za uchukuzi.

16. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia huduma za bandari, Sekta ya Uchukuzi **imeendelea kuchangia zaidi katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali**. Mathalan, kati ya mwaka wa fedha 2020/21 hadi mwaka wa fedha 2024/25 takwimu zinadhihirisha kuwa, mapato yatokanayo na kodi ya forodha za kibandari yanachangia wastani wa asilimia 40 ya mapato yote yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Aidha, mapato hayo yataendelea kuongezeka kadri miradi ya kimkakati ya kibandari inavyoendelea kukamilishwa.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa Taarifa ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ya mwaka 2025, Sekta ya Uchukuzi ilikuwa **miongoni mwa sekta tatu (3) kati ya sekta kubwa 17 zinazochangia zaidi katika upatikanaji wa fedha za kigeni nchini**. Fedha za kigeni zitokanazo na Sekta hii ni kutokana na mauzo ya huduma za uchukuzi (transport services) zinazojumuisha usafirishaji wa mizigo inayopitia bandari za Tanzania kwenda au kutoka nchi jirani za kikanda ikijumuisha nchi za: Jamhuri ya Kidemokrasia ya

Congo, Zambia, Rwanda, Burundi na Uganda pamoja na usafiri na usafirishaji kwa njia ya anga na huduma zinazotolewa na viwanja vya ndege.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Uchukuzi kwa mwaka 2025 ilichangia mauzo ya kiasi cha Dola za Marekani bilioni 2.79 ya fedha za kigeni sawa na ongezeko la asilimia 18.72 ikilinganishwa na Dola za Marekani bilioni 2.35 zilizopatikana katika mauzo ya huduma za uchukuzi kwa mwaka 2024. Kwa ujumla, mauzo yote nje ya nchi kwa mwaka 2025 ni Dola za Marekani bilioni 17.59, ambapo Sekta ya Uchukuzi ilichangia asilimia 15.86 ya mauzo hayo, ikillinganishwa na Dola za Marekani bilioni 15.97 zilizopatikana mwaka 2024, ambapo Sekta ya Uchukuzi ilichangia asilimia 14.72.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukuza upatikanaji wa ajira nchini, Sekta ya Uchukuzi imeendelea kutoa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja wakati wa ujenzi wa miundombinu ya uchukuzi pamoja na utoaji wa huduma za uchukuzi. Mathalan, Mradi wa Ujenzi wa Reli ya SGR hadi sasa umetoa fursa za ajira kwa Watanzania wapatao 181,056, ambapo ajira 30,176 ni za moja kwa moja na ajira 150,880 ni zisizo za moja kwa moja. Ajira nyingine zilizozalishwa na kuajiri Watanzania walio wengi ni pamoja na: ujenzi wa viwanja vya ndege, ajira 11,680; huduma za usafiri wa anga, ajira 3,983; uendelezaji wa miundombinu ya bandari, ajira 1,761; ufungaji wa mitambo na vifaa vya hali ya hewa, ajira 73; na vyuo vya mafunzo vya kisekta vya NIT na DMI, ajira 152.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na manufaa hayo, Sekta ya Uchukuzi kwa ujumla imeendelea kuwezesha kufanyika kwa biashara kikanda na kimataifa na kuwa kiunganishi muhimu kati ya nchi yetu na nchi jirani. Nchi hizo ni pamoja na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Zambia, Rwanda, Burundi, Malawi na Uganda. Hatua hii imeendelea kuijengea Tanzania sifa kimataifa na kuiwezesha kuimarisha diplomasia ya kiuchumi kati ya Tanzania na nchi hizo. Aidha, Sekta ya Uchukuzi imekuwa ni kiungo mahsusi katika ufanyaji wa biashara za ndani kwa kusafirisha bidhaa na huduma zinazouzwa ndani ya nchi yetu.

Mathalan, asilimia 90 ya bidhaa zote zinazoingia nchini zinapitia njia ya usafiri majini.

## C. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26

21. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara ya Uchukuzi (Fungu 62) iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,746,485,018,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 125,438,950,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, sawa na asilimia **4.57** na **Shilingi 2,621,046,068,000** ni fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo, sawa na asilimia **95.43**. Hadi kufikia **Machi, 2026** jumla ya **Shilingi 1,374,938,960,635.04** zilikuwa zimetolewa ikiwa ni sawa na asilimia **66.75** ya **Shilingi 2,059,863,763,500.00** zilizotakiwa kupokelewa katika kipindi hicho. Kati ya fedha hizo zilizotolewa, **Shilingi 99,682,283,088.61** ni fedha za Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 1,275,256,677,546.43** ni fedha za miradi ya maendeleo.

22. ***Mheshimiwa Spika***, baada ya kupokea fedha hizo, Wizara ya Uchukuzi iliendelea kutekeleza shughuli mbalimbali za kiudhibiti, utoaji wa huduma za uchukuzi katika usafiri wa reli, anga, majini na  barabara, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuratibu shughuli za hali ya hewa. Shughuli hizo zinalenga kuimarisha huduma za uchukuzi nchini kwa kuongeza usalama, uhakika na ufanisi wa usafirishaji wa watu na mizigo pamoja na kupunguza gharama za usafirishaji. Aidha, jitihada hizo zimeendelea kuwanufaisha Watanzania na wadau wengine, wakiwemo wafanyabiashara wa nchi jirani wanaotumia miundombinu na huduma mbalimbali za uchukuzi nchini.

### C:1 UDHIBITI NA UTOAJI WA HUDUMA ZA UCHUKUZI

23. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi imeendelea kusimamia na kudhibiti utoaji wa huduma za uchukuzi katika njia ya usafiri wa anga, ardhini, majini pamoja na masuala ya hali ya hewa.

## UDHIBITI WA HUDUMA ZA USAFIRI WA ANGA

24. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza majukumu ya udhibiti wa usafiri wa anga na kuhakikisha usalama wa anga, Serikali kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) imeendelea kusimamia ubora wa viwanja vya ndege vinavyomilikiwa na Serikali na taasisi binafsi pamoja na huduma zinazotolewa. Lengo la Serikali ni kuboresha utoaji wa huduma na kuhakikisha uzingatiaji wa sheria na kanuni za usafiri wa anga nchini.

25. ***Mheshimiwa Spika,*** TCAA pia imeendelea kutoa huduma za uongozaji ndege katika viwanja vya ndege 15. Viwanja hivyo vinajumuisha viwanja vitatu (3) vya kimataifa vya Julius Nyerere (JNIA), Abeid Amani Karume (AAKIA) na Kilimanjaro (KIA). Viwanja vingine 12 ni Mwanza, Bukoba, Arusha, Pemba, Tabora, Kigoma, Dodoma, Iringa, Songwe, Mtwara, Tanga na Songea. Aidha, Shirika la Usafiri wa Anga Duniani (ICAO) limeendelea kuikasimisha Tanzania jukumu la uongozaji ndege zinazoruka na kupita urefu wa futi elfu 25 juu ya anga la nchi ya Burundi.

26. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya ndege 13 zilizosajiliwa zilifanyiwa ukaguzi na kupewa vyeti vya awali vya ubora (Certificate of Airworthiness). Ndege hizo zinajumuisha ATR moja (1), De Havilland DHC8-300 mbili (2), helikopta aina ya Airbus AS350B3 mbili (2), helikopta aina ya Robinson R44 moja (1), microlight mbili (2), Cessna 182 mbili (2), na Cameroon A450 tatu (3). Aidha, ndege mbili (2) ziliondolewa katika daftari la usajili kufuatia kukamilika kwa mikataba ya ukodishaji.

27. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hicho pia ndege nyingine 176 zilifanyiwa ukaguzi hapa nchini na kupewa vyeti vya ubora na kuendelea kufanya kazi nchini, hatua inayodhihirisha uimara wa mifumo ya ukaguzi na usimamizi wa usalama wa anga nchini. Kwa sasa, daftari la usajili wa ndege nchini lina jumla ya ndege 581, jambo linaloonesha kuendelea kuimarika kwa sekta

ya usafiri wa anga na kuongezeka kwa shughuli za usafirishaji wa abiria na mizigo nchini.

28. ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kuongeza soko la usafiri wa anga kwa mashirika ya ndani na nje ya nchi, Serikali kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), imeendelea kufanya mapitio ya utekelezaji na kusaini Mikataba Mipya ya Usafiri wa Anga (Bilateral Air Services Agreements – BASA) kati ya Tanzania na nchi nyingine kwa lengo la kuboresha huduma za usafiri wa anga kwa kuvutia mashirika mapya ya ndege kutoa huduma na kuimarisha ushindani katika sekta ya anga nchini.

29. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Novemba 2025, Serikali ilishiriki Mkutano wa Majadiliano ya Mikataba ya Usafiri wa Anga (ICAN 2025) Jijini Punta Cana, Dominican Republic. Ushiriki huo uliwezesha Tanzania kufanya majadiliano ya mikataba ya usafiri wa anga na nchi 13. Kutokana na Mkutano huo, Serikali iliingia mikataba mipya miwili (2) ya usafiri wa anga na nchi za Dominican Republic na Vietnam, pamoja na kufanya mapitio ya mikataba mingine 11 ili kuendana na mahitaji ya soko la usafiri wa anga.

30. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Machi 2026, Tanzania imesaini jumla ya Mikataba 91 ya BASA na nchi mbalimbali ikilinganishwa na mikataba 89 iliyokuwepo mwaka wa fedha 2024/25. Ongezeko hili linaonesha kuendelea kuimarika kwa ushirikiano wa Tanzania na mataifa mbalimbali duniani katika sekta ya usafiri wa anga, hatua inayochangia kufungua fursa mpya za biashara, utalii, uwekezaji na kuongeza mtandao wa safari za anga nchini na kuitangaza Tanzania kimataifa.

31. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia utekelezaji wa mikataba hiyo, TCAA imewezesha jumla ya mashirika 28 ya ndege za kimataifa kuendelea kutoa huduma kwa utaratibu wa BASA. Aidha, TCAA imeendelea kupokea maombi ya baadhi ya nchi kuleta mashirika ya ndege kwa ajili ya safari za ratiba na zisizo za ratiba kwa utaratibu wa Mikataba ya Anga na Makubaliano ya Kimataifa. Baadhi ya nchi hizo ni Urusi, Ubelgiji, Comoro, Italia na Israeli.

32. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi 2026, idadi ya abiria waliotumia usafiri wa anga iliendelea kuongezeka na kufikia abiria 6,800,111, ikilinganishwa na abiria 6,037,444 waliotumia usafiri huo katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2024/25. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 12.63. Ongezeko hili limetokana na kuendelea kuimarika kwa shughuli za usafiri wa anga nchini, hususan kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watalii, kuimarika kwa huduma za ndege, pamoja na kukua kwa biashara na shughuli za kiuchumi ndani na nje ya nchi.

33. ***Mheshimiwa* Spika**, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi 2026, idadi ya abiria waliosafiri ndani ya nchi imefikia 3,675,143 ikilinganishwa na abiria 3,201,362 waliosafiri katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2024/25. Hili ni sawa na ongezeko la asilimia 14.79. Aidha, idadi ya abiria waliosafiri kimataifa imefikia 3,244,968, ikilinganishwa na abiria 2,836,082 waliosafiri katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2024/25 ikiwa ni ongezeko la asilimia 14.42. Ongezeko hili la abiria lilichangiwa na kuongezeka kwa miruko ya ndege, kuanza safari mpya kwa baadhi ya mashirika ya ndege, kuongezeka kwa njia mpya na kurejesha safari kwa mashirika yaliyokuwa yamesitisha safari.

34. ***Mheshimiwa* Spika,** kwa upande wa mizigo, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya tani 2,549.0 za mizigo zilisafirishwa ndani ya nchi, ikilinganishwa na tani 2,475.3 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2024/25. Vilevile, katika kipindi hicho, tani 32,201.2 za mizigo zilisafirishwa kimataifa, ikilinganishwa na tani 30,637.2 zilizosafirishwa katika mwaka wa fedha 2024/25. Ongezeko la mizigo inayosafirishwa linatokana na kuendelea kuimarika kwa usafiri wa anga pamoja na kuendelea kutoa huduma kwa ndege ya mizigo ya ATCL, jambo ambalo linachangia kuongeza ufanisi wa usafirishaji wa mizigo ndani na nje ya nchi.

35. ***Mheshimiwa Spika,*** takwimu zinaonesha kuwa kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya miruko ya safari za ndege ilifikia 254,138, ikilinganishwa na miruko 222,307 katika kipindi kama

hicho cha mwaka wa fedha 2024/25. Kuongezeka kwa usafirishaji wa abiria, mizigo, na miruko ya ndege kunatokana na jitihada za Serikali katika kukuza biashara ya usafiri wa anga nchini, kuvutia mashirika mapya ya usafiri wa anga, pamoja na kurejeshwa kwa baadhi ya njia za ndege (routes) na njia za kupitia (enroutes). Hali hii imeongeza ufanisi, upatikanaji wa huduma na kupanua mtandao wa usafiri wa anga nchini.

36. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imekamilisha Mradi wa Ufungaji wa Mitambo ya kuongozea ndege kwa njia ya mawasiliano ya sauti *(VHF Radio Communication Systems)* kati ya waongoza ndege na marubani. Mradi huu ulihusisha ufungaji wa mitambo kwa ajili ya mawasiliano ya anga la juu katika viwanja vya ndege 12 na vituo (Relay stations) 18. Mitambo hii imesaidia kuimarisha usalama wa anga nchini kwa kuwezesha mawasiliano ya haraka na ya uhakika kati ya marubani na waongoza ndege; kupunguza uwezekano wa ajali ya ndege angani; kuwezesha utoaji wa maelekezo ya dharura kwa wakati; kupunguza ucheleweshaji wa ndege; na kuboresha mtiririko wa trafiki ya anga.

37. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa nyakati tofauti, Bunge lako Tukufu limekuwa likielekeza Serikali kuhakikisha kuwa utoaji wa mafunzo katika tasnia ya anga unaimarishwa hapa nchini. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita kupitia TCAA imeendelea na ujenzi wa Chuo cha Usafiri wa Anga (CATC) Jijini Dar es Salaam. Ujenzi huo unahusisha: majengo sita (6) yanayojumuisha majengo ya utawala, mgahawa, taaluma, ukumbi wa mikutano na mabweni mawili (2), ambapo utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 11.3. Mradi huu utakapokamilika utawezesha kuongeza udahili wa wanafunzi wa ndani na nje ya nchi, kuongeza ubora na ufanisi wa mafunzo na hatimaye kuongeza idadi ya wataalam wa sekta ya usafiri wa anga nchini.

38. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi 2026, kazi nyingine zilizotekelezwa na TCAA katika kipindi hiki ni pamoja na:-

i. Kukamilika kwa ufungaji wa mitambo ya kutoa taarifa ya hali ya hewa na hali ya barabara ya kurukia ndege kwa njia ya mfumo wa sauti ya radio (*D-ATIS*) Kwenda kwa marubani katika viwanja vya ndege vya Abeid Amani Karume (AAKIA) na Julius Nyerere (JNIA);

ii. Kuendelea na ufungaji wa mfumo mpya wa kutua na kupaa kwa ndege kwa kusaidiwa na vyombo vya kielektroniki (Instrument Landing System – ILS) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA), ambapo utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 60. Mfumo huu unafungwa baada ya uliokuwepo kutumika kwa zaidi ya miaka 20;

iii. Kuendelea kufanya matengenezo kinga (preventive maintenance) katika vituo 16 vilivyopo katika viwanja vya ndege na vituo 18 vilivyopo nje ya viwanja vya ndege. Matengenezo hayo yamehusisha mitambo ya kuongozea ndege, mitambo ya mawasiliano ya sauti na mitambo ya kufuatilia mienendo ya ndege;

iv. Kukamilisha maboresho ya taratibu za uongozaji ndege kwa vyombo vya usafiri wa anga. Maboresho hayo yamefanyika katika viwanja vya ndege vya AAKIA, JNIA na Dodoma. Aidha, Serikali imefanikiwa kuanzisha maeneo ya udhibiti wa anga (Control Zones – CTR) katika viwanja vya AAKIA, JNIA, Iringa na Songwe, hatua inayoongeza usalama na ufanisi katika usimamizi wa anga;

v. Kuanzishwa kwa Eneo la Udhibiti wa Anga la Kituo (Terminal Control Area – TCA) pamoja na (Control Zone - CTR) katika Kiwanja cha Ndege cha Songwe, sambamba na kufanya mapitio katika viwanja vya JNIA, KIA na Mwanza kwa lengo la kuimarisha mtiririko, ufanisi na usalama wa ndege; na

vi. Kuendelea na kaguzi na urekebishaji wa vifaa vya usafiri wa anga (Flight Calibration and inspection) katika viwanja vya ndege vya JNIA, KIA, AAKIA, Dodoma, Pemba, Tabora, Mtwara, Iringa, Songea, Songwe na Mwanza.

## UDHIBITI WA USAFIRI ARDHINI

39. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), imeendelea kusimamia udhibiti wa usafiri ardhini katika maeneo makuu matatu ya usafiri wa barabara, usafiri wa reli na usafiri wa waya (cable transport). Aidha, LATRA imeendelea kutekeleza majukumu mengine ikiwa ni pamoja na usimamizi wa tozo za huduma zinazotolewa, ushindani kwenye usafiri ardhini, ufuatiliaji wa utendaji na usimamizi wa ubora wa huduma zinazotolewa.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza majukumu hayo ya udhibiti, LATRA imeendelea kutoa huduma mbalimbali, zikiwemo utoaji wa leseni za vyombo vya usafiri kibiashara. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, LATRA ilitoa jumla ya leseni 388,715 za usafirishaji ikilinganishwa na leseni 250,519 zilizotolewa katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2024/25, ikiwa ni ongezeko la leseni 138,196, sawa na ongezeko la asilimia 55.16. Kati ya leseni 388,715 zilizotolewa, leseni 22,531 ni za mabasi ya abiria, leseni 173,654 ni za magari ya mizigo na leseni 192,530 ni za magari ya kukodi.

### Kupanga na Kufuatilia Viwango vya Nauli na Ubora wa Huduma za Usafiri Ardhini

41. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia LATRA imeendelea kusimamia kwa karibu upangaji na ufuatiliaji wa viwango vya tozo na nauli elekezi kwa huduma zinazodhibitiwa, hususan katika mazingira ambayo ushindani wa soko haujitoshelezi kulinda ipasavyo maslahi ya watumiaji wa huduma na watoa huduma. Hatua hizi zinalenga kuhakikisha uwepo wa mizania stahiki ili kuwalinda watumiaji, kuboresha mazingira ya watoa huduma pamoja na kuhamasisha uwekezaji endelevu katika sekta. Aidha, LATRA imeendelea kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini ya ubora wa huduma za usafiri wa ardhini ili kuhakikisha huduma zinazotolewa zinakidhi viwango vinavyokubalika na kulinda maslahi mapana ya wananchi.

42. ***Mheshimiwa Spika,*** kama tulivyoona kumekuwa na changamoto za kupanda kwa bei ya mafuta nchini na duniani kote kutokana na vita kati ya Marekani na Israeli dhidi ya Irani. Kutokana na changamoto hiyo, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali kwa lengo la kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala. Moja ya hatua hizi ni kupitia mradi wa *Green Economic Corridor* unaotekelezwa kupitia Wakala wa Kuratibu Uwezeshaji wa Usafirishaji na Biashara katika Ukanda wa Kati (Central Corridor Transit Transport Facilitation Agency - CCTTFA). Lengo la mradi huu ni kuhamasisha wadau kutumia magari ya umeme nchini (emobility). Kwa sasa zipo baadhi ya kampuni ambazo zimeanza kuchukua hatua za awali katika kuanzisha viwanda vya kuzalisha magari yanayotumia umeme. Baadhi ya kampuni ni pamoja na: Plug and Ride inayomiliki kiwanda cha kuunganisha vyombo vya moto vinavyotumia umeme; na Kampuni ya Haofen International Trade iliyoonesha nia ya kuanzisha Kiwanda cha magari ya umeme hapa nchini.

43. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia imeendelea kuhimiza matumizi ya nishati mbadala ikiwemo gesi (CNG) pamoja na matumizi ya usafiri wa umma (mass transit) ili kupunguza matumizi ya nishati ya mafuta katika vyombo vya usafiri. Kwa ujumla, Wizara itaendelea kushirikiana kwa karibu na wadau wa usafirishaji na kuchukua hatua zaidi kadri hali ya soko la dunia itakavyoendelea kubadilika, ili kuhakikisha wananchi wanaendelea kulindwa na uchumi wa Taifa unabaki imara.

44. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inatambua mchango mkubwa unaotolewa na tasnia ya usafiri wa pikipiki nchini, hususan kwa maeneo yasiyofikika kirahisi kwa usafiri wa umma. Takwimu zilizopo zinaonesha kuwa usafiri wa pikipiki una manufaa makubwa kiuchumi ikiwemo chanzo cha ajira nchini. Mathalan, mwaka 2024 vijana takriban milioni 1.1 walikuwa wamejiajiri katika tasnia ya usafiri wa pikipiki nchini. Aidha, asilimia 12.5 ya vijana nchini wanajihusisha na biashara ya matengenezo ya vyombo vya moto zikiwemo pikipiki. Hata hivyo, usafiri huo umekuwa na changamoto zikiwemo kusababisha ajali za barabarani ambazo nyingi zimekuwa zikichangiwa kwa kiasi kikubwa na waendesha pikipiki kwa kutozingatia sheria za usalama barabarani.

45. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na umuhimu wa usafiri wa pikipiki katika maeneo mbalimbali nchini, hususan yasiyofikika kirahisi kwa usafiri wa umma, Serikali imeanza taratibu za kuboresha zaidi usimamizi wa usafiri huo ili kupunguza changamoto zinazojitokeza ikiwemo kufanya mapitio ya sheria zinazosimamia usafiri wa pikipiki ili kuweka mfumo wa pamoja wa kusimamia usafiri huo. Kwa kuwa suala hili ni mtambuka na ni la kisera, tayari Wizara imewasilisha mapendekezo ili yaweze kujadiliwa na kutolewa maamuzi stahiki kwa lengo la kuboresha huduma za usafiri huo. Mapendekezo hayo yamewasilishwa katika ngazi za Serikali kwa ajili ya kuwasilishwa katika Baraza la Mawaziri.

**Udhibiti wa Madereva na Wahudumu wa Vyombo vya Usafiri**

46. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuboresha weledi na kudhibiti mwenendo wa madereva barabarani, LATRA imeendelea kusajili, kuthibitisha na kufuatilia mienendo ya madereva wakiwa barabarani kupitia mifumo ya TEHAMA. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 jumla ya madereva 6,381 walisajiliwa kupitia Mfumo wa Usimamizi wa Usafiri Ardhini (RRIMS), 4,469 walitahiniwa kupitia Mfumo wa Kutahini Madereva (Drivers Testing System - DTS), ambapo kati yao madereva 2,965 walifaulu na kuthibitishwa na LATRA.

47. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kusimamia usalama, Serikali imeendelea kusimamia utaratibu wa lazima wa madereva wa safari za usiku kwa mabasi ya abiria na mabasi ya kukodishwa kuwa na kitufe cha utambuzi wa dereva (i-Button) ambacho kinawezesha kutambua dereva anayeendesha basi husika. Aidha, Serikali imeboresha mfumo huo ili uweze kutumika kuthibitisha madereva wa treni. Kwa upande wa usajili wa wahudumu hadi kufikia Machi 2026, LATRA ilisajili wahudumu 2,299 baada ya kupewa mafunzo ambayo yalitolewa kwa kushirikiana na vyuo vinne (04) ambavyo ni Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), na Chuo cha Ufundi Arusha (ATC).

## Udhibiti wa Usafiri wa Waya (Cable Transport)

48. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu usafiri kwa njia ya waya, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi 2026, LATRA ilishirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo Wizara ya Maliasili na Utalii, Wakala wa Misitu (TFS), Wakala wa Wanyamapori (TAWA), Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA), Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Halmashauri za Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Iringa, Mbeya, Pwani na Dar es Salaam pamoja na Sekta Binafsi katika kutambua uwepo, fursa, utayari na mahitaji ya udhibiti wa huduma hii nchini. Aidha, wadau mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi wameonesha utayari wa kuwekeza katika usafiri kwa njia ya waya. Kutokana na fursa hiyo, Wizara ya Uchukuzi kwa kushirikiana na wadau wa usafiri ardhini, imekamilisha uandaaji wa Kanuni za Udhibiti wa Usafiri wa Waya na kwa sasa zipo katika hatua za kuidhinishwa.

## Mifumo ya Ufuatiliaji wa Usafiri Ardhini

49. ***Mheshimiwa Spika,*** LATRA imeendelea kutumia mfumo wa Ufuatiliaji wa Mwenendo wa Magari (Vehicle Tracking System - VTS) ili kuimarisha usalama kwa kufanya ufuatiliaji wa mwenendo wa mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani, pamoja na treni za TAZARA na TRC. Mfumo huu umeboreshwa na kuunganishwa na mfumo wa utambuzi wa madereva (i-buttons) ili kuwatambua na kuwafuatilia madereva wanaoendesha mabasi hayo usiku na mchana (24/7). Hadi kufikia mwezi Machi 2026, jumla ya mabasi ya masafa marefu 13,843 yaliyopewa leseni yalikuwa yameunganishwa kwenye mfumo wa VTS, ikilinganishwa na mabasi 11,826 yaliyounganishwa na mfumo wa VTS katika kipindi kama hicho cha mwaka 2024/25.

50. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hicho, jumla ya madereva wa mabasi 12,699 walikuwa wamesajiliwa na kupatiwa vitufe vya utambuzi (ibutons). Vilevile, wamiliki wa mabasi yaliyounganishwa na mfumo wa VTS wamepewa akaunti za VTS ili waweze kufuatilia mabasi yao na mwenendo wa madereva wao. Aidha, jumla ya askari 761 wa Jeshi la Polisi, Kikosi cha Usalama Barabarani wamepatiwa akaunti waweze kufuatilia mwenendo

wa mabasi yote yaliyounganishwa kwenye mfumo wa VTS na madereva wake ili kuongeza uwanda wa udhibiti usalama barabarani.

**Tiketi Mtandao kwa Mabasi Yaendayo Mikoani na Nchi Jirani**

51. ***Mheshimiwa Spika,*** kama utakavyokumbuka, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika Hotuba yake Wakati wa Kufungua Rasmi Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dodoma, tarehe 14 Novemba 2025, alisisitiza kuhusu Matumizi ya TEHAMA katika kutekeleza Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali unaotekelezwa kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2024-2034. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu, kuwa LATRA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) na Shirika la Reli Tanzania (TRC) ilikamilisha na kuanza kutumia mfumo wa Tiketi Mtandao (Core e-Ticketing System-CeTS) unaoweka mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani kwenye mfumo huo yaani, Stendi Kiganjani na kumwezesha abiria kukata tiketi za mabasi na treni za TRC kupitia Safari Tiketi App inayopatikana kwenye mitandao ya simu za *Android* na *iOS* au kupitia tovuti ya *tiketi.latra.go.tz.* Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya mabasi 8,126 yameunganishwa na Mfumo huu.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha matumizi ya Mfumo wa Tiketi Mtandao, hadi kufikia mwezi Machi 2026, LATRA ilikuwa na watoa huduma 17 wa Mfumo wa Tiketi Mtandao, kati yao tisa (9) walithibitishwa na kupatiwa leseni, wanne (4) wanaendelea kukamilisha taratibu za kuthibitishwa na wengine wanne (4) wapo katika hatua za mwisho za majaribio ya mifumo yao kabla ya kuthibitishwa na kusajiliwa. Aidha, hadi kufikia mwezi Machi 2026, jumla ya abiria milioni 21.34 waliosafiri kwa mabasi walikata Tiketi Mtandao ikilinganishwa na abiria milioni 13.71 waliosafiri katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2024/25, sawa na ongezeko la asilimia 55.65.

53. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa miamala ya nauli zilizolipwa kupitia Mfumo wa Tiketi Mtandao, hadi kufikia mwezi Machi 2026, jumla ya Shilingi bilioni 718.99 ililipwa na wasafiri

waliotumia Tiketi Mtandao ikilinganishwa na Shilingi bilioni 505.80 iliyolipwa katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2024/25, ikiwa ni ongezeko la Shilingi bilioni 213.19, sawa na ongezeko la asilimia 42.15. Kwa ujumla, utekelezaji wa mfumo wa Tiketi Mtandao umekuwa na mwitikio chanya kwa wasafirishaji, ambapo umewezesha udhibiti wa mapato yao na kuondoa usumbufu kwa abiria kwa kuwa wanaweza kujikatia tiketi na kulipa popote walipo kupitia mitandao.

**Kufikisha Huduma Karibu na Wananchi**

54. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa lengo la kuendelea kufikisha huduma karibu na wananchi, Serikali kupitia LATRA imeendelea kupanua wigo wa huduma ili kufikia wananchi kiurahisi zaidi. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026 LATRA imefungua ofisi tatu (3) katika maeneo ya Mkuranga, Chunya na Karatu na hivyo kufanya jumla ya Ofisi za LATRA kuwa 40 nchi nzima, ambazo zinajumuisha Ofisi 26 za Makao Makuu ya mikoa yote, ofisi ndogo 13 na Ofisi Maalum ya Kituo cha Mikocheni ambayo ni kwa ajili ya kusimamia Mfumo wa VTS. Hatua nyingine zinazoendelea kuchukuliwa ni pamoja na kujenga jengo la Makao Makuu Jijini Dodoma, suala ambalo limeanza kwa hatua za awali ikiwepo kupatikana kwa kiwanja na Mshauri Elekezi.

**Ushirikishwaji wa wadau wa Usafiri na Usafirishaji kupitia LATRA**

55. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia LATRA, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, iliandaa maadhimisho ya kwanza ya Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini yaliyofanyika kuanzia tarehe 24 hadi 29 Novemba, 2025. Maadhimisho hayo yaliongozwa na kaulimbiu "Nishati Safi na Ubunifu katika Usafirishaji". Maadhimisho haya yalifunguliwa rasmi na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kongamano la kitaalam lililofanyika kwa siku tatu (3) kuanzia tarehe 25 hadi 27 Novemba, 2025.

56. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia maadhimisho hayo, mada mbalimbali zilitolewa kuhusu umuhimu wa matumizi ya nishati safi katika usafiri, ufanisi wa mifumo ya usafiri endelevu, matumizi ya teknolojia bunifu na nafasi ya Sekta Binafsi katika kuharakisha mabadiliko ya kimfumo katika usafiri wa ardhini. Aidha, miongoni mwa masuala muhimu yaliyojadiliwa na kuhimizwa ni matumizi ya nishati safi katika vyombo vya usafiri, ambapo jumla ya wadau 1,832 walishiriki katika maonesho hayo na maadhimisho hayo yatakuwa yanafanyika kila mwaka.

57. ***Mheshimiwa Spika,*** LATRA imeendelea kuimarisha utoaji wa elimu kwa umma kuhusu masuala ya udhibiti wa usafiri ardhini kwa kutumia vyombo vya Habari na majukwaa ya TEHAMA. Kupitia studio yake iliyopo jijini Dar es Salaam, LATRA imekuwa ikiandaa vipindi, maudhui na matukio mbalimbali ya elimu kwa umma vinavyorushwa kupitia Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC1) saa 3.30 usiku na Clouds TV saa 3.00 usiku kila siku ya Jumanne, pamoja na kurushwa katika mitandao ya kijamii kupitia "LATRA Online TV" na mitandao ya kijamii ikiwemo Instagram na Facebook. Pamoja na manufaa mengine, hatua hii imesaidia wananchi hususan wa vijijini kufahamu huduma zinazotolewa na LATRA na kutoa maoni ya namna ya kuboresha.

## UDHIBITI WA USAFIRI MAJINI

58. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kusimamia udhibiti wa masuala ya usafiri majini, Serikali kupitia Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) imeendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu yake yakiwemo; kusimamia ulinzi, usalama wa vyombo vya usafiri majini na kudhibiti uchafuzi wa mazingira unaotokana na shughuli za meli katika eneo la Tanzania Bara; udhibiti wa huduma za usafiri na usafirishaji majini; na kutoa huduma ya ugomboaji na uondoshaji wa shehena kwa bidhaa mahsusi.

### Udhibiti wa Watoa Huduma za Usafirishaji Majini

59. ***Mheshimiwa Spika,*** TASAC imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia watoa huduma zinazodhibitiwa. Hii ni pamoja na kutoa leseni na vyeti kwa watoa huduma waliokidhi

vigezo vilivyowekwa, sambamba na kufuatilia utekelezaji wa masharti na viwango vya ubora wa huduma. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi 2026, jumla ya watoa huduma 1,794 walisajiliwa na kupewa leseni pamoja na vyeti vya usajili, ikilinganishwa na watoa huduma 1,556 waliosajiliwa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2024/25, sawa na ongezeko la asilimia 15.29. Watoa huduma hao ni pamoja na mawakala wa meli, wakusanyaji na watawanyaji wa shehena, mawakala wa ugomboaji shehena, watoa huduma melini, wahakiki uzito ghafi wa shehena katika makasha, waendeshaji wa bandari na waendeshaji wa bandari kavu.

60. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa taratibu za kisheria na viwango vya ubora vinazingatiwa ipasavyo kwa watoa huduma za usafiri majini pamoja na watoa huduma za bandari, TASAC imeendelea kuimarisha udhibiti wa huduma hizo kupitia ukaguzi na ufuatiliaji wa mara kwa mara (kila robo mwaka). Katika kipindi husika, jumla ya watoa huduma 1,360 walikaguliwa ikilinganishwa na watoa huduma 1,302 waliokaguliwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2024/25, lengo ni kuhakikisha uzingatiaji wa matakwa ya kisheria na viwango vilivyowekwa.

**Usalama wa Vyombo na Usafiri Majini**

61. ***Mheshimiwa Spika,*** TASAC imeendelea kuratibu shughuli za utafutaji na uokoaji kupitia Vituo vya Utafutaji na Uokoaji Majini vilivyopo Dar es Salaam na Mwanza. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi 2026, jumla ya matukio 18 ya ajali yaliripotiwa na hatua mbalimbali za uokoaji zilichukuliwa. Aidha, katika jitihada za kupunguza ajali na kuongeza usalama wa usafiri majini, TASAC imetekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kutoa elimu kwa wadau na kutoa taarifa za hali ya hewa kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA). Katika kipindi hicho jumla ya taarifa 1,065 zilitolewa kwa wadau, ikiwemo taarifa za onyo 505 (warning reports), hatua ambazo zimeongeza uelewa, udhibiti wa ajali na usalama wa abiria na mizigo katika sekta ya usafiri majini.

62. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi 2026, TASAC imeendelea na kaguzi za usalama kwa vyombo vya usafiri majini 8,239. Kati ya vyombo hivyo, meli kubwa zilikuwa 465 na vyombo vidogo vya usafiri majini vilikuwa 7,774. Ukaguzi huo ulionesha kuwa, vyombo vya usafiri majini 6,345 vilikidhi viwango vya ubora wa kiusalama, ambapo meli kubwa zilikuwa 453 na vyombo vidogo vilikuwa 5,892. Takwimu hizi zinaonesha kuwa, vyombo vilivyokidhi viwango ni asilimia 77.0 ya vyombo vyote vilivyokaguliwa, hali inayodhihirisha kuendelea kuimarika kwa usalama katika usafiri majini. Kaguzi hizi ziliendeshwa katika mikoa 11 nchini, kwa lengo la kuhakikisha usalama wa usafiri majini.

63. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kusimamia usalama wa usafiri majini ndani ya Ziwa Victoria, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Uganda zimeendelea kutekeleza Mradi wa Kikanda wa Kuboresha Mawasiliano na Uchukuzi katika ziwa hilo. Mradi huo unajumuisha ujenzi wa Kituo Kikuu cha Uratibu wa Utafutaji na Uokoaji Ilemela, Mwanza ambacho tayari kimekamilika. Aidha, Serikali ya Tanzania imeendelea na ujenzi wa vituo vidogo vitatu (3) vya utafutaji na uokoaji katika maeneo ya Kanyala – Sengerema ambacho kimefikia asilimia 91, Nansio – Ukerewe (asilimia 85) na Musoma Mjini (asilimia 91).

64. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Serikali imekamilisha ununuzi wa boti mbili (2) za utafutaji na uokoaji pamoja na boti ya matibabu (Ambulance Boat) ambazo zitasaidia kuimarisha usalama katika usafirishaji ndani ya Ziwa Victoria. Ili kuhakikisha matumizi sahihi ya boti hizo, TASAC imefanya mafunzo kwa wataalam kuhusu uendeshaji wa boti hizo. Hatua hizi zinaendelea kuimarisha ufanisi katika utafutaji na uokoaji na hivyo kuongeza usalama wa abiria na mizigo katika Ziwa Victoria.

65. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na utekelezaji wa mradi huo wa kuimarisha usalama katika Ziwa Victoria, Serikali imeongeza uwezo wa nchi yetu kukabiliana na majanga katika usafiri majini kwa kununua boti nyingine mbili (2) za kisasa za utafutaji na uokoaji. Boti hizo tayari zimeanza kutoa huduma

katika bahari na Maziwa Makuu, ambapo boti moja (1) inatoa huduma katika Ziwa Tanganyika na boti moja (1) katika ukanda wa Bahari ya Hindi eneo la Mkoa wa Tanga. Hatua hii imeimarisha uwezo wa Taifa letu wa usalama na uokoaji majini na kuongeza ufanisi katika operesheni za dharura na kuhakikisha usafiri salama wa abiria na mizigo. Aidha, Serikali kupitia TASAC imeendelea na hatua za ununuzi wa boti nyingine mbili (2) kwa ajili ya kutoa huduma katika eneo la mkoa wa Kagera na Mtwara.

**Usimamizi wa Utoaji Mafunzo na Vyeti vya Ubaharia**

66. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha utekelezaji wa miongozo ya kimataifa kuhusu sifa na umahiri wa mabaharia wanaoendesha vyombo vya usafiri majini, TASAC imeendelea kusimamia Mkataba wa Kimataifa wa Mafunzo, Utoaji Vyeti na Utendaji Kazi kwa Mabaharia wa mwaka 1978 (International Convention on Standards of Training, Certification and Watch – Keeping for Seafarers – STCW 1978). Hadi kufika Machi 2026, jumla ya vyeti 15,948 vilitolewa, ikilinganishwa na vyeti 10,270 vilivyotolewa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2024/25, sawa na ongezeko la asilimia 55.28. Kati ya vyeti hivyo, 15,353 vilikuwa ni vyeti vya ustadi (Certificate of Proficiency - COP), 501 ni vitabu vya kumbukumbu za kazi (Continuous Discharge Certificate - CDC), na 94 vyeti vya umahiri kwa maafisa wa meli (Certificate of Competency - COC).

67. ***Mheshimiwa Spika,*** ongezeko hilo la vyeti limetokana na umahiri na mifumo ya utambuzi ya TASAC katika kusimamia utendaji wa kada ya ubaharia. Hatua hii imeimarisha uwezo wa mabaharia wa Tanzania na kuongeza ufanisi wa usafiri majini kwa viwango vinavyokubalika kimataifa. Aidha, TASAC imekaamilisha ujenzi wa mfumo wa TEHAMA utakaowezesha maombi na vyeti kutolewa kidigitali (Maritime Administration Management System - MAMS).

**Uwakala wa Forodha kwa Shehena za Kipekee**

68. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na majukumu mengine yanayotekelezwa, TASAC ina jukumu la kipekee la ugomboaji wa

shehena zenye maslahi mapana kwa Taifa ikiwemo kemikali zinazotumika katika migodi, silaha na vilipuzi kwa mujibu wa Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania Sura 415 na marekebisho ya Sheria ya Fedha Na. 5 ya mwaka 2022. Jukumu hilo limeendelea kutekelezwa kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania na Sekta Binafsi ili kuhakikisha jukumu hilo linatekelezwa kwa ufanisi. Kupitia utekelezaji huo, bidhaa hatarishi zimeendelea kugombolewa kwa wakati na kwa kuzingatia sheria za nchi.

69. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TASAC imeendelea kutoa elimu kwa watumiaji wa huduma za usafiri majini kuhusu tahadhari za kiusalama ili kuongeza uelewa kwa wadau wa usafiri majini na wananchi kwa ujumla. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi 2026, TASAC ilifanya mikutano 263 ya wadau kupitia kampeni za uhamasishaji kwa jamii zinazozunguka maziwa, mito na maeneo ya pwani, semina na mikutano kwa watoa huduma za usafiri majini, pamoja na matumizi ya vyombo vya habari na mabango ya elimu ya usalama. Aidha, TASAC imeendelea kutoa miongozo kuhusu matumizi ya vifaa vya usalama kama vile jaketi za kujiokoa (life jackets), uendeshaji salama wa vyombo na taratibu za dharura wakati wa majanga majini. Hatua hizi za utoaji elimu zimechangia kuongeza uelewa wa watumiaji wa usafiri majini na hivyo kupunguza madhara yanayoweza kutokea.

**UDHIBITI NA UTOAJI WA HUDUMA ZA HALI YA HEWA**

70. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imeendelea na utoaji wa huduma za hali ya hewa, pamoja na kudhibiti na kuratibu shughuli zote zinazohusiana na hali ya hewa nchini na kutekeleza majukumu mengine yakiwemo kufanya tafiti za kisayansi kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa na kubadilishana taarifa za hali ya hewa kupitia mtandao wa mawasiliano wa dunia wa *Global Telecommunication System* (GTS) kwa kuzingatia makubaliano ya kimataifa.

71. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na umahiri wa TMA kimataifa, taasisi hii imeendelea kuiwakilisha Tanzania katika masuala ya hali ya hewa kikanda na kimataifa na hivyo

kuendelea kuchangia katika uimarishaji wa mifumo ya tahadhari za mapema dhidi ya majanga yanayotokana na hali mbaya ya hewa. Vilevile, TMA imeendelea kutoa taarifa za hali ya hewa zinazotumiwa kupanga na kutekeleza shughuli za sekta mbalimbali zikiwemo usafirishaji, ujenzi, kilimo, uvuvi, nishati, madini na utalii.

72. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha usalama wa watu na mali zao, TMA imeendelea kutoa huduma za utabiri wa hali ya hewa wa kila siku, siku 10 na wa msimu, pamoja na tahadhari za matukio ya hali mbaya ya hewa. Wastani wa usahihi wa utabiri hadi mwezi Machi, 2026 umefikia asilimia 87.6 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 86.0 kwa kipindi kama hicho cha mwaka 2025. Ufanisi huo umesaidia kupunguza madhara yatokanayo na hali mbaya ya hewa ikiwemo vifo na upotevu wa mali. Kuongezeka kwa usahihi wa utabiri kumetokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya kisasa vya hali ya hewa, uboreshaji wa mifumo ya ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa za hali ya hewa na kuendelea kuwajengea uwezo wataalam katika kada ya utabiri wa hali ya hewa.

73. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendelea kutoa huduma za hali ya hewa kwa usahihi zaidi nchini, Serikali kupitia TMA imekamilisha ufungaji wa mitambo nane (8) ya kupima hali ya hewa katika maeneo ya Bukombe (Geita), Kahama (Shinyanga), Hanang (Manyara), Meatu (Simiyu), Unguja Kusini (Zanzibar), Korogwe (Tanga), Ikungi (Singida) na Nanyumbu (Mtwara). Vilevile, Serikali imekamilisha ufungaji wa mfumo wa kisasa wa kuandaa utabiri wa hali ya hewa (Complete Forecasting System) ambao utaanza kutoa huduma mwishoni mwa mwezi Mei, 2026.

74. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha huduma za hali ya hewa kwa sekta ya usafiri wa anga, TMA imeendelea kuzihudumia ndege kwa kutoa taarifa mahsusi za hali ya hewa (Flight Folders) zinazowezesha kuruka na kutua kwa ndege, ambapo katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Machi 2026, jumla ya miruko ya ndege 49,174 iliyohudumiwa ikilinganishwa na

miruko 41,256 iliyohudumiwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2024/25, sawa na ongezeko la asilimia 19.19.

75. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuboresha huduma za hali ya hewa kwa sekta ya usafiri wa anga, TMA imekamilisha ufungaji wa mitambo miwili (2) ya uangazi wa hali ya hewa (AVIMET) katika viwanja vya ndege vya Mpanda na Pemba. Aidha, TMA imekamilisha malipo ya ununuzi wa mitambo miwili (2) ya uangazi wa hali ya hewa ya anga za juu (Upper Air Stations) iliyotengenezwa nchini Ufaransa na inatarajiwa kuwasili nchini mwezi Julai, 2026 na kufungwa katika mikoa ya Mtwara na Kigoma ili kuimarisha zaidi utoaji wa huduma nchini.

76. ***Mheshimiwa Spika,*** TMA imeendelea na ujenzi wa miundombinu ya hali ya hewa ikiwemo maabara ya uhakiki wa vifaa vya hali ya hewa (Calibration Center) Dar es Salaam ambayo ujenzi wake umefikia asilimia 46. Maabara hii itapunguza gharama za kuhakiki vifaa vya hali ya hewa nje ya nchi. Kazi nyingine za miundombinu ya hali ya hewa zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa Kituo cha Hali ya Hewa Kilimo (Agromet Station) cha Hombolo (Dodoma) ambao umefikia asilimia 31, ujenzi wa jengo la Kanda ya Mashariki na Kituo cha Kufuatilia Matukio ya Tsunami jijini Dar es Salaam utekelezaji wake umefikia asilimia 67 na ujenzi wa miundombinu ya Rada itakayofungwa mkoani Dodoma umefikia asilimia 96.

77. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kudhibiti ubora wa huduma za hali ya hewa zinazotolewa kwa sekta ya usafiri wa anga, TMA ilifanyiwa ukaguzi wa Kimataifa wa utekelezaji wa mfumo wa kudhibiti ubora wa huduma za hali ya hewa zinazotolewa katika sekta ya usafiri wa anga. Ukaguzi huo ulifanyika kuanzia tarehe 09 hadi 13 Machi 2026, ambapo TMA ilikidhi vigezo vya utoaji wa huduma bora na hivyo kuendelea kumiliki cheti cha ubora (ISO 9001: 2015).

78. ***Mheshimiwa Spika***, katika hotuba ya Wizara ya mwaka 2025/26, Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi iliahidi kuendelea kuimarisha huduma muhimu za hali ya hewa kwa watumiaji wa Bahari ya Hindi na Maziwa Makuu. Napenda kulitaarifu Bunge

lako Tukufu kuwa, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 TMA ilitoa taarifa za hali ya hewa (marine bulletin) 100,802 kwa vyombo vya usafiri majini ikilinganishwa na taarifa 95,548 zilizotolewa katika kipindi kama hicho cha mwaka 2024/25, sawa na ongezeko la taarifa 5,254. Vilevile, TMA imenunua mitambo mitatu (3) ya uangazi (HF Marine Radars) iliyotengenezwa nchini Hispania itakayofungwa katika maeneo ya Dar es Salaam, Bagamoyo na Zanzibar. Hatua hii imelenga kuimarisha ufuatiliaji wa usalama wa baharini, kuongeza usahihi wa utabiri wa hali ya hewa na kusaidia kuimarisha usalama wa mizigo, meli na abiria wanaotumia bahari.

79. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kuwa wananchi wote wa Tanzania wanapata taarifa sahihi na kwa wakati kuhusu hali ya hewa, TMA imeongeza wigo wa kuhabarisha umma ambapo hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya vituo 14 vya redio na televisheni mtandao vimejumuishwa kutoa taarifa za hali ya hewa. Vituo hivyo vinajumuisha: vituo vya Redio nane (8) ambavyo ni Fadhila FM (Mtwara), Blessed Hope FM (Geita), Uplands FM (Njombe), Bomba FM (Mbeya), Big Star FM (Mbeya), Main FM (Kigoma), Wasafi FM (Dar es Salaam) na CG FM (Tabora); pamoja na vituo sita (6) vya Televisheni Mtandao (Online TV) vya Nyumbani Digital TV (Ruvuma), Madelemo News (Dar es Salaam), Torch Media (Dar es Salaam), Jehova Jire TV (Dar es Salaam), Dar24onlineTV (Dar es Salaam) na Maelezo TV (Dodoma). Hatua hii imewezesha kuwa na jumla ya vyombo vya habari 130 vinavyosambaza taarifa za hali ya hewa hapa nchini, hivyo kuongeza upatikanaji wa taarifa kwa wananchi na kuongeza uelewa kwa umma kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa na tahadhari za majanga yanayotokana na hali mbaya ya hewa.

80. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuendana na mabadiliko ya tabianchi na hali ya hewa, TMA ililenga kufanya tafiti tano (5) katika mwaka 2025/26, ambapo kwa kipindi cha mwezi Julai, 2025 hadi Machi, 2026 tafiti hizo zilifanyika na matokeo ya tafiti hizo yamefanikiwa kuchapishwa katika majarida ya kisayansi ya kimataifa. Tafiti hizo ni pamoja na: Mienendo ya ukame; Mabadiliko ya joto katika msimu wa vuli ndani ya Tanzania; Athari za mvua za majira ya joto Afrika Mashariki na Kusini; Uchambuzi

wa taarifa za mvua zinazotokana na setilaiti kwa kurejea mvua zilizopimwa katika Bonde Dogo la Ruaha; na Mienendo ya mvua katika Bonde Dogo la Ruaha, kusini mwa Tanzania. Matokeo ya tafiti hizi yameendelea kutumika katika kuziwezesha sekta za kiuchumi na kijamii kuwa himilivu katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi na hivyo kuchochea maendeleo endelevu.

81. ***Mheshimiwa Spika***, kama unavyofahamu, azma ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Jemedari Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni pamoja na kuitangaza Tanzania kikanda na kimataifa. Katika kuendeleza juhudi hizo, TMA imeendelea kuonesha umahiri wake katika masuala ya hali ya hewa kikanda na kimataifa. Kutokana na ufanisi huo, Tanzania imeaminiwa na kuchaguliwa kuwa mwenyeji wa mikutano miwili ya ngazi za juu ya Taasisi zinazosimamia masuala ya hali ya hewa na mabadiliko ya tabianchi duniani.

82. ***Mheshimiwa Spika,*** mikutano hiyo ni: Mkutano wa Nne wa Wataalam wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) unaolenga kuboresha miongozo ya Utabiri wa Hali ya Hewa na umepangwa kufanyika tarehe 29 Juni hadi 03 Julai, 2026. Mkutano huu ni wa kwanza kufanyika ndani ya bara la Afrika. Tanzania pia itakuwa mwenyeji wa Mkutano wa Tatu wa Wataalamu wa Kikosikazi cha Kwanza cha *Jopo la Kimataifa la Mabadiliko ya Tabianchi (Inter-governmental Panel on Climate Change – IPCC),* unaotarajiwa kufanyika Novemba, 2026. Mikutano hii itakuwa fursa kubwa kwa nchi yetu katika kuchochea shughuli za kiuchumi katika nyanja mbalimbali zikiwemo utalii, biashara, usafirishaji, malazi na utoaji huduma.

83. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza ushirikiano wa kimataifa katika tasnia ya hali ya hewa, Tanzania pia kupitia TMA ilitoa mafunzo mahsusi kwa nchi za Burundi na Sudani Kusini tarehe 12 – 17 Aprili, 2026. Mafunzo hayo yalihusisha: utabiri wa hali ya hewa kwa kutumia modeli za kompyuta (Numerical Weather Prediction); utabiri wa hali mbaya ya hewa (Severe

Weather Forecasting); na mfumo wa usimamizi wa ubora (Quality Management System – QMS).

### C:2 UTOAJI WA HUDUMA ZA UCHUKUZI HUDUMA ZA BANDARI

84. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), inaendelea kusimamia Bandari za Mwambao wa Bahari ya Hindi na Maziwa Makuu kwa kuendeleza miundombinu na utoaji wa huduma za kibandari kwa viwango vinavyokubalika kikanda na kimataifa. TPA pia inasimamia huduma za bandari, kulinda mazingira na kuhakikisha usalama wa bandari. Aidha, TPA imeendelea kuimarisha mazingira ya kuvutia wawekezaji katika bandari na kujitangaza kimasoko kwa kushirikiana na Sekta Binafsi ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma.

85. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi 2026, TPA ilihudumia jumla ya tani milioni 29.66 za shehena, ikilinganishwa na tani milioni 23.18 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2024/25, sawa na ongezeko la asilimia 27.96. Vilevile, TPA ilihudumia makasha 1,005,529, ikilinganishwa na makasha 831,866 yaliyohudumiwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2024/25, sawa na ongezeko la asilimia 20.88. Ongezeko la shehena na makasha yaliyohudumiwa limetokana na utekelezaji wa mikakati mbalimbali, ikiwemo uboreshaji wa miundombinu na utoaji wa huduma za kibandari sambamba na ushirikishwaji wa Sekta Binafsi.

86. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPA inaendelea kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 ambayo inatambua nafasi ya Tanzania kijiografia kama lango la usafirishaji wa bidhaa kwa nchi jirani ambazo hazina bahari. Katika kutumia fursa hiyo, Serikali kupitia TPA, imeendelea na uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam kupitia Mradi wa Maboresho ya Bandari ya Dar es Saaam, ambapo utekelezaji wa mradi huu kwa awamu ya kwanza umewezesha bandari hiyo kuwa na uwezo wa kupokea meli kubwa zenye urefu wa mita 305.

87. ***Mheshimiwa Spika,*** tangu kupata uhuru, nchi yetu imekuwa na changamoto ya kuhifadhi mafuta kwa ajili ya kuyatumia hususan wakati ambao yanatokea majanga ya kitaifa au kimataifa. Serikali ya awamu ya Sita imeamua kulifanyia kazi suala hilo kwa vitendo, ambapo TPA imeanza ujenzi wa miundombinu ya kupokelea na kuhifadhi mafuta (Single Receiving Terminal - SRT) unaohusisha ujenzi wa matanki 15 ya mafuta (tank farms) yenye uwezo wa kuhifadhi kiasi cha mita za ujazo 378,000, ambapo utekelezaji umefikia asilimia 42 na unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2026.

88. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine za uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam, TPA inaendelea na uboreshaji wa Magati mawili katika eneo la Malindi lenye urefu wa mita 500 ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2026 utekelezaji wake umefikia asilimia 13. Kukamilika kwa uboreshaji huu kutachangia kwa kiwango kikubwa katika kuongeza ufanisi wa shughuli za bandari, kuongeza mapato na kuimarisha viwango vya usalama kutokana na uwepo wa mitambo ya kisasa itakayowezesha kupokea meli kubwa badala ya majahazi, hivyo kupanua wigo wa biashara na ushindani wa kimataifa.

89. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi 2026, Serikali kupitia TPA imeendelea kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Kisiwa Mgao unaojumuisha gati jipya pamoja na mfumo wa *conveyor belt*. Bandari hii ni maalum kwa ajili ya kuhudumia shehena ya kichele (Dry Bulk Cargo) kama vile makaa ya mawe na saruji. Kazi zinazoendelea ni pamoja na uchimbaji na uongezaji kina cha lango la kuingilia na kugeuzia meli (entrance channel and turning basin) na ujenzi wa yadi ya kuhifadhia shehena. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 42.

90. ***Mheshimiwa Spika,*** miongoni mwa masuala yaliyoainishwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa 2025, ni pamoja na kujenga Bandari Mpya ya Bagamoyo katika eneo la Mbegani. Napenda kulitaarifu bunge lako Tukufu kuwa, Serikali kupitia TPA inakamilisha maandalizi ya kuanza utekelezaji wa mradi huo wa kimkakati. Bandari hiyo itahusisha ujenzi wa gati lenye urefu wa kilomita 1.32 pamoja na

miundombinu wezeshi kwa ajili ya kuhudumia meli kubwa za kisasa aina ya *Megamax* ambazo haziwezi kuhudumiwa katika Bandari ya Dar es Salaam kwa sasa.

91. ***Mheshimiwa Spika,*** katika utekelezaji wa awamu ya kwanza ya ujenzi wa Bandari Mpya ya Bagamoyo, tayari mitambo kwa ajili ya uchimbaji wa kina cha maji (dredging) imepatikana na kazi hiyo inatarajiwa kuanza rasmi mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2026/27. Bandari hiyo itakuwa ya kisasa na itatumia teknolojia katika utoaji huduma pamoja na usafirishaji shehena kwa njia ya reli ya SGR takriban urefu wa kilomita 60 kutoka Bandari hiyo hadi Bandari Kavu ya Kwala. Vilevile, Bandari hiyo itakuwa na uwezo wa kuhudumia meli zenye uwezo wa kubeba zaidi ya makasha (TEUs) 24,000 kwa mara moja, ikilinganishwa na wastani wa TEUs 6,000 zinazohudumiwa na Bandari ya Dar es Salaam kwa sasa.

92. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kupunguza msongamano katika Bandari ya Dar es Salaam, Serikali imeendelea kuhimiza matumizi ya bandari kavu katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Bandari Kavu ya Kwala iliyopo Mkoa wa Pwani ambayo imeendelea kutoa huduma, ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2026 Bandari Kavu ya Kwala imehudumia jumla ya makasha 14,460. Katika kutekeleza mkakati wa kuimarisha matumizi ya bandari hiyo, Serikali iliainisha maeneo maalum kwa ajili ya kuzipatia nchi zinazosafirisha shehena kwa wingi kupitia Bandari ya Dar es Salaam.

93. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza mkakati huo, tayari Serikali imetenga maeneo kwa ajili ya nchi za Rwanda, DRC, Burundi, Zambia, Uganda, Malawi, Sudan Kusini na Zimbabwe. Maeneo hayo yatatumiwa na nchi hizo kujenga miundombinu ya kuhudumia shehena wakati zikisubiri kusafirishwa kwenda nchi husika. Baadhi ya nchi hizo zimeanza uendelezaji wa maeneo hayo, ambapo Burundi imeanza ujenzi wa uzio na DRC imesaini mkataba wa uendelezaji wa eneo hilo tarehe 12 Machi, 2026. Ili kuendelea kuimarisha na kuboresha huduma za mizigo katika Bandari Kavu ya Kwala, Serikali kupitia TRC inaendelea na Upembuzi Yakinifu ikiwa ni hatua za awali za maandalizi ya

kuunganisha reli ya SGR na Bandari Kavu ya Kwala na kujenga stesheni ya SGR katika eneo hilo.

94. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kupanua wigo wa huduma za kibandari kwa kuendeleza ujenzi na uboreshaji wa bandari katika Maziwa Makuu nchini. Serikali kupitia TPA, imeendelea kuboresha miundombinu ya bandari zilizopo katika Ziwa Victoria kwa lengo la kuongeza uwezo wa kuhudumia abiria na mizigo kwa ufanisi zaidi. Hadi kufikia mwezi Machi, 2026 uboreshaji wa Bandari za Bukoba na Kemondo umekamilika na kazi za uboreshaji wa Bandari ya Mwanza North zikiwa zimefikia asilimia 75. Kukamilika kwa maboresho hayo kutaziwezesha bandari hizo kupokea na kuhudumia meli kubwa zaidi, ikiwemo meli ya MV. New Mwanza, ambayo kwa sasa tayari imeanza safari kati ya Mwanza na Bukoba na inatarajia kuanza safari nchi za jirani katika bandari za Kisumu (Kenya), Port Bell na Jinja (Uganda).

95. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali inaendelea na Mradi wa Uboreshaji wa Bandari ya Kigoma katika Ziwa Tanganyika unaohusisha ujenzi wa njia, gati pamoja na jengo la abiria. Mradi huu unatekelezwa kwa ufadhili wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Japan kupitia Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA). Hadi kufikia Machi 2026, utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 13.

96. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Tanzania inaendelea kuhudumia nchi za Maziwa Makuu kupitia bandari zetu, Serikali imeendelea kuboresha Bandari Kavu ya Katosho yenye ukubwa wa hekta 69 iliyopo mkoani Kigoma. Hatua hii inalenga kurahisisha usafirishaji wa shehena kupitia Ziwa Tanganyika kwenda nchi jirani. Kwa sasa Bandari hii tayari imewekewa miundombinu ya maji na umeme, na ni mradi wa kimkakati utakaowezesha kukuza biashara baina ya Tanzania na nchi jirani. Lengo la Serikali ni kuendelea kuboresha bandari kavu ili kuimarisha na kuleta ufanisi wa uhudumiaji wa mizigo nchini.

97. ***Mheshimiwa Spika***, kwa lengo la kuongeza ufanisi wa huduma za usafiri na usafirishaji kwa wananchi katika Ziwa Nyasa

pamoja na kuimarisha biashara na usafirishaji wa mizigo kwenda nchi jirani za Malawi na Zambia, Serikali kupitia TPA imeendelea na maboresho ya bandari zilizopo katika ziwa hilo. Maboresho hayo yanajumuisha ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya bandari ili kuongeza uwezo wa kuhudumia abiria na mizigo. Miongoni mwa bandari zinazoendelea kuboreshwa ni Bandari ya Mbamba Bay, ambapo kazi za uboreshaji zilianza mwezi Januari, 2024 na hadi kufikia Machi, 2026 utekelezaji wake umefikia asilimia 49. Ujenzi wa bandari hii ni wa kimkakati kwa ajili ya kuchochea ukuaji wa uchumi.

98. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza shehena zinazohudumiwa kwenda na kutoka nchi jirani kupitia bandari nchini, TPA imeendelea kutumia ofisi zake nane (8) zilizoko nje ya nchi kutafuta masoko kwa kujitangaza na kutafuta fursa zaidi za kibiashara kwa nchi jirani zinazotumia Bandari za Tanzania, zikiwemo nchi za Rwanda, Burundi, Uganda, Zambia, Malawi, DRC na Zimbabwe. Kutokana na jitihada hizo, shehena iliyosafirishwa kwenda nchi jirani katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 imeongezeka hadi kufikia tani milioni 10.93, ikilinganishwa na tani milioni 8.24 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2024/25, sawa na ongezeko la asilimia 32.64.

**Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi Katika Shughuli za Uendelezaji na Uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam**

99. ***Mheshimiwa Spika,*** kama inavyokumbukwa, mwaka 2023 Serikali ilichukua uamuzi mahsusi na wa kimkakati wa kushirikisha Sekta Binafsi katika shughuli za uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam. Kutokana na uamuzi huo, Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi iliingia mikataba na waendeshaji mahiri wa bandari duniani. Kufuatia utaratibu huo wa kushirikisha Sekta Binafsi, Serikali na Taifa kwa ujumla imeendelea kushuhudia manufaa mbalimbali katika Bandari ya Dar es Salaam na nchini kwa ujumla. Manufaa hayo ni pamoja na:-

i. Kuongezeka kwa shehena inayohudumiwa katika Bandari ya Dar es Salaam kutoka tani milioni 16.27 zilizohudumiwa kwa mwaka wa fedha 2020/21 hadi kufikia tani milioni 27.76 kwa

mwaka wa fedha 2024/25, sawa na ongezeko la asilimia 70.62. Hali hii imeendelea kuimarika ambapo, kwa kipindi kifupi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026 shehena iliyohudumiwa katika Bandari ya Dar es Salaam ilifikia tani milioni 25.07, ikilinganishwa na tani milioni 19.31 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2024/25, sawa na ongezeko la asilimia 29.83;

ii. Kuongezeka kwa wastani wa shehena ya makasha yanayohudumiwa kwa mwezi kutoka makasha TEUs 61,000 hadi TEUs 102,000, sawa na ongezeko la asilimia 67.21;

iii. Kuongezeka kwa mapato ya kodi ya forodha yanayokusanywa na TRA kutoka Shillingi trilioni 7.33 kwa mwaka wa fedha 2020/21 hadi kufikia Shilingi trilioni 12.31 kwa mwaka wa fedha 2024/25, sawa na ongezeko la asilimia 67.94. Mapato haya yanachangia wastani wa asilimia 40 ya mapato yote yanayokusanywa na TRA;

iv. Kupungua kwa gharama za uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam kutoka Shilingi bilioni 652.83 mwaka 2023/24 hadi kufikia Shilingi bilioni 308.95 kwa mwaka 2024/25 na hivyo kuiwezesha TPA kutumia rasilimali hiyo katika kuimarisha huduma mbalimbali na miradi mingine ya bandari;

v. Kuongezeka kwa makusanyo ya mapato ya TPA yatokanayo na ada za huduma za kibandari kutoka Shilingi bilioni 896.95 kwa mwaka 2020/21 hadi kufikia Shilingi trilioni 1.30 mwaka 2024/25. Hali hii imewezesha TPA kuendelea kutekeleza miradi mikubwa na ya kimkakati yenye thamani ya jumla ya Shilingi trilioni 2.25 kati ya miradi yenye thamani ya Shilingi trilioni 12.12 ambayo imepangwa kutekelezwa. Miradi inayoendelea kwa sasa ni pamoja na: Ujenzi wa matanki 15 ya kupokelea mafuta; Ujenzi wa magati mawili yenye urefu wa mita 500 katika Bandari ya Dar es Salaam; Ujenzi wa Bandari mpya ya Mbegani, Bagamoyo; Ujenzi wa Bandari mpya ya Mbamba Bay, Ziwa Nyasa; Maboresho na ujenzi wa Bandari za Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika; na Ujenzi wa Bandari mpya ya Kisiwa Mgao, Mtwara;

vi. Kupungua kwa muda wa kuhudumia meli za makasha gatini kutoka wastani wa siku 10 hadi siku 3; na

vii. Kupungua kwa muda wa kusubiri meli nangani kutoka wastani wa siku 46 hadi kufikia wastani wa siku saba (7) kwa meli za mizigo mchanganyiko na kichele.

100. ***Mheshimiwa Spika,*** ufanisi huo katika uendeshaji wa bandari umetokana na uwekezaji mkubwa uliofanyika katika ununuzi wa vifaa na mitambo ya uendeshaji, ikiwemo: mitambo 11 ya kushusha na kupakia makasha melini (Ship to Shore Gantry Crane - SSG) ambayo ina uwezo wa kupakua na kupakia makasha 72 kwa saa; mitambo 33 aina ya Rubber Tyred Gantry Crane – RTG kwa ajili ya kupanga mizigo bandarini; na *terminal tractors* 81 kwa ajili ya kuhamisha shehena. Uwepo wa mitambo hiyo umewezesha kuongezeka kwa shehena inayohudumiwa katika Bandari ya Dar es Salaam na itaongeza tani zaidi ya milioni 50.2 ya shehena itakayohudumiwa ifikapo mwaka 2030.

**Hatua za Serikali kutokana na ongezeko la shehena katika Bandari ya Dar es Salaam**

101. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na ongezeko la shehena katika Bandari ya Dar es Salaam, Serikali imeendelea kuchukua hatua madhubuti za kuendelea kuhudumia shehena inayoongezeka kwa kuboresha miundombinu ya Bandari ya Dar es Salaam ikiwemo: kuendelea kukamilisha ujenzi wa njia ya reli ya SGR kuingia Bandarini (port link); Kujenga eneo la kupakilia mizigo katika treni za SGR (Malindi Marshalling Yard).

102. ***Mheshimiwa Spika,*** hatua nyingine iliyochukuliwa ni kukamilisha ujenzi wa kituo cha mizigo Morogoro kitakachounganishwa na reli ya SGR katika eneo la Stesheni ya Morogoro. Kituo hicho kitakuwa na ukubwa wa mita za mraba 68,000 na kitakuwa na uwezo wa kuhudumia makasha 600 kwa siku. Kituo hicho pia kitatumika kuhudumia mizigo inayosafirishwa kupitia barabara kwenda maeneo mbalimbali ikijumuisha mikoa ya Iringa, Mbeya, Songwe, Ruvuma, Dodoma na nchi jirani za Zambia na Malawi. Uondoshaji wa mizigo katika eneo la Malindi

kupitia reli ya SGR na kufikishwa katika Kituo cha Mizigo Morogoro unatarajiwa kuanza mwezi Juni, 2026.

103. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na hatua hizo, Serikali kupitia TPA imeanza ujenzi wa magati mawili (2) katika eneo la Malindi, Bandari ya Dar es Salaam. Magati hayo yakikamilika yatakuwa na uwezo wa kuhudumia wastani wa tani za ziada milioni 3 za shehena kwa mwaka. Magati haya ni kati ya magati 10 ambayo ujenzi wake upo katika hatua za awali ili kuimarisha zaidi uwezo wa Bandari ya Dar es Salaam. Kati ya hayo, magati manne (4) yenye ukubwa wa mita za mraba 528,554, yatahusisha gati 12 hadi 15 katika eneo la Kitopeni – Kurasini.

104. ***Mheshimiwa Spika,*** magati mengine sita (6) kuanzia gati 16 hadi 21 yenye ukubwa wa mita za mraba 536,000 yatatekelezwa katika eneo la Vijibweni – Kigamboni. Kukamilika kwa ujenzi huu kutaiwezesha Bandari ya Dar es Salaam kuongeza idadi ya magati kutoka 12 yaliyopo kwa sasa hadi kufikia magati 22. Hatua hii ni sehemu ya mkakati wa Serikali ya Awamu ya Sita wa kuimarisha miundombinu ya bandari, kuongeza ufanisi wa huduma na kukuza nafasi ya Tanzania katika biashara ya kikanda na kimataifa.

105. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kupunguza msongamano wa makasha katika Bandari ya Dar es Salaam, Serikali inaendelea na upanuzi wa Eneo la Kurasini (Kurasini Port Extension) lenye ukubwa wa mita za mraba 220,000 kwa ajili ya kuhudumia makasha. Eneo hilo litakuwa na uwezo wa kuhudumia makasha 700,000 kwa mwaka. Awamu ya kwanza ya upanuzi wa sehemu ya eneo hilo ambayo ina uwezo wa kuhudumia makasha 150,000 imefikia asilimia 92 ya ukamilishaji. Aidha, awamu ya pili ya upanuzi wa eneo hilo inatarajiwa kuanza mwezi Juni, 2026. Ili kuwa na ufanisi katika usafirishaji wa makasha katika eneo la Kurasini, reli ya SGR itaunganishwa katika eneo hilo.

## Mikakati ya CCTTFA Kuhamasisha Nchi Jirani kutumia Bandari ya Dar es Salaam

106. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi imeendelea kushirikiana na Wakala wa Kuratibu Uwezeshaji wa Usafirishaji na Biashara katika Ukanda wa Kati (Central Corridor Transit Transport Facilitation Agency – CCTTFA), ambayo ni taasisi ya kikanda inayoratibu na kusimamia utekelezaji wa mikakati na programu za kuimarisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji, pamoja na kuwezesha biashara katika nchi saba (7) wanachama wa Ukanda wa Kati ambazo ni Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Malawi, Rwanda, Tanzania, Uganda na Zambia.

107. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuongeza ufanisi, ushindani na usalama wa mifumo ya usafirishaji, CCTTFA imeendelea kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya maboresho ya reli, bandari, barabara, usafiri wa majini na mifumo ya TEHAMA miongoni mwa nchi wanachama na kuchochea Diplomasia ya uchumi. Katika mwaka wa fedha 2025/26, CCTTFA imeendelea kuratibu utekelezaji wa miradi ya kimkakati, kuimarisha mazingira ya biashara, kujenga uwezo wa kitaalam na kusimamia utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya miundombinu katika Ukanda wa Kati.

108. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zilizotekelezwa kupitia uratibu wa CCTTFA ni pamoja na: Kuratibu Upembuzi Yakinifu wa ujenzi wa reli ya SGR kipande cha kutoka Musongati – Gitega – Kindu kinachounganisha Burundi na DRC; Kuwezesha ukarabati wa mabehewa 20 ya mizigo ya Reli ya Meter Gauge (MGR) inayosimamiwa na Shirika la Reli Tanzania (TRC); na Kuwajengea uwezo watalaam katika sekta ya usafiri majini kwa nchi za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Malawi, Rwanda, Tanzania, Uganda na Zambia. Kupitia zoezi hili, jumla ya wanafunzi 15 wamedahiliwa na wanaendelea na mafunzo katika Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI).

109. ***Mheshimiwa Spika,*** CCTTFA kwa kushirikiana na Wizara na Taasisi zake imeendelea kuratibu utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Miundombinu ya Usafiri katika Ukanda wa Ziwa

Tanganyika kutokana na Hati ya Makubaliano (MoU) kati ya Tanzania na DRC iliyosainiwa mwezi Julai, 2022 Kalemie nchini DRC. Makubaliano hayo yamechochea utekelezaji wa miradi ya kipaumbele katika sekta za barabara, reli, bandari na usafiri majini katika Ziwa Tanganyika.

110. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia uratibu huu, mafanikio yaliyopatikana katika nchi hizo ni pamoja na: Ujenzi wa Bandari ya Kalemie; Ukarabati wa Bandari ya Kigoma; na Ubadilishanaji wa hekta 60 za ardhi kwa ajili ya kuanzisha bandari kavu (dry ports) katika nchi za Tanzania na DRC. Aidha, CCTTFA imeendelea kuratibu tafiti za bandari kavu kwa nchi wanachama. Ujenzi wa bandari kavu unatarajiwa kuongeza uwezo wa kuhifadhi na kusafirisha mizigo kwa ufanisi zaidi.

## HUDUMA ZA USAFIRI WA RELI

### Huduma za Usafiri kupitia Reli za MGR na SGR

111. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaishukuru Serikali kwa kuchukua hatua za kuboresha Shirika la Reli Tanzania (TRC), zoezi lililoanza mwaka 2017. Miongoni mwa tunu na suala la kihistoria kwa Serikali ya Awamu ya Sita katika Shirika hili ni kuendeleza ujenzi wa mtandao wa reli ya SGR, rasilimali ambayo nchi nyingi zinatamani kuwa nayo. Tangu kuanzishwa kwa Shirika hili, Serikali imekuwa ikitoa ruzuku ya mishahara. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, katika mwaka 2026/27, TRC haitatengewa tena ruzuku kwa ajili ya mishahara kutoka Serikalini.

112. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita kupitia Shirika la Reli Tanzania (TRC), imeendelea na ujenzi na uendeshaji wa reli mpya ya Standard Gauge Railway (SGR) pamoja na kuboresha mtandao wa reli ya Meter Gauge Railway (MGR) yenye urefu wa takriban kilomita 2,707. Ujenzi wa reli ya SGR unatekelezwa kwa awamu mbili ikihusisha kilomita 1,219 za njia kuu kwa awamu ya kwanza kutoka Dar es Salaam – Mwanza; na kilomita 1,590 za awamu ya pili ikijumuisha vipande vya Tabora – Kigoma na Uvinza – Musongati.

113. ***Mheshimiwa Spika,*** kukamilika kwa awamu hizo mbili za reli ya SGR kutaifanya Tanzania kuwa na mtandao wa jumla ya kilomita 2,809 za reli ya kisasa ya SGR. Vilevile, Serikali inaendelea na juhudi za kuongeza mtandao wa reli ya SGR katika maeneo mengine ya kaskazini na kusini mwa nchi, ikiwa ni mkakati mahsusi wa kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha usafirishaji kikanda.

**Uendelezaji na uendeshaji wa Reli ya Kisasa ya SGR**

114. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TRC imeendelea na ujenzi wa Reli ya SGR ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2026 ujenzi wa kipande cha kwanza Dar es Salam – Morogoro (km 300) na kipande cha pili Morogoro – Makutupora (km 422) umekamilika kwa sehemu kubwa. Kazi zilizopo katika hatua za mwisho za ukamilishwaji ni: ujenzi wa njia kuingia bandarini (port link); Ujenzi wa vivuko vya juu vya kipande cha pili; Ujenzi wa stesheni katika kipande cha pili; na Ujenzi wa uzio. Aidha, TRC inaendelea na utoaji wa huduma ya usafiri wa treni kwa vipande husika.

115. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa Standard Gauge Railway (SGR) nchini katika kipande cha tatu na nne unaendelea ambapo katika kipande cha Makutupora – Tabora (km 368), kazi zinazoendelea ni Usanifu wa Kina, ujenzi wa tuta, madaraja, makalavati na utwaaji wa ardhi; na kipande cha Tabora – Isaka (km 165) kazi zinazoendelea ni pamoja na Usanifu wa Kina, utafiti wa udongo na miamba, ujenzi wa tuta, makalavati, utwaaji wa ardhi na uletwaji wa vifaa. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa vipande hivi vinakamilika kwa wakati na kuanza kutoa huduma. Kwa upande wa kipande cha Mwanza – Isaka (km 341), ujenzi umefikia asilimia 68.77 na kazi zinazoendelea ni Usanifu wa Kina, ujenzi wa tuta, majengo ya stesheni, madaraja, vivuko vya binadamu na wanyama, utandikaji wa reli, mifumo ya mawasiliano na umeme, pamoja na utwaaji wa ardhi.

116. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa ujumla ujenzi wa kipande cha tatu na cha nne katika mradi huu vimekuwa na changamoto kwa muda mrefu, ambazo zilisababisha utekelezaji wake kuwa na kasi ndogo. Katika mkakati wa Serikali kuendelea na utekelezaji wa

ujenzi wa Reli ya SGR, Serikali tayari imefanikiwa kupata mkopo wenye masharti nafuu wenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 1.277, sawa takriban Shilingi trilioni 3.32.

117. ***Mheshimiwa Spika,*** Mkataba huo ulisainiwa tarehe 28 Aprili, 2026 Jijini Dodoma kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa kipande cha tatu (3) na cha nne (4) cha mradi huo, ambavyo ni kutoka Makutupora hadi Tabora kilomita 368 na kutoka Tabora hadi Isaka kilomita 165 na hivyo kufanya jumla ya kilomita 533. Makubaliano haya yanaendelea kuonesha imani kubwa ya wawekezaji na Taasisi za kifedha za kimataifa kwa Tanzania katika juhudi zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita kuboresha miundombinu ya usafiri na usafirishaji na kuchochea ukuaji wa uchumi wa Taifa na maendeleo ya wananchi kwa ujumla.

118. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa lengo la kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, Serikali imeendelea kupanua masoko ya nje kwa kuunganisha reli ya SGR na nchi jirani, hususan Burundi na DRC. TRC imeendelea na ujenzi wa reli kwa awamu ya pili, ambapo ujenzi wa reli ya SGR kutoka Tabora – Kigoma (Km 506) unaendelea na umefikia asilimia 9.59. Kazi zinazoendelea ni: Ujenzi wa tuta; Ujenzi wa vivuko; Ujenzi wa daraja la Malagarasi; na Usanifu.

119. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kwa upande mwingine inaendelea na ujenzi wa Reli ya SGR kutoka Uvinza - Musongati (km 300), ambapo maandalizi ya awali ya utekelezaji wa mradi yanaendelea ikiwemo usanifu na uletwaji wa vifaa, mitambo na wataalam. Hivyo, kukamilika kwa ujenzi wa reli hizi kutafungua nchi ya Tanzania kikanda kwa kuunganisha Bandari ya Dar es Salaam na nchi za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na kurahisisha usafirishaji wa shehena na biashara kati ya Tanzania na nchi hizo.

120. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hayo, ili kuhakikisha Sekta ndogo ya reli inaendelea kuchochea uchumi wa nchi kwa kujikita zaidi katika kutumia nishati safi ya umeme na kupunguza athari zinazotokana na matumizi ya mafuta, Serikali imeendelea

kutafuta fedha kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo, ikiwemo Sekta Binafsi. Miradi inayotafutiwa fedha ni Ujenzi wa reli ya SGR kutoka: Kaliua – Mpanda – Karema (km 321); Mtwara – Mbambabay na matawi yake ya Liganga na Mchuchuma (km 1,000); Tanga – Arusha – Musoma (km 1,028); Reli ya mjini katika Jiji la Dar es Salaam (km 166); na Reli ya mjini katika Jiji la Dodoma (km 107).

121. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na juhudi zinazotekelezwa, wapo wadau ambao wameonesha nia ya kuingia ubia na Serikali katika utekelezaji wa miradi hiyo. Kwa ujumla, kutekelezwa kwa miradi husika kutawezesha kuundwa kwa mtandao wa reli ya SGR unaounganisha miji mikuu na nchi jirani na kuimarisha uchumi wa Tanzania kwa kurahisisha usafirishaji wa mizigo na abiria.

**Usafirishaji wa Abiria na Mizigo kwa Reli za SGR na MGR**

122. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TRC imeendelea na uendeshaji wa reli ya SGR katika usafirishaji wa abiria kati ya Dar es Salaam na Dodoma. Usafirishaji kupitia reli hiyo umezidi kuimarika ambapo katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya abiria 2,515,203 walisafirishwa ikilinganishwa na abiria 2,054,828 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2024/25 sawa na ongezeko la asilimia 22.40. Takwimu zinaonesha kuwa, tangu kuanza kwa uendeshaji mwezi Juni, 2024 abiria waliosafirishwa hadi mwezi Machi, 2026 imefikia 5,512,995. Ongezeko hili limechangiwa na huduma bora na ya uhakika inayotolewa.

123. ***Mheshimiwa Spika,*** usafirishaji huu umeendelea kuchochea biashara na shughuli mbalimbali za kiuchumi kwa kupunguza muda wa safari. Kwa mwenendo huu, inakadiriwa kwamba hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2025/26, zaidi ya abiria milioni 3 watakuwa wamesafirishwa kwa mwaka. Aidha, katika kuongeza ufanisi na kuendelea kuwarahisishia usafiri wananchi, TRC imeongeza safari mbili (2) kati ya Dar es Salaam na Morogoro kuanzia tarehe 18 Aprili, 2026 na hivyo kufanya safari

kati ya mikoa hiyo kuwa safari sita (6) kutoka safari nne (4) kwa siku.

124. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na ufanisi huo, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Machi 2026, jumla ya Shilingi bilioni 82.77 zimekusanywa kutokana na usafirishaji wa abiria kati ya Dar es Salaam na Dodoma. Takwimu zilizopo pia zinaonesha kuwa, Serikali imekusanya jumla ya Shilingi bilioni 169.37 tangu kuanza kwa safari za SGR nchini mwezi Juni, 2024.

125. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi kufikia mwezi Machi 2026, TRC ilisafirisha jumla ya tani 102,452 za mizigo ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Serikali ya kuanza usafirishaji wa mizigo kupitia reli ya SGR. Kwa sasa, kampuni mbalimbali zinaendelea kujitokeza kusafirisha mizigo yao kupitia reli hiyo ikiwemo Kampuni ya Dangote ambayo inasafirisha saruji. Vilevile, TRC imeendelea kubuni na kutekeleza mikakati ya kuongeza upatikanaji wa mizigo ndani ya nchi kwa kuhamasisha Shoroba za Kiuchumi kandokando na sehemu zinazofikika na huduma za miundombinu ya Usafirishaji.

126. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua ya kuendelea kupunguza msongamano wa shehena katika Bandari ya Dar es Salaam, Serikali imeendelea kuhimiza matumizi ya bandari Kavu mbalimbali nchini, zikiwemo Ihumwa (Dodoma) na Isaka (Shinyanga). Katika kutekeleza azma hiyo, mwezi Machi, 2026 TRC imeanza usafirishaji wa shehena kwenda katika Bandari Kavu ya Isaka. Sambamba na hilo, TRC imeendelea kuhakikisha upatikanaji wa mizigo kupitia Reli ya SGR kwa kuunganisha miundombinu ya reli ya SGR na MGR. Hatua hiyo inajumuisha ujenzi wa kuunganisha miundombinu ya reli za MGR na SGR katika eneo la Ruvu ili kuwezesha usafirishaji wa mizigo kutoka Bandari za Dar es Salaam na Tanga, ambapo utekelezaji wake umefika asilimia 85.

127. ***Mheshimiwa Spika,*** TRC pia inaendelea na ujenzi wa kuunganisha reli za MGR na SGR katika eneo la Bahi kwa lengo la kuwezesha uhamishaji wa mizigo (*transhipment*) kati ya reli hizo ili iweze kusafirishwa kuelekea maeneo mbalimbali yakiwemo ya

Isaka, Mwanza, Kigoma pamoja na nchi jirani. Huu ni mkakati wa muda mfupi wa usafirishaji wa mizigo kwa SGR wakati utekelezaji wa ujenzi wa vipande vingine ukiendelea.

128. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na kuendelea na ujenzi wa reli ya SGR nchini, Serikali pia imeendelea na uboreshaji wa Reli ya MGR kwa kuondoa reli nyepesi za ratili 45 na kutandika reli nzito za ratili 80, sambamba na kuongeza uwezo wa madaraja kutoka tani 13.5 hadi 18.5 kwa ekseli. Aidha, ukarabati umeendelea kufanyika katika maeneo mbalimbali ya reli hiyo kupitia fedha zinazotengwa katika Mfuko wa Reli, ambapo hadi kufikia Machi, 2026 ukarabati wa njia ya reli ya MGR ya Kaliua – Mpanda (Km 210) umefikia asilimia 32.72. Kazi zinazoendelea ni pamoja na: Usanifu wa njia na madaraja; Ukarabati wa stesheni za Mpanda, Uyumbu, Kaliua na Katumba; Ujenzi wa kiwanda cha mataruma; Utengenezaji wa makalavati; Usanifu wa njia na mifumo ya maji; Uwekaji wa mitambo ya kuvunja mawe katika machimbo ya kokoto ya Tumbi (Tumbi Quarry); na Uletwaji wa vifaa mbalimbali.

129. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na ukarabati wa reli ya MGR, Serikali imeendelea na juhudi za kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi vya reli ya MGR kwa kuchukua hatua mbalimbali katika kuhakikisha kuwa reli hiyo inafanya kazi kwa ufanisi. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na: kuendelea na ukarabati wa vichwa vitano (5) vya njia kuu katika karakana ya Morogoro na ambao hadi Machi, 2026 umefikia asilimia 17 na ukarabati huo unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba 2026; kuendelea na ukarabati wa mabehewa katika karakana ya Dar es Salaam, ambapo hadi kufikia Machi 2026, mabehewa ya abiria 37 na ya mizigo 369 yamekamilika na yanafanya kazi; Ununuzi wa mabehewa 100 mapya ya mizigo; Uundwaji wa vichwa nane (8), ambapo vichwa viwili (2) tayari vimewasili nchini; na Uundwaji wa vichwa sita (6) unaendelea na hadi kufikia Machi, 2026 kazi imefikia asilimia 88. Kutekelezwa kwa hatua hizi kumeongeza uwezo wa TRC kuhudumia abiria na mizigo ikiwemo usafirishaji wa makasha kutoka Bandari ya Dar es Salaam kwenda Bandari Kavu ya Kwala na maeneo mengine.

130. ***Mheshimiwa Spika,*** TRC imefanikiwa kuongeza mizigo inayosafirishwa kupitia reli ya MGR, ambapo hadi kufikia Machi 2026, jumla ya tani 203,920 za mizigo zilisafirishwa ikilinganishwa na tani 183,048 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2024/25 sawa na ongezeko la asilimia 11.40. Kwa upande wa usafirishaji wa abiria wa masafa marefu kupitia reli ya MGR, hadi kufikia Machi 2026, jumla ya abiria 300,858 walisafirishwa. Dhamira ya Serikali ni kuendelea kuimarisha reli ya MGR ili iendelee kuwezesha usafiri na usafirishaji katika maeneo yanayopitiwa na miundombinu ya reli hiyo.

131. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia changamoto za mafuriko ya mara kwa mara zinazoathiri reli ya MGR katika maeneo ya Kilosa – Kidete – Igandu, Wizara imeendelea kuchukua hatua madhubuti za kukarabati miundombinu katika maeneo yaliyoathirika. Katika jitihada za kukabiliana na hali hiyo, Wizara imeendelea kutekeleza kazi za dharura, za muda mfupi na muda mrefu ikiwa ni pamoja na: Ujenzi wa njia ya reli yenye urefu wa kilomita 6.2 na daraja katika eneo la Godegode – Gulwe, ambapo ujenzi umefikia asilimia 99 na uendeshaji katika eneo hili unaendelea; Kuimarisha tuta la reli; Kujenga mifereji ya kupitisha maji kwa viwango vinavyokidhi mahitaji ya sasa; na Kuweka miundombinu imara zaidi inayoweza kustahimili majanga ya asili.

132. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kupata suluhisho la kudumu kuhusu changamoto ya mafuriko katika maeneo husika, Wizara ya Uchukuzi kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo pamoja na wadau wengine, wakiwemo Wizara ya Maji na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, kupitia Mradi wa Uboreshaji wa Reli ya Kati (TIRP II), zinaendelea na maandalizi ya ujenzi na ukarabati wa mabwawa sita (6) yaliyopo katika eneo la kidakio la Mto Kinyasungwe kwenye mikoa ya Morogoro na Dodoma. Mabwawa yatakayojengwa ni pamoja na Kidete, Kimagai, Buigiri, Ikowa, Hombolo na Dabalo.

133. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi na Wizara ya Maji pia inakusudia kujenga mabwawa mengine mawili, yaani bwawa la Lumuma (Wilaya ya Kilosa, Mkoa wa Morogoro) na bwawa la Mzase (Wilaya ya Mpwapwa, Mkoa wa

Dodoma), na hivyo kufanya jumla ya mabwawa nane (8). Mabwawa haya yatawezesha uhifadhi wa maji na kupunguza athari za mafuriko kwenye miundombinu ya reli, huku yakichangia utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi kama vile kilimo, umwagiliaji na ufugaji. Juhudi hizi zinalenga kuhakikisha kuwa reli ya MGR inaendelea kuwa salama, imara na ya kuaminika kwa usafirishaji wa abiria na mizigo.

**Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi katika matengenezo na utoaji wa huduma za usafirishaji kwa njia ya reli nchini**

134. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa lengo la kuimarisha ushiriki wa Sekta Binafsi na kuongeza ufanisi katika uendelezaji na uboreshaji wa reli nchini, Serikali kupitia TRC imeingia Mkataba na kampuni binafsi kwa ajili ya kufanya matengenezo ya njia za reli za MGR (outsource maintanance) ikiwemo Reli ya Tanga – Arusha, Ruvu – Mruazi *Junction* na Dar es Salaam – Morogoro. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa makalavati; Kushindilia kokoto kwenye reli; Kusafisha njia ya reli pamoja na kuweka mirefeji ya maji. Vilevile, TRC imeingia Mkataba na Kampuni binafsi kwa ajili ya ufufuaji wa vichwa vitano (5) vya njia kuu ambao unaendelea na ukarabati wa vichwa vinne (4) vya Sogeza upo katika maandalizi ya awali.

135. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia imeendelea kuhamasisha Sekta Binafsi kutumia njia ya reli kutoa huduma ya usafiri na usafirishaji kwa kutumia vichwa vya treni na mabehewa yao (open access). Hatua hii inalenga kuongeza ufanisi wa Reli ya MGR na SGR, ambapo kampuni mbalimbali zimeanza kujitokeza na maandalizi ya awali ya uendeshaji ikiwemo kuingia mikataba yanaendelea.

136. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na hayo, kazi nyingine zilizotekelezwa na TRC hadi kufikia Machi 2026, ni pamoja na: Kuendelea na uboreshaji wa mifumo ya ishara, mawasiliano na umeme katika njia ya reli ya MGR; Kuendelea na uboreshaji wa mifumo ya TEHAMA ikiwemo ufungaji wa kamera za CCTV kwa ajili ya ulinzi na usalama katika maeneo ya stesheni; na Mfumo wa kielektroniki wa ukataji tiketi (e-ticketing).

## Huduma za Usafiri kupitia Reli ya TAZARA

137. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Tanzania na Zambia zimeendelea kushirikiana katika kusafirisha mizigo na abiria kwa kutumia Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) ambayo inamilikiwa kwa uwiano sawa wa hisa za asilimia 50 kwa 50 kati ya Tanzania na Zambia. Reli hiyo ina urefu wa jumla ya kilomita 2,153 kuanzia Dar es Salaam, Tanzania hadi New Kapiri Mposhi, Zambia zikijumuisha kilomita 1,860 za njia kuu na kilomita 293 za njia ya reli zilizoko stesheni na zile za michepuko ya reli. TAZARA imeendelea kutoa huduma za usafiri na usafirishaji kati ya nchi wanahisa na nchi nyingine za SADC.

138. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TAZARA imeendelea kutoa huduma ya usafirishaji wa mizigo na abiria, ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2026, jumla ya tani 157,377 zilisafirishwa kupitia reli ya TAZARA. Kati ya hizo, tani 52,991 zilisafirishwa na TAZARA na tani 104,386 zilisafirishwa na kampuni binafsi zilizoingia mikataba ya kusafirisha mizigo kwa kutumia reli hiyo. Reli hii kutokana na usanifu wake ina uwezo wa kusafirisha tani milioni 5 kwa mwaka.

139. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa abiria waliosafirishwa kupitia reli ya TAZARA hadi kufikia Machi 2026, treni za abiria zinazofanya safari kati ya Dar es Salaam na New Kapiri Mposhi, zilisafirisha jumla ya abiria 216,018 ikilinganishwa na abiria 416,768 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2024/25. Vilevile, Treni ya Udzungwa inayosafiri kati ya stesheni za Kidatu na Makambako ilisafirisha jumla ya abiria 80,564 ikilinganishwa na abiria 162,936 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2024/25. Ufanisi mdogo wa reli ya TAZARA umesababisha kupungua kwa mizigo na abiria kutokana na uchakavu wa miundombinu na uhaba wa vitendea kazi vikiwemo vichwa vya treni, mabehewa na vipuri.

140. ***Mheshimiwa Spika,*** utakumbuka kuwa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika Hotuba yake wakati wa kufungua Rasmi Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dodoma, tarehe 14 Novemba 2025, alilitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali yake

kwa kushirikiana na nchi mwanahisa imeanza mkakati mahsusi wa kufanya maboresho makubwa ya reli ya TAZARA.

141. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kulitaarifu Bunge lako kuwa, uzinduzi wa mradi wa ufufuaji wa reli ya TAZARA ulifanyika tarehe 20 Novemba, 2025 jijini Lusaka nchini Zambia. Uzinduzi huo ulifanyika kufuatia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Zambia mnamo tarehe 29 Septemba, 2025 kusaini mkataba wa uendeshaji (Concession agreement) na Kampuni ya CCECC kutoka nchini China kwa ajili ya kuboresha reli ya TAZARA. Kampuni hii itawekeza jumla ya Dola za Marekani bilioni 1.4, ambayo ni sawa na takriban Shilingi trilioni 3.6. Kwa sasa kampuni hiyo imeanza utekelezaji wa awali ikiwemo kufanya upimaji na usanifu wa miundombinu ya reli ili kuanza ukarabati wa njia.

142. ***Mheshimiwa Spika***, maboresho hayo ya reli ya TAZARA yametokana na ubunifu wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambapo katika kipindi cha uongozi wake ameendelea kuiwezesha Sekta ya Uchukuzi kuendelea kutoa mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa Taifa. Ubunifu wake umewezesha kuanza kwa ukarabati wa reli hiyo. Uboreshaji wa reli hii unaenda sambamba na maono ya Serikali ya Awamu ya Sita, ambayo ni kuhakikisha kuwa Serikali inatoa kipaumbele kwa miradi ya ujenzi wa reli zinazofungua nchi kwa ajili ya biashara ili kutumia vizuri fursa ya kijiografia tuliyonayo.

143. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na manufaa mengine, utekelezaji huu wa kimkakati unatarajiwa kuleta mageuzi makubwa katika utendaji wa TAZARA kwa kuongeza uwezo wa kusafirisha mizigo kutoka wastani wa chini ya tani 150,000 ya sasa kwa mwaka hadi kufikia tani milioni 2.4 kwa mwaka wa tatu wa uendeshaji baada ya kukamilika kwa matengenezo makubwa ya miundombinu, ununuzi wa vichwa vya treni pamoja na mabehewa ya kisasa yenye ufanisi zaidi. Maboresho haya yanatarajiwa pia kuzalisha ajira mpya 20,000 za moja kwa moja na ajira 80,000 zisizo za moja kwa moja. Hatua hii itaimarisha usafirishaji wa shehena kupitia bandari ya Dar es Salaam kwenda

na kutoka nchi jirani zikiwemo Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) na kuimarisha usafirishaji wa bidhaa za ndani (local traffic).

144. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba niwataarifu Watanzania wenzangu kuwa, makubaliano haya yamefikiwa ndani ya kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya kutokamilika kwa takriban miaka 20 iliyopita. Hatua hii ni kubwa na ya kihistoria kwa kuwa itawezesha nchi yetu kuendelea kutumia reli zetu kuimarisha huduma na kuinua maisha ya Watanzania kwa ujumla. Wizara itaendelea kusimamia mikataba hii ili iweze kutekelezwa kwa wakati na weledi ili kufikia malengo yaliyokusudiwa na hasa uondoshaji wa shehena katika Bandari ya Dar es Salaam.

145. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuona fursa zitakazopatikana baada ya maboresho haya, Serikali imepokea maombi kutoka Serikali ya Malawi kujenga reli ya kuunganisha na reli ya TAZARA katika Mkoa wa Mbeya au Songwe. Aidha, Serikali ya DRC imeomba kuitumia reli ya TAZARA kwa kuunganisha mtandao wa reli wa Zambia. Mfumo wa reli za DRC unaingiliana na reli ya TAZARA (Cape Gauge). Zipo faida nyingi za kuunganisha reli hiyo kutokana na nchi ya DRC kuwa na mizigo mingi ikiwemo madini.

## HUDUMA ZA UCHUKUZI KATIKA BAHARI NA MAZIWA MAKUU

### Huduma za Usafirishaji katika Bahari

146. ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya Meli ya Serikali ya China na Tanzania (SINOTASHIP) ambayo inamilikiwa kwa uwiano sawa wa nchi hizo mbili (2) imeendelea kutoa huduma za usafirishaji wa mizigo katika masafa marefu kwa njia ya bahari. Aidha, SINOTASHIP imeendelea kutoa huduma za uwakala wa meli kwa washirika wake ambao ni COSCO Shipping Company Limited na Oriental Overseas Container Line katika Bandari ya Dar es Salaam. Kampuni hii imeendelea kuimarisha huduma za

usafirishaji wa baharini na kuongeza ufanisi katika kukuza biashara ya kimataifa.

147. ***Mheshimiwa Spika,*** ndani ya kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita, SINOTASHIP kwa kushirikiana na COSCO Shipping Group imeongeza njia za meli (shipping routes) kutoka tatu (3) hadi kufikia tano (5). Aidha, katika kipindi cha mwaka 2025, Meli ya MV. Changshun II ya SINOTASHIP ilisafirisha shehena jumla ya tani 621,528 ikilinganishwa na tani 615,375 zilizosafirishwa kwa mwaka 2024. Ongezeko hili la tani 6,153 lilitokana na meli kufanya kazi kwa ufanisi baada ya kufanyiwa matengenezo makubwa mwaka 2024.

148. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza mapato ya Kampuni yatokanayo na huduma za uwakala, kwa mwaka 2025, SINOTASHIP ilihudumia jumla ya makasha 84,500 katika Bandari ya Dar es Salaam ikilinganishwa na makasha 81,993 yaliyohudumiwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la makasha 2,507. Ongezeko hilo linatokana na kukua kwa biashara ya uwakala na uwepo wa ongezeko kubwa la meli zinazoleta na kuondosha shehena katika Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara.

**Huduma za Usafiri na Usafirishaji katika Maziwa Makuu**

149. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuchochea usafirishaji wa shehena kufikia masoko ndani ya nchi na nchi jirani zilizopo katika Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa, Serikali kupitia Kampuni ya Meli Tanzania (TASHICO) inaendelea na ujenzi na ukarabati wa meli ili kuboresha huduma za usafiri na usafirishaji wa abiria na mizigo.

150. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TASHICO, imeendelea kutoa huduma za usafirishaji wa abiria na mizigo katika Maziwa Makuu, lengo likiwa ni kuendelea kuwawezesha wananchi wanaoishi katika maeneo hayo kuendelea na shughuli zao za kiuchumi na kijamii. Kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 TASHICO ilisafirisha abiria 128,191. Aidha, katika kipindi hicho, TASHICO ilisafirisha tani 71,796.25 za mizigo ikilinganishwa na tani 58,605.78 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa

fedha 2024/25, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 22.51. Ongezeko hilo la mizigo limetokana na kuanza kutoa huduma kwa meli ya MT. Sangara katika ziwa Tanganyika baada ya ukarabati wa meli hiyo kukamilika.

151. ***Mheshimiwa Spika,*** Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 inatambua umuhimu wa meli katika kuchochea ukuaji wa uchumi, kuifungua nchi na kuimarisha huduma za usafiri kwa wananchi. Katika kipindi hiki, Serikali kupitia TASHICO imeendelea kusimamia ujenzi wa meli mpya na ukarabati wa meli zilizopo ili kuimarisha usafiri wa abiria na usafirishaji wa mizigo. Katika hatua hizo, Serikali imekamillisha ujenzi wa Meli ya MV. New Mwanza katika Ziwa Victoria, ambayo tayari imeanza kutoa huduma kati ya Bandari ya Mwanza na Bukoba.

152. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia imeendelea na ukarabati wa meli katika Ziwa Victoria, ambapo ukarabati wa meli ya uokozi ya MT. Ukerewe umefikia asilimia 79 kutoka asilimia 17 iliyokuwa imefikiwa mwezi Machi, 2025. Vilevile, Serikali kupitia TASHICO inaendelea na maandalizi ya ukarabati wa meli ya MT. Nyangumi yenye uwezo wa kusafirisha shehena ya mafuta ya lita 410,000; ukarabati wa meli ya MV. Clarias yenye uwezo wa kubeba abiria 216 na mzigo tani 10; na kuanza maandalizi ya ujenzi wa meli yenye uwezo wa kubeba tani 3,000 za mizigo katika ziwa hilo.

**Mikakati ya Serikali ya Awamu ya Sita Kutumia Fursa zilizopo ukanda wa Ziwa Tanganyika**

153. ***Mheshimiwa Spika,*** Ziwa Tanganyika limejaliwa kuunganisha nchi nne (4) za Tanzania, Burundi, Zambia na DRC zenye uchumi mkubwa wa jumla ya Pato la Taifa (GDP) linalokadiriwa kufikia Dola za Marekani bilioni 178 kwa mwaka na kuwa na idadi ya watu takriban milioni 213. Ziwa hili linazungukwa na ukanda muhimu wenye shughuli mbalimbali ikiwemo uchimbaji madini ya kimkakati yanayopatikana katika nchi hizo. Ziwa Tanganyika ni la kwanza barani Afrika na la pili duniani kwa kina kirefu. Aidha, Ziwa hili ni la pili barani Afrika kwa ukubwa na ni

eneo pekee kwa umuhimu (hotspot area) kijiografia na hivyo kulifanya kuwa lango kuu la biashara kwa nchi za Burundi kupitia bandari ya Bujumbura, DRC kupitia bandari ya Kalemie na Moba; Zambia kupitia bandari ya Mpulungu.

154. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na sifa hizo, pia ukanda huo wa Ziwa Tanganyika unaongoza kwa utajiri wa madini adhimu (Critical Minerals) duniani ukiunganisha ukanda wa Shaba wa DRC, Zambia na Burundi. Kwa sasa Dunia inaelekea kwenye matumizi ya madini hayo kwa ajili ya Teknolojia ya Betri inayotumika katika magari ya umeme na treni za umeme. Tathmini zinaonyesha kwamba, nchi zenye utajiri wa madini hayo zitaongoza kwa uchumi na zitachukua nafasi ya nchi zenye mafuta.

155. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa Tanzania, kuna bandari kubwa ya Kigoma ambayo kwa zaidi ya miaka 100 imekuwa ni kiunganishi kikubwa kwa nchi zisizo na bahari kupitia mlango wa bahari. Dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kufungua uchumi wa Tanzania kwa kuimarisha nafasi ya Tanzania kama lango kuu la biashara kwa upande mmoja, lakini kama kitovu cha biashara na uchumi kwa kutumia fursa ya kijiografia na mikakati ya kupanua zaidi masoko kupitia Ziwa Tanganyika.

156. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na umuhimu wa ukanda wa Ziwa Tanganyika, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo:

i. Kufufua meli ya MT. Sangara, ambapo imefanyiwa ukarabati mkubwa na kwa sasa imekamilika na inaendelea kutoa huduma za usafirishaji wa shehena ya mafuta kati ya Bandari za Kigoma na Bandari za Kalemie na Uvira zilizopo DRC;

ii. Ujenzi wa meli nne (4) za mizigo katika Ziwa Tanganyika zinazojengwa na TPA kwa kushirikiana na Sekta Binafsi ambazo zina uwezo wa kubeba tani 2,000 za mizigo kila moja na zinatarajiwa kuboresha ufanisi wa usafirishaji na

kuchochea biashara. Meli hizo kwa sasa zimekamilika na ziko katika hatua za majaribio ya mwisho;

iii. Kukamilisha ujenzi wa Bandari ya Karema ambayo kwa sasa inaendelea kutoa huduma;

iv. Kuanza ujenzi wa magati mawili (2) ya kisasa katika Bandari ya Kigoma, ambapo gati moja ni kwa ajili ya kuhudumia abiria ambalo hadi Machi, 2026 utekelezaji wake umefikia asilimia 13; na gati la mizigo liko katika hatua za awali za kuanza ujenzi;

v. Kuendelea na uboreshaji katika Bandari ya Kasanga;

vi. Kuanza kwa maboresho ya Bandari ya Kalemie nchini DRC kutokana na makubaliano ya kuboresha miundombinu ya kuchochea biashara kati ya Tanzania na nchi hiyo. Makubaliano hayo yalifanyika mwaka 2022 na yalilenga kuboresha miundombinu ya reli, bandari, barabara, meli na viwanja vya ndege;

vii. Kuanza ukarabati wa reli ya MGR inayounganisha Bandari ya Kigoma na Bandari kavu ya Katosho, ikiwa ni hatua za kuongeza ufanisi wa uondoshaji wa mizigo katika Bandari ya Kigoma;

viii. Kukamilika kwa Upembuzi Yakinifu na kuanza ujenzi wa reli ya SGR kati ya Uvinza – Musongati (km 300) pamoja na kuendelea kukamilisha Upembuzi Yakinifu wa ujenzi wa reli ya SGR kutoka Gitega – Bujumbura – Uvira – Kindu (km 820) kwa ajili ya kuunganisha nchi za Tanzania, Burundi na DRC kibiashara;

ix. Kuendelea na maboresho ya Kiwanja cha Ndege cha Kigoma kufikia daraja la 3C, ambacho kitakuwa na uwezo wa kupokea ndege kutoka nchi jirani;

x. Kuendeleza majadiliano kati ya Tanzania, DRC na Burundi, ambayo yameendelea kuleta manufaa mbalimbali kutokana

na mijadala inayofanyika kuhusu changamoto zilizopo na mikakati ya kuzitatua. Kongamano la hivi karibuni lilifanyika tarehe 15 – 16 Aprili, 2026 na kushirikisha zaidi ya washiriki 350. Mgeni rasmi katika kongamano hilo alikuwa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye pia alizihakikishia nchi zilizoshiriki kuwa zitaendelea kupata ushirikiano stahiki kutoka Tanzania;

xi. Kuendelea na ukarabati wa meli ya MV. Liemba yenye uwezo wa kusafirisha abiria 600 na tani 200 za mizigo ambao umefikia asilimia 64; na ukarabati wa meli ya MV. Mwongozo tayari mkataba umesainiwa na maandalizi ya kuanza ukarabati yanaendelea;

xii. Kuanza maandalizi ya ujenzi wa meli mpya yenye uwezo wa kubeba abiria 600 na tani 400 za mizigo, ambapo tayari malipo ya awali (Advance Payment) yamefanyika na hatua za utekelezaji zinaendelea;

xiii. Kuendelea na ujenzi wa kiwanda cha kujengea meli chenye uwezo wa kubeba meli yenye uzito wa tani 5,000, ambapo tayari mkandarasi amelipwa sehemu ya malipo ya awali (Advance Payment) na mradi upo katika hatua za awali za maandalizi (mobilization). Ujenzi wa kiwanda hiki utachochea ajira nchini na kuzivutia nchi jirani za Maziwa Makuu kujenga meli zao nchini na kuweka historia ya kuwa na kiwanda kama hicho hapa nchini; na

xiv. Kuwekeza zaidi ya Dola za Marekani milioni 68 kwa ajili ya ujenzi wa kivuko cha treni za kisasa (Wagon Ferry) katika Ziwa Tanganyika. Kivuko hiki kitakuwa na uwezo wa kuvusha treni za SGR kutoka Bandari ya Kigoma hadi Bandari ya Kalemie (DRC), Bandari ya Bujumbura (Burundi) na Bandari ya Mpulungu (Zambia). Vilevile, kivuko hiki kitabeba treni ya Cape Gauge kutoka Bandari ya Kigoma hadi Bandari ya Kalemie (DRC), ambapo kuna treni ya kutoka Bandari ya Kalemie hadi Kindu (km 700), pia kutoka Kindu hadi

Lubumbashi (km 1,300) na kutoka Lubumbashi hadi Kananga - DRC (km 1,000) kwa reli.

**HUDUMA ZA VIWANJA VYA NDEGE**

157. ***Mheshimiwa Spika,*** katika uendelezaji na uendeshaji wa miundombinu ya viwanja vya ndege nchini, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) imeendelea kusimamia na kuendeleza viwanja vya ndege vya Serikali. Usimamizi huo unahusisha kutoa huduma bora zenye ufanisi na salama, kufunga vifaa wezeshi kwa ajili ya usafirishaji wa abiria na mizigo katika viwanja vya ndege; na pia kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Serikali na Umma kuhusu uanzishwaji, uendelezaji, usimamizi, uendeshaji na utunzaji wa Viwanja vya Ndege ili kuhakikisha kuwa vinachangia kikamilifu katika maendeleo ya sekta ya anga, kukuza biashara nchini na uchumi kwa ujumla.

158. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi 2026, TAA iliendesha mazoezi ya utayari wa dharura (Emergency Drills) katika Viwanja vya Ndege vya Tabora, Musoma, Iringa na Mpanda. Hatua hiyo imeimarisha uwezo wa viwanja hivyo kukabiliana na majanga na dharura. Aidha, TAA imefanya ukaguzi wa uendeshaji na kuhuisha leseni za Viwanja vya Ndege vya Mtwara, Mafia, Tabora, Kasulu, Kibondo, Nachingwea, Shinyanga, West Kilimanjaro na Kilwa Masoko ili kuhakikisha viwanja vya ndege vinaendelea kuwa salama na vyenye ubora unaotakiwa kwa kuzingatia viwango vya kitaifa na kimataifa vya usalama na uendeshaji wa viwanja vya ndege.

159. ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kuboresha huduma za Viwanja vya Ndege nchini, Serikali kupitia TAA imeendelea kujenga, kukarabati na kuboresha Viwanja vya Ndege vya kimataifa na vya Mikoa ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi na kuhakikisha nchi inakuwa na miundombinu bora na huduma za kisasa kwa abiria katika viwanja vya ndege. Hadi kufikia Machi 2026, Wizara kupitia TAA imeendelea na uboreshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Arusha, ambapo ufungaji wa mfumo wa taa za kuongozea ndege umefikia asilimia 65; na ujenzi wa Karakana ya matengenezo ya

ndege ya Kilimo Anga na ujenzi wa tabaka la juu la lami la barabara ya kuruka na kutua ndege katika kiwanja hicho unaendelea, ambapo tayari wakandarasi wamekabidhiwa maeneo ya miradi kwa ajili ya utekelezaji.

160. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, Serikali imeahidi kukipandisha hadhi Kiwanja cha Ndege cha Mwanza kuwa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa. Wizara kwa kushirikiana na TAA tayari imekamilisha Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa Mradi wa Ujenzi wa Jengo Jipya la abiria (litakalokuwa na uwezo wa kuhudumia abiria milioni 2.5 kwa mwaka) pamoja na miundombinu wezeshi. Aidha, Wizara kupitia TAA inaendelea na majadiliano na wadau wa ndani na nje kwa ajili ya ufadhili wa mradi huo. Ukamilishwaji wa mradi huu utakiwezesha Kiwanja hiki kuhudumia abiria na ndege za Kimataifa kwa ufanisi.

161. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuitumia Sekta ya Uchukuzi kuifungua nchi, miongoni mwa juhudi zinazofanyika ni kuboresha na kujenga viwanja vya ndege vya kisasa katika maeneo ya kimkakati katika mipaka ya Tanzania na nchi nyingine ili kutoa huduma za kikanda na kimataifa. Aidha, viwanja hivi vinatumika kutoa huduma za kiutalii na kupunguza changamoto ya kuwa na viwanja vingi katika hifadhi. Katika kufikia azma hiyo, Serikali ya Awamu ya Sita imeamua kujenga viwanja vipya vya ndege ikiwemo Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Serengeti.

162. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi 2026, hatua ya kwanza ya uchambuzi wa sifa za awali za Wakandarasi wa Kimataifa (Pre-qualification) imekamilika na kwa sasa taratibu za ununuzi wa Mkandarasi atakayefanya ujenzi na Mhandisi Mshauri atakayesimamia ujenzi huo zinaendelea. Lengo la Serikali la kutekeleza mradi huu wa kimkakati ni kukuza utalii nchini pamoja na kulinda ikolojia ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti. Hivyo mradi huu umesanifiwa kwa kuzingatia utunzaji wa mazingira (Green airport) ambayo kwa ujumla wake itachochea ukuaji wa shughuli za utalii nchini.

163. ***Mheshimiwa Spika,*** wakati mradi wa ujenzi wa miundombinu ya barabara ya kuruka na kutua ndege, barabara ya kiungio, maegesho ya ndege, barabara ya kuingia kiwanjani na maegesho ya magari kwa kiwango cha lami na ujenzi wa miundombinu wezeshi ukiwa unaendelea kutekelezwa na TANROADS katika Kiwanja cha Ndege cha Musoma, ambapo utakelezaji wa jumla umefikia asilimia 63, Wizara kupitia TAA imekamilisha uhuishwaji wa usanifu wa Jengo jipya la abiria na taratibu za ununuzi wa Mkandarasi wa Ujenzi wa Jengo hilo zinaendelea. Pia, kwa upande wa Mradi wa Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mkoa wa Kagera, Mtaalamu Elekezi anayefanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina amekamilisha uandaaji wa taarifa ya Awali (Inception Report) na kwa sasa anaendelea na kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Awali.

164. ***Mheshimiwa Spika,*** Mkoa wa Kilimanjaro ni miongoni mwa mikoa yenye shughuli nyingi za utalii nchini na hivyo kuendelea kuwepo umuhimu wa kuendeleza miundombinu wezeshi ya utalii katika mkoa huo, kikiwemo Kiwanja cha Ndege cha Moshi. Katika kuendeleza Kiwanja hicho, Serikali imeendelea kufanya maboresho mbalimbali yakiwemo: ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege; na ujenzi wa uzio kuzunguka kiwanja husika.

165. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TAA imeendelea na utekelezaji wa maboresho ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA), ikiwa ni sehemu ya kuimarisha mchango wa sekta katika kukuza utalii na biashara ya usafirishaji wa bidhaa za kilimo zinazoharibika kwa haraka katika ukanda wa kaskazini. Serikali imekamilisha taratibu za manunuzi na tayari Wakandarasi wamepatikana kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali, zikiwemo: ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege; ufungaji wa mfumo wa taa za kuongozea ndege (AGL); na ujenzi wa Jengo Jipya la Watu Mashuhuri (New VIP Terminal).

166. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine za kuimarisha kiwanja cha KIA, maboresho ya eneo la kuhifadhi mizigo inayohitaji ubaridi yamekamilika; kazi za ujenzi wa uzio wa usalama wa kiwanja zinaendelea; na kazi ya maboresho ya eneo

la kuhifadhi mizigo mikavu (dry cargo) imefikia asilimia 5. Sambamba na kazi hizo, kazi ya usanifu wa jengo kuu la utawala imekamilika na mkataba wa huduma za ushauri elekezi kwa ajili ya ujenzi wa jengo la mizigo umesainiwa na Mshauri Elekezi tayari amekabidhiwa eneo la mradi.

167. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukidhi ongezeko la mahitaji ya huduma za usafiri wa anga nchini, Serikali kupitia TAA imeendelea kuchukua hatua madhubuti na za kimkakati, ikiwemo utwaaji, upimaji na urasimishaji wa ardhi kwa ajili ya upanuzi na ujenzi wa miundombinu ya viwanja vya ndege nchini. Hadi kufikia Machi 2026, TAA kwa kushirikiana na taasisi nyingine za Serikali inaendelea kukamilisha taratibu za upatikanaji wa hati miliki kwa viwanja vya ndege sita (6), ambavyo ni Kirondatal, Mvumi, Ngara, Liwale, Manyoni na Singida. Aidha, kwa kuzingatia umuhimu wa suala la fidia kwa wananchi waliopisha maeneo yao kwa ajili ya upanuzi wa viwanja vya ndege nchini, Serikali ya Awamu ya Sita imefanikisha kulipa fidia kwa wananchi 737 wa eneo la Kipunguni waliopisha upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA), pamoja na wananchi 58 waliopisha upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Musoma. Serikali itaendelea kushughulikia changamoto za fidia kwa kuendelea kutenga fedha katika bajeti ili kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi wote waliopisha uendelezaji wa viwanja vya ndege.

## HUDUMA ZA USAFIRI WA ANGA

168. ***Mheshimiwa Spika,*** tunaendelea kuishukuru Serikali kwa kufufua Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) kuanzia mwaka 2015. Hatua hii imewezesha kuongezeka kwa ndege zinazoendeshwa na ATCL kutoka ndege moja mwaka 2016 hadi kufikia ndege 16. Manufaa yaliyopatikana baada ya ufufuaji huu wa kimkakati ni pamoja na:

i. Kuongezeka kwa abiria wanaosafirishwa na ATCL kutoka abiria 107,166 mwaka 2016/17 hadi kufikia abiria 1,178,025 mwaka 2024/25;

ii. Kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato ya ndani ya ATCL kutoka Shilingi bilioni 23 mwaka 2016/17 hadi kufikia Shilingi bilioni 595.7 mwaka 2024/25;

iii. Kuongezeka kwa mchango wa ATCL katika kodi kutoka Shilingi bilioni 2.4 mwaka 2016/17 hadi kufikia Shilingi bilioni 52.35 mwaka 2024/25;

iv. Kuongezeka kwa mchango wa ATCL katika Mapato ya Fedha za Kigeni kutoka Dola za Marekani milioni 9.85 mwaka 2017/18 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 157.7 mwaka 2024/25;

v. Kupanuka kwa mtandao wa safari wa ATCL kutoka vituo 4 vilivyokuwepo mwaka 2015/16 hadi kufikia vituo 33 mwezi Machi 2026; na

vi. Kuongezeka kwa mchango wa ATCL katika ajira ambapo idadi ya watumishi imeongezeka kutoka watumishi 171 mwaka 2016/17 hadi kufikia watumishi 1,148 Machi 2026. Miongoni mwa watumishi hao ni marubani ambao wameongezeka kutoka marubani 13 mwaka 2016/17 hadi kufikia marubani 142 mwaka 2026.

169. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na manufaa haya, ufufuaji wa ATCL umechochea ukuaji wa sekta nyingine zikiwemo utalii, kilimo, biashara na madini. Aidha, hatua hii ya kimkakati ya kuendelea kuboresha ATCL imewezesha Tanzania kujitangaza kikanda na kimataifa na kuwa miongoni mwa nchi chache Kusini mwa Jangwa la Sahara kuwa na shirika la taifa la ndege (National Flag Carrier).

170. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na manufaa haya makubwa, kwa muda mrefu kumekuwepo na changamoto ya mtaji mdogo ikilinganishwa na mahitaji ya ndege kwa ATCL, hali inayosababisha kutokuwa na mizania halisi ya kimahesabu na kupelekea deni ambalo halitokani na udhaifu wa utendaji, bali ni kukosa umiliki wa ndege. Kwa kuliona hili, Serikali imeandaa mpango mahsusi wa kuimarisha utendaji na mizania kwa kupitia upya mfumo wa umiliki wa ndege. Utekelezaji huo upo katika

hatua za mwisho na utakapokamilika utaweka taswira nzuri ya mizania ya kimahesabu. Kwa njia hii, ATCL itakuwa na uwezo mkubwa wa kupata mitaji na fedha za uendeshaji kutoka taasisi za fedha kwa masharti nafuu na hivyo kuiwezesha Kampuni kuendesha shughuli zake kwa misingi imara na endelevu ya kibiashara.

171. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Serikali kupitia ATCL imeendelea na taratibu za ununuzi wa ndege mbili (2) aina ya Dash 8 Q400 na imekamilisha ununuzi wa injini moja (1) ya akiba kwa ajili ya ndege aina ya B787- 8 Dreamliner na kufanya malipo ya awali ya injini moja (1) ya akiba ya Boeing 737-9. Upatikanaji wa injini za akiba utawezesha ndege zote kuendelea kufanya kazi bila kusimama wakati wa matengenezo yaliyopangwa (planned maintenance) ya injini. Vilevile, ATCL imeendelea na uboreshaji wa miongozo ya uendeshaji wa shughuli za usafiri wa anga (Operation Manuals).

172. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa sasa, ATCL inaendelea kutoa huduma za usafiri wa anga kwa kutumia ndege zake 16 zikijumuisha ndege nne (4) za masafa marefu ambazo kati yake: tatu (3) ni za abiria aina ya Boeing 787-8 na moja (1) ni ya mizigo aina ya Boeing 767-300F; ndege sita (6) za masafa ya kati zikijumuisha nne (4) aina ya Airbus A220 – 300 na mbili (2) aina ya Boeing 737 Max 9; na ndege sita (6) za masafa mafupi zikiwemo tano (5) aina ya Dash 8 Q400 na moja (1) aina ya Dash 8 Q300.

173. ***Mheshimiwa Spika,*** kama ilivyoelezwa awali, ATCL imeendelea kuongeza vituo vya huduma na uimarishaji wa uendeshaji ambapo hadi kufikia Machi, 2026 ATCL ina jumla ya vituo 33 vya huduma ya usafiri wa anga. Aidha, taratibu za kurejesha safari katika kituo cha Geita zinaendelea. Kati ya vituo 33, Vituo 16 ni vya ndani ya nchi ambavyo ni Arusha, Bukoba, Dar es Salaam, Dodoma, Geita, Kilimanjaro, Kigoma, Mbeya, Mpanda, Mwanza, Iringa, Mtwara, Songea, Tabora, Pemba, na Zanzibar; Vituo (14) ni vya kikanda ambavyo ni Bujumbura, Entebbe, Cape Town, Kinshasa, Victoria Falls, Accra, Lagos, Hahaya, Harare, Lusaka, Ndola, Nairobi, Lubumbashi na

Johannesburg; na Vituo vitatu (3) ni vya kimataifa ambavyo ni Dubai, Guangzhou na Mumbai.

174. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha ufanisi na usalama wa utoaji wa huduma za usafirishaji wa abiria na mizigo, ATCL imeendelea kuboresha miundombinu wezeshi inayojumuisha ujenzi wa karakana mpya ya matengenezo ya ndege, ujenzi wa stoo ya vifaa na vipuri pamoja na ujenzi wa ghala la kuhifadhia mizigo katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA). Wakandarasi wamepatikana na utekelezaji wa miradi hii upo katika hatua za awali.

175. ***Mheshimiwa Spika,*** ATCL pia imeendelea kufanya ukarabati wa karakana za matengenezo ya ndege zilizopo viwanja vya ndege vya JNIA na KIA pamoja na maandalizi ya awali ya ujenzi wa karakana mpya katika kiwanja cha ndege cha JNIA. Karakana hizo, zitawezesha ATCL kufanya matengenezo madogo na makubwa ya ndege na hivyo kuokoa fedha za kigeni na kupunguza gharama za matengenezo nje ya nchi. Mkakati mwingine unaoendelea kutekelezwa ni ATCL kuhudumia ndege zake yenyewe badala ya kukodi makampuni mengine.

176. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi 2026, ATCL ilisafirisha abiria 1,072,528 ikilinganishwa na abiria 876,357 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2024/25 sawa na ongezeko la asilimia 22.38. Kati ya abiria waliosafirishwa, abiria 750,452 walikuwa ni wa ndani ya nchi na abiria 322,076 walikuwa ni wa nje ya nchi. Aidha, ATCL imeendelea kutoa huduma ya usafirishaji wa mizigo ambapo hadi kufikia Machi 2026, ilisafirisha jumla ya tani 4,129.72 za mizigo. Mizigo hii imekuwa ikisafirishwa kutoka maeneo mbalimbali kwa ratiba maalum katika vituo vya Dar es Salaam, Nairobi, Zanzibar na Falme za Kiarabu, pamoja na safari za kukodi kulingana na mahitaji ya wateja katika vituo mbalimbali ikiwemo Guangzhou (China) na Mumbai (India).

177. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi kufikia Machi, 2026 ATCL imekusanya jumla ya Shilingi bilioni 501.62 ya mapato ya ndani ikilinganishwa na Shilingi bilioni

449.90 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho cha mwaka 2024/25, sawa na ongezeko la asilimia 11.5. Kupitia mapato yake ya ndani, ATCL imeendelea kugharamia matumizi yake ya uendeshaji. Matumizi hayo katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 ni pamoja na: Ununuzi wa mafuta Shilingi bilioni 240; Matengenezo ya ndege Shilingi bilioni 157; na Mishahara Shilingi bilioni 87. Hali hii inaonesha kuwa, Kampuni haitegemei ruzuku ya Serikali katika kujiendesha.

178. ***Mheshimiwa Spika,*** ATCL imeendelea kutoa mchango mkubwa katika ukusanyaji wa mapato ya fedha za kigeni, ambapo imefanikiwa kuongeza mapato hayo kutoka Dola za Marekani milioni 43.36 mwaka wa fedha 2020/21 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 157.69 mwaka 2024/25. Aidha, fedha za kigeni zinazokusanywa na ATCL zimeendelea kuongezeka ambapo katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 jumla ya Dola za Marekani milioni 129.71 zilikusanywa ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 104.53 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2024/25.

179. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuiwezesha ATCL kuendelea kutoa huduma bora, Serikali kupitia ATCL imeendelea kuajiri watumishi ambapo hadi kufikia Machi 2026, ATCL ilikuwa na jumla ya watumishi 1,148 ikijumuisha marubani 142 na wahandisi na mafundi wa ndege 231 ikilinganishwa na watumishi 857 waliokuwepo katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2024/25, miongoni mwao 117 walikuwa marubani na 190 walikuwa ni wahandisi na mafundi wa ndege. Ongezeko hilo la watumishi limewezesha kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa na ATCL zinakidhi viwango na matakwa ya kitaifa na kimataifa katika usafiri wa anga, hususan kwa marubani na wahudumu wa ndani ya ndege.

180. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli nyingine zilizotekelezwa na ATCL ni pamoja na kuendelea na ukarabati wa nyumba 38 za watumishi zilizopo katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA), ukarabati wa ofisi zilizopo jengo la ATC House pamoja na ofisi zilizopo katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA) Terminal I ambapo umefikia asilimia 98.

Halikadhalika, ATCL imeendelea kutoa huduma ya mafunzo kwa wahudumu wa ndani ya ndege kupitia Chuo cha ATCL Training Centre, ambapo kimetoa mafunzo ya kada ya wahudumu wa ndani ya ndege kwa wanafunzi 148.

## C:3 VYUO VYA MAFUNZO VYA KISEKTA

181. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Uchukuzi imeendelea kusimamia vyuo vyake vyote vya kitaifa vinavyotoa mafunzo katika sekta ya usafirishaji, ambavyo ni Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI), Chuo cha Usafiri wa Anga (CATC), Chuo cha Teknolojia ya Reli (TIRTEC), Chuo cha Bandari na Chuo cha Hali ya Hewa. Kupitia vyuo hivi, Serikali inaendeleza rasilimaliwatu wenye ujuzi wa kitaaluma na kiteknolojia, ili kuhakikisha sekta ya usafirishaji nchini inakuwa na wataalam wa ndani wanaoweza kutumika katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kitaifa pamoja na utoaji wa huduma za uchukuzi. Katika kuhakikisha vyuo hivyo vinazalisha wataalam husika, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu pamoja na ununuzi wa vifaa vya mafunzo.

### Chuo Cha Taifa Cha Usafirishaji (NIT)

182. ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha NIT kimeendelea kuzalisha wataalam mahiri katika njia za usafirishaji za barabara, anga, reli, maji na mabomba kwa kuzingatia mahitaji ya sekta. Aidha, Chuo kimeendelea kufanya tafiti, kutoa ushauri wa kitaalam pamoja na kuandaa machapisho kwa lengo la kuboresha utoaji wa mafunzo na kutatua changamoto za kisekta.

183. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa masomo 2025/26, Chuo cha NIT kimeendelea kutoa mafunzo katika kozi za muda mrefu 49, zikiwemo kozi za kimkakati zinazolenga kuzalisha wataalam mahiri wenye ujuzi wa kuendeleza na kusimamia miradi mikubwa ya kitaifa katika sekta ya usafirishaji, ikiwemo wataalam wa reli, anga na usafiri majini. Katika mwaka wa masomo 2025/26, idadi ya wanafunzi wa kozi za muda mrefu imeongezeka kufikia 19,544 kutoka wanafunzi 17,701 katika mwaka wa masomo 2024/25, sawa na ongezeko la wanafunzi 1,843.

184. ***Mheshimiwa Spika,*** ongezeko hili la wanafunzi limetokana na mahitaji ya rasilimaliwatu yanayoendelea kukua na uwepo wa miradi mikubwa ya kitaifa inayotekelezwa na Serikali, hususan katika sekta ya usafirishaji. Vilevile, katika mwaka wa masomo 2024/25 jumla ya wanafunzi 4,279 walihitimu katika fani mbalimbali ikilinganishwa na wahitimu 4,176 katika mwaka wa masomo 2023/24. Wahitimu hao wameendelea kupunguza uhaba wa wataalam katika sekta ya usafirishaji.

185. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Machi, 2026 katika mwaka wa masomo 2025/ 26, jumla ya washiriki 4,744 wamehudhuria mafunzo ya kozi za muda mfupi katika fani za menejimenti ya usafirishaji na uchukuzi, ukaguzi wa magari pamoja na weledi wa madereva. Idadi hii imeongezeka ikilinganishwa na washiriki 4,303 waliopata mafunzo ya kozi za muda mfupi katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa masomo 2024/25, sawa na ongezeko la asilimia 10.25**.** Ongezeko hilo limechangiwa na kuimarika kwa uwezo wa Chuo cha NIT na usimamizi wa sheria za uendeshaji wa vyombo vya moto.

186. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hotuba yangu ya mwaka 2025/26, Wizara iliahidi kuanza kutoa mafunzo ya urubani katika Chuo cha NIT baada ya kukamilisha maandalizi yote. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa mwezi Julai 2025, NIT ilipata ithibati na kuanza rasmi kutoa mafunzo ya urubani katika ngazi ya leseni ya awali (Private Pilot Licence – PPL) na leseni ya kibiashara (Commercial Pilot Licence – CPL).

187. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi 2026, kundi la kwanza la wanafunzi 10 wa ngazi ya PPL wamekamilisha mafunzo ya nadharia na wanaendelea na mafunzo ya vitendo, ambapo wanafunzi nane (8) wamefikia hatua ya kurusha ndege bila uwepo wa mkufunzi (solo flight). Aidha, kundi la pili la wanafunzi 12 wa ngazi ya PPL limekamilisha mafunzo ya nadharia na linaendelea kukamilisha taratibu za kupata Leseni ya Mwanafunzi Rubani (Student Pilot Licence – SPL) ili kuanza mafunzo ya vitendo. Utekelezaji wa programu hii unaimarisha juhudi za Serikali za kuongeza wataalam wa ndani katika sekta ya usafiri wa anga na kupunguza utegemezi wa wataalam kutoka nje ya nchi.

188. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kukijengea uwezo Chuo cha NIT kutoa mafunzo kwa umahiri na kukidhi mahitaji ya soko, Serikali imeendelea kutekeleza mradi wa kuboresha miundombinu na vifaa vya kufundishia, ambapo ujenzi wa jengo la maabara (Civil Engineering Labs) kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa vitendo na kuzalisha wataalam mahiri katika sekta ya usafirishaji hususan wataalam wa Reli ya Kisasa (SGR) umekamilika; ujenzi wa barabara za ndani ya Chuo zenye jumla ya urefu wa kilomita 1.25 kwa kiwango cha lami umekamilika; ununuzi wa ndege moja (1) yenye injini mbili (2) kwa ajili ya mafunzo ya urubani unaendelea ambapo uundwaji wa ndege hiyo kiwandani nchini Marekani unatarajiwa kukamilika na ndege kupokelewa nchini mwezi Juni, 2026. Aidha, ununuzi wa Ndege mbili (2) zenye injini moja (1) za mafunzo ya urubani uundwaji wake unaendelea kiwandani nchini Marekani, ambapo ndege moja (1) inatarajiwa kupokelewa nchini mwezi Juni, 2026.

189. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Chuo cha NIT imeendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Kampasi ya NIT Lindi kwa lengo la kuzalisha wataalam mahiri na kukuza uwezo wa kiteknolojia katika sekta ya usafiri kwa njia ya maji, mafuta na gesi. Hadi kufikia Machi, 2026 usanifu wa majengo ya awali ambayo ni jengo la ghorofa mbili (2) linalojumuisha madarasa, maabara, vyumba vya mihadhara na ofisi; jengo la huduma za chakula (canteen); pamoja na miundombinu mingine ikiwemo viwanja vya michezo umekamilika. Aidha, taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi zimefikia hatua za mwisho, ambapo tathmini ya zabuni imekamilika.

190. ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha NIT kinaendelea na utekelezaji wa Mradi wa *East Africa Skills for Transformation* and *Regional Intergration Project* (EASTRIP), ambapo kazi za uanzishwaji wa Kituo cha Umahiri cha Mafunzo ya Taaluma za Usafiri wa Anga na Operesheni za Usafirishaji zimetekelezwa kama ifuatavyo:-

i. Kukamilika kwa ujenzi wa majengo matano (5) katika Kampasi ya NIT Mabibo, Dar es Salaam ambayo ni mabweni mawili (2) ya wanafunzi yenye uwezo wa kulaza jumla ya wanafunzi

1,504; na majengo mengine matatu (3) ambayo ni jengo la Kituo cha Umahiri; Maabara ya kisasa ya mafunzo ya Uhandisi wa Matengenezo ya Ndege na jengo la mafunzo ya wahudumu ndani ya ndege ambayo yana madarasa 10, maabara 15 na karakana tano (5). Aidha, majengo hayo yana ofisi zenye uwezo wa kuhudumia watumishi 25;

ii. Ujenzi wa jengo la karakana ya matengenezo ya ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA) itakayotumika wakati wa mafunzo ya urubani kwa vitendo na uhandisi wa matengenezo ya ndege unaendelea na umefikia asilimia 30; na

iii. Taratibu za ununuzi wa vifaa zaidi vya mafunzo ya urubani ikiwemo *Flight Simulator* zimekamilika na vifaa hivyo vinatarajiwa kupokelewa nchini mwezi Septemba, 2026.

191. ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha NIT kinaendelea na utekelezaji wa kazi za uanzishwaji wa Kituo cha Kikanda cha Umahiri cha Mafunzo ya Usalama Barabarani kilichoanzishwa kwa ufadhili wa Serikali kupitia Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), ambapo kazi zifuatazo zimefanyika:-

i. Kutoa mafunzo ya usalama barabarani na ukaguzi wa usalama wa barabara kwa jumla ya washiriki 35,581 wakiwemo wanafunzi wa shule za msingi, madereva wa pikipiki (bodaboda), bajaji na magari;

ii. Kuandaa mitaala 15 ya kozi za muda mfupi kwa ajili ya kutoa mafunzo ya kuzalisha wataalam wenye uelewa wa usalama barabarani na kupunguza tatizo la ajali za barabarani nchini; na

iii. Kuwajengea uwezo walimu wa shule za msingi 39 kuhusu usalama barabarani na ukaguzi wa barabara kwa ajili ya kutoa mafunzo hayo kwa wanafunzi wa shule za msingi katika manispaa tano (5) za Mkoa wa Dar es Salaam.

192. ***Mheshimiwa Spika,*** katika juhudi za kuendeleza ujuzi wa kitaaluma, Chuo cha NIT kinaendelea kutekeleza mpango wa mafunzo unaolenga kujenga uwezo wa watumishi kupitia kozi za muda mrefu. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya watumishi 61 wanaendelea na mafunzo haya, wakiwemo 42 wa Shahada ya Uzamivu, 17 wa Shahada ya Uzamili, na wawili (2) wanaosomea mafunzo ya Urubani (Integrated Commercial Pilot Licence – ICPL).

**Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI)**

193. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI) imeendelea kutoa mafunzo ya ujuzi na utaalam katika masuala ya usafiri majini kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa na Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) na Shirika la Bahari Duniani (IMO). Pia, Chuo kimeendelea kufanya tafiti, kutoa ushauri wa kitaalam pamoja na kuandaa machapisho mbalimbali kuhusu kutatua changamoto za usafiri majini. Aidha, Chuo kinatoa mafunzo kwa kuzingatia Viwango vya Ubora vya Kimataifa yaani ISO 9001:2015 na kinatambuliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET).

194. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka wa masomo wa 2025/26, Chuo kimeweza kudahili wanafunzi wa kozi za muda mrefu 6,911 ikilinganishwa na wanafunzi 5,921 waliodahiliwa katika mwaka wa masomo wa 2024/25 sawa na ongezeko la wanafunzi 990. Aidha, wahitimu wameongezeka hadi kufikia 2,076 kwa mwaka 2024/25 ikilinganishwa na wanafunzi 1,526 waliohitimu kwa mwaka wa 2023/24. Kwa upande wa kozi za muda mfupi, Chuo kimeweza kudahili wanafunzi 10,220 sawa na ongezeko la asilimia 43.03 ikilinganishwa na wanafunzi 7,145 waliodahiliwa mwaka wa masomo 2024/2025. Vilevile, Chuo kiliweza kuchapisha machapisho ya utafiti 146 na kuratibu Kongamano la Kitaifa la Uchumi wa Buluu lililofanyika jijini Dar es Salaam mwezi Septemba, 2025 lililohusisha washiriki wapatao 700 kutoka ndani na nje ya nchi.

195. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza miundombinu ya Chuo, hatua mbalimbali zimeendelea kutekelezwa katika eneo la Kigamboni lenye ukubwa wa ekari 13. Chuo kinaendelea na

maandalizi ya ujenzi wa Chuo kikubwa cha kisasa, ambapo Mshauri Elekezi anaandaa taarifa za Upembuzi Yakinifu, Mpango Kabambe, tathmini ya athari za mazingira pamoja na michoro ya usanifu. Pia, eneo la Kikwetu mkoani Lindi, Mshauri Elekezi anaendelea kufanya Upembuzi Yakinifu, tathmini ya athari za mazingira pamoja na michoro ya usanifu. Katika eneo la Mkuranga mkoani Pwani, Mshauri Elekezi ameandaa michoro ya usanifu ili kujenga Kituo cha Mafunzo ya Kuzuia na Kuzima Moto Melini.

196. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kukitangaza Chuo kimataifa, Serikali kupitia DMI imeingia mashirikiano (MoU) na Chuo cha Bahari Duniani (World Maritime University) kilichopo nchini Sweden ili kuimarisha utoaji wa elimu ya ubaharia na tafiti katika sekta ndogo ya Uchumi wa Buluu. Mashirikiano haya yanahusisha; Tafiti za masuala ya bahari; Programu za mafunzo ya umahiri kwa pamoja kati ya DMI na Chuo cha Bahari Duniani; Maboresho ya mifumo ya takwimu za elimu ya Bahari; Ubadilishanaji wa taarifa za kitaalam; na Uboreshaji wa mitaala ili kuendana na mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi. Kuwepo kwa mashirikiano haya kutaongeza umahiri kwa wakufunzi na hivyo kuzalisha wahitimu wenye uwezo na sifa za kuhudumia sekta ndogo ya Uchumi wa Buluu.

**Chuo cha Usafiri wa Anga Tanzania (CATC)**

197. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kuongeza wataalam wa usafiri wa anga, Serikali kupitia Chuo cha Usafiri wa Anga (CATC) imeendelea kutoa mafunzo katika kada mbalimbali za sekta ya usafiri wa anga. Mafunzo hayo yanajumuisha: Uongozaji wa ndege; Ufundi wa mitambo ya kuongozea ndege na mawasiliano; na utoaji wa taarifa za anga. Vilevile, kozi nyingine zinazotolewa na chuo hiki ni pamoja na kozi za usalama wa usafiri wa anga, usafirishaji wa bidhaa hatarishi katika ndege na usimamizi na uandaaji wa safari za ndege na mafunzo ya ufundishaji kwa wakufunzi wa sekta ya usafiri wa anga.

198. ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha CATC kimeendelea kutambuliwa na Shirika la Usafiri wa Anga Duniani (ICAO) kupitia

Mpango wa kimataifa wa masuala ya mafunzo ya anga (TRAINAIR PLUS) katika hadhi ya juu ya uanachama (Full Member – GOLD). Kutokana na umahiri wa Chuo hiki katika kipindi cha mwaka wa masomo 2025/26, Chuo kimefanikiwa kuongeza nchi zinazoshiriki mafunzo kutoka nchi 18 mwaka 2024/25 hadi kufikia nchi 21 kwa mwaka wa masomo 2025/26. Nchi zilizoongezeka kwa mwaka 2025/26 ni Malawi, Qatar na Oman. Kuongezeka kwa nchi hizo kumewezesha Chuo hiki kusaidia kuitangaza Tanzania kimataifa na kuongeza fedha za kigeni kutokana na ada za mafunzo.

199. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi 2026, CATC kimefanikiwa kutoa jumla ya kozi 108 ikilinganishwa na kozi 89 za mwaka 2024/25. Kozi hizo zilihudhuriwa na washiriki 1,776. Kati yao, washiriki 205 walitoka nje ya nchi, wakiwemo wanaume 160 na wanawake 45, huku washiriki 1,571 wakitoka Tanzania, wakiwemo wanaume 1,128 na wanawake 443. Washiriki wa ndani wanaoendelea kupata mafunzo CATC wanatoka mashirika ya ndege, viwanja vya ndege vya Tanzania Bara na Zanzibar, Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA), mashirika mbalimbali yanayotoa huduma kwenye viwanja vya ndege, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Jeshi la Polisi, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mabenki, Mamlaka za Bandari Tanzania Bara (TPA) na Zanzibar (ZPC) pamoja na wananchi kwa ujumla.

200. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha na kuboresha ufanisi wa usimamizi wa ukaguzi wa usalama kwa watumiaji wa vifaa vya usalama (security scanners) na usimamizi wa itikio la masuala ya dharura katika viwanja vya ndege na maeneo mengine, Chuo kimeendelea kubuni na kuongeza kozi mpya. Mathalan, kwa mwaka 2025/26, Chuo hiki kilifanikiwa kuanzisha kozi mpya mbili (2), ambazo ni *Security Inspection Techniques* na *Emergency Response Procedure*.

201. ***Mheshimiwa Spika***, Chuo cha Usafiri wa Anga (CATC) ni miongoni mwa vyuo vitatu (3) vya ICAO katika Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini mwa Bara la Afrika vinavyotoa mafunzo ya usalama wa usafiri wa anga. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi

Machi 2026, Chuo kiliendesha mafunzo ya *Crisis Management,* yaliyofanyika mwezi Novemba, 2025 na ilishirikisha washiriki 19 kutoka nchi mbalimbali. Kozi hiyo ilitolewa kupitia Mpango unaoratibiwa na ICAO ambao hutoa kozi mbili (2) kwa kila mwaka kwa kugharamia kozi hizo katika nchi 35 wanachama wa ICAO zinazotoa mafunzo ya Usalama wa Usafiri wa Anga (ICAO *Aviation Security Training Centre*).

**Chuo cha Bandari**

202. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utoaji wa huduma za kibandari, Chuo cha Bandari kilichopo Dar es Salaam kimeendelea kutoa mafunzo, kufanya tafiti na ushauri wa kitaalam katika tasnia ya usafirishaji majini. Chuo hiki kinatoa mafunzo ya muda mrefu ya: Astashahada ya msingi ya ufundi; Astashahada ya ufundi na stashahada katika kozi zifuatazo: Usimamizi wa Upokeaji, Uondoshaji na Usafirishaji Shehena; Usafirishaji Majini na Lojistiki; Usimamizi wa Usafirishaji Shehena na Operesheni za Bandari; Ufundi Mitambo; Usimamizi wa Usafirishaji Shehena na Usalama wa Bandari; na Usimamizi wa Moto na Usalama.

203. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Chuo hiki kilidahili jumla ya wanafunzi 1,051 wa mafunzo ya muda mrefu ikilinganishwa na wanafunzi 1,008 waliodahiliwa katika mwaka 2024/25, sawa na ongezeko la wanafunzi 43. Kwa upande wa mafunzo ya muda mfupi hadi kufikia Machi, 2026 Chuo cha Bandari kilidahili jumla ya wanafunzi 1,849. Kati ya hao, wanafunzi 1,635 walitoka katika Sekta Binafsi, wanafunzi 214 walitoka Taasisi mbalimbali za Serikali wakiwemo washiriki 25 kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA).

**Chuo Cha Taifa cha Hali ya Hewa**

204. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuendelea kujenga uwezo wa wataalam kwenye tasnia ya hali ya hewa nchini, Serikali kupitia Chuo cha Taifa cha Hali ya Hewa kilichopo Kigoma, imeendelea kutoa mafunzo ya hali ya hewa katika ngazi ya awali na stashahada, ambapo jumla ya wanafunzi 63 walihitimu katika

ngazi ya cheti na stashahada. Aidha, Chuo kilidahili jumla ya wanafunzi 83 ambao wanaendelea na masomo katika mwaka wa fedha 2025/26. Kati yao, wanafunzi 31 wanaendelea na mafunzo katika Ngazi ya NTA 4 (12 katika masomo ya Hali ya Hewa na 19 katika TEHAMA), wanafunzi 36 wapo katika Ngazi ya NTA 5 (21 katika masomo ya Hali ya Hewa na 15 katika TEHAMA) na wanafunzi 16 wapo katika Ngazi ya NTA 6. Serikali imeendelea na jitihada za kukiboresha Chuo hicho ili kuimarisha utoaji wa mafunzo na wigo wa udahili.

### Chuo cha Teknolojia ya Reli Tanzania

205. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza ufanisi wa usafirishaji kwa njia ya reli, Chuo cha Teknolojia ya Reli Tanzania kimeendelea kutoa mafunzo, kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalam. Chuo hiki kinatoa mafunzo ya muda mrefu katika fani mbalimbali ikiwa ni pamoja na: Usafirishaji kwa njia ya Reli; Matengenezo ya mabehewa; Matengenezo ya miundombinu ya reli; Teknolojia ya usanifu wa matengenezo ya reli na mabehewa; Ufundi Sanifu wa Mifumo ya Umeme kwenye vichwa vya treni; Mawasiliano na ishara; Usafirishaji na udhibiti wa ajali katika mtandao wa reli; Uchumi katika usafirishaji; Teknolojia ya udereva wa treni; na Usalama kwenye matengenezo ya miundombinu ya reli katika kampasi mbili (2) zilizopo Tabora na Morogoro.

206. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Chuo kilidahili jumla ya wanafunzi 742 sawa na ongezeko la asilimia 32.74 ikilinganishwa na wanafunzi 559 waliodahiliwa katika mwaka wa fedha 2024/25. Ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa kozi mbalimbali ikiwemo; usafirishaji na udhibiti wa ajali katika mtandao wa reli; uhandisi wa mawasiliano; pamoja na kozi ya uchumi katika usafirishaji kwa njia ya reli.

## C:4 MASUALA YA KISERA NA MTAMBUKA

### Maboresho ya Sera za Kisekta

207. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Hotuba yangu ya mwaka 2025/26 niliwasilisha taarifa kuhusu Wizara kufanya mapitio ya Sera

ya Taifa ya Uchukuzi ya mwaka 2003. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara imeendelea kwa ufanisi na zoezi la kuhuisha sera hiyo kwa kuzingatia Tathmini iliyofanyika na maoni ya wadau yaliyokusanywa nchi nzima kupitia kanda tisa (9) za uwakilishi ambazo ni Kigoma, Mwanza, Mbeya, Dodoma, Arusha, Dar es Salaam, Mtwara, Kaskazini Pemba na Mjini Magharibi Unguja. Miongoni mwa masuala makuu yaliyoainishwa katika Tathmini na maoni ya wadau hao ni pamoja na: umuhimu wa kufungamanishwa kwa mifumo ya usafirishaji (inter-modal and Integrated transport systems) kwa njia za usafirishaji hususan reli na barabara, Bandari na Reli; na umuhimu wa kuendelea kushirikisha Sekta Binafsi katika uendelezaji wa miundombinu ya uchukuzi.

208. ***Mheshimiwa Spika***, katika kukamilisha zoezi hilo, Wizara imekamilisha rasimu ya Sera ya Taifa ya Uchukuzi ya mwaka 2026 na Mkakati wake wa Utekelezaji na tayari uhakiki umefanyika kupitia vikao vya wadau kikiwemo kikao cha mwisho cha uhakiki kilichofanyika tarehe 5 – 6 Machi, 2026 Jijini Dar es Salaam na kuhusisha wadau kutoka Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Hatua inayofuata kwa mujibu wa taratibu za Serikali ni kuwasilisha mapendekezo ya kutunga Sera hiyo katika ngazi za maamuzi ndani ya Serikali ili kuidhinishwa na kuanza kutumika.

209. ***Mheshimiwa Spika,*** suala lingine muhimu lililosisitizwa na wadau wakati wa tathmini ya Sera ya Taifa ya Uchukuzi ya mwaka 2003 ni umuhimu wa kuwa na Sera Mahsusi ya Usafiri Majini (National Maritime Transport Policy). Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara imeendelea na maandalizi ya kutunga Sera hiyo. Wizara ilikamilisha Tathmini ya Sekta Ndogo ya Usafiri Majini mwezi Machi 2026, ikiwa ni takwa muhimu la maandalizi ya sera. Hatua inayofuata ni maandalizi ya sera hiyo kulingana na taratibu za Serikali.

**Maboresho ya Sheria na Kanuni zinazosimamia Sekta ya Uchukuzi**

210. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha mfumo wa sheria unaosimamia Sekta ya Uchukuzi, Serikali imefanya marekebisho ya baadhi ya sheria, ikiwemo Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, Sura ya 413 kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa

usalama barabarani na ukaguzi wa vyombo vya usafiri; Sheria ya Bandari, Sura ya 166 ili kuboresha utoaji wa huduma za bandari nchini; Sheria ya Leseni za Usafirishaji, Sura ya 317 kwa madhumuni ya kuongeza udhibiti katika utoaji wa leseni za vyombo vya usafiri; pamoja na Sheria ya Usafiri wa Anga, Sura ya 80, iliyofanyiwa marekebisho ili kuimarisha masuala ya usalama wa usafiri wa anga nchini na kuendana na miongozo inayotolewa na ICAO kuhusu ubora wa ndege, utoaji leseni kwa watoa huduma za usafiri wa anga na kuimarisha uchunguzi wa ajali za ndege.

211. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, katika kuimarisha usalama barabarani Wizara imeandaa kanuni mbalimbali zikiwemo za: vyombo vya usafiri wa kukodi kwa lengo la kutenganisha kati ya huduma za mabasi ya abiria kwa umma na vyombo vya kukodi; Kanuni za leseni za vyombo vya usafiri wa umma; na Kanuni za leseni za vyombo vya kubeba mizigo. Katika kipindi husika, Wizara imeendelea na maandalizi ya Kanuni za Usimamizi wa Madhara ya Uchovu kwa Madereva. Tayari maoni ya wadau yamekusanywa kuhusu kanuni hiyo na Wizara inaendelea kuchakata maoni hayo ili kuboresha kanuni husika. Vilevile, katika kuimarisha utoaji wa huduma katika viwanja vya ndege, Wizara imekamilisha uandaaji wa Kanuni za Uendeshaji, Uwezeshaji, Usalama na Ulinzi wa Viwanja vya Ndege Tanzania, 2026; na Kanuni za Ada na Tozo za viwanja vya Ndege Tanzania, 2026.

**Uridhiaji wa Mikataba ya Kikanda na Kimataifa**

212. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa lengo la kuendana na miongozo ya kikanda na kimataifa, nchi yetu imekuwa ikiridhia mikataba mbalimbali ili kuboresha huduma za uchukuzi. Katika kutekeleza jukumu hilo, Serikali kupitia Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) inaendelea kukamilisha taratibu za ndani ya Serikali ili kuridhia Mkataba wa Afrika wa Usafiri Majini wa mwaka 2010 (Revised African Maritime Transport Charter, 2010 – AMTC, 2010). Vilevile, Tanzania imeendelea na taratibu za kuridhia Itifaki ya mwaka 1997 ya kurekebisha Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Uchafuzi wa Mazingira Utokanao na Meli (the International Convention on Prevention of Maritime Pollution from Ships -

MARPOL Annex VI), hatua itakayowezesha kudhibiti utoaji wa hewa ukaa na kulinda mazingira.

213. ***Mheshimiwa Spika,*** kuridhiwa kwa mikataba hii kutaleta manufaa makubwa ikiwemo; kupunguza hatari ya meli za Tanzania kuzuiwa katika bandari za kimataifa; kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa; kuongeza usalama wa baharini na kupunguza uharamia; na kuwezesha uwekezaji katika teknolojia ya nishati safi. Pindi taratibu za ndani ya Serikali zitakapokamilika mapendekezo ya kuridhia Mkataba na itifaki husika yatawasilishwa hapa bungeni kwa ajili ya kuridhiwa na Bunge lako Tukufu kwa mujibu wa Katiba ya Nchi.

**Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira**

214. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kusimamia uhifadhi na utunzaji wa mazingira, Wizara imekamilisha maandalizi ya Mpango Kazi wa Utunzaji wa Mazingira ya Uchukuzi 2025 - 2030 (Transport Sector Environmental Action Plan - TSEAP). Utekelezaji wa suala hili ni takwa la Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 Sura 191. Aidha, Wizara imeendelea kusimamia utunzaji wa mazingira katika miradi ya uchukuzi inayotekelezwa nchini na shughuli za uendeshaji wa njia za usafiri wa anga, ardhini na majini.

**Ufuatiliaji na Tathmini**

215. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendelea kupima ufanisi wa utendaji na kubaini changamoto za kisekta na kuzitafutia suluhisho la kudumu, Wizara ya Uchukuzi kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM– TAMISEMI) zimeendelea kufanya Mikutano ya Tathmni ya Utendaji wa Sekta ya Uchukuzi kwa kila mwaka (Annual Joint Transport Sector Review – JTSR). Kwa mwaka 2025/26 Tathmini hiyo ilifanyika mnamo tarehe 15 – 17 Desemba, 2025 na ilijumuisha washiriki zaidi ya 1,200 kutoka Sekta ya Umma, Sekta Binafsi na washirika wa maendeleo.

216. ***Mheshimiwa Spika,*** miongoni mwa masuala ambayo yametokana na tathmini hizo ni kuhuisha Sera za kisekta, suala ambalo Wizara imeendelea kufanyia kazi pamoja na kutafuta vyanzo mbadala vya kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ambapo baadhi ya miradi imeendelea kutekelezwa kupitia ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Aidha, tathmini hizo zimewezesha kupatikana kwa ushauri stahiki kwa ajili ya kuboresha utendaji na kufikia malengo ya sekta. Sambamba na hilo, Wizara imekuwa ikiandaa na kuwasilisha taarifa ya utendaji wa Wizara kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kila robo mwaka kwa mujibu wa mwongozo na taratibu za Serikali.

217. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Wizara ya Uchukuzi imeanza maandalizi ya ujenzi wa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini (M&E System) ambao utasaidia kuongeza ufanisi wa shughuli za Ufuatiliaji na Tathmini na utunzaji wa takwimu mbalimbali kutoka Sekta ya Uchukuzi. Mfumo huo utaimarisha upatikanaji wa taarifa za miradi ya maendeleo na kuboresha mchakato wa kufanya maamuzi sahihi kuhusu sera na mikakati ya kisekta.

## Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA na Masuala ya Ununuzi

218. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuboresha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kuongeza ufanisi na kutoa huduma kwa wakati. Matumizi ya TEHAMA yameongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato, kuongeza uwajibikaji katika utoaji wa huduma bora na za haraka kwa wananchi. Vilevile, kufuatia kuimarika kwa mifumo ya TEHAMA, Wizara imepunguza matumizi ya shajala na hivyo kupunguza gharama za kudurufu nyaraka mbalimbali katika utendaji wa Wizara.

219. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara imeendelea kutekeleza Miradi ya Kitaifa ya Maendeleo ikiwemo miradi ya ujenzi wa miundombinu ya uchukuzi kama vile ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR, uboreshaji wa viwanja vya ndege na ununuzi wa vyombo vya usafiri vya huduma za uchukuzi kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma na miongozo mbalimbali

ikiwemo matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST) ili kuhakikisha thamani ya fedha za umma inapatikana.

## Rasilimaliwatu na Maendeleo ya Watumishi

220. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara na Taasisi zake imeendelea kuajiri watumishi, ambapo hadi kufikia Machi 2026, jumla ya watumishi 735 waliajiriwa katika Wizara na Taasisi zilizo chini yake na hivyo kupunguza uhaba wa watumishi katika sekta ikiwemo kada adimu za urubani, ubaharia, reli pamoja na wakufunzi katika vyuo vya mafunzo ya kisekta.

221. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kujenga uwezo wa rasilimaliwatu, Wizara na Taasisi zilizo chini yake imeendelea kuwezesha watumishi kuhudhuria mafunzo mbalimbali ya muda mrefu na mfupi ili kuongeza ujuzi na maarifa, kukidhi matakwa ya Kimuundo na kuendana na mabadiliko ya Kiteknolojia, lengo likiwa ni kuboresha utendaji.

Katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara iliwezesha jumla ya watumishi 45 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi ikijumuisha mafunzo ya ubobezi (Masters degree), Kitaaluma (Proffessional Course) na mafunzo mengine ya kujenga uwezo mahali pa kazi. Kati ya hao, watumishi 7 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 38 mafunzo ya muda mfupi. Aidha, Taasisi zilizo chini ya Wizara ziliwezesha jumla ya watumishi 3,415 kuhudhuria mafunzo mbalimbali ya muda mrefu na mfupi.

222. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara na Taasisi zilizo chini yake imeendelea kusimamia utekelezaji wa anuai za jamii ikiwemo kutoa elimu na kuhamasisha upimaji wa hiari kwa Watumishi dhidi ya VVU/UKIMWI na magonjwa mengine yasiyoambukiza. Vilevile, katika kuhimiza mazoezi ya utimamu wa mwili kwa watumishi mahali pa kazi, Wizara na Taasisi zilizochini yake imeendelea kushiriki katika michezo mbalimbali ikiwemo Mashindano ya Shirikisho la Michezo kwa Wizara (SHIMIWI), Bonanza na Mashindano ya Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi). Ushiriki huo umeendelea kuimarisha afya za watumishi

pamoja na kujenga uhusiano mwema kati ya Watumishi wa Wizara na Taasisi nyingine.

### C:5 MAFANIKIO, CHANGAMOTO NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA

### C:5:1 MAFANIKIO

223. ***Mheshimiwa Spika,*** dhamira ya Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi ni kuhakikisha kuwa Watanzania wanapata huduma stahiki ili kuendelea na shughuli zao za uzalishaji wa kila siku. Ili kufikia dhamira hiyo na kwa kuzingatia miongozo ya Serikali na viongozi wa kitaifa, Wizara imeendelea kubuni na kutekeleza mikakati mahsusi ili kuendelea kuboresha utendaji, kuongeza ufanisi na ubora wa huduma.

224. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa ujumla, kutokana na mikakati hiyo Sekta ya Uchukuzi imeendelea kupiga hatua katika kuimarisha shughuli za udhibiti na utoaji wa huduma za usafiri na usafirishaji nchini kwa kuboresha miundombinu ya bandari, reli, viwanja vya ndege, kufundishia pamoja na utoaji wa huduma za hali ya hewa. Naomba niainishe kwa muhtasari mafanikio makubwa yaliyopatikana katika mwaka wa fedha 2025/26 hadi kufikia Machi, 2026 chini ya uongozi mahiri wa Serikali ya Awamu ya Sita kama ifuatavyo:-

**Kuendelea na ujenzi wa Reli ya SGR kwa Awamu zote mbili**

225. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea na ujenzi wa Reli ya SGR kwa awamu zote mbili (2), ambapo Awamu ya Kwanza kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza unaendelea na uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha, ujenzi wa sehemu ya kuunganisha reli hiyo na Bandari ya Dar es Salaam umefikia asilimia 99.09. Vilevile, ujenzi wa Awamu ya Pili kutoka Tabora – Kigoma (km 506) na Uvinza – Musongati (km 300) unaendelea.

226. ***Mheshimiwa Spika,*** kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa SGR katika ushoroba wa kati kutawezesha usafirishaji wa mizigo kwa ufanisi zaidi kutoka Bandari ya Dar es Salaam hadi nchi jirani

zikiwemo DRC, Zambia, Malawi, Burundi, Uganda, Rwanda na Zimbabwe na hivyo kuchochea shughuli za kibiashara kati ya nchi hizo na hatimaye kukuza uchumi wa nchi yetu.

**Kuendelea kwa Ufanisi wa Usafirishaji wa Abiria kupitia Reli ya SGR**

227. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TRC imeendelea na uendeshaji wa reli ya SGR katika usafirishaji wa abiria kati ya Dar es Salaam na Dodoma. Usafirishaji kupitia reli hiyo umezidi kuimarika ambapo katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya abiria wa SGR 2,515,203 walisafirishwa ikilinganishwa na abiria 2,054,828 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2024/25, sawa na ongezeko la asilimia 22.40. Idadi hii ya abiria ni wastani wa abiria 280,000 kwa mwezi, ambayo ni takriban abiria 9,300 kwa siku, sawa na mabasi makubwa 170 kwa siku. Ongezeko hili limechangiwa na huduma bora inayotolewa na ya uhakika.

228. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwenendo huu, inakadiriwa kwamba hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2025/26, zaidi ya abiria milioni 3 watakuwa wamesafirishwa ikilinganishwa na wastani wa abiria 400,000 waliokuwa wanasafirishwa kupitia reli ya MGR kwa mwaka. Kwa upande wa mapato, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Machi 2026, jumla ya Shilingi bilioni 82.77 zimekusanywa kutokana na usafirishaji wa abiria kati ya Dar es Salaam na Dodoma. Aidha, takwimu hizo zinafanya Serikali kuwa imekusanya jumla ya Shilingi bilioni 169.37 tangu kuanza kwa safari za SGR nchini mwezi Juni, 2024.

**Kuanza Usafirishaji wa Mizigo kwa Reli ya SGR**

229. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Hotuba yangu ya mwaka wa fedha 2025/26, niliahidi kuanza huduma ya usafirishaji wa mizigo kupitia reli ya SGR. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali kupitia TRC imekamilisha taratibu zote na mwezi Julai, 2025 ilianza rasmi usafirishaji wa mizigo kupitia Reli ya SGR kati ya Dar es Salaam na Dodoma (Ihumwa). Katika utekelezaji wa hatua hiyo, hadi kufikia mwezi Machi, 2026 jumla ya tani 102,452 za mizigo zilisafirishwa. Aidha, Serikali imeendelea kubuni na kutekeleza

mikakati ya kuongeza upatikanaji wa mizigo ndani ya nchi kwa kuhamasisha Shoroba za Kiuchumi kandokando na sehemu zinazofikika na huduma za miundombinu ya usafirishaji (Transport and Logistics Economic Corridors).

**TRC kuanza kujiendesha bila Ruzuku kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali**

230. ***Mheshimiwa Spika***, kama tunavyofahamu lengo la Serikali ni kuziwezesha taasisi za umma kujiendesha kibiashara na kujitegemea sambamba na kuongeza ufanisi na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi. Hivyo, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa kuanzia Januari, 2026 TRC imefanikiwa kuanza kujitegemea kwa upande wa mishahara na matumizi mengineyo (OC) bila uwezeshaji kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa kipindi cha takriban miaka 10, kiasi cha Shilingi bilioni 12.92 kilikuwa kinatolewa na Serikali kwa TRC kwa ajili ya mishahara kila mwaka. Ufanisi huu umetokana na mikakati thabiti inayoendelea kutekelezwa na TRC ikiwemo uwekezaji mkubwa uliofanyika, usimamizi thabiti wa miradi ya maendeleo pamoja na matumizi ya mifumo ya TEHAMA.

**Kuongeza Uwezo wa Bandari ya Dar es Salaam Kuhudumia Shehena**

231. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendelea kuiongezea uwezo Bandari ya Dar es Salaam katika kuhudumia shehena, Serikali imefanikiwa kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha miundombinu wezeshi katika bandari hiyo kwa ajili ya kupokelea na kusafirisha shehena. Hadi kufikia Machi, 2026 ujenzi wa matanki 15 yenye uwezo wa kuhifadhi mita za ujazo 378,000 za mafuta umefikia asilimia 42 na ujenzi wa magati mawili katika eneo la Malindi yenye urefu wa jumla ya mita 500 utekelezaji wake umefikia asilimia 13.

232. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia, inaendelea na upanuzi wa eneo la Kurasini (Kurasini Port Extension) lenye ukubwa wa mita za mraba 220,000 kwa ajili ya kuhudumia makasha 700,000 kwa mwaka. Kukamilika kwa miradi hii kutachangia kwa kiwango

kikubwa katika kuongeza ufanisi wa shughuli za bandari, kuongeza mapato na hivyo kupanua wigo wa biashara na ushindani wa kimataifa.

**Ufanisi wa ushiriki wa Sekta Binafsi katika Bandari ya Dar es Salaam**

233. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na kuendelea kwa utaratibu wa kushirikisha Sekta Binafsi katika uendeshaji wa bandari nchini hususan Bandari ya Dar es Salaam, ambapo mwaka 2023 iliongeza mwekezaji mpya katika bandari hiyo, Serikali na Taifa kwa ujumla imeendelea kupata manufaa mbalimbali ikiwemo kuongezeka kwa ufanisi wa Bandari ya Dar es Salaam.

234. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia ushirikishwaji huo, shehena inayohudumiwa katika Bandari ya Dar es Salaam pekee imeongezeka hadi kufikia tani milioni 27.76 zilizohudumiwa mwaka wa fedha 2024/25 ikilinganishwa na tani milioni 16.26 mwaka 2020/21. Ongezeko hilo ni ishara kuwa, ushirikishaji wa Sekta Binafsi umeongeza ufanisi wa shughuli za bandari. Aidha, kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 shehena iliyohudumiwa katika Bandari ya Dar es Salaam ilifikia tani milioni 25.07 na inatarajiwa kuongezeka kufikia wastani wa tani milioni 36.0 kwa mwaka 2026/27 na tani milioni 50.2 kwa mwaka 2030/31.

235. ***Mheshimiwa Spika,*** miundombinu ya sasa hususan barabara imezidiwa na ongezeko la shehena na hivyo kusababisha msongamano wa malori. Kutokana na changamoto hiyo ambayo Wizara inaitazama kama fursa, Serikali imeanza kuchukua hatua mbalimbali za muda mfupi na mrefu kwa ajili ya kupunguza msongamano huo. Hatua za muda mfupi ambazo zinaendelea kuchukuliwa na Wizara ni pamoja na: kuhakikisha kuwa Bandari Kavu ya Kwala na Isaka zinatoa huduma kwa ufanisi na kuhamasisha wadau kutumia bandari hizo; na kuendelea na ujenzi wa Bandari Kavu ya Ihumwa.

236. ***Mheshimiwa Spika,*** hatua nyingine zinazoendelea kuchukuliwa ni: kuendelea kubuni na kuanzisha maeneo ya

maegesho kandokando ya reli ya SGR ili malori yaweze kuchukua mizigo kupitia maegesho hayo, ikiwemo eneo la Stesheni ya Morogoro; uendelezaji wa eneo la Bahi ili litumike kama kituo cha kuhamishia mizigo kutoka SGR kwenda MGR; kuanza ujenzi wa reli ya MGR kutoka Ruvu kwenda Stesheni ya mizigo ya SGR Ruvu; kutumia kituo cha Pugu kwa ajili ya kusafirisha mizigo; na kukamilisha ujenzi wa *Port Link* kati ya Bandari ya Dar es Salaam na reli ya SGR. Hatua za muda mrefu zitakazotekelezwa ni pamoja na: ukamilishaji wa ujenzi wa awamu ya kwanza ya reli ya SGR; kujenga reli ya SGR kutoka Bandari kavu ya Kwala hadi Bandari ya Bagamoyo (km 60); na kuendelea na ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo.

237. ***Mheshimiwa Spika,*** manufaa mengine ni pamoja na kuongezeka kwa mapato ya kodi ya forodha yaliyotokana na ongezeko la shehena inayohudumiwa. Mathalan, katika mwaka wa fedha 2024/ 25, mapato yatokanayo na kodi ya forodha za kibandari yalifikia Shilingi trilioni 12.3 sawa na asilimia 40.8 ya mapato ya Shilingi trilioni 30.09 yaliyokusanywa na TRA. Aidha, mapato hayo yataendelea kuongezeka kadri miradi ya kimkakati ya uboreshaji wa bandari inavyoendelea kukamilishwa.

### Kuongezeka kwa shehena inayohudumiwa katika Bandari zote nchini

238. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na maboresho yaliyofanyika katika miundombinu ya bandari nchini, kiwango cha shehena inayohudumiwa katika bandari nchini kimeongezeka kutoka tani milioni 17.78 katika mwaka 2020/21 hadi kufikia tani milioni 32.57 mwaka 2024/25. Shehena hiyo iliyohudumiwa ni zaidi ya lengo lililokuwa limewekwa la kuhudumia tani milioni 30.00 kwa mwaka 2030/32, ambapo lengo hilo limefikiwa kabla ya kipindi husika.

### Kuimarisha usafiri katika Maziwa Makuu

239. ***Mheshimiwa Spika,*** kama tulivyoshuhudia, miongoni mwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais wakati akilihutubia Bunge lako Tukufu tarehe 14 Novemba, 2025 ni kuhakikisha kuwa

wananchi wanapata huduma stahiki za usafiri na usafirishaji hapa nchini. Nilitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, katika kutekeleza maono haya, Serikali imekamilisha ujenzi wa Meli ya MV. New Mwanza katika Ziwa Victoria na meli hiyo ilizinduliwa rasmi tarehe 23 Januari, 2026 jijini Mwanza na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na tayari imeanza kutoa huduma. Meli hii ni kubwa kuliko zote katika ukanda wa Maziwa Makuu ikiwa na kimo cha ghorofa nne (4), urefu wa mita 92.6 na uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo. Meli hii pia ina kasi ya *knots* 16, sawa na mwendokasi wa kilomita 30 kwa saa na hivyo imepunguza muda wa safari kati ya Mwanza na Bukoba kutoka saa nane (8) hadi takriban saa sita (6).

240. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imekamilisha ukarabati wa meli ya MT. Sangara ambayo imeanza kufanya safari zake. Meli hii, inafanya safari kwa kusafirisha shehena ya mafuta kati ya Kigoma na Kalemie nchini DRC ikiwa na uwezo wa kubeba tani 350 za mafuta ambazo ni sawa na lita 410,000. Aidha, ukarabati wa meli ya MV. Liemba yenye uwezo wa kusafirisha abiria 600 na tani 200 za mizigo unaendelea vizuri.

241. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza huduma za usafiri wa meli katika Ziwa Tanganyika, Serikali kupitia TPA imekamilisha ujenzi wa Meli nne (4) za kisasa za mizigo katika Ziwa katika hatua za Tanganyika, ambazo kwa sasa ziko mwisho za majaribio. Meli hizo zimejengwa kwa utaratibu wa ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP). Meli hizo zina uwezo wa kubeba tani 2,000 kila moja, ambapo zitasaidia kuchochea biashara na usafirishaji kati ya Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC). Kuanza kufanya kazi kwa meli hizo kutapunguza uhaba wa meli za mizigo katika Ziwa Tanganyika.

**Kuongezeka kwa mtandao wa Vituo vya Usafiri wa Anga vinavyohudumiwa na ATCL**

242. ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na juhudi za Serikali katika kuimarisha utendaji wa ATCL, Kampuni hiyo imeendelea kuongeza vituo vya huduma ya usafiri wa anga ambapo hadi

kufikia Machi, 2026 ina jumla ya vituo 33 ikilinganishwa na vituo 23 vilivyokuwepo mwaka 2020/21. Kati ya vituo 33, Vituo 16 ni vya ndani ya nchi ambavyo ni Arusha, Bukoba, Dar es Salaam, Dodoma, Geita, Kilimanjaro, Kigoma, Mbeya, Mpanda, Mwanza, Iringa, Mtwara, Songea, Tabora, Pemba, na Zanzibar; Vituo (14) ni vya kikanda ambavyo ni Bujumbura, Entebbe, Cape Town, Kinshasa, Victoria Falls, Accra, Lagos, Hahaya, Harare, Lusaka, Ndola, Nairobi, Lubumbashi na Johannesburg; na Vituo vitatu (3) ni vya kimataifa ambavyo ni Dubai, Guangzhou na Mumbai.

**Kuimarika kwa Huduma za Usafiri wa Anga kupitia ATCL**

243. ***Mheshimiwa Spika,*** uendeshaji wa Kampuni ya ATCL umeendelea kuimarika mwaka hadi mwaka katika utoaji wa huduma za usafiri wa anga kutokana na dhamira ya Serikali ya kuendelea kuimarisha na kuiboresha kampuni hiyo ili iendelee kuhudumia soko la ndani na la kimataifa. Mathalan, katika mwaka 2021/22 ATCL ilikuwa na ndege tisa (9), ambapo hadi sasa Kampuni hiyo ina ndege 16 ikijumuisha ndege moja ya mizigo yenye uwezo wa kusafirisha tani 54 za mizigo kwa wakati mmoja.

244. ***Mheshimiwa Spika,*** ongezeko la ndege hizo limewezesha kampuni ya ATCL kuongeza mapato hadi kufikia Shilingi bilioni 626.5 kwa mwaka 2024/25 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 175.69 zilizokusanywa mwaka 2020/21. Mapato hayo yameendelea kuongezeka ambapo kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi kufikia Machi, 2026 mapato yaliyokusanywa na ATCL yalifikia Shilingi bilioni 501.62 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 406.23 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2024/25.

**Mkakati wa Kuongeza Ajira na Mapato kupitia LATRA**

245. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia LATRA imeendelea kutekeleza Kanuni ya Huduma za Usafiri wa Kukodi ya mwaka 2020, ambayo inasimamia huduma ya usafiri wa kukodi, ukiwemo wa pikipiki (bodaboda na bajaji). Katika kuongeza ufanisi wa kutekeleza kanuni hizi, mwaka 2023 Serikali ilizifanyia marekebisho kupitia Tangazo Na.254 ili kuruhusu mawakala wa aina nne (4) kutoa na kuhuisha leseni za usafiri wa kukodi. Mawakala

walioruhusiwa ni: Taasisi za umma; Vyama vya ushirika; Kampuni na Watu binafsi. Kupitia ubunifu huu, kwa kipindi cha kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya leseni 249,768 zimetolewa na mawakala 72 na Shilingi bilioni 3.02 zimekusanywa kupitia utaratibu huu ambapo jumla ya ajira 310 zimezalishwa.

**Kuimarika kwa Huduma za Viwanja vya Ndege**

246. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza mtandao wa viwanja vya ndege ili kuimarisha safari za ndege ndani ya nchi, Serikali imeendelea na ujenzi na uboreshaji wa viwanja vya ndege vya mikoa nchini. Hadi kufikia Machi, 2026 Serikali imekamilisha ukarabati wa viwanja vya ndege vya Sumbawanga, Shinyamga, Songea na Tabora. Kukamilika kwa miradi hii kumefungua fursa mbalimbali za kiuchumi katika mikoa husika, kurahisisha huduma za usafiri na pia kuchochea biashara kwa mashirika ya ndege.

247. ***Mheshimiwa Spika***, katika hatua nyingine za kuendelea kuchochea utalii nchini, Serikali imekamilisha Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Serengeti. Mradi huu unalenga kuboresha usafirishaji, kuimarisha utalii pamoja na kulinda ikolojia ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kwa kuwa umesanifiwa kuzingatia utunzaji wa mazingira (green airport) na utaepusha usumbufu wa kelele za kuruka na kutua kwa ndege katika maeneo yaliyomo ndani ya hifadhi hiyo.

248. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuchukua mikakati mbalimbali ya kuimarisha miundombinu ya viwanja vya ndege vilivyopo, kikiwemo Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA). Katika kutekeleza mkakati huu, TAA kwa kushirikiana na Sekta Binafsi imekamilisha ukarabati mkubwa wa jengo la kuhifadhi mizigo inayoharibika haraka (perishables) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro. Hii itawezesha wafanyabiashara wa ndani kuwa na uhakika wa huduma bora na fanisi za kuhifadhi na kusafirisha shehena zao kwenda nje ya nchi na hivyo kuchochea kuimarika kwa mnyororo wa usafirishaji na ukuaji wa uchumi.

## Utekelezaji wa Mpango wa Maboresho ya Mifumo ya Usalama katika Viwanja vya Ndege na Huduma za Uhamiaji (APIS)

249. ***Mheshimiwa Spika,*** tasnia ya usafiri wa anga imeendelea kuwa eneo linalohitaji mifumo madhubuti ya udhibiti katika maeneo mbalimbali, ikiwemo uchambuzi wa taarifa za wasafiri. Ili kuimarisha uwezo wa nchi kutambua na kudhibiti vihatarishi vinavyoweza kuathiri usalama wa safari za ndege, Serikali imeanza utekelezaji wa Mpango wa Maboresho ya Mifumo ya usalama katika viwanja vya ndege na huduma za uhamiaji (Advanced Passenger Information System - APIS). Utekelezaji huu ni kwa mujibu wa Kiambatisho cha 9 cha Shirika la Usafiri wa Anga Duniani - ICAO (Annex 9 of International Civil Aviation Organization - ICAO).

250. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji kwa awamu ya kwanza umeanza katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA) na utaendelea katika viwanja vingine vya: Kilimanjaro International Airport (KIA); Abeid Amani Karume International Airport (AAKIA); na Mwanza Airport. Kwa ujumla, mfumo huu ni muhimu kwa Taifa letu kwa kuwa, pamoja na manufaa mengine utaimarisha usalama wa Taifa kwa kubaini mapema abiria hatarishi, unaongeza ufanisi wa udhibiti wa mipaka, unarahisisha usafiri wa anga na kupunguza ucheleweshaji viwanjani, unaongeza uaminifu wa kimataifa na hivyo kuvutia wawekezaji na utalii nchini. Pia mfumo huu unaiwezesha nchi kukidhi viwango vya kimataifa katika kushirikiana na mashirika ya kimataifa kama Shirika la Forodha Duniani (World Customs Organization) katika kubadilishana taarifa za kiusalama.

## Kuanza Kutolewa kwa Mafunzo ya Urubani Nchini

251. ***Mheshimiwa Spika***, kama nilivyoahidi katika Hotuba yangu ya mwaka 2025/26 kuwa Serikali itaanza rasmi kutoa mafunzo ya urubani katika Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT). Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali kupitia Chuo cha NIT imeanza rasmi kutoa mafunzo ya urubani mwezi Julai 2025, ambapo wanafunzi 22 wamedahiliwa na wanaendelea na

masomo. Mafanikio hayo yamewezesha kupunguza gharama za masomo nje ya nchi kwa kozi za urubani. Kuanza kutolewa kwa mafunzo hayo ni utekelezaji wa maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuimarisha usafiri wa anga.

252. ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mengine yaliyopatikana katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/26 hadi Machi, 2026 ni pamoja na:-

i. Serikali kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Kikanda cha Kuratibu Utafutaji na Uokoaji (Maritime Rescue Coordination Centre – MRCC) katika Ziwa Victoria Mwanza kwa kushirikiana na Serikali ya Uganda. Kituo hiki kitaimarisha usalama wa usafiri majini katika Ziwa Victoria kwa kutumia mifumo ya kisasa ya mawasiliano na kinatarajiwa kuzinduliwa rasmi tarehe 21 Mei, 2026 kupitia uratibu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki;

ii. Kununuliwa kwa Boti maalum ya wagonjwa (Ambulance Boat) kwa ajili ya kutoa huduma katika Ziwa Victoria, ambayo tayari imeanza kufanya kazi. Pamoja na boti hiyo, Serikali imenunua Boti nne (4) za utafutaji na uokoaji na kuanza kutoa huduma katika Ziwa Tanganyika (Boti 1), Ziwa Victoria (Boti 2) na Ukanda wa Bahari ya Hindi (Boti 1 – Tanga), hatua inayoongeza uwezo wa Taifa letu katika kukabiliana na majanga ya majini;

iii. Kuanza kwa maandalizi ya ujenzi wa Bandari kubwa na ya kisasa ya Bagamoyo, ambapo awamu ya kwanza itahusisha ujenzi wa gati lenye urefu wa kilomita 1.32 kwa ajili ya kuhudumia meli kubwa za kisasa (Megamax);

iv. Kuendelea kwa ufanisi na ujenzi wa Bandari ya Kisiwa Mgao - Mtwara kwa ajili ya kuhudumia shehena ya kichele (dry bulk cargo) kama vile makaa ya mawe na saruji. Hadi kufikia Machi, 2026 mradi umefikia asilimia 42 ya utekelezaji na kukamilika kwake kutaimarisha ufanisi wa Bandari ya Mtwara pamoja na usalama na utunzaji wa mizigo;

v. Kuendelea kutoa huduma za usafirishaji wa mizigo masafa marefu baharini kupitia Kampuni ya SINOTASHIP, ambapo imeongeza njia za meli (shipping routes) kutoka tatu (3) hadi tano (5) na kuwezesha kuhudumiwa kwa jumla ya TEUs 289,387 za mizigo;

vi. Kusainiwa kwa Mkataba wa Ufufuaji na Uboreshaji wa Reli ya TAZARA kati ya Serikali za Tanzania na Zambia, kwa kushirikiana na Kampuni ya CCECC ya China;

vii. Kukamilisha ufungaji wa mitambo ya sauti baina ya waongoza ndege na marubani katika viwanja vya ndege 12 ambavyo ni: Dar es Salaam; Unguja–Zanzibar; Pemba; Kilimanjaro; Dodoma; Iringa; Mwanza; Tabora; Tanga; Kigoma; Bukoba; na Arusha, pamoja na vituo vya mawasiliano 18 ambavyo ni Mwaseni, Lubuli, Gairo, Ngiloli, Nyamanyama, Moroninya, Nambunga, Ndisso–Sitalike, Kitulo, Kaluwe, Lolkisale, Oldean Malanja, Matogoro, Mwisi, Mugumu Town, Muganza, Kwenjugo na Michakaini;

viii. Taasisi za kimataifa kuendelea kuiamini Tanzania na kuiwezesha katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati kutokana na uongozi mahiri wa Serikali ya Awamu ya Sita. Kutokana na hatua hii, NIT imeendelea kupokea fedha kutoka Benki ya Dunia, ambazo zimewezesha ujenzi wa kihistoria katika Chuo hicho. Kupitia mradi huo, kwa sasa majengo matano (5) yamekamilika kujengwa kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa mafunzo ya taaluma za anga na operesheni za usafirishaji. Majengo hayo yanajumuisha: Jengo kuu la Kituo cha Umahiri (Center of Excellence); Jengo la mafunzo ya wahudumu wa ndani ya ndege; Jengo la maabara ya kisasa ya mafunzo ya uhandisi wa matengenezo ya ndege; na Mabweni mawili (2) yenye uwezo wa kukidhi mahitaji ya malazi kwa wanafunzi 1,504;

ix. Kuanza kwa hatua za awali za ujenzi wa Kiwanja kipya cha ndege cha Mkoa wa Kagera katika eneo la Kyabajwa wilayani Missenyi. Kiwanja hicho kitakuwa na uwezo wa kuhudumia ndege kubwa zenye kubeba abiria 220 (Daraja

4C). Kwa sasa, Serikali imekamilisha ununuzi wa Mshauri Elekezi ambaye anaendelea na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina;

x. Kujengwa kwa mfumo wa TEHAMA wa LATRA wa Utoaji Leseni za Usafiri wa Reli na Barabara (Railway and Road Information Management System - RRIMS). Mfumo huo unawezesha upatikanaji wa huduma zinazodhibitiwa kwa njia ya mtandao pasipo kulazimika kufika katika ofisi za LATRA. Aidha, mfumo huu unatumika kusajili madereva na wahudumu wa mabasi; kufanya malipo; kutoa taarifa za udhibiti; na kutoa mrejesho kwa wateja;

xi. Chuo cha DMI kukidhi sifa za kuendelea kuwa katika orodha ya vyuo bora duniani (IMO Whitelist) vinavyotoa mafunzo ya usafiri majini ikiwemo ubaharia;

xii. Kuendelea kukuza fursa za ajira nchini kupitia Chuo cha DMI kwa vijana kuunganishwa na kampuni za meli za ndani na nje ya nchi. Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya vijana 77 wameunganishwa katika kampuni mbalimbali za meli nje ya nchi. Kati ya hao 48 wamejiunga na Kampuni ya Danaos Shipping Company ya nchini Ugiriki, 16 wamejiunga na kampuni ya uvuvi nchini Korea Kusini na 13 wamefanya mafunzo kwa vitendo nchini Korea Kusini. Aidha, jumla ya vijana 48 wamepata ajira ndani ya nchi kupitia meli nne (4) zinazojengwa ziwa Tanganyika mkoani Kigoma na Kampuni ya Zijin Mining Company;

xiii. Kuimarisha utoaji wa huduma za hali ya hewa kwa kupanua mtandao wa vituo vya hali ya hewa kwa kununua na kufunga mitambo, vifaa na mifumo ya hali ya hewa ikiwemo vituo nane (8) vya hali ya hewa vinavyojiendesha (Automatic Weather Station - AWS) na vituo viwili (2) vya AVIMET na ufungaji wa mfumo wa uandaaji utabiri (Complete Forecasting System); na

xiv. Tanzania kuendelea kuaminiwa kimataifa, ambapo kutokana na hali hiyo nchi yetu kupitia TMA imechaguliwa kuwa mwenyeji wa mikutano miwili ya ngazi za juu ya Taasisi zinazosimamia masuala ya hali ya hewa na mabadiliko ya tabianchi duniani. Moja ya mikutano hiyo ni Mkutano wa Wataalam wa WMO unaolenga kuboresha miongozo ya utabiri wa hali ya hewa, ambao utafanyika katika bara la Afrika kwa mara ya kwanza. Mikutano hiyo inatarajiwa kufanyika Jijini Arusha na kuhudhuriwa na zaidi ya washiriki 200 kutoka nchi wanachama wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO). Aidha, mkutano huo unatarajiwa kuhudhuriwa na viongozi wakuu wa Shirika hilo, ambayo ni fursa pia kwa nchi yetu.

### C:5:2 CHANGAMOTO

253. ***Mheshimiwa Spika,*** Changamoto zilizojitokeza katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2025/26 ni pamoja na:-

i. Mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya miundombinu na utoaji wa huduma za uchukuzi na hali ya hewa;

ii. Mabadiliko ya tabianchi (Climate Change) yanayosababisha mifumo ya hali ya hewa kubadilika mara kwa mara na kusababisha uharibifu wa miundombinu ya uchukuzi kutokana na mafuriko;

iii. Changamoto za athari za vita zinazoendelea duniani hivyo kuathiri bei za bidhaa zinazoingizwa nchini pamoja na mnyororo wa thamani unaotegemea bidhaa hizo;

iv. Uhaba wa wataalam wenye ujuzi na uzoefu katika sekta ndogo za usafiri kwa njia ya maji, anga, reli na hali ya hewa; na

v. Uvamizi, uharibifu na hujuma kwenye miundombinu ya reli, hususan katika reli zenyewe, mataruma, vifungio na madaraja.

## C:5:3 MIKAKATI YA UTATUZI WA

## CHANGAMOTO

254. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka 2025/26, hatua mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa zikiwemo: -

i. Kuendelea kujadiliana na wawekezaji mbalimbali ikiwa ni pamoja na Taasisi za kifedha ili kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo. Pia, Serikali kuendelea kushawishi Sekta Binafsi kuwekeza katika uendelezaji na uendeshaji wa miradi ya uchukuzi;

ii. Kuendelea kuimarisha huduma za hali ya hewa ikiwemo kufunga rada za hali ya hewa na kupanua mtandao wa vituo vya hali ya hewa ili kuongeza usahihi wa utoaji wa tahadhari ya matukio ya hali mbaya ya hewa;

iii. Kuendelea kufanya ukarabati wa mara kwa mara katika maeneo korofi ya reli ya MGR na CGR;

iv. Kuendelea kuimarisha miundombinu ya uchukuzi ili kupunguza athari zinazoweza kutokea kutokana na mabadiliko ya uchumi wa dunia;

v. Kuendelea kuvijengea uwezo Vyuo vya Kitaaluma vya Sekta ya Uchukuzi kwa kutoa mafunzo kwa wakufunzi, kuimarisha miundombinu na ununuzi wa vifaa vya kufundishia vinavyoendana na teknolojia ya kisasa ili kuzalisha wataalam wanaokidhi mahitaji ya sekta kitaifa na kimataifa;

vi. Kuendelea kushirikiana na vyombo vya Ulinzi na Usalama pamoja na jamii inayozunguka maeneo ya reli pamoja na kutoa elimu na hamasa kwa jamii inayopakana na maeneo hayo ili kuelewa umuhimu wa reli na kuwa walinzi wa miundombinu hiyo; na

vii. Kufanya tafiti mbalimbali zitakazosaidia kubaini athari za mabadiliko ya hali ya hewa kwa ajili ya usanifu wa miundombinu stahiki.

**D. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/27**

255. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kutekeleza majukumu ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2026/27, Wizara imezingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Dira 2050, Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2025, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP IV 2026/27 – 2030/31), Mpango wa Taifa wa Maendeleo kwa mwaka 2026/27, Mpango Mkakati wa Wizara wa Miaka Mitano (2026/27 – 2030/31) pamoja na maelekezo ya viongozi wakuu wa Serikali.

256. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Uchukuzi katika Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2026/27 imepanga kutekeleza vipaumbele mbalimbali vikiwemo: Kuendelea na ujenzi na uendeshaji wa Reli ya Kisasa ya SGR; Kuendelea na ukarabati na uboreshaji wa Reli ya *Meter Gauge Railway (MGR)*; na Reli ya TAZARA ya *Cape Gauge Railway (CGR)*; Kuendelea na uboreshaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL); Uboreshaji wa miundombinu na huduma katika Bandari za Bahari ya Hindi, Maziwa Makuu pamoja na Bandari Kavu; Kuendelea na ujenzi, ukarabati na uboreshaji wa viwanja vya ndege nchini; Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa meli; Kuendelea kuboresha miundombinu na huduma za hali ya hewa; Kuboresha udhibiti, ubora na usalama wa huduma za uchukuzi; na Kuendelea na uboreshaji wa vyuo vya mafunzo vya kisekta.

257. ***Mheshimiwa Spika,*** vipaumbele vingine vitakavyotekelezwa na Wizara ni: Kuimarisha matumizi ya teknolojia katika Sekta ya Uchukuzi ili kuongeza ufanisi wa uendeshaji na utoaji wa huduma; Kuimarisha ushiriki wa Sekta Binafsi katika uendelezaji wa miundombinu na utoaji wa huduma za uchukuzi nchini; Kuendelea kuboresha sera na sheria ili kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara katika sekta; na

kujenga uwezo wa rasilimaliwatu ili kuongeza ufanisi na tija katika utendaji wa sekta.

258. ***Mheshimiwa Spika,*** katika utekelezaji wa shughuli za Wizara na miradi ya maendeleo ya kipaumbele, Wizara ya Uchukuzi (Fungu 62) katika mwaka wa fedha 2026/27 imetengewa jumla ya **Shilingi 2,872,738,082,000** ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi 126,041,236,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, sawa na asilimia 4.38 ya bajeti na **Shilingi 2,746,696,846,000** ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, sawa na **asilimia 95.62**.

259. ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya **Shilingi 126,041,236,000** zilizotengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, **Shilingi 100,135,087,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya watumishi, na **Shilingi 25,906,149,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo kwa Wizara na Taasisi zinazopokea Ruzuku kutoka Serikalini. Aidha, kati ya **Shilingi 2,746,696,846,000** zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, **Shilingi 2,452,512,444,000** ni fedha za ndani, sawa na **asilimia 89.29** na **Shilingi 294,184,402,000** ni fedha za nje, sawa na **asilimia 10.71** ya bajeti ya maendeleo. Miradi ya maendeleo na shughuli zitakazotekelezwa kwa mwaka wa fedha 2026/27 ni kama ifuatavyo:-

## D:1 MIRADI YA MAENDELEO ITAKAYOTEKELEZWA KATIKA MWAKA 2026/27

260. ***Mheshimiwa Spika,*** Miradi ya kielelezo na kimkakati itakayotekelezwa kwa mwaka wa fedha 2026/27 inajumuisha sekta ndogo za bandari, reli, anga, usafiri majini, hali ya hewa na mafunzo ya kisekta.

### Mradi wa Uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam (DMGP)

261. ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu kwa mwaka wa fedha 2026/27 umetengewa **Shilingi bilioni 120.74** ambazo ni fedha za nje. Fedha hizo zitatumika katika kuendelea kufanya maboresho mbalimbali ya Bandari ya Dar es Salaam. Shughuli

zitakazotekelezwa ni pamoja na: Kukarabati eneo la kupangia shehena (stacking area) katika Gati Na. 1 – 7; Kufunga na kusambaza umeme ili kukidhi mahitaji ya sasa katika Gati Na. 1 – 7 na RoRo; Kuwezesha kuanza Ujenzi wa Gati 12 – 15 na Kuwezesha huduma za ushauri kwa ajili ya usanifu na usimamizi.

**Mradi wa Uboreshaji wa Bandari ya Kigoma**

262. ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa uboreshaji wa Bandari ya Kigoma umetengewa **Shilingi bilioni 16.42** fedha za nje katika mwaka wa fedha 2026/27. Mradi huu unahusisha ukarabati wa barabara ya kuingilia, gati la abiria pamoja na jengo la abiria. Utekelezaji wa Mradi huu utawezesha kufanyika kwa biashara kwa ufanisi katika Bandari ya Kigoma na hivyo nchi yetu kuendelea kutumia fursa za kikanda katika kuinua uchumi wa wananchi wake.

**Mradi wa Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza**

263. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, mradi huu umetengewa **Shilingi bilioni 6.0** fedha za ndani kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa jengo la abiria na miundombinu yake katika Kiwanja cha Ndege cha Mwanza. Aidha, Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi inaratibu mazungumzo kati ya TAA na Taasisi za kifedha za Serikali kwa ajili ya kufadhili ukarabati na upanuzi wa kiwanja hiki. Mradi huu unahusisha ujenzi wa jengo lenye uwezo wa kuhudumia abiria milioni 2.5 kwa mwaka wakiwemo abiria wa kimataifa. Mradi huu pia unajumuisha uboreshaji wa miundombinu wezeshi itakayosaidia ndege kubwa za kimataifa kutumia kiwanja hicho.

**Mradi wa Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Arusha**

264. ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu umetengewa **Shilingi bilioni 3.08** fedha za ndani katika mwaka wa fedha 2026/27. Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na: Kuendelea na ujenzi wa karakana ya ndege ya kilimo anga; na ujenzi wa tabaka la juu la lami katika barabara ya kuruka na kutua ndege kwa lengo la kuongeza ufanisi wa huduma kwa mashirika ya ndege na abiria.

### Mradi wa Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mtwara

265. ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu umetengewa kiasi cha **Shilingi bilioni 3.48** fedha za ndani katika mwaka wa fedha 2026/27 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali zikiwemo ujenzi wa jengo jipya la abiria, jengo la kuongozea ndege, kituo cha zimamoto na kituo cha hali ya hewa. Utekelezaji wa miradi hii utakamilisha awamu ya pili ya ukarabati na upanuzi wa Kiwanja hiki baada ya Serikali kukamilisha ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, barabara ya kiungio, eneo la maegesho ya ndege, barabara za kuingia kiwanjani na maegesho ya magari kwa kiwango cha lami; ujenzi wa uzio wa usalama na ufungaji wa mfumo wa taa za kuongozea ndege (AGL) ambavyo vimewezesha kiwanja kuweza kutumika katika majira yote ya mwaka kwa saa 24.

### Mradi wa Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Serengeti

266. ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 100.0** fedha za ndani kwa ajili ya kuratibu maandalizi ya utekelezaji wa Mradi. Utekelezaji wa Mradi huu utahusisha ushirikishwaji wa taasisi za kifedha na Serikali. Aidha, Mradi huu unalenga kulinda ikolojia ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kwa kuwa umesanifiwa kuzingatia utunzaji wa mazingira (green airport) ambayo kwa ujumla wake itachochea ukuaji wa shughuli za utalii nchini.

### Mradi wa Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mkoa wa Kagera

267. ***Mheshimiwa Spika,*** Mkoa wa Kagera ndio mkoa pekee unaopakana na nchi tatu (3) katika ukanda wa Maziwa Makuu, ambazo ni Uganda, Burundi na Rwanda. Mkoa huu una migodi ya madini ya kimkakati kama Mgodi wa Nikeli Kabanga, vivutio mbalimbali vya utalii na reli nyingi zinazotarajiwa kujengwa kuelekea Burundi na Rwanda zitapitia katika mkoa huu. Katika kuboresha huduma za usafiri wa anga zitakazoendana na mnyororo wa shughuli nyingine za kiuchumi na pia kuimarisha usalama wa usafiri wa anga, Serikali ya Awamu ya Sita imeamua

kwa dhati kujenga kiwanja cha ndege cha Mkoa wa Kagera katika eneo la Kyabajwa. Katika mwaka wa fedha 2026/27, Mradi huu umetengewa **Shilingi bilioni 1.9** fedha za ndani kwa ajili ya kukamilisha Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina na kuanza ujenzi wa kiwanja kipya cha ndege cha Mkoa wa Kagera katika eneo la Kyabajwa, Wilaya ya Missenyi.

**Mradi wa Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro – KIA**

268. ***Mheshimiwa Spika,*** ukarabati wa kiwanja hiki umetengewa **Shilingi bilioni 32.0** fedha za ndani katika mwaka wa fedha 2026/27 kwa ajili ya: kuendelea na awamu ya pili ya ukarabati mkubwa wa njia ya kuruka na kutua ndege pamoja na: Ufungaji wa mfumo wa taa za kuongozea ndege; Ujenzi wa uzio kuzunguka mipaka ya eneo la KIA; na Ujenzi wa jengo la utawala na watoa huduma. Aidha, kufuatia jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita za kukuza utalii nchini imepelekea idadi ya watalii kuongezeka katika Kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro. Kufuatia ongezeko hilo, Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa Jengo la Pili la abiria na kwa sasa ununuzi wa Mkandarasi upo hatua za mwisho. Ujenzi wa Jengo hili ambao unatarajiwa kutekelezwa kwa ushirkiano kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo, utaongeza uwezo wa Kiwanja kuhudumia watalii wengi zaidi, kuimarisha ubora wa huduma zinazotolewa katika Kiwanja na pia kuimarisha ushoroba wa utalii.

**Mradi wa Uboreshaji na Upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA)**

269. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Serikali imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 26.75** fedha za ndani kwa ajili ya: Uboreshaji na ujenzi wa majengo ya abiria; Uboreshaji wa mfumo wa taa za kuongozea ndege; Ujenzi wa eneo maalum la usalama kwenye barabara ya kuruka na kutua ndege; ununuzi na ufungaji wa mitambo na mifumo ya TEHAMA ya kuimarisha ulinzi na usalama wa viwanja vya ndege; na Ujenzi wa uzio wa ndani wa usalama.

## Mradi wa Uendelezaji wa Viwanja vya Ndege vya Mikoa

270. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 14.38** fedha za ndani kwa ajili ya ujenzi, ukarabati, upanuzi na uboreshaji wa viwanja vya ndege katika mikoa mbalimbali ili kuviwezesha kutoa huduma bora. Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na: Ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Lindi; Ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Moshi; Ujenzi wa jengo la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Musoma; Ukarabati na uboreshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Singida; Ufungaji wa mfumo wa taa za kuongozea ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Mafia; Ununuzi wa magari mawili ya zimamoto kwa ajili ya viwanja vya ndege vya Shinyanga na Sumbawanga; na Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Njombe kutokana na uwepo wa mazao ya mbogamboga, matunda na maua.

## Mradi wa Kuwezesha Taasisi (Institutional Support)

271. ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 38.10** katika mwaka wa fedha 2026/27 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali zikiwemo: Uendeshaji wa Jengo la Tatu la Abiria katika Kiwanja cha Ndege cha JNIA; Kuanza uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato; na Kuanza ujenzi wa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika kampasi za Chuo cha Bahari Dar es Salaam katika maeneo ya Kimbiji – Kigamboni na Kikwetu – Lindi. Mradi huu vilevile, utahusisha kuendelea kulipa fidia kwa wananchi waliopisha uendelezaji wa viwanja mbalimbali vya ndege vikiwemo: Singida, Julius Nyerere - JNIA, Simiyu, Masasi, Sumbawanga, Nachingwea na Kilwa Masoko.

## Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Meli

272. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 171.00** fedha za ndani. Fedha hizi ni kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali zinazojumuisha: ujenzi wa meli mpya ya mizigo yenye uwezo wa kubeba tani 3,500 katika Ziwa Tanganyika; kuanza ujenzi wa meli

mbili (2) za mafuta katika Ziwa Tanganyika zenye uwezo wa kubeba lita 600,000 kila moja; ujenzi wa meli mpya yenye uwezo wa kubeba abiria 600 na mizigo tani 400 katika Ziwa Tanganyika; ujenzi wa meli mpya ya mizigo yenye uwezo wa kubeba tani 3,000 katika Ziwa Victoria; kukamilisha Upembuzi Yakinifu kwa ajili ya kuiwezesha Kampuni ya Meli Tanzania (TASHICO) kufanya biashara katika Bahari ya Hindi; na ujenzi wa kiwanda cha kujengea meli chenye uwezo wa kuhimili meli zenye uzito wa tani 5,000 katika Ziwa Tanganyika.

273. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi mingine itakayotekelezwa na TASHICO ni: ukarabati Mkubwa wa meli ya MV. Mwongozo katika ziwa Tanganyika; ukarabati wa Meli ya MV. Liemba katika Ziwa Tanganyika; Kuendelea na ukarabati wa meli za MT. Nyangumi na MV. Clarias katika ziwa Victoria; ununuzi wa Mabehewa ya kubeba mizigo katika meli ya MV. Umoja katika Ziwa Victoria; kugharamia ununuzi wa boti za uokoaji katika Maziwa Makuu; uboreshaji wa mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya ukusanyaji mapato; na ukarabati wa Meli ya MV. Songea katika Ziwa Nyasa.

**Mradi wa Ukarabati wa Reli ya TAZARA**

274. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka wa fedha 2026/27, mradi huu unatarajia kutumia **Shilingi bilioni 12.32** fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali zikijumuisha matengenezo ya miundombinu ya reli, ununuzi wa vipuri kwa ajili ya matengenezo ya vichwa vya treni, unununzi na ufungaji wa mfumo wa tiketi mtandao na mtambo wa ukaguzi wa abiria na vifurushi.

**Mradi wa Ukarabati wa Miundombinu ya Reli kupitia Mfuko wa Reli**

275. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, **Shilingi bilioni 294.80** fedha za ndani na **Shillingi bilioni 5.18** fedha za nje zimetengwa kupitia Mfuko wa Reli kwa ajili ya: Kufanya ukarabati na matengenezo ya njia ya reli ya MGR; Ununuzi wa vichwa vya treni, mabehewa na mitambo; Ununuzi wa vifaa na

malighafi kwa ajili ya matengenezo ya reli; Uboreshaji wa mifumo ya TEHAMA na umeme katika njia ya reli; Upimaji na uwekaji wa uzio na alama katika maeneo ya reli; Upembuzi Yakinifu wa ujenzi wa reli ya kisasa ya mjini katika Jiji la Dar es Salaam; na Ujenzi wa chuo cha kisasa cha reli.

**Mradi wa Ujenzi wa Reli ya SGR**

276. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Mradi huu umetengewa **Shilingi trilioni 1.51** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 61.84** fedha za nje kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali. Shughuli zitakazotekelezwa zinajumuisha: Kufanya matengenezo ya kawaida katika kipande cha Dar es Salaam – Makutupora; Kukamilisha kipande cha Morogoro – Makutupora; Kuendelea na ujenzi wa vipande vya Makutupora – Tabora, Tabora – Isaka, Mwanza – Isaka, Tabora – Kigoma na Uvinza – Musongati; Ununuzi wa vitendea kazi vikiwemo vichwa vya treni, mabehewa, mitambo, mashine, vipuri na vifaa vya matengenezo; Kugharamia utekelezaji, ufuatiliaji na usimamizi wa masuala ya mazingira na jamii; pamoja na kugharamia usimamizi na ufuatiliaji wa ujenzi wa reli ya SGR.

**Mradi wa Ukarabati wa Reli ya MGR – *Tanzania Intermodal Railway Project – TIRP II***

277. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, mradi huu umetengewa **Shilingi bilioni 89.90** fedha za nje kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali zikiwemo: Ukarabati wa reli ya MGR kipande cha Dar es Salaam – Tabora; Ukarabati wa reli ya MGR kwa kipande cha Tabora – Isaka; Kugharamia huduma za Ushauri (consultancy services); Kufanya Upembuzi Yakinifu wa ukarabati wa miundombinu ya reli katika vipande vya Kilosa – Mikumi, Tanga – Arusha, na Kilosa – Gulwe – Igandu.

**Mradi wa Rada, Vifaa na Miundombinu ya Hali ya Hewa**

278. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa **Shilingi bilioni 13.50** fedha za ndani na **Shilingi milioni 111.38** fedha za nje kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika mwaka wa

fedha 2026/27. Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na: Kukamilisha ufungaji wa rada mbili (2) katika mikoa ya Dodoma na Kilimanjaro pamoja na ujenzi wa miundombinu yake; Kuimarisha mtandao wa rada tano (5) za hali ya hewa za Dar es Salaam, Mwanza, Mtwara, Kigoma na Mbeya; na Ufungaji wa vifaa vitatu (3) vya uangazi katika Bahari ya Hindi vitakavyofungwa Zanzibar, Dar es Salaam na Bagamoyo.

279. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli nyingine zitakazotekelezwa kupitia Mradi huu ni: Kukamilisha ujenzi wa maabara ya taifa ya uhakiki wa vifaa vya hali ya hewa; Kukamilisha ujenzi wa jengo la Kituo cha Kanda ya Mashariki pamoja na Kituo cha Kufuatilia Masuala ya Tsunami; Kuanza ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mamlaka ya Hali ya  Hewa Dodoma; Kuanza ujenzi wa bweni na jengo la utawala katika Chuo cha Taifa cha Hali ya Hewa; Kuboresha Kituo cha Hali ya Hewa Kilimo cha Igeri ili kuendana na mradi wa kimkakati wa Ikang'asi; na Ukarabati wa vituo vya hali ya hewa vya Iringa na Sumbawanga.

**Mradi wa Ununuzi wa Ndege kupitia Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL)**

280. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) imetengewa **Shilingi bilioni 185.32** fedha za ndani kwa ajili ya ununuzi wa ndege, injini za ndege na ukarabati wa karakana. Fedha hizo zitatumika kwa ajili ya shughuli mbalimbali zikiwemo: Kugharamia malipo ya mwisho ya ndege mbili (2) na malipo ya awali ya ndege mbili (2) aina ya Dash 8 Q400; Ununuzi wa injini za akiba kwa ajili ya ndege mpya na zilizopo za aina ya Boeing 737-9 na Airbus 220-300; Kuwezesha kuanza uendeshaji na utoaji huduma wa ndege mpya; Kukarabati karakana za matengenezo ya ndege za JNIA na KIMAFA; Kuanza ujenzi wa jengo la ofisi za ATCL katika Jengo la Kwanza la Abiria JNIA; Kukamilisha ukarabati wa nyumba 38 zilizoko KIA; na Ujenzi wa jengo la ofisi za ATCL jijini Dodoma.

## Mradi wa Uimarishaji wa Uendeshaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL)

281. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa **Shilingi bilioni 97.73** fedha za ndani katika mwaka wa fedha 2026/ 27. Fedha hizo zitaelekezwa katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali zinazolenga kuboresha uendeshaji wa Kampuni zikiwemo: Ujenzi wa karakana mpya ya matengenezo ya ndege katika Kiwanja cha Ndege cha JNIA; Ujenzi wa jengo la kuhifadhi vifaa; Ujenzi wa jengo la kuhifadhia mizigo; Ufungaji wa mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya kuboresha utendaji wa Kampuni; Ununuzi wa vifaa na vipuri vya ndege; na Ununuzi wa vifaa vya mafunzo ya urubani kwa vitendo (simulators) kwa ndege za Dash 8 Q400.

## Mradi wa Ununuzi wa Mitambo ya Mawasiliano (VHF Navigation Aids)

282. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/ 27, mradi huu unaolenga kuimarisha mawasiliano kati ya marubani na waongoza ndege umetengewa **Shilingi bilioni 1.80** fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza shughuli za: Ununuzi na ufungaji wa mitambo ya kuwezesha ndege kutua kwa usalama (Instrument Lansing System – ILS) katika Kiwanja cha Ndege JNIA; na Kufunga mifumo ya *Space Based ADS-B na CPDLC* katika maeneo mbalimbali nchini.

## Mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Usafiri wa Anga (CATC)

283. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa Chuo cha Usafiri wa Anga umetengewa **Shilingi bilioni 20.88** katika mwaka wa fedha 2026/27 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali. Shughuli hizo ni pamoja na: Ujenzi wa jengo la utawala lenye sakafu tano (5); Ujenzi wa jengo la madarasa lenye sakafu tatu (3) pamoja na ununuzi wa vifaa vya kufundishia; Ujenzi wa jengo la bweni lenye sakafu tano (5) na ununuzi wa samani; Ujenzi wa jengo la mikutano na mgahawa wa chakula; na Ujenzi wa jengo la zahanati pamoja na ununuzi wa vifaa.

**Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu na Ununuzi wa Vifaa vya Kufundishia katika Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT)**

284. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 5.41** fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo: Ujenzi wa karakana ya mafunzo ya uhandisi matengenezo ya ndege katika Kampasi ya Mabibo, Dar es Salaam; Ununuzi wa mtambo wa mafunzo ya mfumo wa umeme wa Ndege (Avionics); Usanifu wa jengo la kitivo litakalojengwa katika Kampasi ya Mabibo, Dar es Salaam; na Kuwezesha matengenezo ya ndege za mafunzo ya urubani.

**Mradi wa Uanzishwaji wa Kampasi ya NIT Lindi katika Sekta ya Usafiri Majini, Mafuta na Gesi**

285. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, mradi huu umetengewa bajeti ya jumla ya **Shilingi bilioni 5.96** fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo: Ujenzi wa wa awamu ya kwanza wa jengo la ghorofa mbili (2) kwa ajili ya madarasa, maabara, vyumba vya mihadhara na ofisi; na Ujenzi wa Jengo la huduma za chakula (Canteen).

**Mradi wa East Africa Skills for Transformation and Regional Intergration (EASTRIP)**

286. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, mradi huu umetengewa bajeti ya jumla ya **Shilingi bilioni 6.0** fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo: Kukamilisha ujenzi wa Karakana ya Matengenezo ya Ndege (Aircraft Maintenance Hangar) katika kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA); na Kuanza ujenzi wa Bweni na nyumba ya watumishi katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA).

## D:2. SHUGHULI NYINGINE ZITAKAZOTEKELEZWA KWA MWAKA 2026/27

### D:2:1 UDHIBITI WA HUDUMA ZA UCHUKUZI UDHIBITI WA USAFIRI MAJINI

287. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) limepanga kutekeleza shughuli mbalimbali zinazolenga kuimarisha usalama, usimamizi wa mazingira na ubora wa huduma za usafiri majini sambamba na kuendeleza mifumo ya TEHAMA. TASAC imeweka lengo la kukusanya **Shilingi bilioni 112.47** kutoka vyanzo vya ndani ili kufanikisha utekelezaji wa shughuli hizo. Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na: -

i. Kuendelea kusimamia utoaji wa leseni na masharti kwa watoa huduma;

ii. Kudhibiti gharama, nauli na tozo za usafiri majini kwa kuzingatia ushindani wa soko;

iii. Kufanya ukaguzi wa meli za ndani na za kimataifa ili kuhakikisha viwango vya ubora na usalama;

iv. Kuendelea kufanya mapitio ya Sheria, Kanuni, Mikataba na Itifaki mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha udhibiti wa usafiri majini;

v. Kuratibu na kuimarisha shughuli za utafutaji na uokoaji;

vi. Kuendeleza mifumo ya vyeti vya mabaharia na kudhibiti uchafuzi wa mazingira kutokana na shughuli za meli;

vii. Kutoa elimu ya usalama na ulinzi kwa wadau wa sekta ndogo ya usafiri majini;

viii. Kuimarisha uwezo wa watumishi na mifumo ya mapato kwa kutumia TEHAMA;

ix. Kusimamia uwakala wa forodha kwa shehena maalum; na

x. Kuendelea kutekeleza mikataba ya kimataifa chini ya Shirika la Bahari Duniani (IMO).

## UDHIBITI WA USAFIRI WA ANGA

288. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) inalenga kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 124.07** kutoka vyanzo vyake vya ndani kwa ajili ya kusimamia ubora wa huduma za usafiri wa anga kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vilivyowekwa na Shirika la Usafiri wa Anga Duniani (ICAO). Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na:

i. Kuendelea kutoa na kusimamia leseni kwa mashirika ya ndege na wafanyakazi wa sekta ya anga;

ii. Kusimamia usalama wa usafiri wa anga kwa kuzingatia viwango vya kimataifa na kitaifa vya usalama;

iii. Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa mashirika ya ndege na huduma zinazotolewa kwa abiria ili kuhakikisha kuwa zinazingatia sheria, taratibu na viwango vya kimataifa vya huduma;

iv. Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa TCAA na wengine katika sekta ya usafiri wa anga, ili kuhakikisha kuwa kuna ujuzi na maarifa ya kutosha ya kusimamia sekta kwa ufanisi;

v. Kuweka mazingira ya ushindani ili kuhakikisha kuwa huduma za usafiri wa anga zinapatikana kwa uhakika kwa bei nafuu;

vi. Kuendelea kuboresha huduma za uongozaji ndege kwa kuboresha mitambo ya uongozaji ndege katika viwanja na vituo vyenye mitambo hiyo;

vii. Kuimarisha udhibiti wa sekta kwa kuendelea kufanya mapitio ya kanuni ili kuhakikisha anga letu linaendelea kuwa salama;

viii. Kuboresha mifumo ya kielektroniki ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato;

ix. Kuimarisha Chuo cha Usafiri wa Anga kwa kuboresha miundombinu pamoja na vifaa vya kufundishia;

x. Kufanya tafiti ili kubaini fursa za uwekezaji katika sekta ya usafiri wa anga ili kuvutia mashirika ya kimataifa ya usafiri wa anga; na

xi. Kuendelea kushirikiana na mashirika ya kikanda na kimataifa ili kuimarisha viwango vya usalama na utendaji bora katika sekta ya anga.

**UDHIBITI WA USAFIRI ARDHINI**

289. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imeweka lengo la kukusanya **Shilingi bilioni 76.87** kutoka katika vyanzo vya ndani kwa ajili ya kugharamia Matumizi ya Kawaida pamoja na utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Taasisi. Katika mwaka husika, LATRA imepanga kutekeleza shughuli mbalimbali kwa lengo la kuboresha usalama, upatikanaji wa huduma za usafiri endelevu ardhini na rafiki kwa mazingira kama ifuatavyo:-

**(a) Usafiri wa Barabara**

i. Kuendelea kutoa na kusimamia masharti ya leseni kwa huduma zinazodhibitiwa, kuthibitisha madereva na kusajili wahudumu wa vyombo vya usafiri vinavyotoa huduma kibiashara;

ii. Kuimarisha upatikanaji na uhakika wa huduma za usafiri mijini na vijijini, kwa kuzingatia watu na maeneo yenye mahitaji maalum, kusimamia tozo za huduma hizo (nauli

elekezi za usafiri wa abiria) na viwango vya ubora wa huduma hizo;

iii. Kuendelea na usimamizi wa utekelezaji wa matumizi ya mifumo ya tiketi mtandao kwa mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani pamoja na kuunganisha mifumo hiyo kwenye mfumo jumuishi wa tiketi mtandao;

iv. Kusimamia usalama wa huduma zinazodhibitiwa ikijumuisha kupanua wigo wa mfumo wa ufuatiliaji magari (VTS), kuongeza ufanisi katika kuthibitisha na ufuatiliaji madereva, kuratibu kanzidata ya madereva wa malori na mabasi kwa kushirikiana na wadau katika kutatua changamoto za usafiri;

v. Kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika utoaji wa huduma kwa wateja ili kuondoa urasimu, kuweka uwazi na kuongeza ufanisi kwenye usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya Serikali;

vi. Kusogeza kwa wananchi wengi zaidi huduma za utoaji wa leseni za vyombo vinavyodhibitiwa kwa kutumia mawakala (authorised agents), hususan kupitia vyama vya ushirika (SACCOS) vya wamiliki na waendesha pikipiki (bajaji na bodaboda), taasisi za umma na kampuni binafsi;

vii. Kujenga mfumo jumuishi wa TEHAMA wa udhibiti na usimamizi wa usafiri wa pikipiki nchini; na

viii. Kutekeleza sehemu ya mradi wa Maboresho ya Usafiri Jumuishi na Endelevu Jijini Dodoma (Dodoma Integrated and Sustainable Transport – DIST) unaohusisha kuchochea mabadiliko ya uendeshaji wa huduma za daladala jijini Dodoma.

**(b) Usafiri wa Reli**

i. Kufanya kaguzi za usalama na ubora wa miundombinu, mitambo, vifaa na mifumo ya reli za Shirika la Reli

Tanzania (TRC), ikiwemo kutoa ithibati ya mitambo ya reli za MGR na SGR kabla ya matumizi;

ii. Kununua vifaa vya kisasa vya ukaguzi wa miundombinu ya reli ili kuboresha usalama wa usafiri huo na kuongeza ufanisi wa ukaguzi wa reli;

iii. Kukagua miundombinu, mabehewa na vichwa vya treni za TAZARA kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na

iv. Kuendesha mafunzo kwa watumishi wanaohudumia reli za TRC na TAZARA (Safety Critical Workers) ili kuboresha usalama na huduma za reli nchini.

**(c) Usafiri wa Waya**

i. Kuanza kutoa vibali na leseni za ufungaji wa miundombinu na utoaji wa huduma za usafiri wa waya nchini; na

ii. Kusimamia utekelezaji wa Kanuni za LATRA zinazohusu Usafiri wa Waya kwenye maeneo yenye vivutio vya utalii kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali ikiwa ni pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maliasili na Utalii, Halmashauri za Miji/ Manispaa/Majiji, Baraza la Taifa la Mazingira (NEMC) na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS).

**(d) Majukumu Mengine**

i. Kusimamia uzingatiaji wa utunzaji wa mazingira kwa vyombo vinavyotoa huduma ya usafiri ardhini kibiashara pamoja na watumiaji wa huduma zinazodhibitiwa ikiwa ni pamoja na kuandaa na kuanza utekelezaji wa Mkakati wa Kimataifa wa Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs);

ii. Kufuatilia na kusimamia viwango vya tozo na nauli, pamoja na ubora wa huduma, kwa lengo la kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma na watoa huduma na

hivyo kuhakikisha ukuaji endelevu wa sekta ndogo ya usafiri ardhini;

iii. Kutoa elimu kwa umma kuhusu huduma na masuala ya udhibiti wa usafiri ardhini, haki na wajibu wa watoa huduma na watumia huduma, pamoja na taratibu za kushughulikia migogoro na malalamiko katika huduma zinazodhibitiwa;

iv. Kutekeleza sehemu ya miradi ya Benki ya Dunia iliyobuniwa kuboresha Huduma za Usafiri katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Arusha;

v. Kuanza ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya LATRA Dodoma, na kukamilisha ujenzi wa majengo ya Ofisi katika mikoa miwili (2) ya Songwe na Simiyu;

vi. Kuendelea kuwezesha Baraza la Watumiaji wa Huduma za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA-CCC), Baraza la Ushindani (FCT), Tume ya Ushindani (FCC) na kuchangia asilimia 15 ya mapato ghafi kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali;

vii. Kuendeleza watumishi kwa kuwapa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ili kuwajengea uwezo, kukuza weledi na ujuzi wa kutekeleza majukumu ya Mamlaka kwa ubora, ufanisi na kwa kuwajali wateja;

viii. Kutoa elimu kwa watumishi kuhusu masuala mtambuka ya kitaifa ikiwemo kukuza maadili, kupambana na rushwa, kuimarisha afya na kudhibiti maambukizi ya Virusi vya UKIMWI, magonjwa yasiyoambukiza pamoja na athari zake;

ix. Kuendelea kutekeleza Mfumo wa Usimamizi wa Ubora (Quality Management System) kulingana na viwango vya kimataifa (ISO 9001:2015) kwa lengo la kuboresha huduma kwa wateja; na

x. Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali kwa kutumia TEHAMA ikiwemo Mfumo Mkuu wa Tiketi Mtandao.

**UDHIBITI NA UTOAJI WA HUDUMA ZA HALI YA HEWA**

290. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imeweka lengo la kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 19.03** kutoka katika vyanzo vya mapato vya ndani ikiwa ni pamoja na mapato yatokanayo na tozo za huduma za hali ya hewa zitolewazo kwa sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Kazi zitakazotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

i. Kuimarisha utoaji wa huduma za hali ya hewa kupitia ofisi tisa (9) zilizopo katika Mwambao wa Bahari ya Hindi na Maziwa Makuu kwa lengo la kuimarisha usalama na ufanisi wa shughuli zinazofanyika ikiwemo usafirishaji;

ii. Kuendelea kutekeleza mfumo wa udhibiti wa ubora wa huduma za hali ya hewa zinazotolewa kwa sekta ya usafiri wa anga pamoja na kuendelea kumiliki cheti cha ubora (ISO: 9001:2015);

iii. Kuongeza vyanzo vya mapato kwa lengo la kuboresha huduma za hali ya hewa;

iv. Kuboresha mfumo wa kuandaa utabiri wa hali ya hewa kwa kutumia mtambo wa kisasa (Complete Forecasting System) na hivyo kuongeza tija kwa sekta za kiuchumi pamoja na utoaji wa tahadhari za matukio ya hali mbaya ya hewa;

v. Kuboresha utoaji wa huduma za hali ya hewa kwa ajili ya kuongeza ufanisi na usalama kwa sekta za nishati, madini, rasilimali maji, usafiri, kilimo, utalii na ujenzi;

vi. Kufanya tafiti za hali ya hewa na mabadiliko ya tabianchi na matokeo ya tafiti husika kutumika katika kuboresha usahihi wa utabiri na kupunguza athari za mabadiliko ya hali ya hewa kwa sekta za kiuchumi na kijamii;

vii. Kuimarisha matumizi ya TEHAMA kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma na uendeshaji wa shughuli za hali ya hewa hapa nchini;

viii. Kuendeleza watumishi kielimu na weledi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku;

ix. Kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa kutumia huduma za hali ya hewa zinazotolewa na TMA;

x. Kudhibiti na kuratibu huduma za hali ya hewa zinazotolewa nchini kwa kuhakikisha taratibu na matakwa ya kisheria yanafuatwa katika utekelezaji wa shughuli za hali ya hewa pamoja na utoaji wa huduma za hali ya hewa hapa nchini; na

xi. Kuendesha na kuimarisha mtandao wa vituo vya hali ya hewa nchini kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa data za hali ya hewa.

**D:2:2 UTOAJI WA HUDUMA ZA UCHUKUZI HUDUMA ZA BANDARI**

291. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imeweka lengo la kukusanya jumla ya **Shilingi trilioni 1.91** kutoka katika vyanzo vya ndani vya mapato vitokanavyo na huduma za kibandari. Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na: -

i. Kuhudumia jumla ya meli 7,162 zenye ukubwa wa GRT milioni 54.50. Kati ya meli hizo meli 1,478 ni za Kimataifa (Deep Sea) zenye ukubwa wa GRT milioni 49.29, meli 1,980 ni za mwambao (coastals) zenye ukubwa wa GRT milioni 2.86 na meli 3,704 zenye ukubwa wa GRT milioni 2.35 zitahudumiwa katika Bandari za Maziwa Makuu;

ii. Kuhudumia shehena ya tani milioni 43.37 ikijumuisha tani za shehena ya makasha (TEUs) 1,515,441 katika Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara;

iii. Kuendelea na uboreshaji wa Bandari ya Tanga, ambapo shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na: Ujenzi wa gati la kuhudumia makasha na abiria na kujenga gati la kuhudumia shehena ya mafuta (liquid bulk handling jetty) Raskazone, litakalowezesha Bandari ya Tanga kuhudumia meli kubwa za shehena ya mafuta; kuendeleza eneo la Mwambani lenye ukubwa wa hekta 174, ambapo kwa sasa sehemu ya eneo hilo linatumika kuhifadhia shehena mbalimbali ikiwemo shehena ya magari; na kuendelea kuhamasisha Sekta Binafsi kuchangamkia fursa za uwekezaji wa maghala na ICDs katika Mkoa wa Tanga ili kuongeza ufanisi wa kuhudumia shehena;

iv. Kuendelea na shughuli za ujenzi wa Bandari ya Mtwara kwa ajili ya kuhudumia shehena ya kichele (dry bulk cargo) ikiwa ni pamoja na makaa ya mawe, saruji na *clinker* katika eneo la Kisiwa Mgao; kuendelea na ukarabati wa maeneo ya kuhudumia shehena na ukarabati wa miundombinu ya barabara zinazoingia na kutoka bandarini;

v. Kuendelea na ujenzi wa bandari mpya ya Mbegani (Bagamoyo) kwa ujenzi wa gati na kutafuta vyanzo vya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi kwa awamu tatu, ikiwemo kuishirikisha Sekta Binafsi kupitia Mfumo wa PPP;

vi. Kuendelea na ujenzi wa Bandari Kavu za Kwala na Ihumwa, ambapo shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha ujenzi wa jengo la utawala, barabara za ndani ya eneo la bandari, ghala na karakana katika Bandari Kavu ya Kwala; na kuanza ujenzi wa Bandari Kavu ya Ihumwa – Dodoma;

vii. Kuendelea na uboreshaji wa Bandari za Maziwa Makuu, ambapo kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa bandari ya Mwanza North na Mwanza South ili kuboresha huduma na kuwezesha meli ya kisasa ya MV. New Mwanza kutia nanga na kutoa huduma. Aidha, kwa upande wa bandari zilizopo katika Ziwa Tanganyika kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na uboreshaji wa Bandari ya Kigoma kwa kujenga barabara za bandari, ujenzi wa gati na jengo la abiria;

viii. Kuendelea na ujenzi wa Bandari ya Mbamba Bay katika Ziwa Nyasa, ili kuwezesha kuhudumia meli na shehena inayokwenda na kutoka nchi jirani za Malawi na Msumbiji;

ix. Kuendelea kuboresha huduma za bandari nchini kupitia uboreshaji wa miundombinu, ununuzi wa mitambo na vifaa mbalimbali vitakavyotumika katika bandari nchini kwa lengo la kuwezesha kuongoza meli na kuhudumia shehena bandarini;

x. Kuendelea na utekelezaji wa ujenzi wa matanki 15 ya kupokelea mafuta (Single Receiving Terminal – SRT); Kuendelea na uboreshaji wa Gati Na. 8 – 11; na Ujenzi wa kituo cha shehena ya mafuta nje ya bahari (offshore liquid bulk terminal) katika Bandari ya Dar es Salaam; na

xi. Kuendelea kushirikisha Sekta Binafsi katika kuendeleza na kuendesha shughuli za bandari nchini kwa lengo la kuongeza tija katika utendaji wa bandari ili kuzifanya zichangie zaidi katika ukuaji wa uchumi na kuipunguzia Serikali gharama za uwekezaji na uendeshaji wa bandari nchini.

292. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na uendelezaji wa magati 10 katika Bandari ya Dar es Salaam, vilevile katika kuwezesha uwekezaji katika magati yaliyopo Kigamboni, TRC imeanza mazungumzo kwa kushirikiana na NSSF kufanya tathmini ya kuunganisha upande wa pili wa Kigamboni na kipande cha reli ya SGR ili kuunganisha magati yote mapya na reli hiyo, pamoja na kuona uwezekano wa kuunganisha maeneo ya viwanda kwa reli hiyo. Kwa kufanya hivyo, TRC itaongeza mizigo inayohudumiwa na SGR pamoja na kuongeza uwezo na matumizi ya bandari kwa ujumla. Aidha, hatua hii pamoja na manufaa mengine, itasaidia kuondoa msongamano wa malori kwa upande wa Kigamboni na Barabara ya Kilwa.

## HUDUMA ZA VIWANJA VYA NDEGE

293. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Mmlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) imeweka lengo la

kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 247.33** kutoka katika vyanzo vya mapato vya ndani. Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na:-

i. Kuendelea kuimarisha huduma za ulinzi, usalama na uwezeshaji wa abiria, ndege na mizigo katika viwanja vya ndege;

ii. Kuendelea kuhudumia viwanja vya ndege vya Serikali nchini kwa kufanya matengenezo ya miundombinu na kusimamia shughuli za uendeshaji;

iii. Kuendelea na ununuzi na ufungaji wa mashine za kisasa za ukaguzi wa abiria na mizigo katika viwanja vya ndege;

iv. Kuendelea kutoa mafunzo kwa watumishi ili kuwaongezea ujuzi na weledi katika utendaji wao wa kazi katika viwanja vya ndege; na

v. Kuendelea na zoezi la upimaji na upatikanaji wa Hati Miliki za ardhi katika viwanja vya ndege vya Serikali.

**HUDUMA ZA USAFIRI WA ANGA**

294. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) imeweka lengo la kukusanya **Shilingi trilioni 1.09** kutokana na shughuli za usafirishaji wa abiria na mizigo katika vituo vya ndani na nje ya nchi vilivyopo na vile vitakavyoanzishwa. Katika kipindi husika, ATCL imepanga kutekeleza shughuli mbalimbali kama ifuatavyo:-

i. Kuongeza idadi ya vituo vya safari kutoka vituo 33 vinavyohudumiwa hivi sasa hadi kufikia vituo 47 vya ndani na nje ya Tanzania;

ii. Kuendelea kusafirisha mizigo kwa kutumia ndege za abiria na ndege maalum ya mizigo;

iii. Kuendelea kufanya matengenezo ya ndege;
iv.

v. Kujenga na kukarabati Ofisi za ATCL;

vi. Kujenga karakana mpya ya ndege katika kiwanja cha JNIA; na

vii. Kuendelea kuboresha mifumo ya TEHAMA.

## HUDUMA ZA USAFIRI WA RELI

295. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Reli Tanzania (TRC) limeweka malengo ya kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 352.87** kutoka katika vyanzo vya ndani vinavyotokana na utoaji wa huduma za usafirishaji wa abiria na mizigo katika reli za MGR na SGR. Katika mwaka wa fedha 2026/27, TRC imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kusafirisha takriban tani 584,000 za mizigo katika reli ya MGR, tani 1,500,000 katika reli ya SGR, abiria 662,000 wa masafa marefu kwa reli ya MGR, abiria 4,750,000 kwa reli ya SGR na abiria 3,128,000 kwa reli ya mjini;

ii. Kuendelea kukarabati na kuimarisha miundombinu ya reli, majengo ya karakana, stesheni na kambi za wafanyakazi;

iii. Kuhakikisha huduma salama za usafiri wa treni ikiwemo kuboresha mifumo ya ishara (signaling) na mawasiliano kwa reli za SGR na MGR;

iv. Kuendelea na ununuzi na ukarabati wa vitendea kazi vikiwemo vichwa vya treni na mabehewa ya abiria na mizigo kwa ajili ya reli za SGR na MGR;

v. Ununuzi wa vifaa na mitambo ya kupakua na kupakia mizigo katika reli ya MGR na SGR;

vi. Kufanya Upembuzi Yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa Reli ya SGR kutoka Isaka – Lusahunga – Mulongo/Kikagati – Mpondwe (Uganda);

vii. Kuendelea na ununuzi wa vitendea kazi vikiwemo: vichwa vya treni; mabehewa; mitambo na mashine za matengenezo ya njia; na ununuzi wa *hybrid locomotives* 10; na

viii. Kuajiri watoa huduma wa matengenezo ya vichwa vya treni ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma za reli nchini kwa zaidi ya asilimia 85.

296. ***Mheshimiwa Spika,*** malengo ya mwaka yaliyoainishwa ya kusafirisha tani milioni 1.5 za mizigo kwa reli ya SGR na tani 584,000 kwa reli ya MGR ni kutokana na hali ya sasa ya miundombinu hiyo. Hata hivyo, kiusanifu reli ya SGR ina uwezo wa kusafirisha tani milioni 17.0 kwa mwaka kati ya Bandari ya Dar es Salaam na bandari zilizopo katika Ziwa Victoria (Mwanza Kusini) na Ziwa Tanganyika (Kigoma na Karema) na reli ya MGR ina uwezo wa kiusanifu wa kubeba tani milioni 5.0 kwa mwaka.

297. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kufikia lengo hilo, Serikali imeweka mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa reli ya SGR kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza ifikapo mwishoni mwa mwaka 2028 na Dar es Salaam – Kigoma ifikapo mwishoni mwa mwaka 2029 na kukamilisha maboresho ya reli ya MGR. Mpango wa Biashara wa TRC unaonesha kuwa, kupitia reli hizo itaweza kusafirisha wastani wa mizigo tani milioni 4.0 kwa mwaka kwa kutumia reli ya MGR na tani milioni 10 kwa mwaka katika reli ya SGR ifikapo mwaka wa fedha 2034/35.

298. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA), Serikali inatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 48.33** katika mwaka wa fedha 2026/27. Aidha, katika kipindi husika, TAZARA itatekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuendelea na uboreshaji wa Reli ya TAZARA kupitia ushirikiano baina ya Serikali ya Tanzania, Zambia na Kampuni ya CCECC ya China;

ii. Kufanya matengenezo kinga ya injini tisa (9), mabehewa 450 ya mizigo na mabehewa 18 ya abiria;

iii. Kusafirisha abiria 350,000 kwa upande wa safari ndefu na abiria 150,000 kwa treni ya Udzungwa inayosafiri kati ya Stesheni za Kidatu na Makambako (km 365);

iv. Kusafirisha tani 100,000 za mizigo kwa kutumia miundombinu iliyopo kabla ya uwekezaji kuanza;

v. Kukamilisha tathimini ya kina ya hali ya miundombinu ya reli ikiwemo njia ya reli, makalavati, madaraja, mifumo ya maji na miundombinu mingine; na

vi. Kuendelea kujenga uwezo wa rasilimaliwatu kupitia mafunzo na ajira.

**HUDUMA ZA USAFIRI KATIKA BAHARI NA MAZIWA MAKUU**

**Huduma za Usafirishaji katika Bahari**

299. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Kampuni ya Meli ya China na Tanzania (SINOTASHIP) imeweka lengo la kukusanya **Shilingi bilioni 20.65** kutokana na shughuli za usafirishaji wa mizigo na uwakala wa meli. Aidha, katika kipindi husika, Kampuni imepanga kutekeleza shughuli mbalimbali kama ifuatavyo:-

i. Kuendelea kusafirisha shehena kati ya Tanzania, China na nchi nyingine ikiwa ni miongoni mwa mikakati ya kuimarisha biashara kati ya Tanzania na nchi nyingine duniani, ambapo Kampuni imepanga kusafirisha zaidi ya tani 622,000 za mizigo;

ii. Kuendelea kuvutia kampuni za meli ili kuongeza idadi ya meli na mizigo itakayoingia katika bandari nchini kufikia makasha 86,700; na

iii. Kushirikiana na Taasisi za fedha nje na ndani ya nchi ili kufanikisha kupata fedha kwa ajili ya kununua meli ya kubeba mizigo (general cargo vessel) itakayofanya safari kati ya China na Tanzania.

## Huduma za Usafiri na Usafirishaji katika Maziwa Makuu

300. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Serikali kupitia Kampuni ya Meli Tanzania (TASHICO) inatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 12.21** kutoka katika vyanzo vya mapato ya ndani kwa kusafirisha abiria na mizigo katika Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Shughuli zitakazotekelezwa kwa kutumia mapato ya ndani ni pamoja na:-

i. Kusafirisha abiria 270,600 kwa kutumia meli zilizopo katika Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa;

ii. Kusafirisha mizigo tani 174,520 kwa kutumia meli ya mizigo ya MV. Umoja na meli nyingine za mizigo na abiria;

iii. Uboreshaji miundombinu ya meli (Shipyard, floating Docks na Slipways) katika bandari za Mwanza na Kigoma;

iv. Kuwezesha upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya ofisi za makao makuu na matawi;

v. Kuwezesha shughuli za uendeshaji wa ofisi ya makao makuu ya Kampuni na matawi yake ya Mwanza, Kigoma na Kyela;

vi. Kuendeleza watumishi kwa kuwajengea uwezo wa umahiri na ujuzi kazini; na

vii. Ununuzi wa vitendea kazi vya ofisi na matengenezo ya magari na mitambo inayowezesha utekelezaji wa majukumu ya Kampuni.

## D:2:3 VYUO VYA MAFUNZO VYA KISEKTA

301. ***Mheshimiwa Spika,*** miongoni mwa malengo muhimu ya Dira 2050 pamoja na mikakati iliyowekwa kwa ajili ya kuhakikisha malengo mengine ya Dira yanatimizwa kwa weledi na ufanisi mkubwa, ni uendelezaji wa rasilimaliwatu. Uwepo wa wataalam wenye ujuzi katika masuala mbalimbali unatoa nafasi

kwa Taifa kuweza kufikia malengo ya uzalishaji na utoaji wa huduma katika sekta mbalimbali, ikiwemo Sekta ya Uchukuzi. Kwa kuzingatia hilo, Wizara ya Uchukuzi imeendelea kutekeleza afua mbalimbali zinazolenga kuboresha vyuo vya kisekta ili viweze kutoa mafunzo yanayoendana na mahitaji ya sekta kwa sasa na wakati ujao. Vyuo hivyo vya kisekta vinajumuisha: Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT); Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI); Chuo cha Teknolojia ya Reli (TIRTEC); Chuo cha Bandari (Bandari College); na Chuo cha Hali ya Hewa.

**Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT)**

302. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, NIT imeweka lengo la kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 34.91** kutoka katika vyanzo vya mapato ya ndani yatokanayo na utoaji wa mafunzo, tafiti na ushauri wa kitaalam. Shughuli zitakazotekelezwa ni: -

i. Kuendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi, kufanya tafiti, kuboresha mitaala na kutoa ushauri wa kitaalam katika maeneo mbalimbali kulingana na mahitaji ya nchi;

ii. Kuendelea kuzalisha wataalam katika maeneo mbalimbali kwa kudahili takriban wanafunzi 20,000 wa kozi za muda mrefu na washiriki 5,000 wa kozi za muda mfupi;

iii. Kuendelea kutoa mafunzo ya kozi za kimkakati zinazoendana na uwekezaji wa Serikali katika Sekta ya Uchukuzi;

iv. Kukamilisha ujenzi wa barabara za ndani ya Chuo kwa kiwango cha lami katika Kampasi ya NIT Mabibo, Dar es Salaam;

v. Kununua Aviation System Trainer (Avionics) kwa ajili ya mafunzo ya usafiri wa anga na Gari la kubebea wagonjwa (ambulance) katika zahanati ya Chuo iliyopo katika Kampasi ya NIT, Mabibo Dar es Salaam;

vi. Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi kupitia ziara za kitaaluma, mafunzo ya muda mrefu na mfupi, mafunzo ya vitendo na kubadilishana wakufunzi na vyuo vya nje ya nchi; na

vii. Kuendelea kutekeleza majukumu ya uanzishwaji wa Kituo cha Kikanda cha Umahiri cha Mafunzo ya Usalama Barabarani na Kituo cha Umahiri cha Mafunzo ya Taaluma za Usafiri wa Anga na Operesheni za Usafirishaji.

### Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI)

303. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, DMI inatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 16.35** kutoka katika vyanzo vya ndani vitokanavyo na utoaji wa elimu na mafunzo, tafiti na huduma za ushauri wa kitaalam. Aidha, shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na: -

i. Kuendelea kutoa elimu na mafunzo kwa kuongeza udahili hadi kufikia takriban wanafunzi 15,500 wakijumuisha wanafunzi 7,000 wa kozi za muda mrefu na wanafunzi 8,500 wa kozi za muda mfupi;

ii. Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya Chuo katika eneo la Mkuranga na kuwezesha upatikanaji wa vifaa vya mafunzo;

iii. Kuboresha shughuli za tafiti na utoaji wa huduma za ushauri wa kitaalam;

iv. Kuwezesha shughuli za uendeshaji wa Chuo;

v. Kuimarisha vyanzo vya mapato ili kutekeleza shughuli za chuo ikiwemo miradi ya maendeleo; na

vi. Kuboresha mifumo ya TEHAMA ili kuongeza ufanisi wa utendaji wa Chuo.

## Chuo cha Teknolojia ya Reli (TIRTEC)

304. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TRC, itaendelea kutoa mafunzo ya reli katika kampasi zote za Tabora na Morogoro kwa lengo la kuendelea kutoa wataalam wabobevu wa masuala ya uendeshaji wa reli nchini. Aidha, katika mwaka wa fedha 2026/27, Chuo kinatarajia kudahili wanafunzi 750.

## Chuo cha Bandari

305. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Serikali kupitia TPA itaendelea kutoa mafunzo katika kozi mbalimbali zinazohusiana na kuhudumia shehena katika bandari nchini kupitia Chuo cha Bandari. Aidha, Chuo hiki katika mwaka 2026/27 kimepanga kudahili wanafunzi 1,160 kwa mafunzo ya muda mrefu na wanafunzi 2,540 kwa mafunzo ya muda mfupi.

## Chuo cha Usafiri wa Anga (CATC)

306. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Serikali kupitia TCAA itaendelea kutekeleza na kukamilisha miradi ya maendeleo ya Chuo cha Usafiri wa Anga (CATC), ikiwa ni pamoja na uendelezaji wa miundombinu ya mafunzo na kuimarisha mazingira ya kujifunzia. Aidha, Chuo kitaendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi zaidi ya 2,084 katika fani mbalimbali za usafiri wa anga, pamoja na kuanzisha na kuendeleza kozi mpya ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira la sekta ya anga nchini na kimataifa.

## Chuo cha Taifa cha Hali ya Hewa

307. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Serikali kupitia TMA itaendelea kuboresha mazingira ya ufundishaji, Chuo kitawezeshwa kwa kupatiwa vifaa vya kisasa vya kufundishia. Aidha, Serikali kupitia TMA imetenga jumla ya **Shillingi bilioni 1.25** katika bajeti ya maendeleo kwa ajili ya kuanza ujenzi wa majengo ya utawala na mabweni katika Chuo cha Taifa cha Hali ya Hewa.

## D:2:4. MASUALA YA KISERA NA MTAMBUKA

### Maboresho ya Sera, Sheria na Kanuni za Kisekta

308. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kunakuwa na udhibiti, ushindani na ubora wa huduma zinazotolewa pamoja na tija ya uendeshaji, Wizara itaendelea kusimamia maboresho ya sera, sheria na kanuni zinazoongoza utendaji wa sekta. Katika mwaka wa fedha 2026/27, Wizara itakamilisha maandalizi ya Sera ya Taifa ya Uchukuzi na kuendelea na maandalizi ya Sera ya Taifa ya Usafiri Majini ili kuhakikisha kuwa inakamilika kwa wakati na kutoa matokeo tarajiwa.

309. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara itaendelea kupitia Sheria na kanuni mbalimbali za kisekta. Miongoni mwa sheria zitakazopitiwa ni pamoja na Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania, Sura 415. Aidha, Wizara itaendelea kuandaa na kuboresha kanuni mbalimbali zikiwemo Kanuni za: Viwanja vya Ndege; Usafiri wa Waya; Bandari za Bahari, Maziwa Makuu na Chuo cha Bandari; na Usafiri Majini ili kuwezesha utoaji wa huduma stahiki katika Sekta ya Uchukuzi.

### Utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa Dhidi ya Rushwa

310. ***Mheshimiwa Spika,*** katika juhudi za kuendelea kuzuia vitendo vya rushwa mahali pa kazi, Wizara kwa mwaka 2026/27 itaendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Rushwa Awamu ya Nne kwa kuendelea kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa watumishi wake ili kujenga uelewa mpana kuhusu vitendo vya rushwa, madhara yake kwa jamii na Taifa kwa ujumla na namna ya kuepuka vitendo vya rushwa.

### Rasilimaliwatu na Maendeleo ya Watumishi

311. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kujenga uwezo wa rasilimaliwatu, Wizara na Taasisi zilizo chini yake itaendelea kuwezesha watumishi kuhudhuria mafunzo mbalimbali ya muda mrefu na mfupi ili kuongeza ujuzi na maarifa, kukidhi matakwa ya

kimuundo na kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia, lengo likiwa ni kuboresha utendaji wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake. Katika mwaka wa fedha 2026/27, Wizara na Taasisi zake imepanga kuwezesha mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa takriban watumishi 3,500.

**Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)**

312. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendelea kuimarisha usalama wa kimtandao kwa matumizi ya mifumo ya kielektroniki, Wizara itaendelea kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika utendaji wa kila siku. Aidha, Wizara itaendelea kuzingatia na kutekeleza miongozo inayotolewa na Mamlaka ya Serikali Mtandao kuhusu matumizi na usimamizi wa mifumo na kinga dhidi ya uhalifu wa kimtandao. Vilevile, kwa kuzingatia sheria na kanuni zinazosimamia ununuzi wa umma, Wizara imeendelea kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST) ili kupata thamani ya fedha katika utekelezaji wa shughuli na miradi ya maendeleo.

**Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira**

313. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza malengo ya Dira 2050, hususan nguzo ya tatu inayohimiza uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi, Wizara ya Uchukuzi itaendelea kusimamia uhifadhi na utunzaji wa mazingira ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa Mpango Kazi wa Utunzaji wa Mazingira ya Uchukuzi 2025 - 2030 (Transport Sector Environmental Action Plan - TSEAP). Utekelezaji wa suala hili ni takwa la Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191. Aidha, Wizara itaendelea kusimamia utunzaji wa mazingira katika miradi ya uchukuzi inayotekelezwa nchini na shughuli za uendeshaji wa njia za usafiri wa anga, ardhini na majini kwa kuzingatia viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Ufuatiliaji na Tathmini**

314. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Wizara itaendelea kutekeleza mikakati yake na miongozo mingine

ya kitaifa inayotolewa katika kusimamia masuala ya ufuatiliaji na tathmini ya shughuli na miradi ya maendeleo. Aidha, Wizara itaendelea kufanya mapitio ya utekelezaji wa shughuli za Wizara na Taifa kwa ujumla, ikiwemo Mkutano wa Pamoja wa Tathmini ya Utendaji wa Sekta ya Uchukuzi (Joint Transport Sector Review – JTSR) ambao unatarajiwa kufanyika mwezi Novemba, 2026. Vilevile, Wizara itaendelea kufuatilia ufanisi wa Taasisi zake kupitia Mikataba ya Utendaji inayoandaliwa na kusainiwa kwa pamoja kila mwaka. Lengo la hatua hizi ni kuimarisha uwajibikaji, kuboresha utoaji wa huduma na kuhakikisha matumizi sahihi ya fedha za umma.

**E. SHUKRANI**

315. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2025/26, umeleta mafanikio makubwa katika kuimarisha huduma za Uchukuzi na hali ya hewa nchini. Mafanikio hayo ni pamoja na: Kuendelea kuhudumia Watanzania kwa ufanisi kupitia reli ya SGR; Kukamilisha ujenzi wa Meli ya MV. New Mwanza na kuanza kutoa huduma; Kuimarika kwa ushirikiano baina ya Serikali na Sekta Binafsi, hususan katika shughuli za bandari ulioanza kuonesha matunda; Uimarishaji wa upatikanaji wa vyombo vya usafiri katika Maziwa Makuu, likiwemo Ziwa Tanganyika ambalo meli nne (4) zimejengwa na kukamilika kwa muda mfupi; Kuimarika kwa usalama katika usafiri majini, hasa katika Ziwa Victoria baada ya kukamilika kwa Kituo cha Kikanda cha Uratibu wa Utafutaji na Uokoaji; Tanzania kuendelea kung'ara kimataifa katika usafiri wa anga na usimamizi wa masuala ya hali ya hewa; na kuanza kutoa mafunzo ya urubani ndani ya nchi yaliyoanza rasmi kutolewa mwezi Julai, 2025 na kupunguza fedha za kigeni zilizokuwa zinatumika kuwasomesha marubani nje ya nchi.

316. ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio ya Wizara yasingeweza kutokea bila ya ushauri na usimamizi wa Bunge Lako Tukufu. Kutokana na mafanikio hayo, naomba nitoe shukrani za kipekee kwako wewe binafsi Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa ushauri na michango yao ambayo imewezesha Wizara kufikia mafanikio hayo. Aidha, niwashukuru

wananchi na wadau wengine kwa kuendelea kutoa michango ya hali na mali katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na kuendelea kushirikiana na Serikali katika kulinda miundombinu hiyo ya usafirishaji ambayo Serikali imewekeza kiasi kikubwa cha fedha za Umma.

317. ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue fursa hii kuwapongeza na kutambua michango inayotolewa na viongozi wanaonisaidia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara, kwa kuanza na Naibu Waziri, **Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile** (Mb.); na Katibu Mkuu, **Prof. Godius Walter Kahyarara**. Vilevile, niishukuru Menejimenti ya Wizara; Wakuu wa Taasisi za Wizara; pamoja na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi kwa juhudi zao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taifa kwa ujumla.

318. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee nishukuru Taasisi na Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa ambayo yameshirikiana na Wizara katika uendelezaji wa Sekta ya Uchukuzi nchini. Ninaomba kutaja baadhi ya Mashirika ya Kitaifa kama ifuatavyo: Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya NSSF na PSSSF; Taasisi za kifedha za CRDB, NMB, AZANIA BANK, NBC na TCB na Asasi mbalimbali za kiraia. Aidha, Mashirika ya Kimataifa/ Wadau wa Maendeleo wanaoendelea kushirikiana na Wizara ambao ni pamoja na: Wakala wa Kuratibu Uwezeshaji wa Usafirishaji na Biashara katika Ushoroba wa Kati (CCTTFA); Trade Mark Africa (TMA); Shirika la Bahari Duniani (IMO); Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO); Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO); Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB); Benki ya Dunia (WB); Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA); Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Korea Kusini (KOICA); Foreign Commonwealth and Development Office (FCDO); World Wildlife Fund (WWF); Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD); Shirika la Nchi Zinazouza Mafuta ya Petroli Nje ya Nchi zao (OPEC); Jumuiya ya Umoja wa Ulaya (EU); Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB); Shirika la Chakula Duniani (WFP); na Shirika la Biashara na Maendeleo la Marekani (USTDA).

319. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia inashukuru ushirikiano katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2025/26 iliyoupata kutoka katika nchi za kikanda kupitia Sekretarieti ya

Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC). Vilevile, kutoka Nchi za Urusi; Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE); Uingereza; Marekani; Uholanzi; Japan; India; China; Sweden, Denmark; Korea Kusini; Ufaransa; Jamhuri ya Czech; Canada; Ubelgiji; Ujerumani na Uturuki. Na mwisho si kwa umuhimu nishukuru Sekta Binafsi, hususan wafanyabiashara wa huduma za uchukuzi kwa kuendelea kutoa huduma za uchukuzi. Wizara inaahidi kuwa itaendelea kutoa ushirikiano katika kuimarisha utendaji wa Sekta ya Uchukuzi.

## F. MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA YA WIZARA YA UCHUKUZI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2026/27

320. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Wizara ya Uchukuzi inaomba kuidhinishiwa bajeti yenye jumla ya **Shilingi 2,872,738,082,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 126,041,236,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 2,746,696,846,000** ni fedha za Miradi ya Maendeleo.

321. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na Hotuba hii, nimeambatisha majedwali mbalimbali yenye taarifa na takwimu kwa ajili ya kutoa uelewa zaidi kwa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla kuhusu Sekta ya Uchukuzi. Naomba majedwali hayo yachukuliwe kama sehemu ya hotuba yangu. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara (**www.uchukuzi.go.tz**).

322. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, kwa hotuba hiyo na imeungwa mkono.

Tunaendelea, sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso kwa ajili ya Taarifa ya Kamati, karibu.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ifuatayo ni taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Fungu 62 Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninaomba taarifa yote ya Kamati iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ilivyowekwa Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025 (Kanuni za Bunge) ninaomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Fungu 62 Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuathiri masharti yanayopatikana katika Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge, taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kwanza ni utangulizi ambayo inaeleza kuhusu muundo wa taarifa pamoja na namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake; sehemu ya pili inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kwa kutathmini uzingatiaji wa ushauri na maoni ya Kamati, makusanyo ya maduhuli, mwenendo wa upatikanaji wa fedha na utekelezaji wa miradi ya maendeleo; sehemu ya tatu inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 na sehemu ya nne ni majumuisho ya maoni na ushauri wa Kamati na sehemu ya tano ni hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026. Ninapenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, kwa sehemu kubwa Serikali imeyafanyia kazi maoni na ushauri uliotolewa na Kamati wakati wa kujadili bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026. Moja kati ya masuala yaliyotekelezwa kikamilifu ni pamoja na shirika la reli *TRC* kuanza kujitegemea kwa 100% katika mishahara ya watumishi kupitia mapato yake ya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Wizara chini ya Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, Mbunge na Waziri wa Uchukuzi na pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa *TRC* Ndugu Machibya Masanja kwa usimamizi madhubuti wa *TRC* hadi kufikia hatua hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo ya maduhuli katika mwaka wa fedha 2025/2026. Wizara ya Uchukuzi pamoja na taasisi zake ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi trilioni 3.3. Hadi kufikia Februari, 2026 makusanyo yalifikia jumla ya shilingi trilioni 1.9 sawa na 57.70% ya lengo. Kwa wastani mwenendo wa makusanyo ya maduhuli ni wa kuridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha. Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Uchukuzi iliidhinishiwa kutumia shilingi trilioni 2.746 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2026 Wizara ilikuwa imepokea shilingi trilioni 1.314 sawa na 67.6%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha hizo kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Uchukuzi. Pamoja na pongezi hizo, Wizara ya Uchukuzi ilikuwa imepokea 47.11% tu ya bajeti kwa maendeleo hadi kufikia Machi, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati haikuridhishwa na hali ya mapokezi ya fedha za maendeleo kwa kuwa inaathiri utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Sekta ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya maendeleo. Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2025/2026 Mikoa ya Tanga, Dar es Salaam na Pwani kati ya tarehe 13 na 19 Machi, 2026. Ukaguzi huu ulifanyika ili kukidhi masharti ya Kanuni ya 120 ya Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Kamati imeridhishwa na hatua mbalimbali zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi chini ya Wizara ya Uchukuzi. Taarifa zaidi ya kuhusu miradi hiyo inapatikana katika ukurasa wa 8 - 22 kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala mahususi yaliyobainika katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026. Kwa upande wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania, Serikali ilifanya uwekezaji mkubwa katika kuboresha miundombinu ya Bandari ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara kati ya mwaka 2021 hadi 2023. Vilevile, Serikali ilifanya uamuzi wa kupangisha baadhi ya gati kuanzia namba moja hadi saba ya Bandari ya Dar es Salaam kwa kampuni ya *DP World* ya Dubai kwa mkataba wa kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika bajeti ya Serikali kwa mwaka wa 2024/2025 Serikali ilifanya uamuzi wa kuruhusu mapato yanayotokana na matumizi ya gati *(Wharfage)* kukusanywa na *TPA* tofauti na ilivyokuwa awali. Hatua hizo zimechangia kuongeza ufanisi na tija katika matumizi ya bandari nchini na kuzifanya kuwa bandari kivutio katika ukanda wetu. Mathalani, katika Bandari ya Dar es Salaam, shehena ya makasha iliyohudumiwa ndani ya miezi tisa ya mwaka 2025/2026 imefikia zaidi ya milioni 1.13 kutoka makasha 725,436 katika mwaka wa fedha wa 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Bandari ya Tanga hadi Machi, 2026, imehudumia shehena ya tani milioni 1.6 wakati katika miezi 12 ya mwaka wa fedha 2024/2025 Bandari hiyo ilihudumia tani milioni 1.33. Vilevile, Bandari ya Mtwara katika eneo la Kisiwa - Mgao itaanza kuhudumia shehena chafu ili kutunza mazingira ya bandari iliyopo Mtwara Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inampongeza sana mbeba maono wa Taifa hili Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ujasiri wa hatua hizi ambazo zimeiwezesha tija na mafanikio haya ndani ya muda mfupi kwenye Sekta ya Bandari. Aidha, Kamati inampongeza Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa, Waziri wa Uchukuzi pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa *TPA* Ndugu Mbosa kwa namna wanavyosimamia sekta ndogo ya bandari nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ufanisi na tija hiyo umeleta changamoto ambayo ni msongamano wa shehena ya makasha katika bandari. Hali hii inatokana na ukweli kuwa miundombinu iliyopo bandarini kwa sasa haitoshi kuhudumia ongezeko hili. Kwa sasa bandari zinahudumia shehena ya tani milioni 32.80 na inakadiriwa kufika mwaka 2030 itakuwa inahudumia shehena ya tani milioni 62.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na changamoto hiyo, tarehe 8 Machi, 2026, *TPA* ilitangaza matumizi ya ada mpya kwa wadau na watumiaji wa bandari. Lengo la ada mpya ni kuanzisha Tozo ya Uendelezaji wa Miundombinu ya Bandari *(Port Infrastructure Development Levy)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji huo wa miundombinu ya bandari utahusu mambo yafuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni ujenzi wa gati mpya nne za namba 12 hadi 15 katika Bandari ya Dar es Salaam, ujenzi wa gati mbili zenye urefu wa mita 500 katika Bandari ya Dar es Salaam, ujenzi wa matanki ya kupokelea mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam, ujenzi wa Bandari Maalumu Kisiwa-Mgao Mkoani Mtwara kwa ajili ya shehena chafu, ujenzi wa Kituo cha Mtandao wa Reli ndani ya Bandari ya Dar es Salaam, ujenzi wa gati la kupokelea mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam na ujenzi wa kuhudumia mizigo mchanganyiko pamoja na gati la kuhudumia mafuta katika Bandari ya Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ada hiyo itatozwa kuanzia tarehe 01 Julai, 2026 kwa kiwango cha asilimia nne nukta tano ya Kodi ya

Forodha. Awali *TPA* ilipanga kutoza kiwango cha asilimia tisa lakini baada ya kukutana na watumiaji wa bandari chini ya usimamizi wa Wizara, pande zote zilikubaliana kiwango cha asilimia nne nukta tano ili kuendeleza miundombinu ya bandari nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ada hiyo itaiwezesha *TPA* kuwa na uwezo wa kukusanya shilingi trilioni 11.2 kwa ajili uendelezaji wa miundombinu hiyo. Aidha, *TPA* inategemea kushirikiana na sekta binafsi kwa kuvutia mtaji na zaidi ya shilingi trilion 4.9 ili kukamilisha kiasi cha shilingi trilioni 16.1 kinachotakiwa katika jukumu hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viwanja vya Ndege vya Kimkakati Nchini. Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali ilipanga kuanza ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Serengeti pamoja na kufanya maboresho ya Kiwanja cha Ndege cha Mwanza. Viwanja hivi ni vya kimkakati nchini kwani vitachochea Utalii kwa kuwa vipo karibu na vivutio vya utalii hususan mbuga ya Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Wizara inaonesha kuwa, Kiwanja cha Serengeti kitatengewa shilingi bilioni 1.3 na kile cha Mwanza kitatengewa Shilingi bilioni 13.80 kwa ajili ya kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu. Hata hivyo, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Kiwanja cha Serengeti kimetengewa shilingi milioni 100 tu huku kile cha Mwanza kikitengewa shilingi bilioni sita tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati haijaridhika na kiasi cha fedha kilichotengwa na Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo katika mwaka ujao wa fedha. Kamati inaitaka Serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa viwanja hivi kwa sababu ya manufaa yake ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Ndege Tanzania *(ATCL)*. Serikali imefanya uwekezaji mkubwa wa shilingi trilioni 2.7 katika kufufua Kampuni ya Ndege Tanzania *(ATCL)*. Fedha hizi zimetumika katika kununua ndege, kukarabati karakana na miundombinu wezeshi pamoja na kulipa malimbikizo ya madeni ya Kampuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji huo umeiwezesha *ATCL* kuongeza mapato kufikia shilingi bilioni 595.7 kwa mwaka 2025 kutoka shilingi bilioni 175 kwa mwaka 2021 kupitia huduma za usafiri wa anga kwa vituo 15 vya ndani ya nchi na vituo 17 nje ya nchi. Hata hivyo, *ATCL* inajiendesha kwa hasara huku ikitegemea ruzuku ya Serikali katika kulipa wafanyakazi wake mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hiyo inachangiwa na uamuzi wa Serikali kuikodishia ndege *ATCL* kutoka kwa Wakala wa Ndege Tanzania *(TGFA)*. *ATCL* hulazimika kulipia kila mwezi huduma ya kukodisha pamoja na fedha za matengenezo ya ndege kwa *TGFA* hali inayoifanya *ATCL* kuwa na gharama kubwa za uendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati mara kadhaa imekuwa ikitoa maoni kwa Serikali kufanya uamuzi wa kuzifanya ndege hizo kuwa chini ya *ATCL.* Mathalani, katika Taarifa ya Shughuli za Kamati ya Mwaka 2024, iliyosomwa Bungeni mwezi Februari, 2025, Kamati ilipendekeza na Bunge kuridhia azimio la kuitaka Serikali kurejesha ndege hizo chini ya umiliki wa *ATCL*. Vilevile, tangu mwaka 2021, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* ametoa pendekezo hilo, lakini hadi sasa Serikali imekuwa na kigugumizi cha kutekeleza jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inataka kujua, ni kwanini hadi sasa Serikali imeshindwa kutekeleza azimio hilo la Bunge? Vilevile, ndege hizo zikiwa mali ya *ATCL,* ni mtaji katika mizania ya vitabu vya hesabu za *ATCL.* Pia, zitaongeza na kuondokana na hasara ya kila mwaka kama inavyoripotiwa na *CAG*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ya huduma ya reli nchini. Huduma ya usafiri wa reli nchini inatolewa na *TRC* na *TAZARA*. Huduma hii inakabiliwa na changamoto ya uchakavu wa miundombinu ya reli, mabehewa na vichwa vya treni. Uwekezaji katika miundombinu hii unahitaji fedha nyingi ambazo kuendelea kutegemea mpango wa bajeti itachukua muda mrefu kuiboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imechukua hatua mbalimbali kwa ajili ya kuendelea kuboresha huduma hiyo muhimu kwa ukuaji wa uchumi wa nchi. Mathalani, tarehe 28 Aprili, 2026, Serikali ilisaini mkataba wa Dola za Marekani bilioni 1.22277 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Reli ya *SGR* vipande vya Makutopora - Tabora, na Tabora - Isaka vyenye jumla ya Kilometa 533.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *TAZARA*, Serikali imekamilisha hatua za kuingia Mkataba wa Ufufuaji na Uboreshaji wa Reli ya *TAZARA*. Mkataba huu ulisainiwa tarehe 29 Septemba, 2025 kati ya Serikali za Tanzania na Zambia, kwa kushirikiana na Kampuni ya *CCECC* ya China. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuanza Juni, 2026 na utaongeza ufanisi katika usafirishaji wa reli na Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hizo na kuendelea kuboresha miundombinu ya huduma za reli nchini. Hata hivyo, mtandao wa reli katika Kanda ya Kaskazini bado unakabiliwa na changamoto ya uchakavu na kusababisha kushuka kwa ufanisi katika matumizi ya reli hiyo. Aidha, Reli ya Tanga hadi Musoma na ile ya *Mbamba Bay* hadi Mtwara bado hazijapata fedha pamoja na kuwa Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu kuhusu reli hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ya usafiri wa majini. Wizara ya Uchukuzi inahusika na usimamizi wa miundombinu ya usafiri katika bahari na maziwa ikiwa ni pamoja na meli na bandari zake kupitia taasisi za *TPA, TASHICO* na *TASAC* kama mdhibiti wa usafiri wa majini. Huduma ya usafiri majini inakabiliwa na changamoto ya upungufu wa meli katika maziwa makuu, uchakavu wa bandari za maziwa makuu pamoja na ajali ambazo wakati mwingine zinagharimu uhai wa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kufanya uwekezaji mkubwa kwa kukamilisha ukarabati wa Meli za *MT Sangara* na kuendelea na ukarabati wa *MV Liemba* ambayo imefikia 70%. Meli hiyo inatarajiwa kukamilika na kuanza kazi Julai,

2026. Aidha, Serikali imekamilisha ujenzi wa meli mbili za mizigo ambazo zinaweza kubeba tani 2,000 kila mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia imeendelea kuchukua hatua za kuimarisha usalama wa usafiri na usafirishaji majini, ambapo kituo cha Uokozi *(Search and Rescue Centre)* kimejengwa katika Ziwa Victoria. Vilevile, *TASAC* imekuwa ikishirikiana na taasisi nyingine katika kufanya doria za usalama na ukaguzi wa vyombo vya majini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo, bado baadhi ya miundombinu ya Bandari na Meli hasa katika maziwa makuu hauridhishi. Mathalani, Bandari ya Musoma katika Ziwa Victoria haifanyi kazi kwa muda mrefu. Aidha, katika mipango yake, Serikali haijaonesha mkakati madhubuti wa kuifufua Bandari hiyo ambayo ni moja ya kitovu cha shughuli za kiuchumi katika eneo la Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa huduma za usafiri wa ardhini. Usafiri wa ardhini ndio unaotumiwa na watu wengi hapa nchini kwa ajili kusafirisha watu na bidhaa katika masoko mbalimbali. Kwa hiyo, usimamizi madhubuti unaolinda watoa huduma na watumiaji katika gharama na usalama ni jukumu la msingi la Serikali kwa ajili ya ustawi wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu, jukumu hili linatekelezwa chini ya Wizara ya Uchukuzi kupitia *LATRA*. Katika mwaka wa fedha 2025/2026, *LATRA* imetekeleza majukumu yake ya kisheria kwa kuhakikisha inafunga vidhibiti mwendo (*VTS*) kwenye magari ya abiria ili kuzuia mwendo kasi ambao umekuwa chanzo cha ajali nyingi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata nafasi ya kutembelea na kuona namna vidhibiti mwendo hivyo vinavyofanya kazi. Kamati inaipongeza Serikali na *LATRA* kwa namna inavyoendelea na udhibiti wa usafiri wa ardhini ikiwa ni pamoja na matumizi ya magari, pikipiki na reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio haya na *LATRA* inakabiliwa na changamoto muundo kiundeshaji kwani kumekuwa na mgongano wa kisheria katika utekelezaji wa majukumu yake na yale ya Jeshi la Polisi, Kitengo cha Usalama Barabarani. Kamati imebaini kuwa, kwa upande wa Zanzibar majukumu yote ya Usalama Barabarani yapo chini taasisi ya Zanzibar *Road Safety Authority (ZARTSA)* ambayo imefanikiwa sana katika kudhibiti ajali za barabarani kwa magari binafsi, biashara, Serikali na hata pikipiki na bajaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kuwa sasa umefika wakati kwa Sheria ya *LATRA* na ile ya Jeshi la Polisi kuangaliwa upya ili kuweza kuondoa mkanganyiko huu. Hali hii itaondoa malalamiko miongoni mwa wananchi na kuongeza uwajibikaji wa moja kwa moja wa Mamlaka ya udhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa 2026/2027. katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara na taasisi zake inalenga kukusanya jumla ya shilingi 4.061 sawa na ongezeko la 19.48% kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaitaka Wizara iweke mikakati madhubuti katika kukusanya maduhuli ya Serikali ili kufikia lengo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi trilioni 2.872 sawa na ongezeko la asilimia 4.60 ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026. Katika fedha hizo shilingi bilioni 126.041 sawa na asilimia 4.38 ni fedha za matumizi ya kawaida huku shilingi trilioni 2.746 sawa na 95.62% zikiwa ni fedha za kugharimia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwani ongezeko hilo litaiwezesha Wizara kutekeleza majukumu na vipaumbele vyake kwa ufanisi. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inatoa fedha kwa wakati ili kupata tija katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati. Baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa Bajeti pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 62 - Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2026/2027, sasa ninaomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla ni kama yafuatayo:-

(a) Serikali ihakikishe inatoa fedha za maendeleo kama zilivyoidhinishwa na Bunge na kusimamia kikamilifu miradi ya kimkakati inayotekelezwa na Wizara hii ili kuleta tija iliyokusudiwa;

(b) Serikali iongeze kasi katika kuboresha miundombinu ya sekta ya uchukuzi ili kuongeza mchango wa sekta hiyo katika kukuza uchumi wa kisasa pamoja na kuzalisha ajira kwa vijana nchini;

(c) Serikali iweke mikakati madhubuti na kuzisimamia taasisi zilizo chini ya Wizara hii katika ukusanyaji wa mapato ili ziweze kujitegemea na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali; na

(d) Serikali iendelee kusimamia na kuweka mazingira ya kuwezesha taasisi za umma na binafsi kutoa huduma bora za usafiri wa abiria na bidhaa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni mahususi kwa upande wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)*. Inashauriwa kuwa:-

(i) Serikali ianze kutekeleza matumizi ya ada mpya kwa watumiaji wa Bandari nchini kuanzia tarehe 1 Julai, 2026 ili kuhakikisha *TPA* inapata fedha za kuendeleza miundombinu ya Bandari nchini;

(ii) Serikali ihakikishe inatekeleza kwa kasi maboresho ya miundombinu ya Bandari ili kuhakikisha kuwa kasi ya ufanisi wa bandari inawiana na maendelezo hayo; na

(iii) Wizara na *TPA* ziendelee kukutana na wadau na watumiaji wa bandari mara kwa mara kwa ajili kutoa elimu kuhusu umuhimu wa ada mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miundombinu ya Viwanja vya Ndege Nchini. Kamati inashauri kuwa: -

(i) Serikali ikamilishe Maboresho ya Viwanja vya Ndege vya Kigoma, Musoma na Shinyanga kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wa maeneo hayo wanapata huduma ya usafiri wa ndege; na

(ii) Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Serengeti pamoja na maboresho ya Kiwanja cha Ndege cha Mwanza kwani viwanja hivyo ni vya kimkakati katika kukuza utalii na kukuza uchumi na kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa huduma ya usafiri wa anga nchini. Kamati inashauri kuwa, Serikali: -

(i) Serikali ihakikishe inarejesha ndege chini ya umiliki wa *ATCL* kutoka *TGFA* uamuzi ambao utaifanya *ATCL* kuanza kujiendesha kwa faida na kutoa gawio kwa Serikali; *(Makofi)*

(ii) Serikali iharakishe ununuzi wa ndege mpya nne na moja ya mizigo ili kuongeza ufanisi katika huduma ya Usafiri wa Anga nchini kupitia *ATCL;*

(iii) Serikali ifanye tathmini kuhusu *ATCL* kuanzisha safari za ndege kutoka Dodoma kwenda mikoa mingine moja kwa moja bila kupitia Dar es Salaam ili kukidhi mahitaji ya wananchi wanaohitaji huduma hiyo; *(Makofi)*

(iv) Serikali ihakikishe *ATCL* inatoa taarifa kwa abiria kuhusu mabadiliko ya ratiba za ndege ili kuondoa usumbufu kwa abiria; na

(v) Vilevile ipitie upya nauli za ndege ili ziweze kuwa na uhalisia na kuondoa malalamiko miongoni mwa abiria wa safari za anga nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za usafiri wa reli nchini. Kamati inashauri kuwa, Serikali: -

(i) Serikali iongeze kasi katika Ujenzi wa Reli ya Kisasa ya *SGR* katika vipande Makutopora - Tabora, Tabora - Isaka, Isaka - Mwanza, Tabora - Kigoma, na Uvinza - Msongati vilivyobaki ili reli hiyo iweze kutumika katika kusafirisha abiria na mzigo kama ilivyokusudiwa; *(Makofi)*

(ii) Serikali ihakikishe inamsimamia mkandarasi *Yep Merkezi* ya Uturuki ili aongeze kasi katika utekelezaji wa miradi hiyo ili kuleta tija iliyokusudiwa kwenye miradi husika;

(iii) Serikali iboreshe huduma ya mawasiliano ya simu ndani ya treni ya *SGR* ili kuwe na uhakika wa abiria kupata mawasiliano wanapokuwa safarini; *(Makofi)*

(iv) Serikali iandae utaratibu wa kuanza ujenzi wa reli ya Mbamba Bay - Mtwara na ile ya Tanga - Musoma kwa njia ya Ubia kati yake na Sekta binafsi *(PPP)* kwa kuweka motisha *(incentives)* kwa sekta binafsi ili kuvutia sekta hiyo katika utekelezaji wa miradi hiyo; na *(Makofi)*

(v) Serikali ihakikishe ukarabati na maboresho ya reli ya *TAZARA* yanaanza na kukamilika kwa wakati ili kuunganisha matumizi ya reli hiyo na Bandari ya Dar es Salaam katika kuendelea kuhudumia sehemu kubwa ya nchi za Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya usafiri wa majini nchini. Kamati inashauri kuwa, Serikali: -

(i) Serikali ihakikishe *TASHICO* inakamilisha ukarabati wa meli ya MV Liemba ili iweze kuanza safari katika Ziwa Tanganyika kwani eneo hilo lina mvuto mkubwa wa kibiashara;

(ii) Serikali iongeze uwekezaji katika kuendeleza Bandari za Maziwa Makuu ikiwemo Bandari ya Musoma ili kuchochea shughuli za kiuchumi katika maeneo hayo; (Makofi)

(iii) Serikali itenge fedha za kutosha katika ujenzi wa Kiwanda cha Meli katika Ziwa Tanganyika pamoja na ujenzi wa meli mbili za mizigo ili uanze haraka na kukuza sekta ya uchukuzi wa majini nchini; na

(iv) Kuendelea kuwekeza katika usalama wa huduma ya safari za majini pamoja na kujenga vituo vya uokozi katika Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na Bahari ya Hindi ili kukabiliana na ajali za majini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa huduma ya usafiri wa ardhini. Kamati inashauri kuwa, Serikali: -

(i) Ifanye marekebisho ya Sheria kuhusu muundo wa *LATRA* ili kuweza kuondoa mkanganyiko wa majukumu kati ya *LATRA* na Jeshi la Polisi katika suala la udhibiti wa usalama barabarani nchini;

(ii) *LATRA* iendelee na ubunifu na matumizi ya teknolojia katika magari ya abiria ili kupunguza ajali ambazo zinasababisha upotevu wa maisha ya watu, kuleta ulemavu na uharibifu wa mali nchini;

(iii) Ihakikishe *LATRA* inakuwa na kazi ya kulea sekta binafsi katika usafiri wa ardhini hasa vijana wanaoendesha pikipiki maarufu kama bodaboda badala ya kukamata na kufungia vyombo vyao mara kwa mara; na

(iv) Ihakikishe *LATRA* inatoa elimu kuhusu haki na wajibu kwa wadau wa sekta ya usafiri wa ardhini nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vya mafunzo vilivyo chini ya Wizara ya Uchukuzi. Kamati inashauri kuwa, Serikali: -

(i) Serikali iweke mpango madhubuti wa kutangaza taaluma zinazotolewa katika vyuo hivyo ili kuvutia udahili wa wanafunzi katika taaluma hizo, kwani imebainika kuwa wazazi na wanafunzi wengi hawana taarifa kuhusu taaluma zinazotolewa katika vyuo hivyo ikiwemo urubani, unahodha na ubaharia;

(ii) Serikali ihakikishe inakamilisha miradi ya kimkakati kwa ajili ya upanuzi wa kampasi na uboreshaji wa vyuo hivi kwa ajili ya mafunzo endelevu katika sekta ya uchukuzi nchini; na

(iii) Serikali ifanye tathmini na kulipa deni la shilingi milioni 721.7 ambalo Chuo cha *DMI* kinadaiwa na Kampuni ya *E1 Limited* kutokana na huduma zilizotolewa kwa chuo na kampuni hiyo katika mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Kwa namna ya kipekee naendelea kukushukuru wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu. Pia namshukuru Spika kwa maelekezo yake ambayo yamekuwa msaada mkubwa katika uendeshaji bora wa shughuli za kila siku za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Aidha, ninamshukuru Naibu Spika, kwa namna anavyomsaidia kutekeleza majukumu yake, pamoja na ninyi Wenyeviti wa Bunge kwa kumsaidia kuendesha vikao vya Bunge kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie fursa hii kumshukuru Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa; na Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, kwa ushirikiano ambao wameipatia Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Aidha, niwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Uchukuzi pamoja na taasisi zake chini ya uongozi wa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Profesa Godious Walter Kahyalala kwa ushirikiano wao kwa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo wa dhati kabisa, ninawashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ambao wamekuwa mstari wa mbele katika kuendelea kuisimamia Wizara ya Uchukuzi pamoja na

taasisi zilizo chini yake kwa niaba ya Bunge lako Tukufu. Kwa hakika, maoni, ushauri na mapendekezo yao yana mchango mkubwa katika kuboresha utendaji wa Serikali. Naomba niwatambue Wajumbe wote ili majina yao yaingie katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama inavyosomeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, ninawashukuru sana watendaji wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Bwana Baraka I. Leonard kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake hadi kukamilika kwa Taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja. Baada ya maelezo hayo, naomba Bunge lako likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha na niunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA FUNGU 62 - WIZARA YA UCHUKUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**1.1 Maelezo ya Awali**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 121 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025 [Kanuni za Bunge] naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Fungu **62 – Wizara ya Uchukuzi** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na maoni ya

Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika**, bila kuathiri masharti yanayopatikana katika Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge, taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo:-

a) Sehemu ya kwanza ni utangulizi ambayo inaeleza kuhusu muundo wa taarifa pamoja na namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake;

b) Sehemu ya pili inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kwa kutathmini uzingatiaji wa ushauri na maoni ya Kamati, makusanyo ya maduhuli, mwenendo wa upatikanaji wa fedha na utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
c) Sehemu ya tatu inahusu uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027;
d) Sehemu ya nne ni majumuisho ya maoni na ushauri wa Kamati; na
e) Sehemu ya tano ni hitimisho.

### 1.2 Namna Kamati Iliyotekeleza Majukumu Yake

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu hutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia masharti mbalimbali yaliyoainishwa katika Katiba, Sheria mbalimbali na Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, katika kufanyia kazi utekelezaji wa Bajeti ya **Fungu 62 - Wizara ya Uchukuzi** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027,
Kamati ilifanya yafuatayo: -

a) Kupokea dondoo (extracts) na randama ya Wizara kwa ajili ya Uchambuzi wa Bajeti [Kanuni ya 118 (1)];

b) Kupokea taarifa na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2025/2026 [Kanuni ya 120 (1)]; na

c) Kuchambua utekelezaji wa Bajeti ya Wizara na taasisi zake kwa mwaka wa Fedha 2025/2026, pamoja na kufanya ulinganisho wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 [Kanuni ya 120 (2)].

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### 2.1 Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 15 Mei, 2025, Bunge lilipokea, kujadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya **Fungu 62- Wizara ya Uchukuzi** kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Katika kikao hicho, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu iliwasilisha maoni yake katika maeneo 13 kuhusu Bajeti ya Wizara hiyo ili kutimiza masharti yaliyowekwa na Kanuni ya 121 (9).

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, kwa sehemu kubwa Serikali imeyafanyia kazi maoni na ushauri uliotolewa na Kamati. Moja kati ya ushauri wa Kamati uliofanyiwa kazi ni pamoja na Wizara kuzisimamia taasisi ili ziweze kujiendesha bila kutegemea ruzuku kutoka Serikalini na kuongeza tija katika utendaji wa taasisi hizo.

**Mheshimiwa Spika,** kuanzia Disemba, 2025, Shirika la Reli Tanzania (TRC) limeanza kujitegemea na kujiendesha bila ruzuku ya Serikali kwa **asilimia 100**. Hatua hii imetokana na kuimarika kwa makusanyo na nidhamu ya matumizi ya fedha kwa Shirika. Aidha, Serikali imeokoa jumla ya **Shilingi 12,922,956,640/=** zilizokuwa zinatolewa kwa ajili ya mishahara kwa wafanyakazi wa Shirika pamoja na kutoa nafasi kwa fedha hizo kuelekezwa katika vipaumbele vingine vya Serikali. Kamati inapongeza Wizara na TRC kwa kufikia hatua hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo, baadhi ya maoni na ushauri uliotolewa na Kamati utekelezaji wake hauridhishi kwa sababu hiyo Kamati inapenda kuweka msisitizo kuhusu umuhimu wa utekelezaji wake. Mathalani, ushauri wa Serikali kuanza ujenzi wa kiwanja kipya cha ndege cha Mkoa wa Kagera (Kyabajwa), Kiwanja cha Ndege cha Moshi pamoja na viwanja vingine vya mikoa. Kamati imebaini kuwa kasi ya utekelezaji wa miradi hii hairidhishi. Kamati inaitaka Wizara kutekeleza miradi hiyo ili wananchi wa maeneo hayo wapate nafasi ya kutumia huduma ya safari za anga.

**2.2 Makusanyo ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Uchukuzi pamoja na taasisi zake ilipangiwa kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 3,399,148,152,880/=.** Hadi kufikia Februari, 2026 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya **Shilingi 1,961,235,214,430.10,** sawa na **asilimia 57.70** ya lengo ikilinganishwa na **asilimia 66.7** ya mpango kazi wa utekelezaji wa bajeti. Kamati inaitaka Wizara na taasisi zake kuongeza ubunifu na kasi katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali ili kufikia lengo la makusanyo lililowekwa.

**2.3 Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Uchukuzi iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 2,746,485,018,000/=** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi Kamati umebaini kuwa, hadi kufikia Machi, 2026, Wizara ilikuwa imepokea **Shilingi 1,314,572,080,299.72** sawa na asilimia **67.6** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge ikiwa ni pungufu ukilinganisha na mpango kazi wa utekelezaji wa bajeti ulioripotiwa ambao ni **asilimia 75**.

### 2.3.1 Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2025/2026, **Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi** iliidhinishiwa **Shilingi 125,438,950,000/=** ikiwa ni fedha za matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Februari, 2026, Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 79,851,314,199.48** sawa na **asilimia 63.66** ya bajeti iliyoidhinishwa kama ilivyoainishwa katika **Kielelezo Na. 2**.

**Kielelezo Na. 1: Mwenendo wa Mapokezi ya Fedha za Matumizi ya Kawaida toka Hazina hadi kufikia Machi, 2026**

| Bajeti (Matumizi) | Kiasi Kilichoidhinishwa 2025/2026 (Shilingi) | Kiasi Kilichopokelewa (Shilingi) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|
| Mishahara (P.E) | 96,654,340,000.00 | 63,048,570,554.48 | 65.23 |
| Matumizi Mengineyo(O.C.) | 28,784,610,000.00 | 16,802,743,645.00 | 58.40 |
| **JUMLA KUU** | **125,438,950,000.00** | **79,851,314,199.48** | **63.66** |

**Mheshimiwa Spika**, fedha za Mishahara (P.E) zimepokelewa kwa **asilimia 65.23** ikiwa ni pungufu ikilingnishwa na **asilimia 75** ya utekelezaji wa mpango kazi wa bajeti. Kamati imebaini kuwa hatua hii imetokana na Shirika la Reli Tanzania (TRC) kuanza kujitegemea kwa **asilimia 100** katika eneo lamishahara kuanzia Disemba, 2025.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine wa fedha za Matumizi Mengineyo (O.C.), Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 16,802,743,645/=** sawa na **asilimia 58.40** tu ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge ikilinganishwa na **asilimia 75** ya mpango kazi wa utekelezaji wa bajeti.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Wizara kwa usimamizi wake katika Shirika la Reli Tanzania ambao umechangia Shirika hilo kuongeza mapato na kujitegemea kwa **asilimia 100** katika matumizi yake ikiwemo mishahara. Hata hivyo, Kamati

inaitaka Serikali kuhakikisha inatoa fedha za Matumizi Mengineyo kama zilivyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu ili Wizara hii iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuleta tija iliyokusudiwa.

### 2.3.2 Fedha za Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Uchukuzi iliidhinishiwa na Bunge jumla ya **Shilingi 2,621,046,068,000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa hadi kufikia Machi, 2026 Wizara ilikuwa imepokea **Shilingi 1,234,720,766,100.24** sawa na **asilimia 47.11** ya makadirio. **Kielelezo Na. 3** kinatoa mchanganuo wa hali ya mapokezi ya fedha za bajeti ya maendeleo.

**Kielelezo Na. 2: Mwenendo wa Mapokezi ya Fedha za Matumizi ya Kawaida toka Hazina hadi kufikia Machi, 2026**

| Bajeti (Matumizi) | Kiasi Kilichoidhinishwa 2025/2026 (Shilingi) | Kiasi Kilichopokelewa (Shilingi) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|
| Ndani | 2,452,512,444,000.00 | 1,201,304,805,664.62 | 49.00 |
| Nje | 168,533,624,000.00 | 33,415,960,435.62 | 19.83 |
| **JUMLA KUU** | **2,621,046,068,000.00** | **1,234,720,766,100.24** | **47.11** |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya uchambuzi wa kina katika mwenendo wa upatikanaji wa fedha za Maendeleo ambapo unaonyesha kwamba hadi kufikia mwezi Machi, 2026:-

(i) Kwa ujumla, Wizara imepokea **asilimia 47.11** ya fedha za miradi ya maendeleo ikilinganishwa na **asilimia 75** ya mpango kazi wa utekelezaji wa bajeti. Vilevile, Fedha za ndani kwa ajili ya Maendeleo zimepokelewa kwa **asilimia 49 tu** ya bajeti iliyoidhinishwa. Mwenendo huu utapunguza kasi pamoja na kuongeza gharama ya miradi; na

(ii) Fedha za Nje zimepokelewa na Wizara kwa **asilimia 19.83** tu ya bajeti iliyoidhinishwa. Mwenendo huu unaonesha kuwa kutegemea fedha za nje kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo kunaweza kuathiri utekelezaji wa miradi husika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haikuridhishwa na mwenendo wa upatikanaji wa fedha za kugharamia miradi ya maendeleo katika Wizara ya Uchukuzi. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuchukua hatua za haraka za kupunguza utegemezi wa fedha za nje kwenye kugharamia miradi ya maendeleo katika Wizara hii.

**2.4 Ukaguzi wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**
**2.4.1 Maelezo ya Awali**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2025/2026. Ukaguzi huo ulifanyika kwa mujibu wa Kanuni ya 120 (1) ya Kanuni za Bunge kwa lengo la kutathmini hali ya mapokezi ya fedha, hatua ya utekelezaji pamoja na kubainisha changamoto za utekelezaji wa miradi hiyo. Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi katika mikoa ya Tanga, Dar es Salaam na Pwani kati ya tarehe 13 na 19 Machi, 2026.

**2.4.2 Miradi Iliyokaguliwa**

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitoe ufafanuzi wa miradi hiyo kwa muhtasari kama ifuatavyo: -

**(a) Mradi Na. 4227– Ujenzi na Maboresho ya Bandari**

**Mheshimiwa Spika**, miradi ya ujenzi na Bandari inatekelezwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA). Kamati ilitembelea na kufanya ukaguzi wa ujenzi na maboresho ya bandari katika Bandari za Tanga, Dar Es Salaam na Bandari kavu ya Kwala kama ifuatavyo:-

(i) Ujenzi na Maboroesho ya Miundombinu ya Bandari ya Tanga

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ukaguzi wa mradi huu tarehe 13 Machi, 2026. Maboresho yalihusisha maeneo manne ambayo ni:-

- Kupanua na kuongeza kina cha lango (entrance channel) la kuingilia meli na kufikia upana wa **mita 135** na kina cha **mita 13**;

- Upanuzi wa eneo la kugeuzia meli (Turning basin) hadi kufikia **mita 400**;

- Ununuzi wa mitambo 16 ya kuhudumia shehena; na

- Usimikaji wa mitambo ya Umeme, Zimamoto na TEHAMA.

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ulianza mwaka 2019 na umegharimu jumla ya **Shilingi Bilioni 429.1**. Mradi umekamilika na tayari umeanza kutumika.

**Mheshimiwa Spika,** kukamilika na kutumika kwa mradi huu kumeongeza ufanisi na tija kubwa katika Bandari ya Tanga. Manufaa yaliyopatikana yanahusisha kuongezeka kwa watumishi wa bandari, kupungua kwa muda wa kuhudumia shehena na ongezeko la shehena ya mzigo unaohudumiwa katika Bandari hiyo. Mapato yameongezeka **kutoka Shilingi Bilioni 17.233** mwaka 2019/2020 hadi kufikia **Shilingi Bilioni 92.415** katika kipindi cha miezi nane tu ya mwaka 2025/2026.

(ii) Ujenzi na Maboresho ya Miundombinu ya Bandari ya Dar Es Salaam

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mradi huu umegharimu jumla ya **Dola za Marekani Milioni 421** ikiwa ni Mkopo toka Benki ya Dunia, Ruzuku toka DFID na mapato ya ndani ya Mamlaka. Mradi huu umehusisha maeneo matano kama ifuatavyo:-

- Kuimarisha Gati namba 1 hadi 7 na kujenga Gati maalumu (RoRo berth);

- Kuongeza kina na upana wa lango la kuingilia meli

- Kuimarisha Gati namba 8 hadi 11;

- Kuboresha mtandao wa reli ndani ya Bandari; na

- Kusimika mfumo wa Umeme Bandarini (Gati namba 1 hadi 7 na ile ya RoRo).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ukaguzi wa mradi huu tarehe 15 Machi, 2026 na kukuta mradi umefikia hatua mbalimbali za utekelezaji wake kama ifuatavyo:-

- Uboreshaji wa Gati 1-7 umekamilika kwa asilimia 100 kwa kuongezewa kina kutoka **mita 8** hadi **mita 14**. Gati hizi kwa sasa zinatumika kupokea meli kubwa zenye urefu wa kufikia **mita 305** zenye uwezo wa kubeba **makasha 8,000** kwa wakati mmoja;

- Ujenzi wa Gati la kushushia magari (RoRo) na yadi yenye ukubwa wa mita za **mraba 73,000** kwa ajili ya kubeba **magari 280,000** kwa mwaka vimekamilika kwa **asilimia 100;**

- Kina cha lango la kuingilia meli kimeongezwa kutoka **mita 12** hadi **mita 15.5** huku upana wa lango ukiongezwa kutoka **mita 140** hadi **mita 170** ambapo umewezesha Bandari kupokea meli zenye urefu wa **mita 305** badala ya uwezo wa zamani wa kupokea meli zenye urefu wa **mita 240** tu;

- Shughuli ya kusimika umeme katika Gati 1 hadi 7 na Gati la RoRo zimekamilika na kuwezesha gati hizo kuanza kazi; na
- Shughuli za Kuimarisha Gati namba 8 hadi 11 na ile ya Kuboresha mtandao wa reli ndani ya Bandari zimefikia hatua mbalimbali za manunuzi ili kuwezesha kuanza kwa shughuli hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Bandari ya Dar Es Salaam imeongeza ufanisi na tija kutokana na matumizi ya Gati 1 hadi 7 na lile la RoRo. Hali hii imesababisha msongamano wa shehena katika Bandari hiyo. Hatua za haraka zinatakiwa kuchukuliwa katika kukamilisha mradi wa Gati 8 hadi 11 pamoja na kuboresha

mtandao wa reli ndani ya Bandari ili kupunguza msongamano wa shehena bandarini.

(iii) Maboresho na Utendaji wa Bandari Kavu ya Kwala.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilianzisha mradi huu ikiwa na lengo la kupunguza shehena na meli katika Bandari ya Dar Es Salaam, kuongeza kasi ya utoaji shehena na kuimarisha ushindani wa Tanzania kama kitovu cha biashara kikanda. Mradi huu umegharimu **Shilingi Bilioni 83.25** kwa ajili ya kusafisha, kujenga uzio, kujenga yadi ya makasha, kujenga reli mchepuko na barabara ya zege. Kamati ilifanya ziara na kukagua utendaji wa Bandari kavu ya Kwala tarehe 19 Machi, 2026.

**Mheshimiwa Spika**, Bandari ya Kwala ina ukubwa wa **hekta 504** ikiwa na uwezo wa kuhudumia takribani **makasha 823** kwa siku sawa na **makasha 300,000** kwa mwaka. Shehena hii ni sawa na **asilimia 30** ya uwezo wa Bandari ya Dar Es Salaam.

**Mheshimiwa Spika**, Bandari hii imeanza kazi ndani ya mwaka huu wa fedha na hadi kufikia Februari, 2026 ilikuwa imehudumia **makasha 13,090**. Zaidi ya **asilimia 90** ya shehena iliyohudumiwa hadi sasa ni Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na umuhimu wa DRC katika matumizi ya Bandari Kavu ya Kwala, TPA ilitoa **hekta 45** kwa ajili DRC kuliendeleza na kulitumia eneo hilo katika kupokea na kuondoa mizigo yao bila kufika Bandari ya Dar Es Salaam. Aidha, tarehe 09 Machi, 2026, nchi ya DRC ilitiliana saini na Kampuni ya Bostoni ya Marekani kwa ajili ya kuendeleza miundombinu ya eneo hilo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ya kuwekeza na kufanya maboresho ya miundombinu ya Bandari za Tanga, Dar Es Salaa na Bandari Kavu ya Kwala. Matokeo ya miradi hii ni kuendelea kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara pamoja na kuongeza ushindani katika matumizi ya bandari zetu dhidi ya washindani wetu katika ukanda wa Maziwa Makuu.

(iv) Miradi ya Maboresho ya Vyuo chini ya Wizara

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Uchukuzi imefanya maboresho ya miundombinu na ununuzi wa vifaa katika vyuo mbalimbali vya mafunzo. Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa miradi hiyo kama ifuatavyo:-

(v) Mradi Namba 6727- Maboresho ya Chuo cha Bahari Dar Es Salaam (DMI)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kukagua uboreshaji uliofanyika katika miundombinu ya kujifunza na kujifunzia katika Chuo cha DMI tarehe 14 Machi, 2026. Kamati ilibaini kuwa, Serikali imekiwezesha Chuo hiki katika ununuzi wa mtambo unaoitwa Full Mission Bridge and Engine Room Simulator kwa gharama ya **Shilingi Bilioni 7**.

**Mheshimiwa Spika,** mtambo huu unakifanya Chuo cha DMI kuwa kituo cha Umahiri (Centre of Excellence) katika taaluma za Baharini katika ukanda wa Afrika. Aidha, Chuo kwa sasa kinaweza kutoa mafunzo bila kutegemea upatikanaji wa meli kwani mtambo huu unaweza kumpa mwanafunzi uzoefu kama nahodha wa meli baharini.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile, Serikali imeboresha Karakana ya chuo hicho kwa kufanya ununuzi wa vifaa vya kisasa vya **Shilingi Milioni 740** pamoja na Rada iliyogharimu **Shilingi Milioni 221.198**. Kupitia maboresho haya yaliyofanywa kwenye Chuo hiki, wanafunzi wanapata ujuzi kwa vitendo katika ufuatiliaji wa vyombo vya majini hivyo kuepusha ajali za majini.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hatua hizo za kuboresha Chuo cha DMI zilizofanywa na Serikali, Chuo hicho kinadaiwa na Kampuni ya E1 Limited jumla ya **Shilingi Milioni 721.7** tangu mwaka wa fedha 2021/2022. Deni hili linatokana na Kampuni hiyo kuiuzia na kusimika mtambo wa kufundishia wanafunzi unaojulikana kama Full Mission Crane Simulator. Ni vyema Serikali ikafanya

malipo ya deni hilo ili kuzuia adhabu ya tozo ya kuchelewesha malipo toka kwa Kampuni ya E1 Limited.

(vi) Mradi Namba 4202- Ujenzi wa Miundombinu ya Chuo cha Mafunzo ya Usafiri wa Anga (CATC)

**Mheshimlwa Spika**, utekelezaji wa mradi huu ulianza tarehe 1 Agosti, 2025 na unatarajia kukamilika tarehe 31 Julai, 2028. Mradi huu unatekelezwa kwa jumla ya **Shilingi 71,004,359,477.54** ukiwa unagharamiwa na Serikali kwa **asilimia 100**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kukagua mradi huo tarehe 16 Machi, 2026 ambapo utekelezaji wa mradi umefikia takribani **asilimia 11.32**, sambamba na ratiba ya ujenzi. Mradi huu unahusisha ujenzi wa majengo 10 na kazi za nje hasa matengenezo ya bustani. Baada ya kukamilika kwa mradi huo, Serikali itafanya manunuzi ya vifaa na samani kwa ajili ya majengo hayo kwa jumla ya **Shilingi Bilioni 10. 51**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeridhishwa na kasi ya utekelezaji wa mradi huu. Hata hivyo, Mkandarasi amewasilisha hati ya malipo ya **Shilingi Bilioni 2.07** ambazo zilikuwa hazijalipwa hadi wakati Kamati inatembelea mradi. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha inafanya malipo kwa wakati ili mradi huo uweze kukamilika kwa wakati na kuleta tija iliyokusudiwa.

(vii) Mradi Namba 4309- East Africa Skills for Transformation and Regional Intergration Project (EASTRIP)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ukaguzi wa mradi wa EASTRIP ambao unalenga kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunzia katika Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) tarehe 16 Machi, 2026. Mradi wa EASTRIP ulianza kutekelezwa Novemba, 2022 na ulitarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2026.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi unagharimu jumla ya **Shilingi 32,034,520,226.02** ukiwa ni mkopo kutoka Benki ya Dunia na ruzuku ya Serikali kuu. Mradi huu unahusisha shughuli za Ujenzi wa mabweni, Ujenzi wa majengo matatu ya Kituo cha Umahiri cha

Taaluma za Usafiri wa Anga na Ujenzi wa Karakana ya Matengenezo ya Ndege katika Kampasi ya NIT iliyopo Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA).

**Mheshimiwa Spika,** Miradi ya ujenzi wa mabweni na kituo cha umahiri cha taaluma za usafiri wa anga imekamilka kwa **asilimia 100** na tayari kinatumika kwa wakufunzi na wanafunzi katika kutoa taaluma chuoni hapo. Aidha, mradi wa Ujenzi wa Karakana umefikia **asilimia 15** na unatarajiwa kukamilika kufikia Julai, 2026.

**Mheshimiwa Spika,** kukamilika kwa miradi hii kutaongeza ufanisi na tija katika mafunzo ya kimkakati kwenye sekta ya usafirishaji nchini. Kamati inaipongeza Serikali kwa uwekezaji mkubwa ilioufanya katika vyuo hivi.

(viii) Mradi wa Uundaji wa Vichwa vya MGR Daraja la 91XX

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unatekelezwa kupitia Shirika la Reli Tanzania (TRC) katika karakana ya Pugu. Lengo la mradi huu ni kuunda vichwa nane vya treni ya MGR vya 9104 hadi 9111 vyenye uwezo wa kuvuta mabehewa 20 toka Dar Es Salaam hadi Morogoro na mabehewa 27 toka Morogoro na kuendelea.

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unagharimu jumla ya **Dola za Marekani 25,405,456.00** na ulianza kutekelezwa tarehe 24 Oktoba, 2022. Uundaji wa vichwa hivyo ulianza kutekelezwa na Kampuni ya SMH Rail ya Malaysia. Kamati ilifanya ukaguzi wa mradi huu tarehe 14 Machi, 2026 ambapo utekelezaji wa mradi ulikuwa umefikia **asilimia 88**.

**Mheshimiwa Spika,** kufikia Machi, 2026, vichwa vinne vilikuwa vimekamilika wakati ambapo vichwa 2 vimeanza kazi na vichwa vingine 2 vinafanyiwa majaribio kabla ya kupakwa rangi. Mradi huu pia umeleta manufaa ya ziada kwa kuwezesha watalaamu 34 nchini kujifunza uundaji wa vichwa vya treni, ujuzi ambao haukuwepo nchini hapo awali.

(ix) Miradi ya Kuimarisha Huduma za Hali ya Hewa Nchini

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata nafasi ya kutembelea miradi ya kuimarisha huduma za hali ya hewa nchini tarehe 16 Machi, 2026. Miradi hiyo inatekelezwa chini ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi hiyo kama ifuatavyo:-

(i) Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Kanda ya Mashariki pamoja na Kituo cha Tahadhari ya Matukio ya Tsunami

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusisha ujenzi wa jengo la ghorofa tano pamoja na majengo madogo ya huduma mbalimbali ikiwemo na ujenzi wa uzio. Lengo la mradi huu ni kuimarisha huduma za hali ya hewa katika ukanda wa mashariki mwa nchi pamoja na kuongeza uwezo wa Taifa katika kutoa tahadhari za mapema dhidi ya matukio ya Tsunami na majanga yanayohusiana na bahari.

**Mheshimiwa Spika,** gharama ya mradi kwa mujibu wa mkataba ni **Shilingi 9,909,693,868.85** na ujenzi wake ulitarajiwa kukamilika ndani ya miezi 18 kuanzia tarehe 24 Januari, 2023 hadi tarehe 24 Julai, 2024. Hata hivyo, muda wa utekelezaji wa mradi uliongezwa hadi kufikia tarehe 30 Mei, 2026.

**Mheshimiwa Spika,** hadi Kamati inafanya ukaguzi katika mradi huo, utekelezaji wake ulikuwa umefikia **asilimia 65** tu. Aidha, Serikali imemlipa mkandarasi jumla ya **Shilingi 2,930,732,569.51** sawa na **asilimia 29.6** tu ya gharama ya mradi.

(ii) Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Urekebishaji wa Vifaa vya Hali ya Hewa

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unahusisha ujenzi wa jengo la ghorofa moja (G+1) ambapo kutakuwa na ofisi, vyumba maalumu vya upimaji vifaa vya hali ya hewa pamoja na vyumba vya mafunzo. Lengo la mradi huu ni kuwa na kituo cha kisasa cha

kurekebisha vifaa vya hali ya hewa kwa ajli kupata majibu sahihi ya vipimo vya hali ya hewa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** gharama ya mradi huu ni **Shilingi 3,646,357,636.20** na ulitarajiwa kukamilika ndani ya miezi 9 kutokea tarehe 09 Julai, 2024. Hata hivyo, muda wa utekelezaji wa mradi huo uliongezwa hadi tarehe 18 Aprili, 2026.

**Mheshimiwa Spika,** hadi Kamati inafanya ukaguzi wa mradi huo, utekelezaji wake ulikuwa umefikia **asilimia 40** tu. Aidha, Serikali ilikuwa imemlipa mkandarasi jumla ya **Shilingi 793,094,252.36** sawa na **asilimia 21.7** tu ya gharama ya mradi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Kamati haikuridhishwa na kasi ya miradi inayotekelezwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini. Vilevile, Serikali imefanya malipo yasiyoridhisha kwa wakandarasi wa miradi hii kulinganisha na kazi iliyofanywa. Kamati ina maoni kuwa, kama Serikali haitachukua hatua za haraka katika usimamizi wa miradi hiyo, ni wazi kuwa haitakamilika kwa wakati hivyo kuathiri tija ya miradi hiyo katika kutoa huduma bora za hali ya hewa nchini.

### 2.5 Masuala Mahsusi Yaliyobainika Katika Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026

a) Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA)

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilifanya uwekezaji mkubwa katika kuboresha miundombinu ya Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara katika kati ya mwaka 2021 hadi 2023. Vilevile, Serikali ilifanya uamuzi wa kupangisha baadhi ya Gati (1-7) ya Bandari ya Dar Es Salaam kwa Kampuni ya DP World ya Dubai kwa mkataba wa kibiashara. Aidha, katika Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/2025, Serikali ilifanya uamuzi wa kuruhusu mapato yanayotokana na matumizi ya Gati (Wharfage) kukusanywa na TPA tofauti na ilivyokuwa awali.

**Mheshimiwa Spika,** hatua hizo zimechangia kuongeza ufanisi na tija katika matumizi ya Bandari nchini na kuzifanya kuwa

Bandari kivutio katika Ukanda wetu. Mathalani, katika Bandari ya Dar Es Salaam, shehena ya makasha iliyohudumiwa ndani ya miezi 9 ya mwaka 2025/2026 imefikia zaidi ya **Milioni 1.13** kutoka makasha 725,436 katika mwaka wa fedha 2020/2021. Kwa upande wa Bandari ya Tanga hadi Machi, 2026, imehudumia shehena ya tani **Milioni 1.6** wakati katika miezi 12 ya mwaka wa fedha 2024/2025 Bandari hiyo ilihudumia tani **Milioni 1.33**. Vilevile, Bandari ya Mtwara katika eneo la Kisiwa-Mgao itaanza kuhudumia Shehena Chafu ili kutunza mazingira ya Bandari iliyopo Mtwara Mjini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inampongeza sana mbeba maono wa Taifa hili Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassani, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ujasiri na na hatua hizi ambazo zimeiwezesha tija na mafanikio haya ndani ya muda mfupi kwenye sekta ya Bandari. Aidha, Kamati inampongeza Mhe. Prof Makame Mbarawa, Mb, Waziri wa Uchukuzi pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa TPA Ndg. Plasduce M. Mbosa kwa namna wanavyosimamia sekta ndogo ya Bandari nchini.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, ufanisi na tija hiyo umeleta changamoto ambayo ni msongamano wa shehena ya makasha katika Bandari. Hali hii inatokana na ukweli kuwa miundombinu iliyopo Bandarini kwa sasa haitoshi kuhudumia ongezeko hili. Kwa sasa Bandari zinahudumia shehena ya tani Milioni 32.80 na inakadiriwa kufika mwaka 2030 itakuwa inahudumia shehena ya tani Milioni 62.

**Mheshimiwa Spika,** ili kukabiliana na changamoto hiyo, tarehe 8 Machi, 2026, TPA ilitangaza matumizi ya ada mpya kwa wadau na watumiaji wa Bandari za Baharini. Lengo la ada mpya ni kuanzisha Tozo ya Uendelezaji wa Miundombinu ya Bandari (*Port Infrastructure Development Levy)*.

**Mheshimiwa Spika,** uendezaji huo wa miundombinu ya Bandari utahusu mambo yafuatavyo:-

- Ujenzi wa Gati mpya nne (4) za namba 12 hadi 15 katika Bandari ya Dar Es Salaam;

➢ Ujenzi wa Gati Mbili (2) zenye Urefu wa Mita 500 katika Bandari ya Dar Es Salaam;

➢ Ujenzi wa Mantanki ya Kupokelea mafuta katika Bandari ya Dar Es Salaam;

➢ Ujenzi wa Bandari Maalumu ya Kisiwa-Mgao Mkoani Mtwara kwa ajili ya Shehena Chafu;

➢ Ujenzi wa Kituo na Mtandao wa Reli ndani ya Bandari ya Dar Es Salaam;

➢ Ujenzi wa Gati la kupokelea mafuta katika Bandari ya Dar Es Salaam; na

➢ Ujenzi wa Kuhudumia mizigo mchanganyiko pamoja na Gati la Kuhudumia Mafuta katika Bandari ya Tanga.

**Mheshimiwa Spika,** ada hiyo itatozwa kuanzia tarehe 1 Julai, 2026 kwa kiwango **asilimia 4.5** ya Kodi ya Forodha. Awali TPA ilipanga kutoza kiwango cha **asilimia 9** lakini baada ya kukutana na watumiaji wa Bandari chini ya usimamizi wa Wizara, pande zote zilikubaliana kiwango cha **asilimia 4.5** ili kuendeleza miundombinu ya Bandari nchini.

**Mheshimiwa Spika,** ada hiyo itaiwezesha TPA kuwa na uwezo wa kukusanya **Shilingi Trilioni 11.2** kwa ajili uendelezaji wa miundombinu hiyo. Aidha, TPA inategemea kushirikiana na sekta binafsi kwa kuvutia mtaji wa zaidi ya **Shilingi Trilion 4.9** ili kukamilsha kiasi cha **Shilingi Trilioni 16.1** kinachotakiwa katika jukumu hilo.

b) Viwanja vya Ndege vya Kimkakati Nchini

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali ilipanga kuanza ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Serengeti pamoja na kufanya maboresho ya Kiwanja cha Ndege cha Mwanza. Viwanja hivi ni vya kimkakati

nchini kwani vitachochea Utalii kwa kuwa vipo karibu na vivutio vya utalii hususani mbuga ya Serengeti.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa ya Wizara inaonesha kuwa, Kiwanja cha Serengeti kilitengewa **Shilingi Bilioni 1.3** na kile cha Mwanza kilitengewa **Shilingi Bilioni 13.80** kwa ajili ya kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu. Hata hivyo, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Kiwanja cha Serengeti kimetengewa **Shilingi Milioni 100** tu huku kile cha Mwanza kikitengewa **Shilingi Bilioni 6** tu**.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haijaridhika na kiasi cha fedha kilichotengwa na Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hii katika mwaka ujao wa fedha. Kamati inaitaka Serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa viwanja hivi kwa sababu ya manufaa yake ya kiuchumi.

c) Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL)

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imefanya uwekezaji wa **Shilingi Trilioni 2.717** katika kufufua Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL). Fedha hizo zimetumika katika kununua ndege, kukarabati karakana na miundombinu wezeshi pamoja na kulipa malimbikizo ya madeni ya Kampuni.

**Mheshimiwa Spika,** uwekezaji huo umeiwezesha ATCL kuongeza mapato yake kufikia **Shilingi Bilioni 595.7** mwaka 2025 kutoka **Shilingi Bilioni 175** mwaka 2021 kupiti huduma za usafiri wa anga kwa vituo 15 vya ndani ya nchi na vituo 17 nje ya nchi. Hata hivyo, ATCL inajiendesha kwa hasara huku ikitegemea ruzuku ya Serikali katika kulipa wafanyakazi wake mishahara.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto hiyo inachangiwa na uamuzi wa Serikali kuikodishia ndege ATCL kutoka kwa Wakala wa Ndege Tanzania (TGFA). ATCL hulazimika kulipia kila mwezi huduma ya kukodisha pamoja na fedha za matengenezo ya ndege kwa TGFA hali inayoifanya ATCL kuwa na gharaama kubwa ya uendeshaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati mara kadhaa imekuwa ikitoa maoni kwa Serikali kufanya uamuzi wa kuzifanya ndege hizo kuwa chini ya ATCL. Mathalani, katika Taarifa ya Shughuli za Kamati ya Mwaka 2024, iliyosomwa Bungeuni mwezi Februari, 2025, Kamati ilipendekeza na Bunge kuridhia azimio la kuitaka Serikali kurejesha ndege chini ya umiliki wa ATCL. Vilevile, tangu mwaka 2021, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ametoa pendekezo hilo lakini hadi sasa Serikali imekuwa na kigugumizi cha kutekeleza jambo hilo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inataka kujua, ni kwanini hadi sasa Serikali imeshindwa kutekeleza azimio hilo la Bunge. Vilevile, ndege hizo zikiwa mali ya ATCL mtaji katika mizania ya vitabu vya hesabu za ATCL itaongezeka na kuondokana na hasara ya kila mwaka kama inavyoripotiwa na CAG.

d) Miundombinu ya Huduma ya Reli Nchini

**Mheshimiwa Spika**, huduma ya usafiri wa Reli nchini inatolewa na TRC na TAZARA. Huduma hii inakabiliwa na changamoto ya uchakavu wa miundombinu ya reli, mabehewa na vichwa vya treni. Uwekezaji katika miundombinu hii unahitaji fedha nyingi ambazo kuendelea kutegemea mpango wa bajeti itachukua muda mrefu kuiboresha.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imechukua hatua mbalimbali kwa ajili ya kuendelea kuboresha huduma hiyo muhimu kwa ukuaji wa uchumi wa nchi. Mathalani, tarehe 28 Aprili, 2026, Serikali ilisaini mkataba wa **Dola za Marekani Bilioni 2.33** kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Reli ya SGR vipande vya Makutopora - Tabora, na Tabora - Isaka vyenye jumla ya Kilomita 533.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa TAZARA, Serikali imekamilisha hatua za kuingia Mkataba wa Ufufuaji na Uboreshaji wa Reli ya TAZARA. Mkataba huo ulisainiwa tarehe 29 Septemba 2025 kati ya Serikali za Tanzania na Zambia, kwa kushirikiana na Kampuni ya CCECC ya China. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuanza Juni, 2026 na utaongeza ufanisi katika usafirishaji wa reli na Bandari ya Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hizo za kuendelea kuboresha miundombinu ya huduma za reli nchini. Hata hivyo, mtandao wa reli katika kanda ya Kaskazini bado unakabiliwa na changamoto ya uchakavu na kusababisha kushuka kwa ufanisi katika matumizi ya reli hiyo. Aidha, Reli za Tanga hadi Musoma na ile ya Mbamba Bay hadi Mtwara bado hazijapata fedha pamoja na kuwa Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu kuhusu reli hizo.

e) Miundombinu ya Usafiri wa Majini

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Uchukuzi inahusika na usimamizi wa miundombinu ya Usafiri katika Bahari na Maziwa ikiwa ni pamoja na meli na Bandari zake kupitia taasisi za TPA, TASHICO na TASAC kama mdhibiti wa usafiri majini. Huduma ya Usafiri Majini inakabiliwa na changamoto ya upungufu wa meli katika maziwa makuu, uchakavu wa bandari za maziwa Pamoja na ajali ambazo wakati mwingine zinagharimu uhai wa watu.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kufanya uwekezaji mkubwa kwa kukamilisha ukarabati wa Meli ya MT Sangara na kuendelea na Ukarabati wa MV Liemba ambayo imefikia **asilimia 54.** Meli hiyo inatajiwa kukamilika na kuanza kazi Julai, 2026. Aidha, Serikali imekamilisha ujenzi wa Meli mbili za Mizigo ambazo zinaweza kubeba Tani 2000 kila mmoja.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali pia imeendelea kuchukua hatua za kuimarisha usalama wa usafiri na usafirishaji majini, ambapo kituo cha Uokozi (Search and rescue Centre) kimejengwa katika Ziwa Victoria. Vilevile, TASAC imekuwa ikishirikiana na taasisi zingine katika kufanya doria za usalama na ukaguzi wa vyombo vya majini.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo, bado baadhi ya miundombinu ya Bandari na Meli hasa katika maziwa makuu hauridhishi. Mathalani, Bandari ya Musoma katika Ziwa Victoria haifanyi kazi kwa muda mrefu. Aidha, katika mipango yake, Serikali haijaonesha mkakati madhubuti wa kuifufua Bandari

hiyo ambayo ni moja ya kitovu cha shughuli za kiuchumi katika eneo la Ziwa Victoria.

f) Usimamizi wa Huduma ya Usafiri wa Ardhini

**Mheshimiwa Spika**, usafiri wa ardhini ndio unaotumiwa na watu wengi hapa nchini kwa ajili kusafirisha watu na bidhaa katika masoko mbalimbali. Kwa hiyo, usimamizi madhubuti unaolinda watoa huduma na watumiaji katika gharama na usalama ni jukumu la msingi la Serikali kwa ajili ya ustawi wa wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, katika nchi yetu jukumu hili linatekelezwa chini ya Wizara ya Uchukuzi kupitia LATRA. Katika mwaka wa fedha 2025/2026, LATRA imetekeleza majukumu yake ya kisheria kwa kuhakikisha inafunga vidhibiti mwendo (VTS) kwenye magari ya abiria ili kuzuia mwendo kasi ambao umekuwa chanzo cha ajali nyingi nchini. Kamati ilipata nafasi ya kutembelea na kuona namna vidhibiti mwendo hivyo vinavyofanya kazi. Kamati inaipongeza Serikali na LATRA kwa namna inavyoendelea na udhibiti wa usafiri wa ardhini ikiwa ni pamoja na matumizi ya magari, pikipiki na reli.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio haya na LATRA inakabiliwa na changamoto muundo kiundeshaji kwani kumekuwa na mgongano wa Kisheria katika utekelezaji wa majukumu yake na yale ya jeshi la Polisi kitengo cha Usalama barabarani. Kamati imebaini kuwa, kwa upande wa Zanzibar majukumu yote ya Usalama Barabarani yapo chini taasisi ya Zanzibara Road Safety Authority (ZARTSA) ambayo imefanikiwa sana katika kudhibiti ajali za barabarani kwa magari binafsi, biashara, Serikali na hata pikipiki na bajaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kuwa sasa umefika wakati kwa Sheria ya LATRA na ile ya Jeshi la Polisi kuangaliwa upya ili kuweza kuondoa mkanganyiko huu. Hali hii itaondoa malalamiko miongoni mwa wananchi na kuongeza uwajibikaji wa moja kwa moja wa Mamlaka ya udhibiti.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

### 3.1 Mpango na Vipaumbele vya Wizara

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Fungu **62- Wizara ya Uchukuzi** itatekeleza vipaumbele na majukumu yake kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa, 2050, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2025-2030 pamoja na Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa (FYDPIV) wa mwaka 2026/2027-2030/2031.

**Mheshimiwa Spika**, bajeti inayoombwa na Wizara ina lengo la kutekeleza vipaumbele mbalimbali vya Wizara ikiwemo vifuatavyo: -

a) Kuendelea na Miradi ya Ujenzi, Ukarabati na Matengenezo ya Miundombinu ya Reli [SGR, MGR na CGR] Nchini;

b) Kuendelea na Miradi ya Ujenzi, Ukarabati na Matengenezo ya Miundombinu ya Bandari na Meli za Usafirishaji wa abiria na bidhaa katika Bahari ya Hindi pamoja na zile za Maziwa Makuu;

c) Kuendelea na Ujenzi, ukarabati na uboreshaji wa viwanja vya ndege nchini pamoja na ununuzi na matengenezo ya ndege ili kuimarisha huduma za usafiri wa anga nchini;

d) Kuendelea kusimamia shughuli za udhibiti wa huduma za uchukuzi nchini kwa kushirikiana na wadau;

e) Kuendelea kuimarisha miundombinu na huduma za hali ya hewa nchini;

f) Kuendelea kuimarisha Taasisi za mafunzo ya sekta ya uchukuzi kwa miundombinu na vifaa;

g) Kuimarisha usalama, ulinzi na matumizi ya teknolojia katika sekta ya uchukuzi ili kuongeza ufanisi wa uendeshaji;

h) Kuimarisha ushiriki wa Sekta Binafsi na Ufuatiliaji na Tathmini (M&E) ili kuongeza uwajibikaji na thamani ya fedha katika utekelezaji wa miradi ya Uchukuzi; na

i) Kuongeza tija katika utendaji wa sekta kwa kuendeleza Rasilimali watu.

### 3.2 Makadirio ya Mapato

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara na taasisi zake inalenga kukusanya jumla ya **Shilingi 4,061,615,733,000/=** sawa na ongezeko la **asilimia 19.48** ukilinganisha na malengo ya kukusanya **Shilingi 3,399,148,152,880/=** katika mwaka wa fedha 2025/2026. Mapato hayo yatakusanywa kupitia ada na tozo mbalimbali kwa ajili ya huduma zinazotolewa kupitia sekta ya uchukuzi nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapongeza Wizara na taasisi zake kwa kuongeza lengo la makusanyo ya maduhuli ya Serikali. Aidha, Wizara iweke mikakati madhubuti ya usimamizi na ufuatiliaji wa taasisi zilizo chini yake ili ziongeze ufanisi katika kukusanya madhuli ya Serikali na kufikia lengo hilo.

### 3.3 Makadirio ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2026/2027, **Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi** inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,872,738,082,000/=** sawa na ongezeko la **asilimia 4.60** ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026. **Kielelezo Na. 3** kinaonesha ulinganisho wa makadirio ya matumizi kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 na bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027.

**Kielelezo Na. 3: Ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi kwa Bajeti ya Mwaka 2025/2026 na 2026/2027**

| FUNGU 62-WIZARA YA UCHUKUZI | MWAKA WA FEDHA 2025/2026 (SHILINGI) | MWAKA WA FEDHA 2026/2027 (SHILINGI) | TOFAUTI ASILIMIA (%) |
|---|---|---|---|
| *Matumizi ya Kawaida* | *125,438,950,000.00* | *126,041,236,000.00* | *0.48* |
| *Bajeti ya Maendeleo* | *2,621,046,068,000.00* | *2,746,696,846,000.00* | *4.8* |
| **JUMLA KUU** | ***2,746,485,018,000.00*** | ***2,564,441,414,000.00*** | ***4.60*** |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwani ongezeko hilo litaiwezesha Wizara kutekeleza majukumu na vipaumbele vyake kwa ufanisi. Serikali ihakikishe inatoa fedha kwa wakati ili kupata tija katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

### 3.3.1 Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara ya Uchukuzi inaomba kuidhinishiwa **Shilingi 126,041,236,000/=** kwa ajili ya matumizi ya Kawaida**.** Fedha hizo zinajumuisha Mishahara ya Watumishi (P.E) **Shilingi 100,135,087,000 /=** na Matumizi Mengineyo (O.C) **Shilingi 25,906,149,000/=** kama ambavyo **Kielelezo Na. 4** kinaonesha.

**Kielelezo Na. 4: Ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Bajeti ya Mwaka 2025/2026 na 2026/2027**

| FUNGU 62-WIZARA YA UCHUKUZI | MWAKA WA FEDHA 2025/2026 (SHILINGI) | MWAKA WA FEDHA 2026/2027 (SHILINGI) | TOFAUTI ASILIMIA (%) |
|---|---|---|---|
| Mishahara (P.E) | 96,654,340,000.00 | 100,135,087,000.00 | +3.60 |
| Matumizi Mengineyo (O.C) | 28,784,610,000.00 | 25,906,149,000.00 | -10.00 |
| **JUMLA KUU** | ***125,438,950,000.00*** | ***126,041,236,000.00*** | ***0.48*** |

**Mheshimiwa Spika**, Kufuatia kielelezo Na. 4 hapo juu, fedha za Mishahara ya Watumishi (P.E) katika mwaka wa fedha 2026/2027 zimeongezeka ukilinganisha na mwaka wa fedha 2025/2026. Ongezeko hili limechangiwa na Serikali kutenga bajeti kwa ajili ya kulipa malimbikizo ya mishahara kwa wafanyakazi wa reli ya TAZARA.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa fedha za matumizi mengineyo (O.C) kiwango hicho kimeshuka kwa **asilimia 10** katika mwaka wa fedha 2026/2027 kulinganisha na mwaka 2025/2026. Hii imetokana na uamuzi wa Serikali kupunguza matumizi yasiyo yalazima na kupeleka fedha kwenye shughuli zenye tija zaidi katika kuhudumia wananchi.

**3.3.2 Bajeti ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,746,696,846,000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Fedha inayoombwa ni sawa na ongezeko la **asilimia 4.80** ukilinganisha na bajeti ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 5**.

**Kielelezo Na. 5: Ulinganisho wa Makadirio ya Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka 2025/206 na 2026/2027**

| Bajeti (Matumizi) | Mwaka wa Fedha 2025/2026 (Shilingi) | Mwaka wa Fedha 2026/2027 (Shilingi) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|
| Ndani | 2,452,512,444,000.00 | 2,452,512,444,000.00 | 0.00 |
| Nje | 168,533,624,000.00 | 294,184,402,000.00 | 74.56 |
| **JUMLA KUU** | **2,621,046,068,000.00** | **2,746,696,846,000.00** | **4.80** |

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake wa bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027 kulinganisha na mwaka wa fedha unaoisha, Kamati imebaini kuwa fedha za nje zimeongezeka kwa **asilimia 74**. Hata hivyo, mwendelezo wa upatikanaji wa fedha

hizo katika mwaka wa fedha 2025/2026 haukuwa wa kuridhisha kwani hadi Februari, 2026, Wizara ilikuwa imepokea **asilimia 19** tu ya bajeti hali inayoweza kuathiri utekelezaji wa miradi inayotegemea fedha za nje.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya uchambuzi wa kina kuhusu Utekelezaji wa Bajeti pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya **Fungu 62- Wizara ya Uchukuzi** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, sasa naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo: -

### 4.1 Maoni ya Jumla

(a) Serikali ihakikishe inatoa fedha za maendeleo kama zilivyoidhinishwa na Bunge na kusimamia kikamilifu miradi ya kimkakati inayotekelezwa na Wizara hii ili kuleta tija iliyokusudiwa.

(b) Serikali iongeze kasi katika kuboresha miundombinu ya sekta ya uchukuzi ili kuongeza mchango wa sekta hiyo katika kukuza uchumi wa kisasa pamoja na kuzalisha ajira kwa vijana nchini;

(c) Serikali iweke mikakati madhubuti na kuzisimamia taasisi zilizo chini ya Wizara hii katika ukusanyaji wa mapato ili ziweze kujitegemea na kuchangia katika mfuko mkuu wa Serikali; na

(d) Serikali iendelee kusimamia na kuweka mazingira ya kuwezesha taasisi za umma na binafsi kutoa huduma bora za usafiri wa abiria na bidhaa nchini.

### 4.2 Maoni Mahsusi

a) Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA)

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) Ianze kutekeleza matumizi ya ada mpya kwawatumiaji wa Bandari nchini kuanzia tarehe 1 Julai ,2026 ili kuhakikisha TPA inapata fedha za kuendeleza miundombinu ya Bandari nchini;

(ii) Ihakikishe inatekeleza kwa kasi maboresho yamiundombinu ya Bandari ili kuhakikisha kuwa kasi ya ufanisi wa Bandari inawiana na maendelezo hayo; na

(iii) Wizara na TPA ziendelee kukutana na wadau nawatumiaji wa Bandari mara kwa mara kwa ajili kutoe elimu kuhusu umuhimu wa ada mpya.

b) Miundombinu ya Viwanja vya Ndege Nchini

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) Ikamilishe Maboresho ya Viwanja vya Ndege vya Kigoma, Musoma na Shinyanga kwa ajili kuhakikisha wananchi wa maeneo hayo wanapata huduma ya usafiri wa ndege; na

(ii) Itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kuanza Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Serengenti pamoja na Maboresho ya Kiwanja cha Ndege cha Mwanza kwani Viwanja hivyo ni vya Kimkakati katika kukuza Utalii na kukuza Uchumi nchini.

c) Huduma ya Usafiri wa Anga Nchini

Kamati inashauri kuwa, Serikali: -

(i) Ihakikishe inarejesha ndege chini ya umiliki wa ATCL kutoka TGFA uamuzi ambao utaifanya ATCL kuanza kujiendesha kwa faida na kutoa gawio kwa Serikali;

(ii) Iharakishe ununuzi wa ndege mpya nne (4) na 1 ya mizigo ili kuongeza ufanisi katika huduma ya Usafiri wa Anga nchini kupitia ATCL;

(iii) Ifanye tathmini kuhusu ATCL kuanzisha safari zandege kutoka Dodoma kwenda Mikoa mingine moja kwa moja bila kupitia Dar Es Salaam ili kukidhi mahitaji ya wananchi wanaohitaji huduma hiyo;

(iv) Ihakikishe ATCL inatoa taarifa kwa abiria kuhusu mabadiliko ya ratiba za ndege ili kuondoa usumbufu kwa abiria; na

(v) Ipitie upya nauli za ndege ili ziweze kuwa na uhalisia na kuondoa malalamiko miongoni mwa abiria wa safari za anga nchini.

d) Huduma ya Usafiri ya Reli Nchini

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) Iongeze kasi katika Ujenzi wa Reli ya Kisasa ya SGR katika vipande Makutopora - Tabora, Tabora-Isaka, Isaka - Mwanza, Tabora - Kigoma, na Uvinza - Msongati vilivyobaki ili reli hiyo iweze kutumika katika kusafirisha abiria na mzigo kama ilivyokusudiwa;

(ii) Ihakikishe inamsimamia mkandarasi Yep Merkeziya Uturuki ili aongeze kasi katika utekelezaji wa miradi hiyo ili kuleta tija iliyokusudiwa kwenye miradi husika;

(iii) Iboreshe huduma ya mawasiliano ya simu ndaniya treni ya SGR ili kuwe na uhakika wa abiria kupata mawasiliano wanapokuwa safarini;

(iv) Iandae utaratibu wa kuanza Ujenzi wa Reli yaMbamba Bay-Mtwara na ile ya Tanga-Musoma kwa njia ya Ubia kati yake na Sekta binafsi (PPP) kwa kuweka motisha (incentives) kwa sekta binafsi ili kuvutia sekta hiyo katika utekelezaji wa miradi hiyo; na

(v) Ihakikishe ukarabati na maboresho ya reli yaTAZARA yanaanza na kukamilika kwa wakati ili kuunganisha

matumizi ya reli hiyo na Bandari ya Dar Es Salaam katika kuendelea kuhudumia sehemu kubwa ya nchi za Kusini mwa Afrika.

e) Huduma ya Usafiri wa Majini Nchini

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) Ihakikishe TASHICO inakamilisha ukarabati wa meli ya MV Liemba ili iweze kuanza safari katika Ziwa Tanganyika kwani eneo hilo lina mvuto mkubwa wa kibiashara;

(ii) Iongeze uwekezaji katika kuendeleza Bandari za Maziwa Makuu ikiwemo Bandari ya Musoma ili kuchochea shughuli za kiuchumi katika maeneo hayo;

(iii) Itenge fedha za kutosha katika ujenzi wa Kiwanda cha Meli katika Ziwa Tanganyika pamoja na ujenzi wa meli mbili za mizigo ili uanze haraka na kukuza sekta ya uchukuzi wa majini nchini; na

(iv) Kuendelea kuwekeza katika usalama wa huduma ya safari za majini pamoja na kujenga vituo vya uokozi katika Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na Bahari ya Hindi ili kukabiliana na ajali za majini.

f) Usimamizi wa Huduma ya Usafiri wa Ardhini

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) Ifanye marekebisho ya Sheria kuhusu muundo wa LATRA ili kuweza kuondoa mkanganyiko wa majukumu kati ya LATRA na Jeshi la Polisi katika suala la udhibiti wa Usalama barabarani nchini;

(ii) LATRA iendelee na ubunifu na matumizi ya teknolojia katika magari ya abiria ili kupunguza ajali ambazo zinasababisha upotevu wa maisha ya watu, kuleta ulemavu na uharibifu wa mali nchini;

(iii) Ihakikishe LATRA inakuwa na kazi ya kulea sektabinafsi katika usafiri wa ardhini hasa vijana wanaoendesha pikipiki maarufu kama bodaboda badala ya kukamata na kufungia vyombo vyao mara kwa mara; na

(iv) Ihakikishe LATRA inatoa elimu kuhusu haki na wajibu katika kwa wadau wa sekta ya usafiri wa ardhini nchini.

g) Vyuo vya Mafunzo Zilizo chini ya Wizara ya Uchukuzi

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) Iweke mpango madhubuti wa kutangaza taaluma zinazotolewa katika vyuo hivyo ili kuvutia udahili wa wanafunzi katika taaluma hizo, kwani imebainika kuwa wazazi na wanafunzi wengi hawana taarifa kuhusu taaluma zinazotolewa katika vyuo hivyo ikiwemo urubani, unahodha na ubaharia; na

(ii) Ihakikishe inakamilisha miradi ya kimkakati kwa ajili ya upanuzi wa kampasi na uboreshaji wa vyuo hivi kwa ajili ya mafunzo endelevu katika sekta ya uchukuzi nchini; na

(iii) Ifanye tathmini na kulipa deni la **Shilingi Milioni 721.7** ambalo Chuo cha DMI kinadaiwa na Kampuni ya E1 Limited kutokana na huduma zilizotolewa kwa chuo na kampuni hiyo katika mwaka wa fedha 2021/2022.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 HITIMISHO

### 5.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee naendelea kukushukuru wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu na kwa maelekezo yako ambayo yamekuwa msaada mkubwa katika uendeshaji bora wa shughuli za kila siku za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Aidha, namshukuru Naibu

Spika, kwa namna anavyokusaidia kutekeleza majukumu yako, pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kukusaidia kuendesha vikao vya Bunge kwa Ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa moyo wa dhati kabisa, niwashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ambao wamekuwa mstari wa mbele katika kuendelea kuisimamia Wizara ya Uchukuzi pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa niaba ya Bunge lako tukufu. Kwa hakika, maoni, ushauri na mapendekezo yao yana mchango mkubwa katika kuboresha utendaji wa Serikali. Naomba niwatambue Wajumbe hao ili majina yao yaingie katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Moshi Selemani Kakoso, Mb. | **Mwenyekiti** |
| 2. | Mhe. Abubakar Damian Asenga, Mb. | **Makamu Mwenyekiti** |
| 3. | Mhe. Kapt. Said Hassan Ali Mwinyi, Mb. | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Condester Michael Sichalwe, Mb. | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Anne Kilango Malecela Mb. | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb. | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Nuru Issa Kashakari, Mb. | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako, Mb. | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Isack Joseph Copriano, Mb. | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Eng. Johnston J. Mutasingwa, Mb. | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Sara Msafiri Ally, Mb. | Mjumbe |
| 12. | Mhe. John Stephano Luhende, Mb. | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Ibrahim Mohamed Shayo, Mb. | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Kellen Rose Rwakatare, Mb. | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Fatma Ally Rembo, Mb. | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Saidi Salim Hamad, Mb. | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Mgore Miraji Kigera, Mb. | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Hija Hassan Hija, Mb. | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Nabil Ahmed Abdallah, Mb. | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Hamis Mwagao Tabasamu, Mb. | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Abdulaziz Mohamed Abdood, Mb. | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Said Ali Mbarouk Mb. | Mjumbe |
| 23. | Mhe. Mariam Said Khamis, Mb. | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kumshukuru Waziri wa Uchukuzi, Mhe. Prof Makame Mnyaa Mbarawa, (Mb) kwa ushirikiano ambao ameipatia Kamati katika kipindi chote cha Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati akisaidiwa na Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mhe. David Mwakiposa Kihenzile (Mb).

Aidha, niwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Uchukuzi pamoja na taasisi zake chini ya uongozi wa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof Godious Walter Kahyalala. Kamati inaendelea kuwatia moyo katika utekelezaji wa majukumu yao kwa kuzingatia weledi ili kuleta tija katika Sekta ya Uchukuzi nchini.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, nawashukuru sana watendaji wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Bw. Baraka I. Leonard kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

**5.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naomba Bunge lako likubali kupokea na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya **Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Moshi Selemani Kakoso, Mb.
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU**
13 Mei, 2026

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Mheshimiwa Moshi Suleiman Kakoso.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza michango yetu naomba tuwatambue wageni walioko Bungeni asubuhi hii.

Tunao wageni wa Mheshimiwa Spika ambao ni Mchungaji Mstaafu Richard Hananja wa Kanisa la KKKT, na Mkurugenzi wa *Hananja Compensation Foundation*, karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine pia ambao wamekaa jukwaa la Mheshimiwa Spika. Hawa ni wageni wa Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa Mbunge na Waziri wetu wa Uchukuzi Ndugu Endaely Mziray Mkurugenzi wa Sheria Bank ya Azania, karibu. *(Makofi)*

Tunaye Profesa Tumain Gurumo, Mkuu wa Chuo cha Bandari Dar es Saalam, Ndugu Erick Hamisi Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Meli Tanzania, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunaye mgeni wa Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile na Naibu Waziri wetu wa Uchukuzi, Ndugu Lucia Pande, Katibu Mkuu wa *Red Cross Tanzania*, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni wengine ambao ni wa Waheshimiwa Wabunge. Kuna wageni wa Mheshimiwa Profesa Mbarawa, wengine ni Maafisa wa Wizara ya Uchukuzi, wawakilishi wa taasisi za fedha, wafadhili kutoka *TradeMark Africa*, Wakuu wa Vyuo vilivyo chini ya Wizara ya Uchukuzi, Washauri wa Wizara ya Uchukuzi, Wadau wa Uchukuzi kutoka Kampuni ya *Bakhresa Limited,* Mwakilishi wa Kampuni ya Usangu *Logistics*, wadau wa uchukuzi kutoka *LATRA*, mwakilishi kutoka *UN World Food Program,* wawakilishi wa makampuni yanayotoa huduma za uchukuzi, wawakilishi wa vyama na mabaraza yanayotoa huduma za uchukuzi, wawakilishi wa manahodha *TASHICO* na *TASAC*, wawakilishi wa viwanja vya ndege kutoka Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania, wawakilishi wa wanafunzi wa Kozi ya Usafiri wa Anga kutoka Chuo cha Taifa cha Usafirishaji *(NIT),* karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wawakilishi wa club ya michezo ya Wizara ya Uchukuzi, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunao wageni wengine wa Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge na Naibu Waziri wetu wa Uchukuzi, ambao ni Watumishi wa *Red Cross Tanzania* na watumishi wa ofisi ya Mbunge, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Hawa ni viongozi 27 wa Umoja wa Vijana wa CCM Tawi la Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* kutoka Jijini Dodoma. Wageni wetu tunawakaribisha sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza sasa na mjadala wa jumla, tutaanza na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao ajiandae.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kuchangia hotuba ya Wizara ya Uchukuzi. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Rais. Mimi nipo Kamati ya Miundombinu, kwa hiyo ninaifahamu vizuri Wizara ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Waziri Mbarawa, ana Wizara ambayo mkiiangalia mnaweza mkaiona ndogo, lakini ni Wizara nzito kwa sababu Wizara hii ndiyo inayohusika na kuhamisha vitu au watu kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ya kuwahamisha hawa watu ni barabara, reli, maji, viwanja vya ndege na kadhalika. Sasa leo ninaomba nizungumizie bandari, hasa ya Dar es Saalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Dar es salaam ndiyo bandari kuu kwenye nchi yetu, na katika Afrika Mashariki Bandari ya Dar es Salaam ni namba mbili kwa ukubwa na ufanisi wa kazi baada ya Bandari ya Mombasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Dar es Salaam pamoja na kazi ambazo inafanya, kwanza inaajiri, inahudumia takribani 95% ya biashara ya Kimataifa. Hiyo ni moja. Pili, Bandari ya Dar es

Salaam inahudumia nchi saba zisizo na bandari. Inahudumia *DRC Congo*, Zambia, inakwenda Burundi, inahudumia Rwanda, Malawi, Uganda na Zimbabwe. Inatoa ajira kwa Watanzania takribani 45,000. Pia bandari hii inachangia shilingi bilioni 800 hadi 900 kwa mwezi. Aidha, huchangia takribani 36% ya mapato yote ya kodi yanayokusanywa na *TRA*. Bandari

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze Serikali kwamba imefanya maboresho makubwa sana katika Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wafugaji ng'ombe, yule ambaye anatoa maziwa, ndiye anayepewa mashudu mara kwa mara. Mchango wa Bandari ya Dar es Saalam kwa nchi yetu ni mkubwa, na mimi sikushangaa Serikali ilitoa fedha za Kimarekani dola milioni 421 kutoka kwenye mkopo wa Benki ya Dunia na kuingia kwenye mamlaka yenyewe kwa ajili ya kuiboresha Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Watanzania wakajua kwamba sasa tuna bandari yenye hadhi kubwa. Kwanza ninampongeza Waziri, ninaipongeza hotuba yake, na ninaiunga mkono moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwenye maboresho ya kina cha maji. Kabla ya maboresho ya kina cha maji, wastani ulikuwa mita nane mpaka 12, lakini kina cha maji sasa hivi ni meta 14.5, hilo ni la kwanza. Pili, kina cha maji katika mlango wa kuingilia meli meta 12 ni kabla ya maboresho, sasa hivi ni meta 15.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa watu ambao wanaelewa haya mambo, haya ni maboresho makubwa sana. Upana wa mlango wa kuingia meli ulikuwa meta 140 kabla ya maboresho, sasa hivi umeongezwa hadi meta 170. Eneo la kugeuzia meli kabla ya maboresho kipenyo kilikuwa meta 400, lakini sasa hivi eneo limepanuliwa hadi kufikia meta 520.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo wa ukubwa wa meli zinazoweza kupokelewa, meli zenye urefu hadi meta 240 ilikuwa ni

kabla ya maboresho, lakini baada ya maboresho sasa hivi, meli zenye urefu hadi meta 305 na uwezo wa kubeba makasha hadi 8,000. Haya ni maboresho makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya gati, gati 12 zenye kina cha wastani wa meta nane mpaka 12 ilikuwa ni kabla ya maboresho, lakini baada ya maboresho makubwa yaliyofanywa, gati 13 zenye kina cha meta 14.5 zina uwezo wa kuhudumia meli kubwa aina ya *post panamax*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gati la magari roro halikuwepo kabla ya maboresho, sasa hivi limejengwa gati maalumu lenye uwezo wa kuhudumia hadi magari 6,000 kwa wakati mmoja na magari 280,000 kwa mwaka. Gati la kuhudumia makasha, kabla ya maboresho tulikuwa na gati nne tu, gati saba baada ya maboresho na kuongezwa kwa gati namba tano mpaka saba. Maboresho haya ni makubwa sana. Yapo mengi, lakini yote sitaweza kuyazungumza hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe shukrani za dhati kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Nitoe shukrani za dhati kwa Rais Samia kwa kufanya maboresho haya. Mengi ameyaongea Mheshimiwa Waziri, na mengi sisi kama Kamati ya Miundombinu tumeyazungumza kupitia kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, haya maboresho yawe ni ya kudumu. Serikali iendelee kufanya maboresho makubwa kwa Bandari ya Dar es Salaam na nyingine, lakini kwa leo ninapenda kuongelea Bandari ya Dar es Salaam. Baada ya shukrani nitoe maombi, isiwe ni Serikali tu ambayo inatoa maboresho, niziombe na sekta binafsi nazo zisaidie kuleta maboresho kwenye Bandari ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta binafsi zina uwezo mkubwa sana na sasa nina uhakika Serikali imezungumza kwamba inakaribisha sana sekta binafsi na mimi kama mjumbe kutoka Kamati ya Miundombinu, ninaomba sekta binafsi nazo zisaidiane

na Serikali ili tuweze kuleta maboresho makubwa kwa Bandari yetu ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Anne Kilango Malecela. Nilimtaja Mheshimiwa Rashid Shangazi, atafuatiwa na Mheshimiwa Tabasam Hamis, na Mheshimiwa Joseph Musukuma ajiandae.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi hii. Naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa uwekezaji mkubwa sana ambao ameuweka kwenye sekta hii ya uchukuzi na kwa kweli tunaona tija kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimpongeze sana Waziri Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, Naibu Waziri na Katibu Mkuu Profesa Kahyarara pamoja na wakuu wa taasisi zote zilizopo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafarijika tunaposimama mbele ya Bunge lako Tukufu tunapoanza kusema mafanikio ambayo Bunge hili limeyasimamia katika miaka ya hivi karibuni. Eneo la kwanza ni hili la uboreshaji wa miundombinu ya Bandari ya Dar es Salaam, lakini kupitia uwekezaji mkubwa wa Kampuni ya *DP Word* ambayo imekuja kuongeza ufanisi kwa kiasi kikubwa sana katika Bandari ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo la kujivunia sana na tunafarijika kuona kwamba kazi ya mikono yetu imeanza kuleta matunda. Sasa hivi uwezo wa Bandari ya Dar es Salaam ni takribani makasha 105,000 yanatolewa kwa mwezi, kiasi kwamba sasa imefikia hatua miundombinu imeanza kuzidiwa. *ICD* zinazidiwa lakini pia usafirishaji, reli bado haijawa tayari *SGR, MGR* pia *connection* hazipo vizuri. Sambamba na *TAZARA* tunataka wafanye kazi kwa haraka, ili kuondoa shehena kwa wepesi kutoka katika Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kwenye sekta hii ya usafirishaji, kuna eneo ambalo leo ndiyo ningependa mchango wangu uelekee hapo. Malori yanayosafirisha mizigo kutoka Bandari ya Dar es Salaam na kwenda nchi jirani hasa korido ya katikati kutoka Dar es Salaam kwenda Tunduma, barabara hii na yenyewe imekuwa nyembamba sana. Ni muhimu sana ikajengwa angalau maeneo mengi yakawa yanapita magari manne kwa wakati mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetaka nichague sekta hii kwa sababu ina mchango mkubwa sana kwenye kutoa mzigo ama shehena bandarini, pia katika usafirishaji kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo ambalo ninataka nichangie kwa upekee ni madereva wa malori na madereva wote kwa ujumla. Eneo hili hatujafanya vizuri, na mimi binafsi ni Mwana-CCM na ndani ya Chama chetu tunaamini kwamba chama hiki ni cha wakulima na wafanyakazi, lakini sijajua kwamba madereva tumewaweka katika kundi gani? Maana yake ukienda kwa wakulima, huwaoni, ukienda kwa wafanyakazi wanapigwa dana dana. Kwa hiyo, ningetamani sana kuleta mchango katika eneo la usafirishaji. Ni vizuri tukalitazama eneo hili vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, madereva wengi hawana mikataba, wanafanya kazi kwenye kampuni na kwa bahati mbaya sana kampuni nyingi ni za ndani na za nje, lakini hawapewi mikataba. Wanasafirisha mizigo ya thamani kubwa kutoka kwenye bandari yetu kwenda maeneo mengine, lakini madereva hawa stahiki zao za msingi hawazipati. Hata kodi ambazo tungepaswa kuzipata kama *Pay As You Earn* hatuwezi kuzipata kwa sababu hatujawaweka katika mfumo rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na maoni ya Kamati kwamba tuangalie namna *LATRA* na Wizara ya Mambo ya Ndani kwa sababu hapa ndiyo tunaweza tukapata mwafaka wa hili jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza ziko semina mbalimbali, madereva hawa kila wakati wanatakiwa

wakaongeze masomo. Sasa hivi dereva ili aweze kuendesha lori kubwa kwa Daraja *E* na Daraja *C* ni lazima alipe shilingi 300,000 kwenye mafunzo. Sasa pata picha mtu huyu ambaye hana mkataba wa ajira, maana yake hana mshahara, anatakiwa akae darasani kwa siku 14 halafu analipa shilingi 300,000. Hii fedha ataitoa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona katika kada nyingine zote za taaaluma kwenye vyuo na kadhalika, watu wanapata mikopo, lakini hawa madereva ni kada ya chini ambayo haipo katika fursa za kupata mikopo, lakini bado inanyonywa kwa kutoa shilingi 300,000 kwa ajili ya mafunzo ili aweze ku-*renew* leseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda *VETA* ambapo wameanzisha madarasa pale Buza, wana-*charge* shilingi 350,000; *NIT* shilingi 550,000; na Kilwa *Road* Polisi shilingi 310,000. Katika madereva hawa, wapo madereva wa daladala, wapo madereva wa magari ya shule, wanapaswa kulipa hiyo fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba sana, ukisoma taarifa ya Waziri, unaona kwamba hadi Machi, *LATRA* wametoa leseni zaidi ya 388,715 za vyombo vya moto. Maana yake nini? Maana yake kila chombo kimoja kina mtu anakiendesha, na kwa Bahati, kwenye sekta ya udereva wakati mwingine mabasi yanakuwa na madereva wawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake, hii sekta inawezekana ina watumishi wasiopungua 500,000 mpaka 600,000 lakini hawajawekwa katika mfumo rasmi wa kusimamia masilahi yao, na wao pia kutoa mchango kwa Taifa. Kwa hiyo, ni muhimu sana eneo hili tulitazame hasa tukilioanisha na suala zima la kuongeza ufanisi katika eneo la usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani, na Wizara hii ya Uchukuzi zikae kwa pamoja, tuondoe hivi vikwazo ambavyo vinawasababishia Watanzania hawa ambao na wenyewe wana mchango mkubwa sana katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiwachukulie poa. Tujiulize kwamba labda asubuhi unaamka dereva wako hayupo, inakuwaje? Tuangalie katika maeneo ya utoaji wa huduma, daladala zinabeba wanafunzi kupeleka shuleni, zinabeba walimu, zinabeba watumishi wa afya, zinabeba kila aina ya mtumishi ili aweze kufika kwenye eneo lake la kazi. Kwa hiyo, eneo hili ni muhimu sana, tulitazame kwa kina ili liongeze tija katika eneo zima la uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Rashid Shangazi. Nilimtaja Mheshimiwa Tabasam Hamis, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Musukuma, na Mheshimiwa Abubakari Asenga ajiandae.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *mic* yangu kidogo imegoma, naomba nitumie *mic* ya upande wa pili. Ninaona huku inasomeka.

**MWENYEKITI:** Haina shida, tumia tu.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na mimi nichangie bajeti hii ya Wizara ya Uchukuzi. Pamoja na mambo makubwa sana, sekta hii ya uchukuzi, Rais wetu, Mama yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuja kwa moyo wa dhati kabisa kuirekebisha sekta hii. Tutake tusitake, tukubali kwamba maboresho yamefanywa katika Bandari ya Dar es Salaam, Bandari ya Mtwara, na Bandari ya Tanga. Mimi ni sehemu ya Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu, tumetembea maeneo yote hayo tumeyaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninazungumzia habari ya bandari, hawakunielewa watu wengi kwamba tulikuwa tuna hali mbaya na tulikuwa tuko nyumba sana katika bandari. Ukiangalia bandari ambazo ni shindani Durban, Beira, Mombasa na wenzetu sasa hivi wanajenga bandari nyingine ya *Lamu* ya kisasa kabisa, sisi bandari zetu zilikuwa zinapwaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo katika maboresho haya yaliyofanywa ya bandari, na usimamizi mzuri sana uliofanywa na Waziri, Mheshimiwa Profesa Mbarawa pamoja na msaidizi wake, pamoja na hawa *DG* waliopo kule, Wakurugenzi wa hizi bandari na mameneja wao, wanafanya kazi usiku na mchana kwa hali iliyopo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuwa sisi Watanzania, watu wa kukosa shukrani, leo hii mizigo inayoshuka Bandari ya Dar es Salaam, Bandari ya Mtwara na Bandari ya Tanga, bandari zinaonekana kuelemewa kwa sababu ya kuwa na maeneo madogo. Kwa nini tunaelemewa? Ni kwamba sasa barabara za kuingia na kutoka katika miji yetu ya Tanga, Dar es Salaam hata Mtwara sasa hivi, zimekuwa *busy* hakuna mfano wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba pamoja na maboresho haya yanayofanyika, tunaomba sana sekta nyingine ya watu wetu wa ujenzi sasa wafanye haraka kuboresha na kufungua milango ya bandari ya kuingia na kutoka, ili hizi bandari ziweze kufanya kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati, nianze na bandari ya Tanga. Bandari ya Tanga inayo magati matatu na yanafanyiwa maboresho, lakini ukiangalia mshindani wake ambaye ni Bandari ya Mombasa, yuko kilometa kama 140 tu kutoka Bandari ya Tanga, na ana magati 24, anapokea mzigo wa zaidi ya tani 45,000 kwenda tani 50,000 na mizigo mingine inatoka huko huko kwake Mombasa inapita hapo hapo pembeni ya Bandari ya Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kama vile kutukanwa kwa wananchi wa Tanzania. Sasa tunachomwomba Mheshimiwa Profesa Mbarawa katika jambo hili, tunajua anafanya maboresho ya kutanua ile Bandari ya Tanga. Tunaomba sana Bandari ya Tanga badala ya kufikiria maboresho ya magati mawili, tunahitaji magati 20. Bandari ya Tanga inapokea mzigo wa *loose cargo*. Leo ukifika Bandari ya Tanga nafasi ya kutembea mtu haipo, pamejaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, njia ya kutokea Tanga kwenda mpaka Segera, kutoka Segera kuja moja kwa moja mpaka Chalinze na kwenyewe kumekuwa kuna foleni kubwa ya magari msururu hakuna mfano. Wakaeni wasomeke kati ya Waziri wa Uchukuzi na Waziri wa Ujenzi, waliopewa nafasi hii kurekebisha hili jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hali hiyo, Bandari ya Dar es Salaam hali ni hiyo hiyo. Tumezungumzia habari ya Bandari kavu ya Kwala. Tunashukuru sasa hivi *SGR* tumezungumza na Mkurugenzi Machibya wa *TRC,* sasa hivi wanapeleka treni inaanza kazi. Imeshaanza kazi kwa ajili ya kutoa mabehewa pale kuyapeleka Kwala. Jamani Watanzania, hii ni hatua kubwa hatuna mfano wake, lazima tupongeze vitu vinavyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na hali hiyo na maboresho, tunaomba wenzetu wa *SGR* sasa wafanye kazi usiku na mchana kwa ajili ya kupunguza mzigo. Tunachoomba, makasha yote sasa, badala ya kuwa yapo Dar es Salaam, yashushwe Kwala, yasombwe kwa *SGR* kupelekwa pale, kwa sababu hali ya bandari kama tunavyoiona, imejaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Mtwara inafanya zaidi kazi ya kupakia makaa ya mawe na kushusha na kupakia korosho na bidhaa nyingine. Tunachozungumza ni kwamba tunakushukuru sana kwa kuboresha Bandari ya Mtwara, na sisi tunaunga mkono kama Kamati kwa hayo yote tuliyoyaelekeza yanakwenda kufanyiwa kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la viwanja vya ndege. Uboreshaji wa viwanja vya ndege, tumeona hapo Waziri amezungumzia. Tumezungumza mpaka ndani ya Kamati ya kwamba, pamoja kuweka upembuzi yakinifu kwa ajili ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Serengeti, huwezi ukaweka fedha nyingi kule Serengeti wakati Uwanja wa Ndege wa Mwanza uko pale unauwekea shilingi bilioni sita, halikubaliki hili.

**MHE. MARY D. SURATI:** Taarifa, Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Taarifa wapi?

**TAARIFA**

**MHE. MARY D. SURATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaomba kumpatia taarifa mchangiaji kwamba uwanja wa ndege unaotarajiwa kujengwa Serengeti; Serengeti ndiyo mbuga inayochangia 25% ya fedha za kigeni. Sambamba na hivyo, zaidi ya 52% ya mapato yote ya Wizara ya Maliasili na Utalii yanachangiwa na Hifadhi ya Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia maono makubwa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ametegemea kama Taifa tufikie watalii 8,000,000 kufikia 2030, uwanja huu ni mkakati muhimu kwa sababu unakwenda kurahisisha suala la utalii na kuhakikisha Tanzania kama nchi, tunaongoza katika utalii Afrika Mashariki na duniani kwa ujumla. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tabasam unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mungu leo nimelala Msikitini, ninafanya *dhikri.*

**MWENYEKITI:** Malizia Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa siipokei. Ninaomba unilindie dakika zangu nimalizie. Nasikitika sana maskini dada yangu ni Mbunge mgeni, haijui Mwanza kama ndiyo imebeba kanda nzima ya ziwa. Mwanza ndiyo kwenye… *(Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wake umeisha nimempa amalizie tu sentensi yake.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa muhimu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tabasam malizia sentensi yako ya mwisho.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba tu Uwanja wetu wa Ndege wa Mwanza urekebishwe na tuumalizie ulivyo. Tunataka baada ya Uwanja wa ndege wa Mwanza waujenge Uwanja wa Ndege wa Serengeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ninachotaka kuzungumza hapa, la muhimu sana ni *route* ya ndege ya kutoka Dodoma kwenda Mwanza. Hii ndege, Mkoa wa Mwanza unabeba zaidi ya mikoa nane ya kanda ya ziwa. Kukosa *route* ya kutokea Dodoma kwenda Mwanza, tunamwomba sana Mheshimiwa Profesa Mbarawa pamoja na uchache wa ndege, asipokuja na majibu ya suala la ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Mwanza, pamoja na kupata *route* ya Dodoma – Mwanza, kweli mimi pamoja na kwamba ni ndugu yangu, kaka yangu hapa tutalokiana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Musukuma, Mheshimiwa Abubakari Asenga ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Waheshimiwa Wabunge, mimi sijasoma *dhikri,* kwa hiyo, mnipe nafasi niweze kuchangia vizuri, msinipige taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Profesa Mbarawa kwa kazi nzuri ambayo ameifanya bandarini. Pamoja na yote, tutamkumbuka kwa mengi sanakwa siku zinazokuja kuhusiana na suala la bandari. Ninajua Watanzania wengi hawakumwelewa na walimpiga mawe sana wakati wa *DP,* lakini leo hakuna tena hayo maneno, tunasubiri maneno mengine kwa sababu bandari imekuja kumaliza kiu ya Watanzania wengi ambayo tulikuwanayo. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, huwa ninaongea humu mara nyingi, inabidi

tujirekebishe kwenye teuzi hizi, vijana wanatakiwa sana kwenye Taifa hili. Hongera sana Mkurugenzi wa Bandari kwa umri wake amefanya kazi kubwa sana ya kuionesha mamlaka kwamba, tusiwaamini watu kuwapa vyeo vikubwa kwa maumbo yao, tuwaamini kwa akili zao, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme wazi kwamba, tunaboresha Bandari ya Dar es Salaam. Ni vizuri tuzipe nafasi na benki za ndani. Uwekezaji wa bandari unahitaji fedha na tunakimbilia kwenye mikopo ya nje. Mikopo ya nje ina masharti mengi ambayo unaweza ukaona kama riba za benki za wazawa za Tanzania ni kubwa. Kule ni rahisi, lakini masharti unayopewa, ili ukidhi ule mkopo, ni makubwa, ambayo ni hasara kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa mfano, unaweza ukapewa sharti labda unaambiwa ubinafsishe *TANESCO*, ubinafsishe elimu, ubinafsishe mambo mengi. Kwa hiyo, ninadhani kuna nafasi ya kuziunganisha benki zetu ziweze kutoa mikopo kwenye hizi taasisi ambazo zina miradi ambayo tunaona kabisa ina uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Bandari ya Dar es Salaam. Tunaipongeza sana Serikali, wewe Mheshimiwa Mbarawa na timu yako, leo ukienda Dar es Salaam ni kitu cha kujifunza, wenzetu waliona mbali. Sasa hivi kila mtaa kuna *ICDs*, lakini ukienda Kwala kuna maeneo, maelfu ya eka watu walichukua, wamejiandaa, kwa nini? Nizigo inashushwa Dar es Salaam, hatuwezi kuja na mkakati wa kusema *ICDs* zote zirudi Kwala mkaondoa foleni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wa Dar es Salaam wakisimama hapa, kila mahali sasa hivi mnajenga barabara. Baada ya miezi sita, zinaharibika, yanapita magari yaliyozidisha tani. Ninawaomba sana, tuna Bandari kavu ya Kwala, ina eneo kubwa, tuhamishie *ICDs* zote kule. Hata ukienda Dubai mambo haya ya *ICDs* yako Sharjah kule, haiwezi kuwekwa mjini. Ninawaomba sana, kwa kuepusha foleni bandarini mje na huo mkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili. Kwenye hili nitakuomba sana Mheshimiwa Mbarawa anisamehe. Mimi ni Mbunge wa awamu

ya tatu, na nilikuwa mshabiki kwenye Bunge nikiwa na umri mdogo. Wabunge wenzetu wa Kanda ya Ziwa wamelia sana na *International Airport. Technic* wanayokujanayo kwa kweli, tutaendelea kubaki hivi hivi Wabunge wa Kanda Ziwa. Ninawaomba wananchi wa Kanda ya Ziwa mtuangalie kwa sababu, tukishindwa kutetea vitu ambavyo mnatutuma tukaanza kujibishana humu ndani, haitujengei kuwasaidia watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmekuja na mkakati ambao uking'amua tu wewe mwenye akili unatuletea *International Airport* ya Serengeti; hauna barabara, hauna hoteli, halafu tunaanza kujibishana humu ndani. *International Airport* ya Mwanza miaka zaidi ya 15 tunazungumza humu ndani na tunaweka bajeti. Ninamwomba Mheshimiwa Mbarawa, mimi nimeenda mbali, nimefanya *research* yangu ya kunitosha mimi na elimu yangu, nimesafiri nimeenda Marekani…

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Minnesota, ukienda Caribbean, *airports* zao ni kama ya Mwanza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waitara.

**TAARIFA**

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Ninaomba nimpe Taarifa Mheshimiwa Musukuma kwamba, kujengwa Uwanja wa Ndege wa Serengeti hakuondoi kabisa mpango wa Serikali kujenga *International Airport* ya Mwanza. Sisi Uwanja wa Ndege wa Serengeti *target* yetu ni kwamba, tupate watalii wengi, tuongeze pato la nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakenya wanajenga Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Maasai Mara ili watalii washuke kule. Hapa watakuja kuchungulia na kurudi kwao. Kwa hiyo, ninaomba viongozi wenzetu wa Kanda ya Ziwa tusigombane katika jambo

hili. Uwanja wa Ndege wa Serengeti ujengwe, Uwanja wa Ndege wa Mwanza ujengwe, Uwanja wa Ndege wa Musoma umalizike na maeneo mengine. Ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma, unaipokea Taarifa?

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei. Ninakushukuru, hatuzungumzii Uwanja wa Ndege wa Serengeti, tunazungumza kwa maelezo ya Waziri, siyo ya mtoa taarifa. Tunazungumzia *International Airport* ya Mwanza. Sasa kama sisi tu Kanda ya Ziwa, Mwanza, ambako wote tunategemea hata aliyechangia naye ametoka Serengeti, amekuja kujenga Mwanza; sisi tu, pamoja na hoteli zote, na barabara, leo mwaka wa 30 tunaomba *International Airport*, tunakuja kuweka tena Serengeti. Inahitaji kuwa na *degree* kweli! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda Minnesota pale Marekani, nenda *Caribbean* pale Marekani, *Airport* zao ni nzuri. Sisi sasa tumekuja na mkakati; ninatoa ushauri, ninadhani kutujengea yale majengo ya vioo na nini ndiyo inakuwa kidogo shida. Uwanja wetu kwa ukubwa, unakidhi, yale yale majengo yaliyopo tuongeze tu *facility* ndogo za *immigration* na vyombo vingine, ile *VIP* ya binafsi itatumika *International,* ile nyingine mtuache, mtuletee *International Airport*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukipanda ndege za kwenda nje, hata ya *Air Tanzania,* robo tatu ya wasafiri wanaoenda nje wanatoka *Lake Zone*. Tuna Wachina, tuna watu wamewekeza kwenye samaki, msitufanyie haya maneno ya kutupanga. Mnakuja kutuchonganisha, mnaweka Serengeti ili tuanze kujibishana! Mheshimiwa Mbarawa asipokuja na maelezo mazuri kuhusu Mwanza, ninachukua shilingi, atakuwa wa pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni treni. Suala la treni kwa sasa tunaona linaenda vizuri, lakini ule Mfuko wa *Wharfage* wameuhamisha, wameupeleka Hazina, na Sheria inataka uwe kwa ajili ya kukarabati treni. Tuna kitu kikubwa sana, juzi tumeona imetokea *accident* kidogo hapa, tukaanza kushikana, hela

zimetoka wapi? Tusihamishe hizo fedha waachieni wafanye maendeleo ya reli yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni *LATRA*. Mimi ni mdau wa usafirishaji, nina-*declare interest*. Kama kuna sehemu Mheshimiwa Waziri anahitaji kutusaidia hasa, ni wasafirishaji wa mabasi. Nimefurahi sana ushauri wa Kamati kwamba tumwombe *LATRA* ageuke kuwa mlezi. Kwa sasa *LATRA* ndiyo tatizo, ndio chanzo kikubwa cha watu kufilisika kwenye *transport* ya mabasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nikupe mfano, sasa hivi kuna shilingi tano kila tiketi moja inayokatwa. Kwa mfano, kwenye basi utakata tiketi shilingi 10,000, kuna wapiga debe, kuna nini, kuna nini, mpaka inafika pesa kwako unatakiwa upate labda shilingi 7,000 shilingi tano ndiyo lazima iende *LATRA* kwenye 10,000 ile ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitoka tu mita 100 ukikumbana na tatizo, labda umezidisha abiria au haukufunga mkanda au hauna *dustbin,* unapigwa tena shilingi 250,000. Sasa nakuuliza, ninatoa mfano mdogo, tunaye Mkurugenzi wa Dawa za Kulevya, tunaona kazi nzuri anayoifanya, angekuwa anashirikiana na watu wa Dawa za Kulevya, wanampa hela kidogo ataenda kuwatangaza? Wewe huku tumegawana shilingi tano, umenikuta tu na kosa la *dustbin* tena unachukua hela zote!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba sana, *LATRA* ageuke kama chombo cha kumkuza mfanyabiashara, siyo kugeuka kitega uchumi cha Serikali. Naomba sana, yako matatizo mengi ambayo Mheshimiwa Waziri mwenyewe ameyaona juzi baada ya matatizo ya mafuta. Sisi tumekubali kukaa na Serikali, kujitolea kula hasara, lakini tatizo ni *LATRA,* kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwingine, kondakta, sisi tunachukua watu wa darasa la saba kwa sababu mishahara ni midogo. Kondakta anatakiwa akasome, analipa shilingi 300,000 apewe cheti cha ukondakta. Akipata kile cheti, ukimfukuza ukondakta, akienda kukisajili Serikalini, cheti hakitambuliki. Sasa hiyo ni kazi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipeleka kwa Kihampa asajili cheti chake kama cha *Form Four,* naye apate chochote, anaambiwa wewe hujasoma, umechukua shilingi 300,000 yake. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, tulizingatie hilo kwamba, *LATRA* igeuke kama chombo cha kuwasaidia wasafirishaji wa mabasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Abubakari Asenga, muda ukitosha atamalizia Mheshimiwa Paschal Chinyele.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi hii, na mimi kuchangia Wizara yetu nyeti ya Uchukuzi. Ninaomba kusema mapema kabisa, sitagusa Kiwanja cha Ndege cha Sengerema ama cha Mwanza, nitagusa kile cha Ifakara kwa sababu nacho ni muhimu kiboreshwe, ili ndege ziweze kutua Ifakara pale, zisaidie wananchi wetu wa Malinyi, wa Ulanga na Kilombero. Hiyo itanisaidia sana kutokupata miongozo ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaanza. Mimi ninataka kutoa shukrani zangu za dhati hapa kwa Mheshimiwa Waziri, na ninaunga mkono taarifa iliyosomwa na Mwenyekiti wangu, mzee wangu, baba yangu, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, kwamba, sisi katika Kamati yetu ya Miundombinu amekuwa akituongoza vizuri sana katika Sekta hii ya Uchukuzi na miundobinu kwa ujumla, ambayo yeye ana uzoefu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ni mzoefu sana, atakiri kwamba, Kamati yetu imepata Mwenyekiti ambaye kwa kweli, ushauri wake na wa kamati kwa ujumla mkiuzingatia, basi Sekta hii ya Wizara tatu tunazozisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninataka nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Waziri na uzoefu wako katika Sekta hii, wanafanya kazi nzuri. Katibu Mkuu wa Wizara, Mheshimiwa Naibu Waziri, *DAS* mwenzangu Mwakiposa, a.k.a kipilipili, anamsaidia

hapo, wote ninawapongeza sana. Ninawapongeza sana wakuu na ma-*DG* wote wa sekta ambazo tunazisimamia, wako wengi. Mheshimiwa Musukuma amemtaja *DG* wa Bandari, ninataka nimwambie katika Sekta ya Miundobinu, karibu Wakurugenzi wote…

*(Hapa kulitokea changamoto ya vipaza sauti)*

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kule *TASAC* yule Mohamed ni mwili tu, Mheshimiwa Msukuma; lakini ni kijana hata *forty* hajafika. Ukija *TRC* huku alipotoka Mheshimiwa Kadogosa, yupo kijana anaitwa *Engineer* Machibya. Tuna *engineer* kijana pale, ambaye amesomea kabisa reli, pamoja na vijana wengine ambao ni Wakurugenzi walioaminiwa na Mheshimiwa Rais na nchi hii imeamini. Kama wanataka kuangusha Sekta ya Miundobinu ni wao. Wameaminiwa na wanafanya kazi kubwa sana. Kama wanavyosema, matunda makubwa tuliyoyapata kwenye bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naanza kwenye *SGR*. Kila mtu anakiri kwamba, Dar es Salaam – Dodoma treni inafanya kazi nzuri, pamoja na changamoto zote tunazopata. Maombi ya Watanzania wote ni kwamba, Serikali itafute fedha kwa wakati, tuhakikishe tunaenda kujenga reli ifike Kigoma na Mwanza 2027/2028, ili mradi wetu wa makaa ya mawe kule ulete mapato katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hii Sekta ya Uchukuzi, Serikali ikiitazama kwa jicho zuri, tutapata mapato ya kuendesha nchi yetu. Tukumbuke Hotuba ya Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, wakati tunataka wawekezaji wa bandari alisema tuache uoga, tukiwekeza vizuri kuna siku bandari hizi na miundobinu itatupatia nusu ya bajeti ya nchi hii. Hiyo ni hotuba ya kutembea nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu sasa hivi, Rais akikopa, maneno; tukitumia vyetu vya ndani kuviwekeza kwa nguvu tupate mapato ya kuviendesha, nako maneno. Lazima

Watanzania tujifunge tuhakikishe tunaunga mkono Wizara ya Uchukuzi iipatie fedha *TRC* iweze kukamilisha reli kwenda Kigoma na Mwanza kwa wakati. Ukienda Mwanza sasa hivi, ukiingia tu pale mjini, utaona, palivyokuwa na vurugu-vurugu. Kwa hiyo, ni vitu ambavyo tunaomba kwa dhati sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza mtusaidie kuhakikisha reli ile inakamilika kwa wakati. Mimi nina reli yangu ya Kidatu kwenda Kilosa, tumesema kuisaidia Bandari ya Dar es Salaam. Pia, uki-*connect* Kilosa kuja Kidatu hapa, kontena linaweza kwenda *Joburg, South Africa*. *Engineer* Machibya ameniahidi kwamba, ameanza kutengeneza mataruma kwa ajili ya maboresho ya reli hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza kuhusu *SGR,* nataka kuzungumza kuhusu *TAZARA* kidogo. Tumeona kule Ifakara sasa hivi kuna wawekezaji wa Kichina wanachukua namba, wanachukua *data* za uboreshaji wa Reli ya *TAZARA* ambayo Mheshimiwa Rais amesaini mkataba wa fedha zile. Tunaomba sana ukarabati wa dharura wa hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nimepokea taarifa na nimempa Mkurugenzi wa *TAZARA* kwamba, kipisi kile kinavuja na kilikuwa kinaenda upande, kimeleta hofu sana jana. Tunaomba hali ya dharura kwa sababu, kwa mfano barabara ya kwenda Mlimba kwa kweli, ina changamoto kubwa sana. Ninataka kusisitiza hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaenda kwenye bandari. Kama Wabunge wengine walivyosema hapa, wakati tunasisitiza kuhusu uwekezaji wa bandari, maneno yalikuwa mengi sana, leo bandari imetupa haya matunda iliyotupatia. Lazima tupige makofi ya kutosha kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwamba, aliona vizuri kuhakikisha analeta *DP World* na watu wa Adani, maboresho haya tuliyoyapata. Sasa tunaunganisha nini katika mipango na uwekezaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa nilizonazo pale yanaingia ma-scania, magari 2,400 kwa siku, kuchukua makontena.

Tukiweka *SGR* ikachukua mzigo, itachukua makontena labda 10 kwa kichwa kimoja, vikiingia vichwa 10 vitatoa makotena 200 katika makontena 2,400. Tuna makontena 2,200; suluhu ya haraka ya kuondoa makontena 90% yanayopita Barabara ya Mandela kuja Barabara ya Ubungo ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajenga *SGR* kwa ajili ya abiria. Lazima tutafute barabara ya bandari maalum itakayotoa malori bandarini kwenda nje huko 90%, vinginevyo hapa tutakuwa tuna patapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ya Dar es Salaam, hasa iliyo karibu na bandari, ihakikishe inasikiliza bandari. Nimepata taarifa hata taa za barabarani. Kuna maeneo mengine wameweka fupi, makontena yanagusa. Kwa hiyo, ombi langu ni Mheshimiwa Waziri akija hapa tutafurahi sana akitufafanulia kwamba, kuna magari yanachukua makontena bandarini yanaondoka moja kwa moja. Hata usiku wa manane barabara hii ya mwendokasi itumike kutoa magari yale yaondoke pale bandarini kwa sababu, sisi Dar es Salaam ni tofauti na Nairobi, ni tofauti na *Joburg, South Africa.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Kenya, majirani, bandari iko Mombasa matumizi yao yako Nairobi, ndiyo maana unakuta msongamano hawana, wanashindana na sisi. Sisi Dar es Salaam pale pale kuna makontena ya kubaki pale, maelfu ya makontena. Ndiyo changamoto ambayo ninaiona, kwamba utapeleka makontena ya wawekezaji, wana viwanda Mikocheni, utapeleka makontena ya wawekezaji maeneo ya pale pale, matumizi yao ni makubwa sana. Kwa hiyo, pamoja na makontena ambayo tunayatoa, basi tuanze kufikiri sasa njia mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Morogoro iko karibu na Dar es Salaam, tuwe na mpango mkakati wa Kiserikali kuhakikisha mji wa viwanda sasa unasogea Morogoro, ili bandari yetu iweze kupumua kwa baadaye. Vinginevyo mtu ana mzigo wake pale *GSM* anashusha, wewe utaniambia mimi unipelekee Kwala, sitakubali, nitabaki pale na msongamano utaendelea kubaki.

Kwa hiyo, tunasema yale malori yanayotoa ile mizigo ya nchi jirani yapite barabara maalumu, yaende, na sisi ambao tuna makontena yetu, yanabaki pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi tuanze kufikiria sasa kuweka kongani ya viwanda mbali na Dar es Salaam kwa ajili ya kuweka uwekezaji wa kutosha. Vinginevyo, mapato na uwekezaji huu mkubwa ambao Mheshimiwa Rais alisema, tukapingwa nchi nzima! Hii nchi nikwambie, watu wanasahau sana. Watu wanajaribu kuvuta fikra, vita tuliyopambana wakati wa uwekezaji huu. Leo hakuna mtu, tumekaa baridi hii leo. Matusi ambayo Mheshimiwa Rais alikuwa anatukanwa, leo watu baridi. Ukimpongeza, wanasema unampongeza Rais! Unampongeza Rais!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaunga mkono hoja. Nasisitiza, ili tupate matunda ya bandari tusikilize bandari katika uwekezaji wa miundobinu, ili tuweze kutoa kontena kwa wakati, tuweze kupata mapato ya kutosha, yatusaidie katika sekta nyingine za ujenzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. Ninashukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

*(Hapa kulitokea changamoto ya vipaza sauti)*

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kuchangia kidogo, wakati *mic* zinaendelea kukaa sawa. Hapa ninasisitiza sana uwekezaji katika bandari wakati ma-*technicians* wetu wanaendelea na vipaza sauti, ninataka niguse kidogo kuhusu *LATRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote, sisi tunasimamia pia *LATRA*. Ushauri wangu katika *LATRA* ni kwamba, ni muhimu sana Jeshi la Polisi wakakaa na *LATRA* kuhakikisha wanaondoa mvutano ambao upo. Polisi wetu wanafanya kazi nzuri sana, lakini kweli kupiga faini, Askari anapiga faini, gari na *LATRA* wanapiga faini, lazima tuweke utaratibu, kuna changamoto hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwaige wenzetu wa Zanzibar. Zanzibar wana *LATRA* yao, lakini kwa kweli *LATRA* ya pale ina majukumu makubwa sana. Vinginevyo *LATRA* ndani yake kuwe na kitengo cha Jeshi la Polisi, ili waweze kusaidia na kuondoa malalamiko ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaza sauti tayari, kwa hiyo, baada ya kusema hayo, ninataka kusema kuhusu ya *Air Tanzania*. Leo tunaona maua mazuri yanapendeza pale. Wakati Mheshimiwa Rais anawekeza katika *Air Tanzania,* kuna watu walikuwa na maneno mengi, sijui *Air Tanzania* hakuna maua mazuri. Leo kuna maua mazuri yanapendeza, lakini hizi Taarifa za CAG wetu kuhusu *Air Tanzania* bado watu hawajajua kiuchumi. Nimesoma *Economics,* kwa nini *Air Tanzania* inaongeza safari na inazidi kujiwekeza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, sasa hivi wamezindua safari ya Visiwa vya Shelisheli, nimeambiwa karibuni kuna Moscow, hii inatutangaza nchi yetu. Sisi tumeenda Ghana na *Air Tanzania,* tumeshuka pale Waghana wenyewe wanashangaa kwamba, dude limetua pale, lina ramani ya twiga. Kwa hiyo, Serikali iendelee kuilea *Air Tanzania,* ichukue madeni yake, iisaidie kwa sababu, kwa kweli hii ni heshima kubwa sana. Hata timu zetu zinapocheza nje, zikishuka na *Air Tanzania*…

*(Hapa kulitokea changamoto ya vipaza sauti)*

*(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na majadiliano yetu. Nitawaita wachangiaji watakaoanza, lakini kabla sijawaita, tutachangia kwa dakika sita, wachangiaji bado ni wengi. Tutaanza na Mheshimiwa Paschal Chinyele, atafuatiwa na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, na Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula ajiandae.

**MHE. PASCHAL I. CHINYELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniruhusu kuwa mchangiaji wa kwanza katika *session* hii, na nitajadili jambo moja la bandari na muda ukiruhusu nitakwenda *SGR*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana na kwa kweli ninampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo amekuwa akiifanya ya kuimarisha bandari zetu za hapa nchini. Mheshimiwa Rais ameimarisha sana bandari zetu za Bahari ya Hindi, Dar es Salaam, Tanga, Mtwara na kadhalika. Pia ameimarisha sana Bandari zetu za Ziwa Tanganyika, Bandari za Kabwe, Kasanga na Karema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia Mheshimiwa Waziri Profesa Mbarawa, pamoja na msaidizi wake Ndugu yangu Mheshimiwa Kihenzile, kwa kazi kubwa ambayo wameifanya kutuletea bajeti hii muhimu sana ya uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijikite kwanza kwenye suala la bandari. Kama tunavyofahamu, bandari ili iweze kufanya vizuri ni lazima zile njia za kupeleka kwenye *destination* yaani kwenye lengo ziwe nzuri. Ninashukuru juzi wakati tunajadili kwenye

semina, wawasilishaji walitueleza namna ambavyo barabara na reli vinakwamisha upelekaji wa mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nipendekeze, kwa kuwa barabara hizi za reli ndiyo hasa, tuseme ndiyo *blood stream*, ninapendekeza Mamlaka ya Bandari iangalie namna ya kuimarisha barabara yetu ya *TANZAM*, pia iangalie uwezekano wa kufungua barabara nyingine. Ninaomba hapa niende moja kwa moja kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Dodoma tunayo barabara, nilikuwa nikisema mara nyingi na nitaendelea kusema, tunayo barabara ambayo haijafunguliwa, barabara inayotoka hapa katika Jiji la Dodoma kuelekea Sanza Singida mpaka Rungwa napo ni Singida, halafu unaingia kushoto, unaingia Makongolosi, unafika mikoa inayoenda Nyanda za Juu Kusini kirahisi sana kwa kilomita ambazo hazifiki 370. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua hili ni jukumu la *TANROAD*, lakini nilikuwa napendekeza, Mamlaka ya Bandari pamoja na wabia wake kama *DP World,* fedha wanazo, waingie ubia, waijenge hii barabara pamoja na nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuijenge barabara ifikishe mzigo mapema. Kwa kufanya hivyo mizigo ambayo itakuwa-*handled* Bandari ya Dar es Salaam na nyingine itakuwa mikubwa zaidi, kuliko sasa ambapo tunategemea barabara moja ya TANZAM, ambapo mizigo inapokwenda Mbeya kupitia Morogoro na Iringa, wote tunashuhudia foleni ambazo zinakuwepo njiani. Ukishafika Tunduma ndiyo unakuta kabisa kwamba malori yanakaa mpaka wiki mbili hayajavuka kwenda Zambia na Congo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni muhimu, ingekuwa ni vizuri sana wenzetu wa bandari watafute shilingi bilioni 400 au 500, siyo shida kwao kuzipata na kuisaidia *TANROADS*. *TANROADS* inafanya kazi vizuri sana, lakini lazima tukubaliane ukweli, *TANROADS* wana mzigo mkubwa sana wa barabara katika nchi hii. Kama tunataka tuimarishe bandari, tuingize fedha nyingi zaidi,

tutengeneze barabara hii. Itasaidia sana, ikiwa ni pamoja na kuimarisha barabara nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niseme tu, hii barabara ikijengwa, itaufikisha mzigo haraka sana, katika mpaka wetu wa Kasesha uliopo katika Mkoa wa Rukwa, utapeleka haraka zaidi. Siyo kwamba kila mzigo upite Tunduma, barabara hii itasaidia kupeleka mzigo haraka kufika Kasesha na pia hata kupitia katika bandari zetu za Kabwe pamoja na Kasanga na hata Karema kule Katavi, tutafikisha mzigo wetu kwa haraka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halitakuwa jambo jipya hili, *NSSF* wamejenga Daraja la Kigamboni, pia *NSSF* sasa hivi wanajenga *twin towers* kule Nairobi ambayo ni mali ya Ubalozi wetu wa Tanzania kule nchini Kenya. Kwa hiyo, siyo jambo la ajabu kwa bandari kutafuta fedha, hata kukopa benki ya Kimataifa ili kujenga miundombinu hii ambayo itasaidia kukuza utendaji wa bandari yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara itakapotengenezwa, itakuza uwezo wa bandari na itaweza kupeleka mizigo katika maeneo mengine mengi zaidi, na nchi nyingine kwa maana ya maeneo ambayo yatapokea mizigo yetu. Hii itasaidia kwa kiasi kikubwa sana kukuza uwezo wa bandari zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, sasa inajenga Bandari ya Bagamoyo. Bandari hii ya Bagamoyo itabeba mizigo mikubwa sana. Sasa namna gani itafikisha mizigo katika nchi tunazozilenga, ni pamoja na kujenga barabara hii. Kwa haraka haraka niishie hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine niongelee kuhusu *SGR*. Tunashukuru sana Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutujengea na kukamilisha kipande cha barabara kati ya Dodoma na Dar es Salaam. Kwa kweli tunafurahia usafiri nzuri kabisa, usafiri wenye tija na haraka. Pamoja na kazi nzuri ambayo imefanywa na Serikali, lakini wakazi wa maeneo ambayo reli hii inapita, wamekuwa wakipata adha kubwa sana

ya kuvuka kutoka upande mmoja kwenda upande mwingine. Hali hii imekumba maeneo mengi kutoka Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma. Hapa kwa namna ya pekee, Kata za Mkonze, Kata ya Kikuyu pamoja na Zuzu ni moja ya Kata ambazo zimeathiriwa sana na reli hii ambayo kwa kweli ni reli yenye manufaa makubwa sana kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba, kuna madaraja haya ya juu, katika bajeti ya Waziri Mheshimiwa Profesa Mbarawa, naomba sana atuwekee fedha kwa ajili ya kujenga *overpass*, madaraja ya juu ambayo yatawasaidia watu wetu kuvuka kutoka upande mmoja kwenda upande mwingine, kwa sababu imefika mahali sasa....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umeisha, malizia.

**MHE. PASCHAL I. CHINYELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba dakika moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wetu wanavuka upande mmoja kwenda upande mwingine, wanapita kwenye zile njia za kupita maji ya mvua. Hali hii siyo nzuri. Ninapendekeza Wizara iweke fedha kwa ajili ya kutengeneza madaraja haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kengele ni moja tu, ikipigwa unamalizia sentensi na kuunga mkono hoja.

Waheshimiwa Wabunge, nilimwita Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, atafuatiwa na Mheshimiwa Agnes Hokororo, Mheshimiwa Sylvia Sigula ajiandae, Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa ajiandae.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji. Awali ya yote niunge mkono hoja, na nitoe shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais, kwa kazi kubwa ambayo ameifanya na uthubutu aliouonesha hasa kwenye maamuzi ya uwekezaji wa Bandari ya Dar es Salaam kupitia wawekezaji wa *DP World*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maamuzi yale ambayo yalifanywa na Serikali yamepelekea kuwa na mafanikio makubwa sana kwenye sekta ya Bandari. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. Siyo hivyo tu, mabadiliko yaliyofanyika yameleta tija, makusanyo yameongezeka, karibu nusu ya kile kilichokuwa kikikusanywa. Bandari ilikuwa ikikusanya shilingi bilioni 800, leo tunavyozungumza bandari ina makusanyo ya zaidi ya trilioni mbili, ni mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata wale ambao walikuwa wakipinga maono ya Mheshimiwa Rais, kwa sasa walishakaa kimya kwa sababu wanaona mabadiliko yaliyofanyika. Tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuwaamini vijana, karibu Wizara ya Uchukuzi imeamini vijana ambao wamefanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Mamlaka ya Bandari, yupo *CEO* ambaye anafanya kazi nzuri sana, na tunawapongeza sana. *TRC* nayo ina kijana ambaye amefanya kazi nzuri sana, mnaweza msijue kazi aliyoifanya, lakini kuna mafanikio makubwa sana hasa kwenye *design* za reli zote zilizojengwa na amefanya kazi mpaka nje ya nchi kwa ajili ya kufanya *design* na kuaminiwa kwa kiwango kikubwa sana. Bado *TASAC* iko chini ya vijana, wanafanya kazi, ukienda Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ni vijana ndio ambao wameaminiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba tu vijana waliopewa dhamana hiyo, waende wakafanye kazi kwa kujituma ili waweze kutimiza ndoto na maono ya Mheshimiwa Rais yaliyowafanya waaminiwe. Tunampongeza sana Mheshimiwa Profesa Mbarawa akisaidiana na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri ambayo ameifanya, tunaomba yale ambayo tunayashauri wakayafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Shirika la Reli tunahitaji nguvu kubwa ielekezwe kwenye maeneo ya kukamilisha reli ya kutoka Makutupora kwenda Tabora, Tabora - Isaka, Isaka kwenda Mwanza ili hiyo *line* iweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua tayari Serikali imefanya juhudi kubwa sana, imepata fedha ambazo zitaweza kufanya na kukamilisha hiyo reli. Jukumu la Mheshimiwa Waziri ni kusimamia *Yapi Merkezi*, ambayo kimsingi haikufanya vizuri kwenye maeneo mengine. Tunaomba eneo hili lifanyiwe kazi na lisimamiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika usafiri wa majini Serikali iliahidi sana kutoa usafiri wa majini kwenye Ziwa Tanganyika. Bado kule hakujafanyika kazi ile iliyokusudiwa. Ni vyema, Serikali ikajipanga kukamilisha ile miradi ambayo iliahidiwa na wananchi wakawa na matumaini makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Tanganyika ndiyo Ziwa pekee ambalo halina usafiri wa meli ya aina yoyote. Tunafanya kazi ya kuwatumikia wananchi na wananchi walioko kule wanahitaji huduma ya Serikali. Ninaomba sana msukumo ufanyike kwenye ile meli ya MV Liemba ikamilike haraka ili iweze kutoa huduma. Tutakuwa tumeepusha ajali zinazotokea za mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye viwanja vya ndege, tunaiomba na kuishauri Serikali iharakishe kujenga Kiwanja cha Ndege cha Mwanza sambamba na ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Serengeti. Viwanja vyote hivi vinahitaji vijengwe, na kila kiwanja kina sababu yake ya kujengwa. Nafikiri kwenye eneo hili hapa, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wa Kanda ya Ziwa na wale wanaotoka Mkoa wa Mara, tusigombane kwenye maeneo haya ya kujenga viwanja, kila kiwanja kina bajeti yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanja cha Mwanza ni *priority* kubwa sana kwa Serikali, na sisi tumeona mipango ambayo imewekwa kwa ajili ya kukiimarisha ili kiweze kufanya kazi ya kuhudumia mikoa inayozunguka pale Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanja kile cha Serengeti ni kiwanja mahsusi kinachojengwa kwa nia ya kwenda kukuza utalii kwenye maeneo ya Hifadhi ya Serengeti. Hata *design* ya uwanja ule ipo tofauti na ule uwanja ambao upo Mwanza. Majengo yatakayojengwa Serengeti ni yale ambayo yana mfumo wa utalii, sambamba na *cage* ile ya wanyama, hoteli na viwanja vya *golf* vitakavyojengwa pale Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nilimwita Mheshimiwa Sylvia Sigula, atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa, Mheshimiwa Esther Malleko ajiandae.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuweka mchango wangu katika Wizara hii ya Uchukuzi kwenye bajeti yake ya mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mungu, Mwingi wa Rehema ambaye amenijalia afya njema na kibali kuweza kusimama katika Bunge hili kutoa mchango wangu. Nitumie nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na timu nzima ya Wizara, hakika tumeona dhamira ya Serikali, pia tumeona namna ambavyo wanapambana kutuletea maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wahenga wanasema asiyeshukuru ni kafiri. Sisi Wanarukwa tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa mara ya kwanza Mkoa wa Rukwa tunaenda kuonekana kwenye ramani ya dunia kwa kupata kiwanja cha ndege kizuri, katika Mji wa Sumbawanga. Haijawahi kutokea tangu tumepata uhuru, leo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameenda kutuheshimisha Wanarukwa. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na sisi wananchi wa Rukwa tunamwombea kila la heri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maslahi ya muda, nitajielekeza kwenye mambo mawili. Jambo la kwanza ni upatikanaji wa meli katika Ziwa Tangayika. Ninadhani hii ni zaidi ya awamu mara ya tatu, ya nne tunazungumza katika bajeti kuhusiana na upatikanaji wa meli katika Ziwa Tanganyika. Tuna zaidi ya miaka saba, Ziwa Tangayika hatuna usafiri wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongelea Ziwa Tanganyika, tunazungumza maisha ya wananchi zaidi ya milioni tano. Tunapoongelea Ziwa Tanganyika, tunazungumza mikoa zaidi ya mitatu, macho yetu tumetazama katika Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi letu kwa Wizara. Tunajua MV Liemba ipo kwenye ukarabati, na MV Mwongozo nayo ipo kwenye *process* za ukarabati, lakini haujaanza. Tunaomba sana Mheshimiwa ProfesaMbarawa jambo hili alichukue kwa uzito. Sisi watu wa Ukanda wa Ziwa Tanganyika, maisha yetu tunatamani sana kuwa na usafiri wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua mkataba wa ukarabati unatakiwa uishe mwezi wa Tano ambao ndiyo huu, lakini mpaka mwezi wa Tatu ulikuwa umefika 54%, hatuoni kama utaenda kukamilika. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, suala la meli alichukue kwa kipaumbele chake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nilitamani kuongea katika Wizara hii, ninawapongeza sana Wizara, nimeona tayari tumetoa boti mbili za uokoaji katika Ziwa Tanganyika, lakini kama ambavyo nimesema unapozungumzia Ziwa Tanganyika unazungumza mikoa mitatu. Kweli zinaweza zikawa boti mbili zimetolewa, lakini uwiano wa ugawanyo katika Ziwa Tanganyika hauwezi kuleta matokeo yale tunayoyatarajia. Leo Ukiangalia Ziwa Tanganyika urefu uliopo kwa boti mbili, ni ngumu sana kufanya kazi na ikaleta tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi letu wananchi wa Rukwa, tunajua dhamira ya Serikali hata katika uokoaji, ni kuokoa maisha ya Watanzania wanapopata changamoto, lakini Wanarukwa

tuna vijiji ambavyo hawana barabara, hawana *alternative* yoyote ya kufikia huduma za kijamii bila kutumia maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda Wilaya ya Nkasi, Kata ya Wampembe, Kijiji cha Izinga hawawezi kufika Makao Makuu bila kupita kwenye maji. Ukienda Kijiji cha Mwinza hawawezi kufika Makao Makuu bila kupita kwenye maji. Pia ukienda Kata ya Ninde hivyo hivyo, kuna baadhi ya vijiji hawezi kufika makao makuu bila kupita kwenye maji. Hata ukienda Wilaya ya Kalambo, Kata ya Kasanga, kuna Kijiji cha Kipwa, hawawezi kufika makao makuu bila kupita kwenye maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri sisi wananchi wa Rukwa tunaomba sana tupate *boat*, tunatamani tupate *ambulance boat* ambayo itawasaidia wananchi, siyo pale tu inapotokea maafa, bali hata kuwatoa sehemu moja kuwaleta sehemu nyingine, kwa sababu hawana *alternative*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, tunajua dhamira ya Serikali ni nzuri, lakini ni lazima tufanye ili watu wetu waone namna ambavyo Serikali yao inawapenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukiwaangalia hawa watu wa Wampembe, Serikali imejenga zahanati, vituo vya afya, na miradi mingine mingi, lakini hawawezi kuifurahia kwa sababu hawana *access* ya kufika kupata huduma kwenye miradi hiyo. Watu wanafariki siyo kwa sababu vituo vya afya havipo, hapana; vituo vya afya vipo. Mheshimiwa Rais Samia amejenga vituo vya afya vingi, na zahanati nyingi, lakini namna ya watu kufika kwenye huduma imekuwa ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua kwamba wanashirikiana na TAMISEMI. TAMISEMI wao wana *ambulance* za ardhini, lakini wao wanaweza kuwa na *ambulance* boti kwa ajili ya watu wetu hawa wa vijiji ambavyo vipo kwenye ukanda wa Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Malleko.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa maoni au mchango wangu kwenye bajeti hii ya Wizara ya Uchukuzi katika mwaka huu ambao tunaendelea nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, maana kwenye bajeti tumesikia matokeo makubwa, hasa kutoka kwenye Bandari yetu ya Dar es Salaam. Kazi imefanyika ni kubwa. Miaka miwili mitatu iliyokuwa hapa tulikuwa kwenye kimbembe kikubwa, tukisemwa kila sehemu kama Bunge, lakini kile tulichokisimamia na kukiamini leo kinazaa matunda na kila mmoja anaona. Kwa hiyo, tunachojifunza, kama kuna jambo la muhimu kwa ajili ya masilahi ya nchi, tusimame kama Bunge tuiunge mkono Serikali ili jambo liweze kufanyika kwa manufaa ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya, lipo jambo ambalo limekuwa linaendelea hasa kwenye Mji wa Dar es Salaam. Baada ya uwekezaji huu mkubwa nilitaka tu kidogo kutoa ufafanuzi, maana unajua wengi baada ya kuona *SGR* imeanza ni kama vile tunadhani malori au magari hayana kazi tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zote duniani, pamoja na kuwa na reli, lakini malori kwa ajili ya usafirishaji wa mizigo kuingia na kutoka bandarini bado yanaendelea na kazi. Ni *almost* 60% mpaka 65% ya mizigo inabebwa na malori. Labda 40% mpaka 35% ndiyo yanaenda kwenye reli, na reli inafanya masafa marefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano leo tumejenga Bandari Kavu ya Kwala, mizigo inayotumika Buguruni na Vingunguti huwezi

kuipeleka Kwala *then* ukairudisha kule. Ndiyo maana unaona baada ya upanuzi mkubwa wa bandari, na ikizingatia kwamba *more than* 50% ya mizigo mingi inoyopita kwenye Bandari ya Dar es Salaam inabaki kwa ajili ya matumizi ya nyumbani hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vingi viko Mkoa wa Pwani na Mkoa wa Dar es Salaam. Kwa hiyo, tunategemea pia lazima tuone *ICD* nyingi na makontena mengi yanaongezeka mjini pale kwa sababu uwekezaji mkubwa uliofanyika una-*attract* hivyo vitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa nina maoni kama ya aina mbili tofauti. Tunaomba Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia *TISEZA*. Kwa sasa kwa sababu tuna *line* hii ya *SGR* wanapotenga maeneo ya uwekezaji hebu wajikite kwenye *line* huko ambapo inapita ili tuondoe msongamano kwenye ule mji, kwa sababu hata iweje, uwekezaji wa viwanda ni mkubwa maeneo ya Mikocheni, Vingunguti, Kipawa Temeke, ndivyo vinavyozalisha. Ni lazima tuone ongezeko la *ICDs* nyingi zikiongezeka. Kwa hiyo, *population* na *congestion* itakuwa kubwa sana kwenye ule mji kiasi kwamba bado wananchi wanapata shida na inachelewesha uzalishaji pia. Kwa hiyo, tulione hilo ili tuweze kulishughulikia. Uzuri wa barabara uongezwe ili malori yanapotoa mizigo bandarini foleni zisiwe kubwa sana, yaweze kutoa na kurudi na hatimaye tuwa-*save* hata wale watu ambao wanakuja kuwa *end users*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko jambo nilikuwa najaribu kupitia hapa. Wakati mwingine unakuta mtu ana *BL* moja ina kontena 100. Kwa nini usifanyike utaratibu hata wa kuwa wanafanya *partial clearance* ili hatimaye siyo mtu mmoja tu kwa wakati fulani anakuwa ameshikilia bandari pekee yake wakati wengine wakiwa wanasubiri? Kwa hiyo tulione hilo kwa sababu kontena zile zinakuwa na *BL* namba pale, kwenye *BL* kontena zimeorodheshwa, wawe wanafanya *partial clearance,* asiwe mtu mmoja akianza kufanya *clearance* mpaka yeye tu amalize ndipo watu wengine waweze kuingia pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuangalie hilo ili tuweze kurahisisha kazi. Huyo akitoa kontena 20, mwingine anatoa hizo ili

wote waweze kurahisisha na hatimaye waweze kwenda haraka na kufanya shughuli zao kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaenda haraka haraka kwa sababu ya dakika sita. Nilikuwa ninajipanga kuchangia dakika 10, ninaona sasa tunakimbizana haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine, wako watu wa usafirishaji, madereva, wamekuwa wanapata shida. *Drivers* wamesoma tayari wana leseni zao. Wakati wa ku-*renew* leseni hawa madereva wanaonyesha magari makubwa na madaladala na vitu vingine, anaambiwa akatoe shilingi laki tatu ya kuingia darasani siku 14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi haya mambo, mtu ameharibu gari tu, tajiri anapiga simu gari yangu wacha hapo hapo, ninatuma dereva mwingine umwambie mtu akakae darasani siku 14 atarudi akute mwajiri bado hajachukua dereva mwingine? Kwa hiyo, *let us see this,* tusiwatese madereva; hawa watu hawana kitu kingine. Kama mtu hajakosea, hajafanya adhabu yoyote barabarani, hana *penalty*, hana nini, kwa nini wakati wa ku-*renew* leseni yake mtu aanze kupitishwa huko? Ninalisema kwenye Wizara ya Uchukuzi kwa sababu hawa ndio wanao-*deal* na uchukuzi, wawasaidie madereva. Hata kama ni *TRA* wameweka, au nani ameweka, wawasaidie ili madereva waweze kufanya kazi *comfortably*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine tunachukiwa tu na watu kwa vitu vidogo kama hivyo. Mtu anawaza shilingi 300,000 aingie darasani tena kwa hela yake yeye mwenyewe. Shilingi 300,000 kwa dereva wa kawaida wa Kitanzania ni nyingi sana. Kwa hiyo, tuwasaidie madereva hawa kwa sababu ndio wanatunza familia zao na wao ni maskini, wanataka wajikwamue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema mambo mazuri yaliyofanywa na bandari, lakini mimi niko kwenye Kamati ya *PAC*. *One of the issues* tulikuwa tunapitia ni pamoja na Mamlaka ya Viwanda vya Ndege. Tunajua, wakati mwaka 2025 tunapitisha bajeti hapa, *wharfage* ilikuwa bado inachukuliwa na hazina.

Kama Bunge, tukasimama tukasema, *TPA* warudishiwe, na leo tumeona *improvement* kubwa iliyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa *TANAPA* walikuja hapa, fedha yao yote ilikuwa inachukuliwa, tukasema warudishiwe *some parts,* leo tunaona wanafanya vizuri. Tunaomba na *TAA* pia wasaidiwe. Huwezi kwenda kwenye *competition* kama hela huna, kila wakati uende ukaombe kila kitu wakati huku unashindana *private sector.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa ninaomba wasaidiwe na hilo ili warudishiwe fedha yao wanayoikusanya, mwisho wa mwaka tunakutana kwenye kutoa gawio Serikalini, shida iko wapi? Si wataleta hesabu zao wakaguliwe! Yataonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Esther Malleko atafuatiwa na Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye sekta hii muhimu ya uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa uwekezaji mkubwa sana aliofanya wa miundombinu katika sekta hii ya uchukuzi. Niwapongeze pia Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na pongezi. Ninaipongeza sana Wizara hii kwa kazi kubwa iliyofanyika tukianza na *TPA*. Tunapongeza sana *TPA,* tumeona kazi kubwa iliyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati bandari hii inaanza kufanya kazi baada ya kuboreshwa walikuwa wanapokea mizigo tani

milioni 17.7, lakini mpaka Juni, 2025 wamefika tani milioni 32. Tunawapongeza sana. Kwa upande wa makasha ilikuwa ni 750,000 lakini kwa sasa ni 1,100,000. Huo ni uwekezaji mkubwa, tunaipongeza sana Wizara kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye *TRC*. Tunawapongeza sana kwa kujitegemea na kujiendesha bila kutumia ruzuku inayotoka Serikalini kwa 100%. Tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua mradi wa reli ya kisasa ni alama ya maendeleo kwa Taifa letu. Tumeona kwa kiasi kikubwa baada ya ujio wa reli hii ya kisasa kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma imeongeza ufanisi mkubwa sana wa safari, na imepunguza muda mrefu wa wananchi au abiria kusafiri. Pia kumekuwa na usalama mkubwa sana katika usafirishaji wa abiria na mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunaishauri Serikali ione ni namna gani sasa inaweza kufanya kazi kubwa zaidi kuunganisha vipande vilivyobaki vya reli hii ya kisasa katika mikoa yote muhimu ili tuweze kuongeza pato la Taifa na kuwapatia wananchi wetu usafiri wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika kanda yangu ya Kaskazini. Tumesikia hapa kwamba wamemaliza upembuzi yakinifu kwa ile reli ambayo itaanza Tanga kwenda Musoma kupitia Arusha. Tulikuwa tunaiomba Serikali, kwa kuwa upembuzi yakinifu umekamilika, itafute namna ya kupata fedha ili reli hiyo iweze kujengwa mapema. Kwa sababu tunajua kwamba kwanza iko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, lakini pia ina faida kubwa kwa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua tunaweza kusafirisha mizigo. Tuna madini ya soda kule Engaruka, tuna *nickel* Dutwa pamoja na *potassium* kule Minjingu. Kwa hiyo, kukamilika au kujengwa kwa reli hii itatusaidia sana katika eneo la mizigo, kusafirisha abiria na pamoja na utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu Kilimanjaro tunao Uwanja wa Ndege wa Moshi. Tunaomba sana Serikali imlipe mkandarasi ili uwanja ule uweze kukamilika na kutumika kwa wananchi wetu na pia kwa Taifa letu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, ninaomba uunge mkono hoja; muda wako umekwisha.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nimwite sasa Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mheshimiwa Suleiman Mohamed Rashid ajiandae.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie Wizara hii ya Uchukuzi. Kwanza kabisa nianze na bandari. Tumeona miradi mikubwa ambayo imefanyika, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri pamoja na *DG* wa bandari, wanafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikia hapa kwenye taarifa ya Kamati pamoja na taarifa ya Mheshimiwa Waziri kwamba bado tuna changamoto za miundombinu ambayo tunatakiwa tuboreshe zaidi. Nimeangalia, hapa kuna ile ada mpya ambayo wameiweka ya 4.5, ninaunga mkono waende wakafanye kazi. Nia ni kuhakikisha kwamba miundombinu hii tunaitengeneza na inakuwa mizuri kwa ajili ya usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilikuwa nataka kusema, kama tuna uwezo wa kukusanya. Tumeona hii 4.5 *percent* wanaenda kukusanya takribani shilingi bilioni 350. Kama tunaweza kukusanya shilingi bilioni 350 kwa mwaka, ni dhahiri kwamba sasa tunaweza kuiruhusu *TPA* kukopa kwa kutumia *balance sheet* yake. *TPA* inaweza kukopa kwa kutumia vitabu vyake vya hesabu. Ikishakopa, itaendesha na kutengeneza miradi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaweza wakopa takribani shilingi trilioni mbili, wakatengeneza miradi, kwa sababu wanaweza kukusanya shilingi bilioni 350 kupitia hii 4.5, wanaweza kulipa ndani ya miaka mitano hadi sita, wanakuwa wamemaliza deni. Pia miradi hii itakuwa imekamilika kwa wakati na itakuwa imeanza kufanya kazi kwa wakati, wakati tunaendelea kulipa deni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha msingi, tuangalie *balance sheet* zao tu-*calculate quick ratio*, na pia tu-*calculate current ratio*. Ikiwa *more than one, let them do*. Tuangalie *date ratio,* ikiwa *less than one* tuwaruhusu wafanye. Nia ni Serikali kupata mapato kwa wakati huku tukisubiri kukusanya kidogo kidogo. Tumechelewa sana katika uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakope wenyewe, waende benki wakakope, watekeleze miradi, gati namba 12 hadi 15, gati la kushushia mafuta na mambo mengine. Hata hii barabara ya njia nne kutoka Dar es Salaam kwenda Morogoro kwenda hadi Songwe kule. Tukitengeneza hii ndiyo itakayokuwa mantiki ya uchumi tunaoutafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitamani niseme hapa, kwa sababu ya ndugu zetu wa bandari wamefanya kazi nzuri, kwa hiyo, tuwaruhusu wakope wenyewe ili waweze kutengeneza miradi hii kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni Uwanja wa Ndege wa Mwanza. Tukizungumza *International Airport* ya Mwanza, mpaka sasa hivi kuwa haina jengo la abiria, kwa kweli ni kitu ambacho hakiwezekani. Ninatamani kuona kwamba Uwanja wa Ndege wa Mwanza unatengenezwa na unaimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kuwa Uwanja wa Ndege wa Mwanza unapokea abiria kuanzia 400,000 hadi 500,000 kwa mwaka. Sasa, kuwa hauna jengo la abiria, kwa kweli siyo sawa kiuchumi. Kuwa hakuna huduma za Kimataifa, siyo sawa kwa wananchi wa kanda ya ziwa, na wananchi wa Mwanza. Pia, nchi

za maziwa makuu nazo zinategemea uwanja huu wa Mwanza. Twendeni tukaujenge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kwamba wametenga shilingi bilioni sita kati ya shilingi bilioni 13. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, twendeni tukatekeleze mradi huu, tuache haya mambo ambayo yamekuwa yakitokea huko. Tunaanza lakini tunaacha. Twendeni tukafanye na watu wa Kanda ya Ziwa, ambao ni wananchi wa Tanzania kupitia uchumi wa Uwanja wa Ndege wa Mwanza wanufaike. Hii ni kwa sababu tunajua kwamba Uwanja wa Ndege wa Mwanza ni uwanja wa nne kwa nchi yetu ya Tanzania kwa kupokea wasafiri wengi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja mwingine ambao ninataka nichangie ni Uwanja wa Ndege Serengeti. Uwanja wa Ndege Serengeti hakuna namna tunaweza kuukwepa. Kwanza jina lenyewe la Serengeti limeshajitangaza vya kutosha. Ukitazama Serengeti kama jina, limeshajitangaza. Kwa hiyo, twende tukawekeze pia katika Uwanja wa Ndege wa Serengeti kwa sababu ya utalii...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** ...tunajua watalii tunapokea takribani 500,000 hadi 600,000.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Arusha – Serengeti kilomita 300 ni nyingi. Twende tukawekeze pale Serengeti ili wananchi tupate utalii wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango. Nilimwita Mheshimiwa Suleiman Mohamed Rashid, Mheshimiwa Yannick Ikayo Ndoinyo atafuatia.

**MHE. SULEIMAN MOHAMED RASHID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niwe mchangiaji wa jioni ya leo katika hotuba ya bajeti ya Wizara ya Uchukuzi. Awali ya yote niungane na wenzangu wote waliotangulia kwanza kutoa shukrani, pia niipongeze Wizara yetu kwa kazi nzuri ambayo inaendelea kufanywa ili kuhakikisha kuwa mipango ya Serikali inakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninapomshukuru ni kwa namna ambavyo amefikiria kwamba sekta hii ya uchukuzi siyo sekta ya uchukuzi tu, bali ni sekta inayohusiana na uchumi wa miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, Mheshimiwa Rais amekuja na maoni ya kuona kuna haja ya kuanzisha mfumo fungamanishi; ikiwa na maana *multimodal transport system* ambayo itawezesha sekta zetu hizi za *railway*, bandari pamoja na viwanja vya ndege, tunaviunganisha pamoja ili dhana ya usafirishaji wa mizigo pamoja na abiria uwe rahisi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda nilikuwa ninaomba niweze kuainisha changamoto ambazo zinatukabili sekta yetu hii ya uchukuzi ili hatimaye niweze kutoa ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto kubwa ambayo tunayo ni msongamano wa mizigo katika Bandari yetu ya Dar es Salaam. Ipo kazi nzuri ambayo inafanywa na *TPA* kupitia *DP World*. Utendaji wa kazi wa bandari ni mchakato wa ushirikishwaji, kwamba bado baadhi ya sekta na taasisi nyingine ya ushirikishaji, wao katika utoaji wa huduma ya upokeaji na utoaji wa mizigo umekuwa ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukaona, hata muda wa masaa ya kazi huwa hayafanyi kazi masaa 24. Kwa hiyo, katika hili

ninaomba Wizara pamoja na sekta nyingine tuondoke katika mfumo wa utendaji wa kazi wa masaa 11, tuweze kufanya kazi masaa 24. Pia katika siku za kazi tutoke siku tano hadi sita tuweze kufanya kazi siku zote saba. Hii itakwenda kusaidia urahisishaji wa utoaji wa mizigo yetu, na itakwenda kutusaidia kuondoa msongamano pale bandarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni miundobinu wetu ya reli pamoja na barabara. Pamoja na kazi nzuri ambayo *DP World* wanaifanya ya kutoa mizigo pale bandarini, lakini bado hakuna kiunganishi baina ya mizigo ambayo tunaitoa na kuweza kuisafirisha. Unaweza ukaona mizigo inafika na kuweka msongamano sana katika barabara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuje na mkakati mahsusi wa kuifanya mizigo yetu ambayo tunaitoa, kuiunganisha katika bandari zetu kavu, kwa njia ambazo zitakuwa ni mbadala badala ya barabara ambazo tunaendelea kutumia pamoja na wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la upungufu wa uwekezaji katika maeneo katika bandari nyingine za Maziwa Makuu. Tunaweza tukaona kwamba moja ya kazi nzuri ambayo imefanywa na Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuweza kuridhia bandari yetu kubinafsishwa katika utoaji wa huduma kupitia *DP World*. Pia unaweza ukaona kwamba bado baadhi bandari nyingine hizi za maziwa makuu, utoaji wake wa huduma umekuwa ni hafifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba na ninashauri, dhana kubwa ambayo itaweza kutusaidia hapa ni *PPP*. Ni kuona kwamba tunaweza kuzishirikisha taasisi nyingine binafsi ambazo zitashirikiana na Serikali katika utoaji wetu wa huduma. Katika hili tukiweza kulifanya, tutaweza kuboresha utoaji wetu wa huduma na tutahakikisha kwamba mambo yetu yanaenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la ushindani kutoka kwa bandari zetu za jirani Mombasa pamoja na *Beira* ya *Mozambique*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tuna changamoto hiyo, na wakati mwingine unaweza ukaona hata viwango vyetu vya tozo zinaonekana kwamba ni kubwa tofauti na bandari nyingi. Kwa hiyo, nishauri Wizara, ione kwamba kuna haja ya kufanyia kazi mapendekezo haya ambayo tumeainisha ili tuweze kufikia malengo ya Dkt. Samia Suluh Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mwera, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimwite Mheshimiwa Yannick Ikayo Ndoinyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Cornel Lucas Magembe. *(Makofi)*

**MHE. YANNICK I. NDOINYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kuniona na kunipa nafasi ili na mimi niweke maoni kwenye hotuba hii ya Wizara ya Uchukuzi kama ambavyo imewasilishwa kwetu leo asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tumefurahishwa. Mimi binafsi nimefurahishwa sana na kazi iliyofanyika kwenye bandari, usafiri wa anga, na usafiri wa reli, ni kubwa sana. Kwa kweli nimefurahishwa binafsi na ninaendelea kuwapongeza sana Wizara, na ninaomba waendelee hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio haya yasingepatikana isipokuwa kwa maono na *commitment* ya Rais wetu tulinaye Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ninampongeza huko aliko, na ninamwambia aendelee kuongeza nguvu kwa sababu hapo alipo anaendeleza mambo vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile muda ni mchache sana, ninaomba niseme kitu muhimu sana kwa Wilaya yangu ya Ngorongoro. Kama ambavyo nimeshasimama hapa mara kadhaa kuiomba Serikali tuifungue ile Wilaya ili iweze kufikika na kufufua uchumi wa ile Wilaya, ni kwa sababu Wilaya ya Ngorongoro hasa eneo la Loliondo ni eneo la uchumi uliolala. Bila kuwekeza na kuweka miradi ya kimkakati, hatutaweza kufurahia

hii *speed* ambayo Mheshimiwa Mama Samia anatupeleka kwenye nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaiomba Wizara japokuwa nimeshawasilisha, lakini ninaomba sasa tujenge kile kiwanja cha Waso. Mwaka 2025 tulipokuwa tunafanya kampeni niliwasilisha ombi letu hilo kwa Mheshimiwa Rais kwamba tujengeeni Kiwanja cha Waso cha Ndege ili kiwe mradi wa kimkakati kwa ajili ya eneo letu la Loliondo, na kwa ajili ya Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile tunajadili Wizara hii ya Uchukuzi, ninaomba Mheshimiwa Waziri alichukue hili, ni ombi maalum kwamba Uwanja wa Ndege wa Waso ujumuishwe katika mipango ya Wizara na kuelekea kuijenga kwa sababu ina umuhimu wa kipekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wilaya ya Ngorongoro hatuna barabara ya lami mpaka sasa, tukipata Uwanja wa Ndege itaongeza chachu ya ukuaji wa uchumi, itaongeza ajira, itakuwa ni eneo muhimu sana la mgawanyiko wa utalii kwenda Serengeti, Ngorongoro na Oldonyolengai kwa sababu ni eneo la katikati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bila kupoteza muda, nilisema niweke ombi langu lisajiliwe kabisa kwamba ni mahitaji ya Wilaya ya Ngorongoro kuwa na kiwanja cha Ndege ili tuweze kuhudumia kanda hiyo ya Kaskazini mwa Tanzania, kutoa ajira kwa vijana na kuhakikisha kwamba inakuza uchumi wa Mji ule wa Waso.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuunga mkono hoja hii na ninaomba wenzangu wote tuendelee kuungana kuunga mkono hotuba hii kwa sababu inaenda kuleta mageuzi makubwa sana katika sekta hii ya uchukuzi Tanzania. Ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Cornel Lucas Magembe atafuatiwa na Mheshimiwa Nabil Ahmed

Abdallah, Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ng'anzi Ulenge ajiandae.

**MHE. CORNEL L. MAGEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Waheshimiwa Wabunge wote kwanza waliotoa maneno ya faraja kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kumpongeza kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli atakuwa ni mtu mwendawazimu pekee ambaye atapingana na pongezi hizi za Wabunge za kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, na mimi niwe miongoni mwa hao kumshukuru sana Mheshimiwa Rais. Ni kweli tunazungumza kuhusu Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya uchukuzi imeweka mipango mizuri mingi ya kwenda kujenga viwanja vya ndege katika mikoa yetu na mikoa ambayo imewekewa mpango huo wa kujengewa viwanja hivi vya ndege. Kila Mheshimiwa Mbunge hapa anashukuru na kupongeza sana, lakini na mimi niendelee kushirikiana nao kwa kupongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe tahadhari moja tu. Viwanja hivi ni kweli tumekuwa tukivijenga, vinatumia matrilioni na mabilioni ya fedha za Watanzania kwenda kuwekeza, lakini vinapowekezwa, viwanja hivi haviendi kutumika. Mfano mzuri mara zote nimekuwa nikisimama hapa kuzungumzia Uwanja wa Ndege wa Chato. Uwanja wa Ndege wa Chato umejengwa kwa mabilioni mengi ya fedha, na ndege zilianza kwenda pale lakini ilifikia mahali ndege zikakata kuja pale Chato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Wizara hii ya Uchukuzi kwamba kuna kila sababu ya kuendelea kuleta ndege kwa watu wa Chato kwa sababu Kiwanja cha Ndege cha Chato ndiyo kinaunganisha mikoa karibia mitatu ikiwemo Kigoma, Shinyanga kwa maana ya Kahama, hapo wanakuja kupandia Ndege pale kwetu, lakini wako Kagera wanakuja kupandia Ndege kwenye Uwanja wa Chato pamoja na Geita yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunazungumzia Uwanja wa Ndege wa Mwanza. Ninaomba na mimi niungane na Wabunge wa Mwanza wanaozungumzia Uwanja huu wa Mwanza. Uwanja wa Mwanza ni Uwanja ambao umekuwepo katika viwanja vitatu muhimu vya nchi hii katika majiji matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanza ni sehemu ya majiji matatu muhimu katika nchi hii, na katika Kanda yetu ya Ziwa Victoria, lakini mpaka leo ukifika pale unazidiwa Uwanja ule na viwanja ambavyo vimejengwa kwenye Wilaya mbalimbali huko siyo kama unatoka kwenye jiji. Pale kulianzishwa jengo kubwa la abiria lakini limeenda likafika mahali likatelekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunapozungumza kwamba Wizara imetenga shilingi bilioni sita za kwenda kujenga pale, mimi ninaomba niungane na Wizara kuwapongeza kwamba sasa imefika wakati wa kuhakikisha kiwanja hiki kimejengwa, lakini kimepandishwa hadhi na kuwa ni kiwanja cha Kimataifa kwa maana ya kanda ya kule ambako tunatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, niungane na Wizara kwa sababu tumesema tutakwenda kujenga viwanja kila mahali; kujenga Uwanja wa Serengeti, ni wakati wake mwafaka wa kuendelea kuujenga pia na haijazuia hata kama tungelikuwa na viwanja vya Kimataifa 30 kwenye nchi yetu, hakuna atakayetuuliza. Kwa hiyo, tukijenga Uwanja wa Kimataifa pale Serengeti ni sawa, lakini Mwanza ni lazima ubadilike sasa ukawe ni Uwanja wa Kimataifa ambao utakuwepo hapo kanda ya ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kabla hujaenda la pili, muda umeisha naomba uunge mkono hoja.

**MHE. CORNEL L. MAGEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi ninaomba niunge mkono hoja, lakini Uwanja wa Ndege wa Chato unahitaji kupata ndege. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Nabil Ahmed Abdallah, Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ng'anzi Ulenge atafuatia, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga ajiandae.

**MHE. NABIL AHMED ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia katika Wizara hii ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya katika mageuzi makubwa katika nchi yetu. Nijielekeze kwenye hoja ya Bandari, hapa juzi juzi Mheshimiwa Rais alizindua mapipa 15 Kigamboni ya kuhifadhia mafuta yenye uwezo wa kuhifadhi *metric tonnes* 357,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale mapipa yakikamilika, yatakuwa na faida mbili; ya kwanza, tutakuwa na uwezo mkubwa wa kuhifadhi mafuta kwa muda mrefu, na jambo la pili, itasaidia kukabiliana na changamoto ya kupanda na kushuka kwa bei ya mafuta.

*(Hapa kengele ya kuashiria hatari ililia)*

**MWENYEKITI:** Hiyo ni *sign* ya *emergency*, lakini ninaomba tutulie. Ninaomba tu-*evacuate the building!*

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walianza kutoka Ukumbini kufuatia maelekezo ya Mwenyekiti)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, nimeambiwa kulikuwa na *error*. Ninaomba tutulie, ninaomba tutulie!

**MBUNGE FULANI:** Waheshimiwa tukae.

**MWENYEKITI:** Ninaomba tutulie, mchangiaji endelea.

**MHE. NABIL AHMED ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nishauri pia *TPA* na Serikali iangalie namna ya kutoa nafasi au fursa katika sekta binafsi kushiriki katika ujenzi wa matenki haya katika Bandari ya Tanga na Mtwara. Faida zake ni kwamba itaongeza wigo katika Serikali katika kuhudumia mikoa na kanda zote nchini, na pili, itatoa nafasi katika sekta binafsi kushiriki kwenye ujenzi wa uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ninaomba nizungumzie suala la kuhudumia makasha. Bandari ya Dar es Salaam imezidiwa. Tulikuwa tunabeza uwekezaji wa *DP World* katika Bandari ya Dar es Salaam, lakini sasa hivi hakuna pa kukanyaga. Sisi kama Kamati ya Miundombinu tulitembelea Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam kuna *ICD* 14 zote zimejaa. Ukiangalia Jefag, Galco na *Azam ICD* mizigo imejaa. *Verification* ya kontena inachukua mpaka wiki mbili kutoa kontena. Tulikuwa tunashauri, kama tuna Bandari ya Kwala, kwa nini mizigo ya *transit* yote ambayo inajulikana kwa sababu makontena yana namba, isomwe *BL* namba, makontena ya *transit* yote yapelekwe Kwala ili magari ya *transit* ambayo yanakuja Dar es Salaam kuongeza msongamano, yapungue, yaishie Kwala, kubebwa kwenda katika nchi jirani za *DRC*, Zambia, Congo, Rwanda na Burundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nizungumzie suala la umeme. Bandari yetu ya Dar es Salaam inatumia umeme takribani matumizi ya mkoa mzima wa Dar es Salaam. Kwa nini tusitumie mfumo wa *IPP (Independent Power Production)* kukawa kuna chanzo chake pekee kizalishe kiweze kupeleka kwenye Bandari ili tuweze kupunguza gharama za mitambo ile kutumia mafuta? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa wapi? Mheshimiwa Makamba.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Pamoja na mchango mzuri wa Mheshimiwa Mbunge ninaomba kumpa taarifa kwamba Wizara ya Nishati imetenga miradi yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 4.8 ambayo itatekelezwa kwa njia ya kuzihusisha *private sector,* na ukiacha hilo, kwa sasa hivi tumerahisisha sana. Tunayo *model power purchase agreement* na *model implementation agreement* ambayo tayari inasaidia kufupisha muda kwa ajili ya wawekezaji binafsi kuingia mkataba na *TANESCO* au Wizara ya Nishati ili kuweza kushiriki katika ujenzi wa miradi ya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimtoe wasiwasi na kama wapo wawekezaji, tunawakaribisha Serikalini kwa sababu bila wao hatuwezi kufikia lengo la kuzalisha *megawatt* 8,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nabil unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. NABIL AHMED ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea na ninashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Endelea.

**MHE. NABIL AHMED ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ninaomba kuzungumzia suala la *bulk cargo*. Tuna viwanda vya ngano Dar es Salaam vya kampuni ya Bakhresa (kampuni ya Azam) wanaagiza ngano kwa *bulk,* lakini mpaka leo tunashusha ngano kwa mfumo wa kizamani. Tunachota kwenye meli, tunaingiza kwenye *hopper*, magari yanapakia yanaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri tuwawezeshe *TPA* au waweze kutengeneza mfumo wa kisasa wa *suction effect,* kwamba yanaingia mabomba, yanafanya *suction,* ile ngano inaondolewa kwenye meli. Badala ya meli kukaa wiki mbili, au wiki tatu, itakuwa inakaa siku tatu, au nne kwa ajili ya uondoa ngano hiyo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, muda umeisha Mheshimiwa Nabil.

**MHE. NABIL AHMED ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimwite Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge atafuatiwa na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Shayo, ajiandae.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote, ninamshukuru Mungu Mwenye Enzi na Utukufu kwa kuniwezesha kusimama mahali hapa jioni ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali kwa ufanisi mkubwa katika sekta hii ya uchukuzi na mafanikio mbalimbali kama ambavyo yameelezwa na Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake. Ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake pamoja na watendaji kwa mafanikio hayo makubwa pamoja na tija na ufanisi ambao umeelezwa na Kamati ya Miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizungumzia ufanisi na mafanikio yanayopatikana kwa kumweka mwendeshaji binafsi Bandari ya Dar es Salaam tukumbuke jambo moja ambalo ni mafanikio makubwa yamefanyika. Maana, kuwa na mwendeshaji binafsi ni jambo moja, lakini kuweza kumsimamia mwendeshaji binafsi, ni jambo la pili. Hapa ninataka kuzungumzia mfumo wa *TMS (Terminal Monitoring Solution)*, ambao umetengenezwa na wana-*TEHAMA*, wana-*ICT* wa ndani ya Mamlaka ya Bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri tuka-*recognize* uwezo wa vijana hawa wa ndani ya Mamlaka ya Bandari ambao wamewezesha kutengeneza mfumo ambao una *function* nyingi. Mfumo huo huo unaweza kumsimamia mwekezaji ambaye ni mwendeshaji binafsi, mfumo huo huo unaweza ku-*track* namna

ya utekelezaji wa mkataba, mfumo huo huo unaweza kukusanya tozo ya *wharfage*. Tunapozungumzia mafanikio kwenye tozo ya *wharfage,* hatuwezi kuwaacha mbali vijana hawa wataalamu wa ndani wa *TEHAMA* wa Mamlaka ya Bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi wananunua mifumo kutoka nje ya nchi, lakini vijana wa Kitanzania wameweza kutengeneza mfumo mzuri kabisa. Inabidi tutambue uwezo huu wa ndani na tuweze kuuimarisha kwa maendeleo endelevu wa Bandari zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amezungumza vizuri suala la kutumia mifumo ya *TEHAMA* lakini mfumo huu *specifically* ni lazima tuu-*recognize* uwezo wake wa kukusanya tozo kama vile *wharfage* na kuweza kumsimamia mwendeshaji yule binafsi kwa maana hata zile *performance indicator* zinaweza kuonekana ndani ya mfumo ule. Kwa hiyo, ni mfumo mzuri sana ambao kiukweli vijana wale wa Kitanzania walioutengeneza wanapaswa kuongezewa uwezo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema kwenye malengo, Waziri ameeleza kwamba wanao mpango wa kuimarisha mifumo ya kiutendaji, mfumo mmojawapo ni huu. Vijana hawa waongezewe nguvu na uwezo wa kwenda kuimarisha mfumo huu uweze kudhibiti *attacks* zile, mashambulio mbalimbali ili kuweza kuwa *sustainable* zaidi. Tutambue uwezo wa vijana wa Kitanzania, lakini tuwajengee uwezo zaidi vijana hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuzungumzia suala la Bandari ya Tanga. Sisi wananchi wa Tanga tunafahamu maumivu ya kina cha Bandari kupungua. Ni muda mrefu Bandari ya Tanga ilikuwa haijiendeshi kwa faida mpaka pale ambapo Serikali ilikwenda kuingiza zile fedha shilingi bilioni 429 kwa ajili ya kuongeza kina. Tunatamani Serikali isiishie tu kuweka fedha hizi Bandari ya Tanga, lakini ituambie sababu ya kwa nini kina cha Bandari ya Tanga kilipungua? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, waje na *solutions* ya kwa nini kina cha Bandari ya Tanga kiendelee kuwa *sustainable*? Tunatamani hii tafiti ifanyike. Jambo hili ninalizungumza zaidi ya mara ya tatu ndani ya Bunge hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ulenge, muda wako umeisha.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimwite Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga atafuatiwa na Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Shayo.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kwa maono makubwa na uwekezaji mkubwa ambao ameufanya kwa ajili ya ujenzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote, pamoja na viongozi wote wa taasisi zilizoko chini ya Wizara hii. Wanafanya kazi nzuri sana ndiyo maana tunaona matunda mazuri. Hongereni sana. Pia, ninapongeza pia kupata maoni mazuri kutoka kwenye Kamati yetu ya Miundombinu, imeleta maoni mazuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za uchukuzi na usafirishaji kama Mheshimiwa Waziri alivyoeleza zimesaidia sana katika kuboresha biashara hapa nchini na kuhakikisha bidhaa zinafika kwa walaji pamoja na kutengeneza ajira, kujenga uchumi na kuleta fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1963 mpaka 1965 nafikiri Waziri Mkuu wa Singapore alipoingia madarakani na wakati anataka kuiendeleza Singapore aliwauliza wataalamu, akasema, Singapore ina nini ili iweze kuendelea? Wakamwambia kwamba Singapore haina maliasili, haina ardhi, haina madini isipokuwa ina

bahari na ina watu. Aliamua kutumia vigezo hivyo kuiendeleza ile nchi. Mpaka leo Singapore ni nchi ya tatu mpaka ya tano duniani kiuchumi kutokana na uwekezaji mkubwa alioufanya kwenye Bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, ndiyo maana uwekezaji unaofanywa na Serikali katika kupanua Bandari ya Dar es Salaam uwekezaji kwenye Bandari ya Tanga, Bandari ya Mtwara na Bandari nyingine za kwenye maziwa, ni kitu muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri tuendelee kuwekeza zaidi lakini katika kuwekeza pale Dar es Salaam, tunahitaji na kupanua Bandari Kavu mbalimbali, nyingine zianzishwe ikiwemo Bandari Kavu ya Mpemba, Tunduma kwani ni muhimu sana. Hivyo basi, tunahitaji uwekezaji mkubwa pia kwenye *TAZARA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TAZARA* ndiyo itasafirisha mzigo, itatokanao Dar es Salaam, itaupeleka mpaka pale Tunduma na utaenda nchi za nje na tutafanya biashara. Tunaona uwekezaji wa Serikali uliofanywa kwenye Shirika la Ndege, tumefanya vizuri na watu wanasema Shirika la Ndege halifanyi vizuri. Mimi ninasema linafanya vizuri sana na tunahitaji kuongeza uwekezaji, tupate ndege zaidi ya 30 ili twende dunia nzima na Tanzania iwe sasa ni *hub* mahali ambapo tunaweza kupata fedha za kigeni na kujenga uchumi mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji fedha kwa ajili ya ujenzi wa *SGR*. *SGR* tumeona uwekezaji ambao umefanyika tunahitaji ikamilike ili iweze kuchangia katika uchumi wetu. Tunahitaji viwanja vya ndege vijengwe kila mahali, hakuna sababu ya kulumbana. Tunahitaji kila mahali viwanja vya ndege kwa sababu tutajenga uchumi mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza hayo, tuliamua hapa ndani ya Bunge, tukatunga sheria, tukaweka tozo. Tozo ya ujenzi wa reli *TRC Levy* tuliweka hapa, tukaweka tozo kwa ajili ya viwanja vya ndege ili kuendeleza viwanja vya ndege na maeneo mengine. Zile tozo haziendi kwenye taasisi hizi, ndiyo maana kuna

changamoto za uendeshaji. Fedha zote zinaingia kwenye mfuko mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifike mahali fedha za tozo tulizozifungia, tumezi-*ring fence*, ziende kwenye taasisi ili zikajenge uchumi, ili wakajenge viwanja, ili tukawekeze *SGR* ikajengwe, *TAZARA* ikajengwe na maeneo mengine tuweze kufanya biashara na mambo yaende vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, ninaunga mkono hoja, lakini mchango ni mzuri sana kwa sekta hii, na watendaji hongereni sana kwa kazi nzuri. Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Ninamwita sasa Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Shayo, Mheshimiwa Charles Mhando Njama atafuatia, na Mheshimiwa Aeshi Khalfan Hilaly ajiandae.

**MHE. IBRAHIM M. SHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii nami kuweza kuchangia Wizara hii ya Uchukuzi. Ninaomba kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa maono makubwa aliyoyaona katika nchi yetu na kuhakikisha kwamba bandari sasa hivi zinapanuliwa, viwanja vya ndege vinajengwa na kazi zinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kutokana na muda, ninaomba niende kwa haraka haraka. Kwa kweli nisirudie suala la bandari, tumeona *DP World* walivyobadilisha bandari, kazi zinaendelea…

*(Hapa kulitokea changamoto ya kipaza sauti)*

**MWENYEKITI:** Washa hatukusikii.

**MHE. IBRAHIM M. SHAYO:** *Hallow!*

**MWENYEKITI:** Endelea.

**MHE. IBRAHIM M. SHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maono mazuri ya Mheshimiwa Rais pamoja na Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema tu kwamba pale bandarini, pamoja na pongezi, turekebishe matatizo ambayo yako pale bandarini. Pale bandarini kwa kweli magari yanakuja kwa muda mrefu, mizigo inakuja kwa muda mrefu. Utakuta inakaa pale takribani wiki mbili, au wiki tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Wizara ijitahidi kutoa ile mizigo kwa wakati. Mizigo inakaa na watu wanachajiwa, badala ya mizigo ikikaa watu ndiyo wawa-*charge* nyie kuwakalishia mizigo yao, lakini Serikali inachelewesha mizigo ya wananchi na mizigo ile inapata *charge*. Ninawaomba sana Wizara ihakikishe mizigo ile inatoka kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, wapo wafanyabiashara wanalalamika kuhusu magari yao. Magari yale yanakuja pale, yanakaa wiki mbili na baadhi ya vipuli vinachukuliwa kwenye magari. Sasa ninaiomba Wizara ihakikishe kwamba magari yanapoingia bandarini, yahakikishe yanatoka kama yalivyowekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nichangie kuhusu Chuo cha *NIT*. Tumetembelea Chuo cha *NIT,* ni chuo kikubwa sana, kikubwa mno. Pale tumekuta vijana wanajifunza masuala ya ubaharia, na masuala ya urubani. Ukiangalia miundombinu ambayo Mheshimiwa Rais amewekeza pale, ziko ndege mbili zinakuja, zipo ndege za kufundishia pale. Kwa kweli chuo kile ni kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba tu Wizara itangaze kile chuo. Tumemsikia Baba Levo kwenye mitandao wakati anamwambia mwanaye, unataka kufanya nini? Mwanaye akamwambia nataka kuwa rubani. Akamwambia kwamba utakwenda kusomea ualimu kwa sababu sina hela za urubani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri Serikali kwamba vijana wetu wanaosomea urubani, sasa waende kupata mikopo kwa ajili ya kujifunzia urubani kama vile wanafunzi wengine wanaofaidika kwenye vyuo vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wameongelea kuhusu uwanja wa ndege, lakini niongelee Uwanja wa Ndege wa *Moshi Airport*. Kama kuna dhambi Wizara ambayo itakayoipata ni kutokuendeleza Uwanja wa *Moshi Airport*. Uwanja huu wa *Moshi Airport* umeanzishwa mwaka 1952 na ulitengenezwa na Malkia Elizabeth. Uwanja ule ulimsaidia sana Mwalimu Nyerere kwenye kutafuta Uhuru. Sasa uwanja ule unahitaji tu, mbali hata na abiria, ile historia, ile heshima ya ile historia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tuko salama kwenye Taifa letu kwa sababu ya ule uwanja, tuna kila sababu ya kuuenzi ule uwanja. Mbali na kuuenzi ule uwanja, ninaishukuru sana Serikali kwamba imewekeza pale zaidi ya 68%, zimebaki kama 32% tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkandarasi *Electronic* yuko pale ameingia, anadai *4.8 billion*. Tukimpa *4.8 billion,* anarudi *site* na kumalizia ile kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Moshi sasa imekua, ina vyuo vikuu vingi, Chuo cha Udaktari *KCMC*, Chuo cha Ushirika, Chuo cha Maliasili, viko viwanda vikubwa kama viwanda vya bia, viko viwanda vya sukari, *TPC*; *Bonite Bottlers*; tuna wageni wengi sana. Vilevile tuna mlima mkubwa Afrika, Mlima wa Kilimanjaro. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kuhakikisha kiwanja kile kinafanya kazi ili kukuza uchumi wa Taifa na uchumi wa Mkoa wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. IBRAHIM M. SHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie *LATRA* kidogo sana kwenye mafuta. *LATRA* hali ya mafuta nchini

ni ngumu na tunafahamu. Tatizo kubwa *LATRA,* ninawaomba, mafuta yanabebwa na magari, na magari yale yanayobeba mafuta yanahitaji mafuta. Ninawaomba waende wakarekebishe bei ya mafuta kwenye magari yanayobeba mafuta…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. IBRAHIM M. SHAYO:** …ili kufanya mafuta yaweze kuwa katika sehemu zote za nchi yetu. Ahsante, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, ninashukuru kwa mchango wako. Ninamwita Mheshimiwa Charles Mhando Njama, atafuatiwa na Mheshimiwa Aeshi Hilaly.

**MHE. CHARLES M. NJAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nami ninaanza kwa kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa uwekezaji mkubwa alioufanya katika Wizara hii ya Uchukuzi kuanzia bandari, reli pamoja na viwanja vya ndege na ndege zenyewe. Uwekezaji huu ni mkubwa na umeenda kufungua uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na upande wa bandari, Bandari yetu ya Tanga imerudisha ule uchumi wetu wa Tanga wa zamani. Uwekezaji uliofanyika katika Bandari ya Tanga umeongeza ufanisi, meli zimeongezeka kutoka meli 170, sasa hivi tunaongelea karibia mieli 600 katika mwaka. Mzigo unaoingia umeongezeka kutoka tani 750 mpaka sasa tunaongelea karibia tani 600. Haya yote yanaonesha namna gani ufanisi umeongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio yanakuja na changamoto, mafanikio haya tuliyoyapata yameleta changamoto katika barabara yetu ya Tanga – Segera ambayo msongamano umekuwa ni mkubwa sana. Pia tunayo fursa kubwa ya kutumia Bandari Kavu ya Korogwe kwa ajili ya kuleta mzigo kuutoa kwa kupitishia reli badala ya kutumia barabara ya kutoka Tanga kuja Segera. Mzigo huu utatokea Korogwe sasa na

utakuwa ume-*decongest* barabara ya Tanga – Segera na itaongeza ufanisi zaidi katika Bandari yetu ya Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, anapokuja kuhitimisha, aseme neno kuhusiana na ujenzi wa Bandari Kavu Korogwe kwa sababu hii ilikuwa ni moja ya ahadi ya Mheshimiwa Rais wakati akihutubia wananchi wa Korogwe wakati wa kampeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona ufanisi mkubwa uliopo katika bandari baada ya kupewa tozo zinazotokana na *wharfage*. Vivyo hivyo, tumeona kwa taasisi nyingine kama *TPA* na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongelea uwekezaji katika miundombinu ya uchukuzi kwa maana ya reli pamoja na ndege pamoja na bandari zenyewe, tunaongelea ongezeko kubwa la ajira, viwanda, fursa mbalimbali za kiuchumi ikiwemo utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninashauri na ninaomba Mheshimiwa Mwenyekiti pamoja na Waziri wa Fedha, pamoja na Waziri wa Uchukuzi mwenyewe, waone namna gani zile tozo ambazo zinaenda moja kwa moja katika Mfuko Mkuu wa Serikali, zitolewe sasa ziende moja kwa moja katika mashirika haya ili ziweze kuleta ufanisi na kuboresha zaidi miundombinu ambayo imeshafanyika na kuendelea kuongeza mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tumewekeza karibia shilingi trilioni 30 na zaidi katika *SGR*. Tunahitaji kuendelea kuitunza *SGR*. Tunahitaji kuendelea kufanya *expansion* ya maeneo yaliyobakia. Haya tunaweza kwenda kuyafanya vizuri tukihakikisha kwamba zile tozo za *RDL* ambazo zipo kwa ajili ya *TRC*, zinaenda moja kwa moja katika Mfuko wa *TRC* ili waendelee kufanya uwekezaji na ku-*maintain* reli hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pasipo kufanya hivyo, kuna hatari uwekezaji mkubwa uliofanyika katika Shirika la Reli, tukaja kushindwa kuuendesha na tukaja kuchekwa zaidi na vizazi

vitakavyokuja baadaye. Kwa hiyo, ninaomba sana, tozo hizi zielekezwe moja kwa moja kwa *TRC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo, tunapoongelea upande wa *TAA*, tumeona namna ambavyo *Royal Tour* ya Mheshimiwa Rais ilivyoleta watalii wengi nchini. Tunahitaji kuelekeza sasa hizi tozo zinazohusiana na *TAA* ziende kwa watu wa *TAA* ili waweze kuboresha zaidi miundombinu inayohusiana na viwanja vya ndege pamoja na viwanja vilivyopo ikiwemo hata Kiwanja cha Ndege cha Mwanza kinachoendelea kusuasua. Kwa kutumia tozo hizi, tuna uwezo wa kwenda kukikamilisha kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ninamwita sasa Mheshimiwa Aeshi Khalfan Hilaly, atafuatiwa na Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, Mheshimiwa Mariam Said Khamis ajiandae. Tuendelee na anayefuata, Mheshimiwa Aeshi yupo kule.

**MHE. AESHI K. HILALY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwa hizi dakika tano ambazo ninaamini kwa Wizara kama hii tungepewa angalau hata dakika 10 au dakika 15, lakini tunaona sasa tunatoka kwenye dakika 10, tumekuja dakika tano, mwisho tutapewa kuchangia kwa dakika mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, lakini ninampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi kubwa na nzito wanayoifanya. Pia ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa ukamilishaji wa uwanja wetu wa Ndege ndani ya Jimbo letu la Sumwanga Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumwuliza tu Mheshimiwa Waziri, lini sasa uwanja ule utaanza kutumika rasmi? Je, ndege zitaanza kufika kwa muda gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ninataka kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, na hili ninaomba mnisikilize vizuri. Wengi hapa tumeusemea Uwanja wa Ndege wa Mwanza kwamba uboreshwe. Tumetenga shilingi bilioni sita zikaenda kukarabati uwanja. Ninataka kushauri kwamba tusiende kukarabati uwanja, twende tukajenge uwanja mpya wa kisasa ambao utakuwa ni uwanja wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuiangalie miaka 50 ijayo, miaka 100 ijayo ili uwanja uweze kutumika. Hili la kwenda kuvunja na kubomoa mwisho wa siku hata tukipeleka shilingi bilioni 30, ipo siku tutapata fedha tutakwenda kubomoa tuanze kujenga upya, tutapoteza fedha nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge mniunge mkono katika hoja hii ili sasa Mwanza uende ukajengwe uwanja mpya wa kisasa ambao pia utatumika na jirani zetu ambao wanatuzunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeuangalia Uwanja wa Ndege wa Mwanza, lakini ninaiongelea *SGR*. Tumewekeza fedha nyingi sana na hii *SGR* Mheshimiwa Waziri tutamwonea tukimwambia zile asilimia mbili akazirudishe. Ile ni kazi ya sisi Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge humu ndani tulipitisha, tukasema asilimia mbili ziende zikatengwe kwa ajili ya ujenzi wa reli. Sasa aliyetoa idhini ya zile hela kwenda maeneo mengine, ni nani? Inatakiwa sasa Wabunge tujiulize, na kama sheria imevunjwa, Bunge lina wajibu gani kwenda kufuatilia kujua kwa nini fedha hizi zimehamishwa kwenda kwenye mfuko mwingine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameongea Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na viwanja vya ndege, tunataka viwanja vijengwe, lakini na wenyewe tozo baada ya kupelekwa moja kwa moja kwenye taasisi husika, zinaenda kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Fedha hizi hazirudi kwa wakati na ndiyo maana leo hii Waheshimiwa Wabunge tumesifia bandari kwa sababu wamepata fedha. *Wharfage* imerudi ndiyo mnaona kuna

maendeleo. Basi na hizi taasisi nyingine zirudishiwe fedha zao ili ziweze kuleta maendeleo kwa kujenga miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kuongelea *Lake Tanganyika*. Mheshimiwa Waziri hapo atanisamehe kidogo, amesema uongo ndani ya Bunge. *Lake Tanganyika* hatuna meli hata moja mpya. Ninasema kwa ushahidi, hatujajengewa meli. Kule Kigoma tulitangaza tenda ya kujenga karakana ya meli, ninaamini ukamilishaji wa karakana ile ya meli ndiyo chanzo cha kujenga meli zetu mpya. Karakana ile tumepata mkandarasi, tumempa tenda, tumemlipa 15%, mpaka leo mwaka wa nne hakuna hata chuma kimoja kilichojengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunakuwa tunapitisha bajeti hapa kwamba tutajengewa meli, haipo huu ni mwaka wa saba, ninasimama kila siku hapa. Pia kule wananchi wengi wanakufa, wengi wanapoteza maisha yao na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa twende, ninaomba kidogo dakika moja nimalizie. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, atoe fedha amlipe mkandarasi ili karakana ile iweze kujengwa na meli zetu ziweze kujengwa kama ambavyo tuliwaahidi wananchi tutawajengea meli mbili za mizigo na meli mbili za abiria, lakini mpaka ninaposimama hapa, hatuna meli hata moja. Meli zilizopo kule ni meli za mchina, siyo za kwetu, na zimeandikwa kabisa *Gold Voyage* Kifaransa huko…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. AESHI K. HILALY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri akirudi hapa, ninaomba atusaidie, lini sasa meli za *Lake Tanganyika* zitaanza kujengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. Nayasubiri majibu ya Mheshimiwa Waziri, ninaweza nami nikashika shilingi hapo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ninamwita Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Said Khamis, Mheshimiwa Said Ali Mbarouk ajiandae.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kwanza ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambazo zinaendelea kwenye Wizara hii. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wasaidizi wake. Pia ninaendelea kumpongeza sana Mkurugenzi wa *TPA* pamoja na Mkurugenzi wa Reli kwa namna ambavyo wanaendesha mashirika haya. Hawa wawe *role model* kwa vijana ambao wanaaminiwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwanja wa Mwanza ni uwanja wa kiuchumi. Viwanda ambavyo vimejengwa Kanda ya Ziwa vinahitaji *International Airport.* Madini yanayochimbwa Kanda ya Ziwa yanahitaji *International Airport*. Kwa hiyo, kutoijenga, kutoikamilisha *Airport* ya Mwanza, ni kama ndege kupaa bila abiria. Ni hasara ya mwenye mali. Walikuja wakasaini mkataba wa shilingi bilioni 33, Mheshimiwa Waziri ni mwenyewe alishuhudia huo mkataba, leo mkandarasi ameondoka kazini, na leo mnatutengea shilingi bilioni sita, sisi Watanzania tunawaelewaje? Sisi wachumi ambao hatuna vyeti, tunawaelewaje wachumi wenye vyeti? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani tukawa tunatenga fedha kidogo kwa *Airport* ya Mwanza. Kwa nini tusitenge fedha za kukamilisha *Airport* ya Mwanza tukamaliza? Jengo la abiria lilikuwemo kwenye Ilani ya Mwaka 2020 – 2025 na limekuwemo kwenye Ilani ya 2025 – 2030, ina maana Serikali inakihujumu Chama cha Mapinduzi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafika mahali tunazungumza haya mambo kwa uchungu hata kama mtatuona sisi ni tofauti, lakini tunaisema haki, hamtutendei haki. Ninaomba kwenye kifungu hiki cha kukamilisha *Airport* ya Mwanza, kama hamtakuja na marekebisho, nitaondoka na shilingi, huo ndiyo ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili Mwanza ni *hub*. Mikoa ambayo inategemea *Airport* ya Mwanza ni mikoa mingi. Leo hatuna ndege ya kuja hapa, ndege ya Mwanza kuja Dodoma haipo. Walianza watu wa *Precision,* baadaye *ATC* nayo ikaanza, ikawaondoa watu wa *Precision*. Mnatupeleka wapi Watanzania? Kwa nini mnataka tutembee masaa manane bila sababu? Hapo tutakuza uchumi? Tunataka mtupe ndege ya kutoka Mwanza angalau mara tatu kwa wiki ili kukuza uchumi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watumishi wa Serikali wanaokuja hapa Makao Makuu ni wengi. Kila siku wanatumia mafuta, kila siku wanatumia tairi, kila siku ajali nazo zinaongoza. Wapumzisheni watumishi pamoja na viongozi na wafanyabiashara wapande ndege kuja hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana, hatuna sababu ya kuendelea Makao Makuu hapa halafu uwanja wa ndege. Jiji halina ndege ya kuja hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kama tunataka kukuza uchumi na uwezo wa Serikali, ndiyo huu tuliofikia, viwanja vya ndege vinatakiwa kujengwa kila mahali ili wawekezaji wasafiri wakati wote kufikia mahitaji yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, ninakushukuru. Ninamwita sasa Mheshimiwa Mariam Said Khamis, atafuatiwa na Mheshimiwa Said Ali Mbarouk.

**MHE. MARIAM SAID KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia fursa kwa mara ya kwanza kutoa mchango wangu kwenye Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninapenda kuchukua fursa hii kuungana na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye leo hii ameniwezesha kusimama katika Baraza lako Tukufu. Ninamwomba Mwenyezi Mungu azidi kunisaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchukua fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaifanya na sisi sote ni mashahidi, anaisimamia Tanzania kwa Taifa na maslahi makubwa ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nichukue fursa hii kumpongeza sana Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kazi kubwa anayoifanya Zanzibar, ni hakika ameleta mabadiliko makubwa na ametekeleza Ilani ya Chama chetu Cha Mapinduzi kwa 100%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijikite katika mchango wangu kama ifuatavyo: ninapenda niipongeze Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia *TRC*, *TRC* inaendelea na uendeshaji wa *SGR* katika usafirishaji wa abiria kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma. Kwa kweli *TRC* inafanya kazi kubwa sana mpaka sasa hivi (Julai mpaka Machi) takribani abiria 2,515,000 wamesafiri kwa kutumia usafiri wa *SGR*. Imefanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote ni mapenzi makubwa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha amekamilisha mradi huu na kuturahisishia wananchi wake usafiri wa haraka. Zamani tulipokuwa tunataka kuja Dodoma sisi kutoka Zanzibar lazima tunatumia siku mbili, lakini kwa mapenzi makubwa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan leo tunakuja Dodoma kwa siku moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nichukue fursa hii kumpongeza Waziri Mheshimiwa Profesa Mbarawa, Naibu Waziri na timu nzima ya Wizara ya Uchukuzi kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Kwenye bajeti leo, Waziri Mheshimiwa Profesa Mbarawa amesema kwamba kwa muda mfupi ambao sasa hivi Shirika tayari linajitegemea mishahara, pesa za *OC* na matumizi mengi; ninalipongeza sana Shirika la *TRC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi ambazo nimezitoa, ninashauri kama itawezekana kuweza kupatiwa usafiri

wa Dodoma kwa *SGR*. Tupate muda wa saa tatu, usafiri wa Dodoma kwenda Dar es Salaam kwa muda wa masaa matatu kama vile ambavyo tunavyotoka Dar es Salaam kuja Dodoma saa tatu kufika hapa tunafika *around* ya nane, ninaomba nishauri kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda vilevile nichukue fursa hii niipongeze *ATCL* kwa kuongeza vituo vya usafiri, hapo awali 2020/2021, vituo vya ndege vilikuwa 23, lakini ninaipongeza sana sasa hivi ina vituo 33. Kati ya vituo hivyo 33, vituo 16 vipo katika Nchi yetu ya Tanzania na vituo vitatu vya kimataifa na vituo 14 vipo kwa kanda. Ninalipongeza sana Shirika la *ATCL*…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako, ninaomba uunge mkono hoja…

**MHE. MARIAM SAID KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimwite sasa Said Ali Mbarouk atafuatiwa na Mheshimiwa Kafiti William Kafiti na Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza ajiandae.

**MHE. SAID ALI MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kutujalia na mimi kupata nafasi ndogo ya kuchangia Hotuba hii muhimu sana katika nchi yetu ya Wizara ya Uchukuzi. Wizara hii ni muhimu sana inagusa maisha ya watu wetu wote na ninashukuru kwa jitihada ambazo zinazofanywa za kuisimamia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuiomba Serikali isaidie Wizara, *paragraph* ya 21 ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba katika fedha aliyoiomba ya maendeleo hadi miezi tisa kapata 48.6%. Sasa hili ni tatizo na ninaomba Serikali iongeze umakini katika suala hili, vinginevyo yale ambayo yamepangwa yatakuwa hayaendi vizuri Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, tunahitaji pesa nyingi ili yale ambayo wananchi wanayazungumza na Wabunge

wanayazungumza yanahitaji yaweze kutekelezwa lakini kwa mpango huu wa chini ya 50% ya pesa ya maendeleo kwa kweli tutakuwa tunadai mambo ambayo kifedha Serikali haijawekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninazungumzia suala la bandari, tuangalie wenzetu Kenya wana bandari kubwa ya Mombasa, lakini pia wamewekeza bandari kubwa sana Lamu ambayo kwa kweli itaweza kufanya mambo makubwa. Mabilioni ya fedha wamewekeza pale, sasa sisi kama pesa ndogo ambayo Waziri ameomba na bado tu hata 50% haijafika, hili ni tatizo. Tunaomba kwa kweli Serikali ifanye kila linalowezekana kuongeza pesa katika Fungu la Maendeleo la Wizara hii ili Watanzania waweze kufaidika na yale ambayo yamezungumzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninaomba nilizungumze; nimwombe Mheshimiwa Waziri na timu yake asaidie kutekeleza ahadi ya Rais wa Muungano Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mwaka jana katika kampeni yake Pemba aliahidi kwamba atasaidiana na Mheshimiwa Dkt. Mwinyi kuhakikisha kwamba Bandari ya Asili ya Zamani ya Wete inajengwa na kwamba Serikali ya Mapinduzi tayari imeshafanya *feasibility study* na michoro ya bandari ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipouliza mwezi uliopita Zanzibar nikaambiwa wanasubiri fedha. Kwa hivyo, haitakuwa jambo la maana kwamba Mheshimiwa Rais ameahidi jambo, lakini watendaji wake, wasaidizi wake wakashindwa kuitekeleza ahadi yake itakuwa ni kumdhalilisha sana. Kwa hivyo, ninaomba sana katika hili Mheshimiwa Waziri atakapokuja aniambie mipango gani ameipanga ya kuona kwamba ahadi ya Mheshimiwa Rais anamsaidia kuitekeleza katika ujenzi wa Bandari ya Wete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninaomba nilizungumze ni suala la Shirika la Ndege, hili ni Shirika ambalo kwa kweli Serikali ime-*invest* pesa nyingi, lakini taarifa tulizonazo ni kwamba kila mwaka inapata hasara. Sasa hili jambo Mheshimiwa Waziri na Naibu wake waone ni namna gani watalisimamia Shirika

hili lipate faida badala ya kupata hasara kwa sababu fedha nyingi zimewekezwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo pia sisi Zanzibar ambao uchumi wetu ni wa huduma ya utalii tunategemea sana uimara wa Shirika hili ili liweze kwenda katika nchi ambazo watalii wa daraja la kwanza wanaweza kuchukuliwa wakaja Zanzibar. Huko mwanzo kulikuwa na ahadi kwamba Shirika hili litaweza kwenda katika Nchi nyingine za Ulaya kama Uingereza, Ujerumani na Ufaransa ambapo kuna utalii wa daraja la kwanza wanataka kuja Zanzibar, lakini kutokwenda…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. SAID ALI MBAROUK:** …mpaka leo kumesababisha kupata watalii wa daraja la chini. Kwa hivyo, ninaomba hili Waziri na wasaidizi wake walitekeleze…

**MWENYEKITI:** Ahsante, muda wako umekwisha.

**MHE. SAID ALI MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Kafiti William Kafiti atafuatiwa na Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza. *(Makofi)*

**MHE. KAFITI W. KAFITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Ilemela na Wabunge, sasa wanisikilize mwenye uwanja wake wa Mwanza ndiyo ninaongea sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunijalia afya njema. Pili, ninaomba niendelee kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuimarisha sekta hii ya uchukuzi ambayo ndiyo dira na tija kuu ya uchumi wetu wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme kwamba na kwa niaba ya Wabunge wote, wananchi wa Mkoa wa Mwanza na Jimbo la Ilemela leo tunasema tumechoka na ninaomba niseme leo ninaondoka na mshahara wa Waziri mpaka nitakapopata majibu mazuri ya Uwanja wa Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja huu umetajwa na Ilani tatu, umetajwa na Ilani ya nne, umetajwa na Ilani ya tano, umetajwa na Ilani ya sita. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tarehe 28 wakati anafunga kampeni aliahidi Uwanja wa Mwanza sasa unakwenda kuwa uwanja wa kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimwombe Waziri suala hili lizingatiwe, kwa nini tunasema Uwanja wa Kimataifa wa Mwanza? Ndugu zangu Wabunge tunahitaji uwanja huu kwa sababu zifuatazo: *issue* siyo kuwa na uwanja *issue* ni je, uwanja huo una tija katika eneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wa Mwanza na Kanda ya Ziwa 75% ya mapato ya *ATCL* yanachangiwa na Mkoa wa Mwanza, ndege zinazoruka kwa siku tunarusha zaidi ya *airbus* nne, nani humu anarusha *airbus* nne zaidi ya Mwanza? Kwa hiyo, niombe sana; Mwanza tunaongea leo kwa ukali kwa sababu sasa tumechoka, tunahitaji tuangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, Mwanza ndiyo *strategic hub* ya *economy* ya Kanda ya Ziwa na Maziwa Makuu. Leo Mwanza tukiongea eneo la uchukuzi sisi tuna *SGR* inakwenda kukamilika, kwenye upande wa maji tuna ziwa ambalo tuna Meli ya *MV Mwanza* tayari katika eneo la uchukuzi tuko vizuri, tuna *ATCL*. Tunachopungukiwa ni Uwanja wa Kimataifa wa Mkoa wa Mwanza.  Tunaomba hili liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunataka Uwanja wa Mwanza? Tunahitaji ukuzaji wa biashara katika Kanda ya Ziwa Victoria kwa sababu sisi *advantage* tuliyonayo kubwa kwanza tumezungukwa na nchi za kimkakati. Tumezungukwa na Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi, kwa nini tusiwe na Uwanja wa

Kimataifa na mikoa yote ya jirani ya Mkoa wa Mwanza, tunategemea Uwanja wa Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe hata ukiangalia eneo la utalii Mkoa wa Mwanza bado una fursa nzuri, tuangalie sasa takwimu zifuatazo: ukitoka Nairobi kwenda Mwanza ni kilometa 420, ukitoka *KIA* kuja Serengeti ni kilometa 420, lakini Mwanza – Serengeti ni kilometa 135, kwa nini tusitake Uwanja wa Kimataifa wa Mwanza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Mwanza na wananchi wa Ilemela tunayo fursa na tunayo haki sasa ya kupata uwanja huu. Kwa sababu uwanja huu ni fursa kubwa siyo tu kwa nchi na ukiangalia Mwanza ni *second largest* ya *collection* baada ya Dar es Salaam. Kwa hiyo Dar es Salaam ikitoka inafuata Mwanza zaidi ya 7.2% ya *GDP* inatoka Mwanza lakini pamoja na hayo zaidi ya trilioni 14 zimekuwa *collected* kutoka Mwanza… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. KAFITI W. KAFITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. KAFITI W. KAFITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MWENYEKITI:** Ahsante, muda wako umekwisha, unga mkono hoja.

**MHE. KAFITI W. KAFITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Agnesta Lambert Kaiza atafuatiwa na Mheshimiwa Saidi Salim Hamad, Mheshimiwa Ali Haidar Madeweya ajiandae.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi kwa uchache jioni ya leo niweze kuchangia machache katika hii Wizara ya Uchukuzi. Kwanza kabisa ninaomba niungane na wachangiaji wengine kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu nzima kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuleta tabasamu kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo nikiri kwamba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anafanya kazi nzuri sana kupitia hii Wizara ya Uchukuzi na hivyo ninampongeza sana. Kwa ajili ya muda leo nitajikita katika eneo moja tu na niseme leo Mheshimiwa Waziri kama sitapata maelezo yako mazuri kabisa kwa mara ya kwanza baba yangu nitakwenda kuondoka na shilingi yako leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakwenda kujikita katika ukurasa wa 199 mpaka ukurasa wa 200 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri ambapo ameongelea vema namna ambavyo wamejipanga kwenda kuhakikisha wanalipa fidia kwa wananchi ambao walipisha maeneo yao kwa ajili ya upanuzi wa viwanja vya ndege na jumla ya viwanja hivyo ni tisa. Hivi viwanja tisa deni ambalo Serikali inadaiwa lilikuwa ni shilingi 175,000,000,000 lakini mpaka sasa ninaongea kiasi cha shilingi 71,000,000,000 kimeshalipwa na hivyo deni kubakia shilingi 104,000,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri amesema kinagaubaga kwamba wametenga kiasi cha shilingi 10,000,000,000 tu kwa ajili ya kulipa fidia ya wananchi hawa. Hivi ninavyoongea pamoja na maeneo mengine hayo ya viwanja tisa na ukiangalia kiasi ambacho kimetengwa ni shilingi 10,000,000,000 tu wakati madeni ni shilingi 104,000,000,000. Niseme kwamba hatuko *serious* katika eneo hili. Hakika tuseme na tuambizane ukweli kwamba hii siyo dhamira kabisa ya Mheshimiwa Rais, hakuna namna ambavyo tunaweza tukatenga shilingi 10,000,000,000 *against* shilingi 104,000,000,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya hii shilingi 104,000,000,000 wananchi wa Kata ya Kipawa, Mtaa wa Kipunguni wanadai kiasi cha shilingi 72,000,000,000. Unaweza kuona kwamba karibu shilingi 32,000,000,000 tu ndizo zinazodaiwa na vile viwanja nane. Ni miaka 29 sasa wananchi wa Kipawa wamekuwa wakisubiri kwa ajili ya kulipwa fidia kiasi kwamba humu ndani tunao Waheshimiwa Wabunge ambao walikuwa hawajazaliwa Wananchi wa Kipunguni tayari walikuwa wanadai fidia hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Mbunge wa Jimbo la Segerea ambapo wananchi wa Kipunguni wamenituma kusimama kwa ajili ya changamoto zao, jioni ya leo ningependa kufahamu hiki kiasi cha shilingi 10,000,000,000 kinakwenda kulipa fidia wapi? Pamoja na kwamba ni kiasi kidogo nitapenda kufahamu kinaga ubaga kutoka kwa Waziri hizi shilingi 10,000,000,000 wanakwenda kuzigawa namna gani? Kwa sababu haiwezekani tukazipeleka maeneo mengine wakati kuna wananchi ambao wanadai kwa takribani miaka 29 na wengine wameshatangulia mbele za haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Mtaa ule wa Kipunguni ukifika pale utalia machozi, hakuna huduma zozote za kijamii, lakini hakuna huduma yoyote ya kiuchumi. Niseme wananchi wa Kipunguni wanatembea mwendo mrefu wa bodaboda kwa kulipa mpaka shilingi 5,000 kwenda kufuata kiberiti tu kwa sababu maeneo yale yote hakuna huduma zozote za jamii. Kwa heshima na taadhima na kwa nia njema hii ya Serikali na kwa sababu ninatambua dhamira njema ya Mheshimiwa Rais ya kuwaacha wananchi wakiwa na tabasamu… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnesta, ninaomba umalizie kwa ku…

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize kwa kusema wakati Mheshimiwa Waziri anakuja hapa ku-*wind up* anieleze, wananchi wa Kata ya Kipawa kutoka Mtaa wa Kipunguni ambao wamesubiri kwa takribani miaka 29 ni lini fidia yao italipwa na hii…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Saidi Salim Hamad, atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Haidar Madeweyya na Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo ajiandae.

**MHE. SAIDI SALIM HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Awali ya yote, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu na niupongeze uongozi wa hii Wizara ya Uchukuzi chini ya Waziri wetu Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa na Msaidizi wake Mheshimiwa Kihenzile. Kwa kweli Wizara hii wanaifanyia haki na wanafanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inamiliki vyuo mbalimbali miongoni mwa chuo ambacho inakimiliki ni Chuo chetu cha *NIT*. Chuo hiki kimeanzishwa mwaka 1975 mpaka sasa kina takribani miaka 50, siku hadi siku kimekuwa kiki-*undergo positive changes* lakini kwa kipekee kabisa katika Awamu hii ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kimeenda kupata mabadiliko ambayo ni ya kihistoria nayo ni kuanzisha kozi ya urubani ndani ya chuo hiki ambacho kinamilikiwa na Serikali hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa jumla ya wanafunzi ambao wanasomea urubani 22 wamekuwa *enrolled* pale na wanafunzi wawili kati ya hao wameshamaliza kozi ya awali ambayo ni *Private Pilot License* na leo walikuwepo hapa katika wageni ambao wamekuja kuorodheshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri sasa Wizara ya Uchukuzi kwa jitihada kubwa alizozifanya Mama Samia kwenye *NIT* hii ikae kitako na Wizara ya Elimu kuhakikisha kwamba wanafunzi wanaosomea urubani waweze kupatiwa mikopo na Bodi ya

Mikopo ili kila kijana wa Kitanzania ambaye ana sifa za kusomea urubani aweze kupata mkopo na kusomea urubani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo tu kwamba chuo cha *NIT* kinasomesha urubani, lakini kimewezeshwa na Serikali hii ya Awamu ya Sita kumiliki ndege mbili za *engine* moja ambazo wanafunzi wanazitumia kwa kufanyia *practical* juu ya kozi za urubani wanazosoma hapa. Kwa hiyo, wanapotoka chuoni hapa wapo vizuri *theoretical,* lakini vilevile kwenye *practical* kwa kuwa Serikali imekiwezesha chuo hiki kumiliki ndege mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, *ATCL* kwa kushirikiana na *NIT* imenunua *simulator* ambayo ni *full motion* yenye thamani ya shilingi bilioni saba. Kila mwaka kwa mujibu wa Sheria za Anga za Kimataifa *cabin crew* wanapaswa waende waka-*renew* leseni zao. Sisi hapa tunamiliki ndege yetu hii ya *787MAX* na tunawachukua *cabin crew* wetu wa Kitanzania tunawapeleka *South Africa* na *Ethiopia* kwenye kozi zao hizi ku-*renew* leseni zao kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya *ATCL* kukaa kitako na *NIT* kununua hii *simulator* ya kisasa kwa shilingi 7,000,000,000, vijana wa Kitanzania sasa hivi wanafanya kozi zao za ku-*renew* ndani ya nchi yetu hii, hapa hapa Tanzania. Hapa tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa jitihada yake hii, lakini kama haitoshi ninaishauri Wizara ya Uchukuzi tusitosheke tu na *cabin crew* wanaotokea *ATCL,* twende tukautangaze mtambo huu ambao tukonao *NIT* katika Nchi za jirani, Kenya, Uganda na Congo na hao wote waje wafanye kazi, waje wafanye leseni zao hizi katika chuo chetu cha...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. SAIDI SALIM HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ninamwita Mheshimiwa Ali Haidar Madeweyya.

**MHE. ALI HAIDAR MADEWEYYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu, *Subhana wataala,* kwa kunijaalia kuwa na afya njema na uhai. Ikiwa ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako Tukufu kuchangia hoja ya Serikali, Wizara ya Uchukuzi, ninachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuupiga mwingi, lakini pia, ni Mwenyekiti wetu wa Chama Cha Mapinduzi. Katika hili sina haya wala sioni vibaya, katika Wabunge wachache waliorejeshwa na Kamati Kuu na mimi nimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua pia fursa hii kumpongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Nchimbi na vilevile ninampongeza kaka yangu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, jembe, kwa kuchaguliwa na kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu. Hivyo hivyo kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Mheshimiwa Spika Azzan Zungu, *CEO*, pamoja na Wenyeviti wetu wa Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajielekeza moja kwa moja kwenye mchango wangu, nitagusia *TPA, TRC,* pamoja na *TAA*. Tukiangalia *TPA* inafanya vizuri na sitaki kuamini kama kaka yangu Mbossa, *DG* wa *TPA,* anashindwa kuibadilisha ile *baggage room* au *terminal passenger.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, *terminal passenger* ile, ambayo tunatumia sisi Watanzania, hususan Wazanzibari na wengineo, ni ya muda mrefu na ni chakavu toka mwaka 1950 au 1960 ilivyojengwa, kwa ajili ya kumpokea Malkia kwa shughuli za uhuru, haina hadhi kwa kiongozi wetu huyu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tunaomba sana, kaka yangu Mbossa ni mtu wa kufanya maajabu, kwenye *DP World* tumemshuhudia, aende akaibadilishe *terminal* hii ya *passenger,* kama wawekezaji hana wapo. Ni muda umefika kuelekea Mbweni au Msasani, tukajenge *terminal* mpya ya abiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninamshauri kaka yangu Mbossa, *DG,* kwa ruhusa yake; muda si mrefu tumeshuhudia kupanda kwa *wharfage*. Kwa kweli, *wharfage* imebadilika na imeongezeka kutoka asilimia tatu imekuwa tano, ukitumia Bandari ile ya *TPA* ya majahazi, lakini vilevile kuna mwekezaji amewekeza pale *DMI* zaidi ya shilingi bilioni 15, ni mzawa huyu, lakini vilevile analipa kodi ya shilingi milioni 140.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha maajabu leo hii mwekezaji huyu aliyewekeza *DMI* anatozwa *wharfage* ya dola nane. Jamani hiki kitu hakikubaliki, mwanafunzi hodari anapewa *incentive,* hebu waliangalie hili. Sitaki kuamini Mheshimiwa Profesa Mbarawa na timu yako kama atashindwa kuliangalia hili. Mzee wetu Mheshimiwa Ruto amesema, mwekezaji siyo lazima awe mzungu. Tujali wawekezaji wetu wazawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaelekea katika *issue* ya *TRC*. Labda niwakumbushe tu, ilipovunjika *East Africa*, iliporudi tena Mwaka 2001, Mzee Daniel Arap Moi, Benjamin Mkapa pamoja na Mzee Museveni walikaa na kukubaliana kwa kina hizi reli zetu tuziundie mifuko. Leo tunashangaa sana asilimia mbili ya Mfuko wa *TRC* ya *Tanzania Railway Development* inakuwa bado inang'ang'aniwa na Hazina! Si jambo la busara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niwaambie uwekezaji uliofanywa na Mheshimiwa Dkt. Mama Samia Suluhu Hassan wa shilingi bilioni 3.138 ni sawa na shilingi trilioni 8.15 kutoka Dar es Salaam – Makutopora. Tunatakiwa tuweke 25% ya miaka 20 ya *maintenance,* vinginevyo tutakuwa tunashabikia, hii reli itakuja kufa na tusije kuwalaumu watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, si kwa umuhimu; ninapenda kuishauri Serikali katika masuala ya viwanja vya ndege, *TAA* ni taasisi inayosimamia viwanja vya ndege. Tunaishukuru *TANAPA* kwa maono yake makubwa, ambayo wanafanya kuendeleza viwanja vya ndege kwenye utalii, lakini muda umefika sasa *TAA* wapewe *mandate* ya kusimamia wenyewe. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. ALI HAIDAR MADEWEYYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ninamwita sasa Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, atafuatiwa na Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde. Mheshimiwa Naibu Waziri David Kihenzile ajiandae.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Ninaanza kumpongeza sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana katika Sekta hii ya Uchukuzi na hasa lile la kuleta mwekezaji katika Bandari yetu ya Dar es Salaam, ambapo watu wengi walipinga, lakini sasa ninaamini wanamwelewa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, ninaomba nijikite kwenye hoja iliyopo mezani kuhusu ujenzi wa Reli ya Kusini. Yapo mambo kadhaa ambayo yanasababisha kuiomba Serikali yangu sikivu izingatie kwa umuhimu mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni, tathmini ya umuhimu wa Reli ya Kusini ulifanyika na Serikali ilijibu hapa kwamba, ina umuhimu mkubwa. La pili ni, usanifu wa kina tayari umefanyika. La tatu ni, ukarabati wa Bandari ya Mtwara, tayari Serikali ilitoa fedha shilingi bilioni 157. La nne ni, fidia kwa wananchi wa Ludewa, tayari Serikali imetoa fedha shilingi bilioni 15.4 ikiwa ni maandalizi ya Mradi mkubwa wa Kimkakati wa Liganga-Mchuchuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano ni, ujenzi wa bandari ya mizigo michafu inayojengwa kule Mtwara, kwetu Kisiwa Mgao, yenye thamani ya shilingi bilioni 434 umeanza na unaendelea vizuri. La sita ni, ujenzi wa *Mbamba Bay* kule Ziwa Nyasa umefikia

48%. La saba ni, uzalishaji wa chuma kwenye yale machimbo, tathmini ama utafiti unaonesha tani 106,000,000 zinaweza kupatikana kwa mwaka kwa eneo dogo lililofanyiwa upembuzi, lakini inaweza kuchimbwa kwa zaidi ya miaka 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la nane ni Ilani ya chama changu kikubwa sana, Chama Cha Mapinduzi, imeelekeza ujenzi wa Reli ya Kusini. Tunachohitaji hapa ni kuyaishi maono ya viongozi wetu wa Kitaifa. Tunahitaji kufungamanisha sasa ujenzi na ukarabati wa Bandari ya Mtwara, ujenzi wa Bandari ya *Mbamba Bay* na mradi mkubwa wa kimkakati wa Liganga-Mchuchuma ili uweze kusafirishwa kwa Reli ya Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninachoiomba Serikali ni kule nyuma ilionekana kuna *EPC+F,* ninadhani huko tusizungumze. Ninaiomba Serikali ifanye kila linalowezekana kutuambia ni kwa namna gani tunaweza tukaanza ujenzi wa Reli ya Kusini kwa kutafuta fedha ama mwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni ujenzi wa meli katika Mwambao wa Pwani, *along the coast line*, hii inazungumzia Bahari ya Hindi. Tunafahamu sote kwamba, sisi tunanufaika sana na matumizi ya meli zinazosafirisha mizigo na nyingi zimekuwa zikiingia. Leo Wabunge hapa wamesema, mafanikio yale ya mwekezaji wa *DP World* imefanya barabara na malori kuwe na *jam.* Hayo ni mafanikio makubwa sana ya kupigiwa makofi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaiomba Serikali kwa kuwa, hatujaanza kujenga meli zetu wenyewe kwenye Ukanda wa Pwani, tunajua kwenye Ziwa Victoria imejengwa, ni wakati muafaka wa kuanza kujenga hiyo meli, ili tuweze kuongeza mapato makubwa na ifungamanishe Tanzania, Msumbiji na Malawi ambako pia, kuna mizigo mikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ninamwita sasa Mheshimiwa Livingston Joseph Lusinde.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adhimu kabisa. Kwanza ninakupa taarifa tu kwamba, Dodoma Jiji ameifunga Yanga goli tatu kwa mbili na mpira umekwisha kwa hiyo, mpate taarifa hiyo. Tunawapongeza sana Timu ya Dodoma Jiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya taarifa hiyo nzuri, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri kabisa ya kusimamia Sekta ya Uchukuzi, yeye ndiye kiranja mkuu. Sambamba na hilo tunampongeza Waziri, Naibu Waziri na kama ilivyo ada, kuna wapishi ambao wanahangaika kutengeneza chakula pamoja na *menu* nzuri inayotengenezwa na Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, ambao ni vijana wazalendo *Engineer* Machibya kwa *TRC* pamoja na mwenzake *DG* Mbossa wa Bandari. Tuwapongeze sana vijana hawa wa Kitanzania kwa kazi kubwa ambayo wameifanya. Ni alama ya kutosha ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingi sana za Kitaifa zimetolewa na hapa watu waelewe kwamba, hii ni Wizara inayochangia kwenye Mfuko Mkuu wa Nchi karibu kwa 40% kwa hiyo, ni lazima Wabunge wawe wakali kwa kiwango ambacho wamezungumza. Jambo kubwa kuliko yote ni hii inaonesha kwamba, nchi iko kwenye joto la maendeleo ndiyo maana watu wengi wanaitaka Serikali ya Rais Samia isukume ujenzi wa viwanja vya ndege kwa *speed*, isukume ujenzi wa reli kwa *speed,* ili maendeleo sehemu zote yawe chanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaunga mkono kabisa watu wa Kanda ya Ziwa kwa Mwanza kupandishwa kuwa *International Air Port*. Ninataka niunge mkono bila ubishi kwa kujengwa kiwanja kipya kabisa cha Kimataifa pale Mugumu, Serengeti kwa sababu, nacho kile ni kiwanja cha mkakati ndugu zangu na kipo ndani ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa hapa na sisi tunaiomba Serikali sehemu zote, hata tuki-*google* humu kwenye

mitandao, taasisi kubwa kama bandari na reli hawatumii bajeti ya nchi kuendesha. Zipewe uhuru wa kukopa zenyewe, ili zipate pesa za kutosha ziweze kuendeleza miundombinu. Miundombinu hii ikijengwa ndugu zangu, wewe angalia Jiji la Mwanza namna wanavyohangaika kwenye ndege tu; ukipeleka ndege Mwanza dakika mbili imejaa, haina nafasi. Ukiwatengenezea Uwanja mkubwa pale wa Kimataifa uchumi wa nchi unakua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo siyo ya kubishana kikanda, ni ya Taifa, tunazungumzia uchumi wa Taifa zima la Tanzania. Taasisi hizi zikiimarishwa; ukiimarisha bandari sasa hivi inatema mzigo mwingi hauwezi kupita barabarani, tumeambiwa hapa. Yaani uwezo wao kwa sasa hivi ni maroli 110,000 ambayo yakijipanga barabarani mara moja yanatoka Dar es Salaam mpaka Singida! Sasa foleni hiyo utapitaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tusaidie mzigo mwingine uhamie kwenye reli. Mzigo ukihamia kwenye reli, tumeokoa na barabara. Ujenzi wa barabara utakuwa mdogo sababu, hazitaharibika kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunapongeza sana ujenzi wa Uwanja wa Msalato. Tumeona namna ambavyo Serikali inatujengea uwanja mkubwa, lakini tunataka *speed* ya kukamilisha hii miradi mikubwa. Kwa mfano reli, tusipowaruhusu hawa wakope wajiendeshe wenyewe, ujengaji utakuwa wa kusuasua mwisho wake itakuwa ya gharama kubwa. Hebu tuwape kwanza ile tozo yao, Sheria ya reli imetungwa siku nyingi, Mfuko wa Reli umewekwa siku nyingi, sisi ukakasi wetu unatoka wapi na kazi nzuri wanaifanya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuwaache hao waendelee kufanya kazi na bandari kavu zijengwe, ili ziifanye Bandari ya Dar es Salaam ipungue. Dodoma hapa tumependekeza bandari kavu ijengwe Bahi. Kuna bandari kavu ile ya Isaka, hizi zijengwe kwa *speed,* ili Bandari ya Dar es Salaam ipumue, watu wachukulie mizigo huku badala ya maroli yote kwenda Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako.

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. MWANAENZI HASSAN SULUHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ninakushukuru kwa nafasi. Ninapenda kuichangia Wizara hii ya Uchukuzi katika makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninapenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Tanzania kwa dhamira yake ya dhati ya kuendelea kuimarisha sekta ya uchukuzi nchini. Nimpongeze pia Waziri na Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za usafiri na usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka ya hivi karibuni tumeshuhudia maboresho makubwa ya miundombinu ya Uchukuzi nchini. Serikali imeendelea kuimarisha reli ya kisasa ya SGR, kupanua bandari, kuboresha viwanja vya ndege, pamoja na kuunganisha maeneo mbalimbali kwa mtandao wa barabara. Hatua hizi zimeongeza fursa za biashara, ajira na kukuza uchumi wa Taifa letu. Kwa kweli kazi inayofanywa na Serikali inastahiki pongezi kubwa mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo wa dhati kabisa ninapenda kuipongeza tena Serikali ya Tanzania kwa hatua kubwa iliyoendelea kuchukuliwa katika kuimarisha sekta ya anga nchini. Serikali imeendelea kuboresha viwanja vya ndege, kuongeza uwezo wa mashirika ya ndege na kufungua milango ya biashara, utalii pamoja na uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kuwa *Julius Nyerere International Airport* mwaka 2024 ilihudumia zaidi ya abiria milioni 2.8 pamoja na ndege zaidi ya safari 58,000 kwa

mwaka. Hii inaonesha wazi kuwa sekta ya anga inaendelea kukua na kuwa mhimili muhimu wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imeendelea kufanya uwekezaji mkubwa katika reli ya kisasa ya SGR inayounganisha maeneo ya kimkakati ya biashara na usafirishaji. Reli hiyo yenye urefu wa zaidi ya kilomita 541 kati ya Dar es Salaam na Dodoma imegharimu takribani dola bilioni 3.1 za Marekani, jambo linaloonesha dhamira ya Serikali katika kuboresha usafiri wa kisasa nchini. Hata hivyo, pamoja na mafanikio hayo, bado sekta ya anga inakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazohitaji hatua za haraka:-

(1) Baadhi ya viwanja vya ndege vya mikoani bado havina vifaa vya kisasa vya kutua ndege wakati wa mvua au ukungu;

(2) Gharama za usafiri wa anga bado ni kubwa kwa wananchi wengi;

(3) Baadhi ya maeneo yenye vivutio vya utalii bado hayana miundombinu ya kutosha ya anga; na

(4) Uhaba wa wataalam wa ndani katika sekta ya anga bado ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika baadhi ya viwanja vya ndege vya mikoani, safari huahirishwa kutokana na changamoto za vifaa vya mawasiliano na mifumo ya usalama wa anga, hali inayopunguza ufanisi wa huduma na kuathiri shughuli za biashara na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Suluhisho; ili kusawazisha hali hii, ninaiomba Serikali:

(1) Kuendelea kuboresha viwanja vya ndege vya mikoani kwa teknolojia za kisasa;

(2) Kupunguza gharama za huduma za anga ili wananchi wengi waweze kutumia usafiri huo;

(3) Kuongeza uwekezaji katika mafunzo ya wataalam wa anga nchini; na

(4) Kuimarisha ushirikiano kati ya sekta ya anga na utalii ili kuongeza mapato ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kuipongeza Serikali kwa maboresho makubwa yanayoendelea katika Bandari ya Dar es Salaam. Takwimu zinaonesha kuwa bandari hiyo inahudumia takribani 95% ya biashara ya kimataifa ya Tanzania na pia kuhudumia nchi jirani zisizo na bandari kama Zambia, Rwanda, Burundi, DRC, Malawi na Uganda. Zaidi ya hapo, Bandari ya Dar es Salaam ilifanikiwa kuhudumia tani milioni 27.7 za mizigo katika mwaka wa fedha 2024/2025, ikiwa ni ongezeko la 15% ukilinganisha na mwaka uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio haya yametokana na uwekezaji mkubwa wa Serikali, maboresho ya miundombinu pamoja na matumizi ya teknolojia ya kisasa bandarini. Hii ni ishara kuwa Tanzania inaendelea kuwa kitovu muhimu cha biashara katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Tanzania inaendelea kufungua milango ya uchumi kupitia anga, reli, bandari na barabara. Jukumu letu sasa siyo tu kupongeza mafanikio haya, bali kuhakikisha uwekezaji huu mkubwa unawanufaisha wananchi wa kawaida, vijana, wafanyabiashara na wakulima ili uchumi wa Taifa uweze kukua kwa usawa na ustawi wa wananchi wote.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono Hoja na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa mambo makubwa aliyoyafanya kwenye Wizara hii. Kuanzishwa kwa treni ya SGR na kuitoa Bandari ya Dar es Salaam kwa Mwekezaji ambaye ameleta maendeleo makubwa sana katika Bandari yetu ambayo mafanikio yako wazi kwa wananchi wa Temeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kweli yeye ni Waziri wa mfano, mwenye hekima na busara na mchapakazi hakika yeye ni kiungo kizuri katika jamii na uongozi. Mwenyezi Mungu ambariki na *Insha Allah* atampa fungu lake. Ninampongeza pia Naibu Waziri kijana imara, mwana mapinduzi imara kabisa. Ninampongeza Katibu Mkuu kwa kweli Profesa tunamwamini, ni mchapakazi, aendelee kutusaidia na kuisaidia nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza watendaji wote wa Wizara ya Uchukuzi, wanafanya kazi nzuri sana. Mungu awabariki wote kwa utendaji wao uliotukuka Mungu awabariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, *TRC* na Bandari hata Viwanja vya Ndege kule Yombo Vituka, ninaomba wasaidie Temeke, ni Jimbo ambalo lina umaskini mkubwa kwa wananchi wetu. Tuna changamoto kwenye elimu, afya na miundombinu ya barabara. Bado tuna upungufu mkubwa wa madawati watoto wanakaa chini kwenye sakafu. Ninaomba sana wadau wangu wanisaidie katika hayo na mengine. Ninawatakia kila la heri, wachape kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

**MHE. RAMADHANI H. SINGANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunipa fursa ya kuchangia kwa njia ya maandishi. Ninampongeza kwa dhati ya moyo wangu Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita, Dkt. Samia Suluhu Hassani kwa kuwa na mipango mizuri na endelevu kwa kila sekta nchini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi Profesa Makame Mbarawa Mnyaa, pamoja na Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa David Kihenzile. Kwa kuiongoza vizuri Wizara ya Uchukuzi. Hakika mipango yenu ni mizuri mno na yenye matumaini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninawapongeza watendaji wote wa Wizara kuanzia Katibu Mkuu hadi mtendaji wa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushauri na Maoni; ninapenda kutoa ushauri kwa Serikali yangu sikivu ya Awamu ya Sita kuhusu namna ya kuongeza ufanisi na kuleta tija katika utekelezaji wa majukumu ya Taasisi ya *LATRA* chini ya Wizara ya Uchukuzi ikishirikiana na *DART* chini ya Wizara ya TAMISEMI ili kuboresha usafiri wa umma Jijini Dar es Salaam. Taasisi hizi mbili zina mchango mkubwa katika maendeleo ya sekta ya usafiri nchini, hususan katika Jiji la Dar es Salaam ambalo lina ongezeko kubwa la watu na mahitaji ya usafiri wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ni muhimu kuelewa kuwa *LATRA* na *DART* zinafanya kazi zinazotegemeana kwa kiwango kikubwa. *DART* ina jukumu la kupanga njia *(route planning)* za usafiri wa Mabasi yaendayo kasi (au kama ilivyozoeleka, Mabasi ya Mwendokasi); kujenga miundombinu *(BRT infrastructures)* kwa maana ya barabara, vituo, karakana pamoja na mifumo ya kielektroniki ya kukusanya nauli; kusimamia utoaji wa huduma ya mabasi ya Mwendokasi *(Monitoring Bus Operations)* na kuhakikisha huduma za usafiri zinatolewa kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine, *LATRA* ndiyo mamlaka yenye jukumu la kutoa leseni kwa watoa huduma *(route licenses)*, kudhibiti huduma za usafiri wa umma mijini *(regulating public transportation)* zikiwemo huduma za daladala na mabasi ya mwendokasi, lakini vilevile *LATRA* ndiye mpangaji wa nauli za usafiri wa umma. Kutokana na majukumu hayo niliyoyaeleza, ni wazi kwamba Taasisi hizi mbili ni lazima zishirikiane kwa dhati kabisa katika kuleta tija na ufanisi wa usafiri wa umma jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa inayojitokeza ni ukosefu wa uratibu wa haraka kati ya taasisi hizi mbili. Mara nyingi *DART* inakuwa tayari kuanza huduma katika njia mpya za mwendo kasi, lakini *LATRA* inachelewa kutoa tamko rasmi la kuondoa daladala katika njia hizo. Matokeo yake ni mabasi ya mwendo kasi kukosa abiria wa kutosha, baadhi ya mabasi

kusimama bila kufanya kazi, Serikali kupata hasara ya uwekezaji mkubwa uliowekwa, pamoja na wananchi kuendelea kupata msongamano na mkanganyiko wa usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapendekeza, ili kuondoa changamoto hii, ninaiomba Serikali ichukue hatua zifuatazo ambazo zitasaidia kuongeza ufanisi na tija kwa Taifa:

(1) Kuanzishwa kwa Mfumo wa Pamoja wa Maamuzi *(Integrated Transport Coordination System)*; Serikali iunde mfumo wa pamoja wa uratibu kati ya *DART* na *LATRA* utakaojumuisha:

(i) Ratiba za pamoja za utekelezaji wa miradi;

(ii) Vikao vya lazima vya uratibu kabla ya uzinduzi wa njia mpya; na

(iii) Mfumo wa kidigitali wa kushirikishana taarifa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo hili litasaidia kuhakikisha kuwa mara DART inapokamilisha miundombinu, LATRA nayo tayari imetoa maamuzi ya kisheria kuhusu daladala na leseni za usafiri.

(2) Kutungwa kwa Sheria ya usafiri wa Umma mijini (Urban Mass Transport Act); Serikali iweke utaratibu wa kisheria unaoelekeza *DART* kutoa taarifa kwa muda muafaka kuhusu kuanza kwa *route* mpya na *LATRA* kufanya maamuzi ndani ya muda maalum kuondoa daladala kwenye *route* hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, siku 90 kabla ya uzinduzi wa njia mpya, *LATRA* itoe taarifa rasmi kuhusu daladala zitakazoondolewa au kubadilishiwa njia;

Mheshimiwa Mwenyekiti, waendesha daladala wapewe muda wa kujiandaa mapema ili kuondoa migogoro. Hali hii itaondoa ucheleweshaji unaosababisha hasara kwa Serikali na Wawekezaji, lakini pia ni usumbufu kwa wananchi.

(3) Kuanzishwa kwa Kitengo cha Pamoja cha Operesheni; Serikali ianzishe kitengo maalum kinachojumuisha wataalam kutoka *LATRA, DART*, Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani pamoja na TAMISEMI. Kitengo hiki kisimamie:

(a) Mabadiliko ya njia za usafiri;

(b) Uondoshaji wa daladala katika njia za *BRT*;

(c) Uondoshaji wa bajaji, bodaboda na vyombo visivyohusika kwenye barabara maalum za *BRT*;

(d) Usimamizi wa msongamano wa magari;

(e) Elimu kwa wananchi kuhusu mabadiliko ya huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii itasaidia maamuzi kutekelezwa kwa haraka na kwa ufanisi zaidi.

(4) Kutumia Teknolojia ya Kisasa ya Usafiri; Serikali iongeze matumizi ya mifumo ya TEHAMA kwa:

(a) Kufuatilia mabasi yote kwa GPS;

(b) Kusimamia muda wa safari;

(c) Kutangaza taarifa za huduma kwa wananchi kwa njia ya simu na mitandao;

(d) Kuunganisha mfumo wa DART na LATRA katika kituo kimoja cha taarifa;

(e) Teknolojia itasaidia kuongeza uwazi; na

(f) Kupunguza migogoro na kuboresha huduma kwa wananchi.

(5) Kulinda Uwekezaji wa Serikali; Serikali imewekeza fedha nyingi katika Mradi wa Mabasi Yaendayo Kasi. Ni muhimu

kuhakikisha mabasi haya yanatumika kikamilifu bila kukaa muda mrefu bila safari kutokana na ucheleweshaji wa maamuzi. Hivyo, ninaiomba Serikali:

(a) Kuwa na mpango wa dharura wa matumizi ya mabasi pale huduma mpya zinapochelewa;

(b) Kufanya tathmini ya kiuchumi kabla ya kuchelewesha maamuzi yoyote; na

(c) Kuwawajibisha watendaji wanaosababisha ucheleweshaji ucheleweshaji usio wa lazima.

(6) Ushirikishwaji wa Wadau wa Usafiri; Serikali ihakikishe wamiliki wa daladala, madereva, wananchi na viongozi wa maeneo wanashirikishwa mapema kabla ya mabadiliko ya njia. Hii itasaidia:

(a) Kupunguza migogoro;

(b) Kuongeza uelewa wa wananchi; na

(c) Kujenga ushirikiano badala ya malalamiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuhitimisha kuwa, *LATRA* na *DART* si taasisi zinazopaswa kufanya kazi kwa mashindano, bali kwa ushirikiano wa karibu kwa manufaa na maslahi mapana ya wananchi na Taifa la Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ikiboresha uratibu, matumizi ya teknolojia, uwajibikaji na mawasiliano kati ya taasisi hizi mbili, tutaongeza ufanisi wa usafiri wa umma, kupunguza foleni, kuongeza mapato ya Serikali na kuboresha maisha ya wananchi wa Dar es Salaam na Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. ADONIS A. BITEGEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania kwa uongozi mahiri na wenye maono uliowezesha mageuzi makubwa katika sekta ya uchukuzi. Ninawapongeza pia Waziri wa Uchukuzi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa sekta ya uchukuzi na sekta binafsi kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa ushauri ufuatao:-

(1) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iongeze kasi ya utekelezaji na ukamilishaji wa mradi wa kimkakati ikiwemo ukamilishaji wa miundombinu ya Bandari Kavu ya Kwala (Pwani) ili iweze kutoa huduma zote kikamilifu zilizotarajiwa na kupunguza msongamano katika Bandari ya Dar es Salaam. Ujenzi wa bandari hii umechukua muda kukamilika.

(2) Serikali iongeze kasi na kuanza ujenzi wa Uwanja wa Ndege mpya wa Kagera.

(3) Serikali *(ATC)* ianzishe safari za ndege kutoka Uwanja wa Ndege wa Dodoma kwenda mikoa mingine.

(4) Serikali iamishe umiliki/usimamizi wa ndege zinazotumiwa na *ATCL* kutoka Wakala wa Ndege za Serikali kutoka *TGFA* Kwenda *ATCL*. Pia iangalie namna nzuri ya uendeshaji wa *ATCL* (ikiwezekana kutumia makampuni/wataalam kutoka nje) ili iweze kujiendesha kwa faida.

(5) Serikali ipitie na kuweka vizuri mipaka ya majukumu ya *LATRA* na Jeshi la Polisi, Kikosi cha Usalama Barabarani hasa katika udhibiti wa vyombo vya moto.

(6) Katika kuwezesha bandari zetu ziwe shindani, uwekezaji wa Serikali uendane na kufanya mapitio ya utendaji wa watumishi wa umma wanaofanya katika bandari hizo ili kuongeza ufanisi wa utoaji mizigo.

(7) Kuimarisha mifumo ya TEHAMA/kanzidata ya taasisi zinazofanya kazi katika mipaka ikiwemo bandari na viwanja vya ndege ili iweze kusomana na kufanya kazi kwa ufanisi.

(8) Kuendelea kujenga uwezo wa wataalam wetu wa kusimamia miradi mikubwa kama Reli ya *Standard Gauge (SGR)* na *ATCL*. Wataalam wetu waendelee kujengewa uwezo katika teknolojia za kisasa katika sekta ya uchukuzi.

(9) Kupitia Sheria na Kanuni za uchukuzi na sekta mtambuka ili kuimarisha ufanisi wa sekta ya uchukuzi ili iwe shindani zaidi ya nchi jirani.

(10) Kusimika mashine za ukaguzi za kutosha mipakani ili kurahisisha ukaguzi wa mizigo mipakani.

(11) Ili kuendana na Dira ya 2050 ni vizuri Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi ikaja na mikakati na kuitekeleza kwa lengo la kuongeza ushirikishwaji zaidi wa sekta binafsi katika sekta ya uchukuzi. Uwekezaji huo wa sekta binafsi uendane na matumizi ya sayansi na teknolojia za kisasa. Maeneo ya *Peri-urban* na *rural areas* yapewe kipaumbele katika uwekezaji huo.

(12) Serikali iimarishe usimamizi wa vyombo vya usafiri katika maziwa na bahari kupunguza ajali.

(13) Itekeleze ujenzi wa bandari ndogo katika Mwalo wa Kyamkwikwi, Kata ya Izigo, Wilaya ya Mulaba, Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kuwepo kwenye kikao hiki muhimu cha kujadili na kutoa maoni yangu kwenye hotuba hii ya Wizara ya Uchukuzi. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote kwa kuandaa hotuba nzuri itakayokwenda kutekeleza yale yote yaliyoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali kwa maendeleo makubwa kwenye Mradi wa *SGR*, mradi huu umekuwa na tija kubwa hasa kwenye sekta ya usafirishaji kwa njia

ya reli, hotuba inasema awamu ya Dar–Dodoma–Mwanza imekamilika 100% na sasa inatumika kwa abiria na mizigo, kontena linafika Mwanza kutoka Dar es Salaam ndani ya masaa nane badala ya siku tatu kwa barabara. Bajeti 2026/2027 imetenga trilioni 1.8 kwa *SGR*. Kati ya hizo, Trilioni 1.1 ni kwa ujenzi wa awamu ya Mwanza–Isaka kilomita 341 na shilingi 700,000,000,000 ni kwa ununuzi wa mabehewa 1,200 na injini 20 mpya za umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo ni kuongeza uwezo wa kubeba mizigo kutoka milioni 1.2 hadi milioni 4.5 kwa mwaka. Ajira zimeongezeka. *TRC* imeajiri watu 3,800 wapya kwa ajili ya uendeshaji na matengenezo. Pia madereva 1,200 wa malori wamepata mafunzo ya kuendesha treni za umeme. Aidha, ushindani na malori umeanza. Barabara ya Morogoro–Dodoma imeshuhudia upungufu wa malori 1,800 kwa siku. Hii imepunguza ajali kwa 22% na kuongeza umadhubuti wa barabara zetu. Hata hivyo viwanda vinakaribia *SGR*. Viwanda 47 vipya vimejengwa kando ya njia ya *SGR* Dar es Salaam – Morogoro mwaka mmoja uliopita kwa sababu ya uhakika wa usafiri. Hii ndiyo dhamira ya viwanda vya Dira ya 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna changamoto mbalimbali kwenye mradi huu, kwanza, *SGR* haijaingia vijijini. Hotuba haijasema chochote kuhusu vituo vidogo vya mizigo vijijini. Kibaha Vijijini tuna viwanda na mashamba makubwa, lakini hatuna *siding*. Matokeo ni kwamba wakulima na wazalishaji bado wanategemea malori ghali kufikisha mizigo hadi kituo kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, usafiri wa mizigo usiku haujazinduliwa. Sasa *SGR* inafanya safari za mizigo mchana tu. Barabara bado inachukua malori 4,500 kwa siku usiku. Hotuba inapaswa kutangaza ratiba ya usiku ili kupunguza msongamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, nauli kwa wananchi wa kawaida bado ni kubwa, kwa maana hiyo ni nyingi kwa mwananchi wa kawaida. Hakuna mfumo wa punguzo kwa wanafunzi, wazee, na wagonjwa kama ilivyo reli za nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuishauri Serikali nini kifanyike 2026/2027 kuhusu *SGR*. Kwanza, wajenge kituo kimoja kidogo cha mizigo Mlandizi, kitakachogharimu shilingi 12,000,000,000. Hii itaondoa idadi ya malori barabarani na kuokoa uchumi shilingi 240,000,000,000 kwa mwaka. Pili, kuanzishwa safari za mizigo usiku kuanzia Oktoba, 2026. Lengo liwe malori 2,500 yaondolewe barabarani kwa siku. Hii itapunguza ajali kwa 30% na kuongeza maisha ya lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kuanzishwe nauli ya kijamii. Wanafunzi wapate punguzo 50%, wazee 30%. Serikali itoe ruzuku ya 80,000,000,000 kufidia pengo hilo. Hii itaongeza idadi ya abiria na kuifanya *SGR* ijitegemee haraka. Nne, kuunganishwa SGR na Bandari ya Bagamoyo. Hotuba inasema ujenzi wa Bagamoyo umeanza. Ni muhimu *SGR* iunganishwe moja kwa moja ili mizigo isipitie Dar es Salaam tena. Hii itafanya Tanzania iwe kitovu cha usafirishaji wa nchi zisizokuwa na bahari. *SGR* ni mradi sahihi na bajeti ya 2026/2027 imeonyesha dhamira nzuri kwa kutenga trilioni 1.8, lakini *SGR* haitasaidia uchumi kwa kasi kama itabaki kuwa mijini tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo Kidogo cha Mizigo Mlandizi na safari za usiku ni lazima kama tunataka viwanda vya Mlandizi na mazao ya Kibaha Vijijini yafike sokoni kwa gharama nafuu. Bila hayo, *SGR* itabaki kuwa treni ya abiria wa Dar es Salaam na Dodoma tu, wakati lengo kubwa ni kuondoa mzigo barabarani na kupunguza gharama za uzalishaji nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya mambo makubwa kwenye sekta hii ambayo ni nguzo ya kiuchumi. Tumeshuhudia uwekezaji mkubwa katika maeneo mbalimbali kama bandari, reli na kadhalika. Aidha, tumeshuhudia eneo la Bandari Kavu ya Kwala uwekezaji wa shilingi 80,000,000,000 za walipa kodi, ni fedha nyingi kwenye uwekezaji ambao tunategemea utupe matokeo chanya. Tuliahidiwa kuwa Kwala itakuwa suluhisho la msongamano wa Dar es Salaam na itapunguza gharama za usafirishaji kwa 40%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli mchungu ni huu, leo Mei 2026, miaka miwili na nusu tangu kuzinduliwa kwa majaribio, Kwala bado ni maegesho ya makontena. *SGR* inafika, lakini treni za mizigo hazifiki. Wafanyabiashara wa *DRC*, Rwanda, Burundi bado wanalilia Dar es Salaam kutoa mizigo yao na kupelekea dhana nzima ya kusudio la mradi huo kutokamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi usiofanya kazi ni dhambi kwa walipa kodi. Kila siku Kwala inakaa kimya, tunapoteza mapato. Tunapoteza ajira 3,000 zilizotabiriwa. Tunapoteza maisha ya wananchi wanaokufa kwa ajali za malori Chalinze – Kibaha kwa sababu mizigo haijapanda reli, tunasababisha msongamano wa malori njia kuu Dar es Salaam - Chalinze, ndoto ilikuwa nzuri mizigo ishuke Dar es Salaam, ipande *SGR*, ishukie Kwala, isambazwe nchi kavu. Ajali Chalinze zipungue na bei za bidhaa zishuke. Ili hali kwa kutumia bandari ya Kwala kwa kusafirisha mizigo na treni tungepunguza changamoto zote hizi. Leo hali ikoje? Kwala ni kimya. Treni moja ya mizigo kwa wiki siyo biashara, ni kejeli kwa walipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepoteza nini kwa kuchelewa? Kwanza, fedha; kila kontena linalokwama Dar es Salaam ni kodi inayopotea. Wataalam wanakadiria hasara ya zaidi ya shilingi 2,000,000,000 kila mwezi. Pili, maisha; malori 1,200 kwa siku bado yanapita Chalinze – Morogoro. Kila moja ni hatari ya ajali. Tatu, Imani; Mwekezaji wa *DRC* na wengine wanajiuliza kama kweli tuko *serious* kwenye uwekezaji huu ambao umetusaidia kukuza uchumi wetu na kutuongezea imani kwa wawekezaji wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua dhamira nzuri ya Serikali kwenye mradi huu ila ninaiomba Serikali mambo matatu wakati Waziri akihitisha aje na majibu. Kwanza, kabla ya bajeti hii kupita, Waziri ataje tarehe kamili ambapo Kwala itaanza kuhudumia treni tano za mizigo kwa siku. Pili, kiundwe kikosi kazi maalum, Kamati ya Wizara Tatu; Uchukuzi, Fedha na TRA. Wapewe siku 90 kuwasha Kwala. Wakishindwa, wawajibike. Tatu, Waziri alete Bungeni hesabu: Tumepoteza mapato kiasi gani tangu Disemba, 2023 mpaka leo kwa Kwala kutofanya kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo siyo majengo. Maendeleo ni majengo yanayofanya kazi. Kwala ifanye kazi au turudishiwe shilingi 80,000,000,000 zijenge *X-Ray* 160 za hospitali za wilaya. Ninaomba kuishauri Serikali namna gani tunaweza kutatua changamoto hizi, suluhisho lipo na ni rahisi, kwanza Serikali iamue Kwala ni dharura ya kiuchumi, ifungue masaa 24 na iunganishe mifumo ya *TRA* na Bandari ndani ya siku 30. Ipunguze tozo kwa miezi sita ya kwanza kuvutia wateja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufanya hivyo kutasaidia na kupelekea Kwala kufanya kazi na kuzalisha kiuchumi. Shilingi 80,000,000,000 zisitoe jasho bure. Kwala lazima ilipe deni lake kwa Taifa. Kama Mbunge wa Kibaha Vijijini, sitakaa kimya Mradi wa Kwala ukigeuka kuwa ukumbusho wa fedha zilizopotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

**MHE. REGINA H. MIKENZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha mchango wangu wa maandishi katika bajeti ya Wizara ya Uchukuzi. Nianze kwa kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuwekeza katika miundombinu ya uchukuzi yenye tija kwa uchumi wa Taifa letu. Leo, ninapenda kujielekeza katika suala moja muhimu kwa maendeleo ya Kanda ya Ziwa na Taifa kwa ujumla - Uwanja wa Ndege wa Chato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwanja wa Ndege wa Chato ni miundombinu ya kimkakati iliyojengwa kwa kuangalia mustakabali wa uchumi wa Taifa kwa miongo ijayo. Uwanja huu haukujengwa kwa ajili ya abiria pekee, bali kama kitovu cha uchumi *(economic hub)* kwa Mikoa ya Geita, Kagera, Kigoma na maeneo yote yanayozunguka Ziwa Victoria. Hata hivyo, pamoja na uwekezaji mkubwa uliofanyika, uwanja huu bado hautumiki ipasavyo kulingana na uwezo wake, fursa zilizopo na matarajio ya Taifa. Hili ndilo linahitaji mjadala wa kitaifa na hatua za makusudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fursa ya Kusafirisha Mazao ya Ziwa Victoria Ndani na Nje ya Nchi Ziwa Victoria; ni hazina ya Taifa

katika uzalishaji wa samaki. Kwa sasa, sehemu kubwa ya mazao haya husafirishwa kwa njia zisizo na ufanisi, jambo linalopunguza thamani ya bidhaa zetu katika masoko ya kimataifa. Uwanja wa Chato unaweza kuwa kitovu cha kimataifa cha kusafirisha mazao ya samaki *(fish export hub)* kwenda masoko ya Ulaya, Mashariki ya Kati na Asia. Hii itasaidia:-

(a) Kuongeza thamani ya mazao ya ziwa;

(b) Kuongeza ajira kwa vijana na wanawake; na

(c) Kuongeza mapato ya halmashauri na Taifa, lakini kwa sasa, hakuna mfumo wa mizigo, cold storage, wala miundombinu ya export logistics inayotumika kikamilifu, ndiyo maana ninasisitiza kuwa uwanja huu hautumiki ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fursa za Utalii: Rubondo Island na Chato, Burigi Wildlife Corridor. Uwanja wa Chato upo karibu na vivutio muhimu vya utalii:

(i) Kisiwa cha Rubondo – kivutio adimu duniani kwa ndege, sokwe na uvuvi wa michezo; na

(ii) Mbuga za Chato–Burigi – eneo lenye wanyamapori na mandhari ya kipekee. Kwa uwekezaji sahihi, Chato inaweza kuwa lango kuu la utalii wa Kanda ya Ziwa, kama ilivyo Kilimanjaro kwa Kanda ya Kaskazini, lakini hadi sasa, hakuna mkakati wa kuunganisha uwanja huu na sekta ya utalii, hivyo fursa hizi hazijatumika ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilimo, Mifugo na *Horticulture* – Fursa ya Usafirishaji wa Mazao Fresh. Mikoa ya Geita, Kagera na Kigoma ina ardhi yenye rutuba kwa: Matunda, mbogamboga *(horticulture)*, mazao ya ufugaji (nyama ya ng'ombe, mbuzi na kondoo). Uwanja wa Chato unaweza kuwa kituo cha kusafirisha mazao *fresh* kwenda masoko ya nje kwa ndege za mizigo. Hadi

sasa, hakuna ndege za mizigo zinazotumia uwanja huu na wakulima wetu hawajafaidika na fursa za kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wito kwa Wizara ya Uchukuzi: Kuufanya Chato *Airport* kuwa Kitovu cha Uchumi; ili uwanja huu utoe matokeo chanya kiuchumi, ninaomba Wizara ya Uchukuzi:

(i) Iongoze mjadala wa kitaifa Kuufanya Uwanja wa Chato kuwa *Economic & Logistics Hub* kwa Kanda ya Ziwa;

(ii) Ishirikiane na Wizara nyingine muhimu: Wizara ya Uwekezaji; Wizara ya Fedha; Wizara ya Kilimo; Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Maliasili na Utalii; na Wizara ya Madini; na

(iii) Iandae mpango maalum wa kuvutia wawekezaji katika sekta za: Usafirishaji wa mizigo na madini ya dhahabu; Viwanda vya kuchakata samaki; *Horticulture export*; Hoteli na utalii; *Logistics* na *warehousing;* na Chuo Cha Mafunzo ya Urushaji, Uongozaji na Ukarabati wa Ndege *(Aviation Training & Maintenance)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hitimisho; Uwanja wa Ndege wa Chato siyo mradi wa kawaida. Ni nguzo ya uchumi wa baadaye kwa Kanda ya Ziwa na Taifa, lakini ukweli ni kwamba hautumiki ipasavyo na hivyo hatujavuna matokeo ya uwekezaji huu mkubwa. Ninaiomba Wizara ya Uchukuzi iuchukulie uwanja huu kama mradi wa kimkakati wa Taifa na si wa mkoa mmoja na ichukue hatua za makusudi kuhakikisha unafanya kazi kwa kiwango kinacholingana na uwezo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ninamwita sasa Naibu Waziri, Mheshimiwa David Kihenzile. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili kutoa mchango

wangu kwenye hoja iliyowasilishwa leo na Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa Mnyaa. Pia, ninatumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu anayetupa uzima sisi sote kukutana hapa leo. Kipekee ninamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuniamini na kuniteua, ili niweze kumsaidia Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi kwenye nafasi ya Naibu Waziri wa Uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana pia Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kutuunga mkono kwenye Sekta hii nyeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa kutoa fedha mara kwa mara na hatimaye miradi mingi inakwenda vizuri. Ninawashukuru wasaidizi wakuu wa Mheshimiwa Rais, akiwemo Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, kwa jinsi wanavyoendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu na kusimamia sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa Mufindi siyo muda mrefu, akiwa amebeba begi la tabasamu ambalo amewaachia Wanamufindi, basi ninamshukuru sana pia, kwamba, Wanamufindi wanakumbuka begi lile na ahadi na maneno mazuri aliyowaachia. Wanamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia kwa jinsi anavyotekeleza tabasamu kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia nafasi hii pia kukushukuru, kumshukuru Mheshimiwa Spika, pamoja na viongozi wote. Naibu Spika, Wenyeviti, Kamati yangu, pamoja na Wabunge wenzangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upekee ninatumia nafasi hii kumshukuru Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa Mnyaa, kiongozi wetu wa Sekta ya Uchukuzi; baba mlezi, kiongozi mwenye maono, anayetusimamia sote vyema. Chini yake tunafanya kazi vizuri sana kwa utulivu mkubwa. Tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu ampe afya njema, ili aendelee kuisimamia sekta yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Profesa Kahyarara, watendaji wote walioko Makao Makuu ya Wizara, Wakurugenzi, Wenyeviti wa Bodi na Watumishi kwa ujumla. Kipekee, watumishi wenzangu kwenye Ofisi ya Naibu Waziri ambao kwa pamoja, tunafanya kazi hii ya kuweza kutoa huduma katika Sekta hii ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakishukuru Chama changu Cha Mapinduzi kwa ngazi zote. Uongozi wangu wa Mkoa, chini ya Mwenyekiti Mzee Yassini, Mwenyekiti, Mkuu wetu wa Mkoa, Viongozi wangu wa Wilaya, Viongozi wa Kata, Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM, wananchi wenzangu na wadau wote kwa kuendelea kuniamini na kunipa fursa kuendelea kuwa Mbunge wao, ili kuendelea kutimiza majukumu ya kuwahudumia Wanamufindi Kusini. Pia, ninaishukuru familia yangu kwa kuendelea kunisaidia katika majukumu haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunajadili hoja ya Sekta ya Uchukuzi, ambayo Mheshimiwa Waziri wetu ameiwasilisha vyema, karibu vitu vingi vimeshazungumzwa. Ninasimama kwa ajili ya kuongezea ama kufafanua tu kwa udogo, lakini hoja imewasilishwa vizuri na wote tumeweza kuielewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana Wabunge waliopata fursa ya kuchangia kwa maandishi, pamoja na kwa kusema. Wametimiza jukumu la msingi la Bunge hili kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu kwamba, Bunge hili lipo, kwa ajili ya kutunga Sheria, kuishauri na kuisimamia Serikali. Hongereni sana Wabunge wote kwa kusimama kidete kupigania maslahi ya wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niongelee eneo dogo la reli. Kama unavyofahamu, alipoingia madarakani mwaka 2021 Mheshimiwa Rais alikuta nchi yetu ikiwa na changamoto kubwa ya kiuchumi, ikiwa na fursa kubwa ya kujiendeleza, akaamua kuiendeleza Sekta ya Bandari. Wakati huo mzigo uliokuwa unakusanywa na Bandari ya Dar es Salaam ilikuwa ni tani milioni 16.6. Wakati huo hali ilivyokuwa kulikuwa na changamoto kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo mengi amefanya; mojawapo ni maboresho ya miradi na mbili ni pamoja na kushirikisha sekta binafsi, ili kuweza kutoa huduma. Leo ninavyozungumza kwa siku moja tunahudumia makontena karibu 4,000, wakati huo yalikuwa ni makontena karibu 1,500 hivyo, kwa mwaka inakwenda kuwa karibu makontena 1,300,000 kutoka kwenye makontena 700,000 yaliyokuwepo wakati ule. Matokeo yake ni nini? Utitiri wa bandari kavu, msongamano wa malori barabarani, pamoja na vitu vingine vingi. Ni nini Mheshimiwa Dkt. Samia anakifanya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Sekta ya Reli, ambayo inakusudiwa, kutarajiwa na kutegemewa itusaidie kwenye kupunguza msongamano Bandari yetu ya Dar es Salaam na bandari nyingine. Cha kwanza, Mheshimiwa Dkt. Samia anachokifanya kwa sasa, ni kuunganisha reli moja kwa moja kwenye bandari, iko 99% na hivi ninavyozungumza tunafanya majaribio. Ikikamilika inaweza kuanza kupunguza mzigo huo kwa takriban 20% mpaka 30% na hivyo kuifanya bandari yetu iweze kupumua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili ni, Mheshimiwa Dkt. Samia amewezesha kuanza kwa reli yetu kutoka Dar es Salaam – Morogoro mpaka Dodoma. Kipindi kifupi hiki abiria waliosafiri ni 5,510,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale abiria waliosafirishwa kwenye treni ni sawa na mabasi 150 barabarani kila siku, maana yake ni kwamba kwa *SGR* peke yake tumeondoa msongamano wa mabasi 150. Je, tukifika Kigoma itakuwaje? Je, tukifika Mwanza itakuwaje? Je, ikienda mpaka Arusha, mpaka Musoma itakuwaje? Je, tukiboresha ya *TAZARA* itakuwaje?Tuendelee kumwombea Dkt. Samia Suluhu Hassan ili ndoto hizi ziweze kutimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Dkt. Samia Suluhu Hassan ili kuiboresha Bandari yetu ya Dar es Salaam na bandari zingine na kuzijengea uwezo mkubwa, ameshatafuta fedha kuanzia Dodoma mpaka Makutupora na fedha zimepatikana.

Makutupora mpaka Mwanza mpaka Kigoma sasa hivi kazi iliyopo ni kuendelea kujenga ili zikamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ukiacha kwenye *SGR* kwenye upande wa reli zinazotoka Dar es Salaam mpaka Kapiri Mposhi - Zambia yenye urefu wa kilometa 1,860 ambayo Tanzania tunachukua 52%. Kwa kutambua kwamba Mwalimu Nyerere wakati huo na Dkt. Kaunda pamoja na Mao Zedong, walikuwa na dhamira ya kuiboresha Bandari yetu ya Dar es Salaam iweze kupitisha mzigo mkubwa zaidi ili ipitishe mzigo wa 5,000,000 na haikuwezekana mpaka mwaka jana, mwaka juzi tulikuwa tunaweza kufika asilimia nane mpaka 10% tu peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dkt. Samia Suluhu Hassan, amefanya mazungumzo na Wabunge wameuliza hapa ni lini itaanza, mkataba umeshasainiwa hatua ya kwanza imekamilika. Tumeshaanza kutoa taarifa kwa wafanyakazi na hivi ninavyozungumza maandalizi ya awali yanaendelea, ikiwezekana ndani ya miezi michache ijayo mwaka huu ukarabati huo uweze kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi trilioni 3.3 zimeelekezwa kwenye eneo hili, ikikamilika reli hii itatupa uwezo Watanzania wa kuhudumia nchi zote za upande wa *SADC*, itatupa uwezo Watanzania wa kuhudumia kipande chote cha Mikoa ya Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo reli ya *SGR* ikikamilika itatupa uwezo wa kuhudumia upande wa Mashariki kwa maana ya *East Africa Community* na nyingine ipo upande wa *SADC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi na kwa sababu mzigo unaotegemewa kuhudumiwa kwenye bandari yetu utakuwa ni mkubwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan hataki kuitupa reli ya *Meter Gauge* ambayo upana wake ni mita 1,000 anaendelea kuiboresha ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na namna mbalimbali za kuutoa mzigo bandarini.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona unaniangalia, umeniongezea dakika mbili?

**MWENYEKITI:** Malizia dakika moja.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa hoja ya Kusini ya Bandari ya kutoka Mtwara mpaka Mbamba Bay, imezungumzwa Kaskazini. Serikali imeshakamilisha upembuzi yakinifu pamoja na maandalizi ya awali, hatua inayofuata ili kutii Ilani ya CCM kama ilivyosema kwamba tutajenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu tunakwenda kutafuta wawekezaji, tunakwenda kutafuta wadau au fedha ili tujenge reli hiyo. Reli hizi zote zikikamilika tutakuwa na mtandao ukichukua 1,860 ya upande wa *cape gauge* ambayo ni *TAZARA*. 2,700 ya *meter gauge* pamoja na elfu nne karibu na 700 ya *SGR*, Tanzania inakwenda kuwa na reli karibu zote tatu na inaenda pengine kuwa reli ndefu kuliko zote kwa Bara la Afrika, ukitoa *cape gauge* ya Afrika Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wajibu wetu Watanzania ni nini? Kwanza ni kumwombea Dkt. Samia; Pili, kuombea amani ya nchi yetu kwa sababu pia maadui zetu wanatamani tufarakane ili miundombinu hii isiweze kuwa na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimwite sasa mtoa hoja aje ahitimishe hoja yake, Mheshimiwa Profesa Mnyaa Mbarawa.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninaomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kukutana katika Bunge hili Tukufu la Bajeti ili kukamilisha kazi tuliyoanza leo asubuhi ambapo niliwasilisha hoja yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kulisimamia, kwa kusimamia hoja hii vizuri mpaka hapo tulipofika. Aidha, nichukue fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa wawazi na kutoa michango yao ya kina wakati wa majadiliano hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwathibitishie kwamba michango yenu yote tunaichukua kwa uzito mkubwa na kwenda kuifanyia kazi ili kuendelea kuleta ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara na sekta ya uchukuzi kwa ujumla kwa maslahi mapana ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia kipekee nimshukuru Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso na Waheshimiwa Wabunge wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, kwa hoja nzuri zilizotolewa na Kamati yake. Ninakiri kwamba hoja hizo ni muhimu sana kwa maendeleo na ukuaji wa miundombinu na huduma za usafiri na usafirishaji hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutumia fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii ya bajeti ya Wizara ya Uchukuzi. Waheshimiwa Wabunge 27 wamechangia wakati wa majadiliano haya, ambapo Wabunge 24 wamechangia kwa kuongea na Wabunge watatu wamechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda mfupi uliopita Mheshimiwa Naibu Waziri, ameanza kujibu baadhi ya hoja hasa hoja zilizohusiana na masuala ya reli. Ninaomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba Wizara itajibu hoja zote kwa maandishi na kuziwasilisha Bungeni kabla ya kuhitimishwa kwa Mkutano Mkuu wa Bunge hili la bajeti unaoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa nianze kuhitimisha hoja yangu kwa kutoa ufafanuzi wa kijumla wa baadhi ya hoja zilizojitokeza kwenye maeneo makubwa yaliyojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ambayo kwanza ilijitokeza na imezungumzwa kwa hisia kali na kwa mtazamo tofauti ni hoja ya uwanja wa ndege wa Mwanza na Serengeti. Kwanza, ninaomba tufahamu kwamba Mwanza tunao uwanja wa ndege, Mwanza tunayo *runway* ya kupita ndege na ndege kubwa inakwenda, changamoto ya Mwanza kwa sasa ni jengo la abiria, hilo ndiyo changamoto kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaomba nianze kujibu hoja hizo kwa hatua. Ujenzi na maboresho wa viwanja vya ndege hivi vinatekelezwa kwa malengo tofauti na vyote ni muhimu kwa Taifa letu, hilo ninaomba walielewe. Uwanja wa Ndege wa Mwanza ni muhimu na Uwanja wa Ndege wa Serengeti ni muhimu. Kila uwanja wa ndege una malengo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu kutambua kwamba, Mwanza siyo mji wa utalii pekee, Mwanza ni kitovu cha biashara cha Kanda ya Ziwa. Ni lango la uchumi linalounganisha biashara za madini, viwanda, uvuvi, usafirishaji wa mizigo na masoko ya nchi za jirani. Hivyo basi, hata kama kutakuwa na mabadiliko katika mtiririko wa watalii, Mwanza *airport* itaendelea kuwa nguzo muhimu ya uchumi wa ukanda kutokana na nguvu yake katika mizigo na biashara. Kwa hivyo, ni lazima tujenge jengo la kisasa katika Uwanja wa Ndege wa Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, abiria kwenye uwanja wa ndege wa Mwanza wanaongezeka kila siku, hivi ninavyozungumza abiria 400,000 kwa mwaka wanakwenda kwenye uwanja wa ndege wa Mwanza, miaka miwili inayokuja tunategemea watafika abiria milioni 1.5 kwa vile kuna mahitaji makubwa ya kubadilika kujengwa jengo la kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapaswa kuangalia viwanja viwili hivi kama vinavyokamilishana badala ya kushindana. Viwanja vya ndege hivi havishindani. Serengeti inaweza kuwa lango maalum

la watalii wa kitaifa wanaokwenda kwenye hifadhi, wakati Mwanza ikabaki kuwa kitovu kikuu cha biashara, huduma na usafirishaji wa mizigo. Mfumo huu unaweza kuongeza ajira, mapato ya ndani na uwekezaji katika Mikoa yote ya Mwanza na Mkoa wa Mara kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwape *data* ndege zinazokwenda Serengeti kutoka Mwanza, Zanzibar na Arusha wakati wa *high season* (mwezi wa Disemba na Januari).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wastani wakati wa *high season* (kuanzia Disemba mpaka Januari) ndege 20 kwa siku zinatoka Arusha kwenda Serengeti na ndege hizo nyingine ni kubwa. Ndege 10 zinatoka Zanzibar kwenda Serengeti kwa siku. Ndege moja inatoka Mwanza kwenda Serengeti kwa siku, kwa ujumla ndege 31 zinatoka maeneo hayo kwa siku kwenda Serengeti. Kwa mtazamo huo ipo haja kujenga Kiwanja cha Ndege Serengeti, ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaonesha umuhimu wa maboresho ya Kiwanja cha Ndege cha Mwanza, kwa sababu Mwanza ni lango kubwa la biashara, pia ni muhimu sana kujenga Kiwanja cha Ndege cha Serengeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo sababu pia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuendelea kutekeleza mpango wa kimkakati wa kuboresha na kukipandisha hadhi Kiwanja cha Ndege cha Mwanza ili kiwe cha kimataifa kutokana na umuhimu wake wa kuimarisha uchumi wa Ukanda wa Ziwa. Hakuna suala lolote, Mwanza ni uwanja muhimu namba nne kwa Tanzania nzima na lazima tujenge jengo la kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe historia fupi ya jengo la Kiwanja cha Ndege cha Mwanza lililopo sasa hivi. Mwaka 2021 Halmashauri ilijenga jengo la abiria pale Mwanza lakini jengo lile lilijengwa kwa viwango vya chini sana ambavyo haviendani na kimataifa. Mwaka 2024, kwa mapenzi makubwa tulitafuta mkandarasi afanye maboresho ya jengo lile, lakini

alishindwa kufanya maboresho kutokana na viwango vya kimataifa. Tukaona sasa kuendelea na mkandarasi kujenga na jengo ambalo halitotupa hadhi ya kimataifa bora tutafute mkandarasi ajenge jengo jipya ambalo litakuwa na uwezo mkubwa wa kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu mkubwa ambao tunategemea kuujenga utakuwa na jengo jipya lenye uwezo wa kuchukua abiria milioni 2.5 kwa mwaka. Pili, tunaenda kufanya upanuzi wa njia ya kurukia na kutua ndege kutoka upana wa mita 45 hadi kufikia mita 60 ambapo ndege kubwa *Boeing* 777 - 747 na *Airbus* 350 zitaweza kuingia Mwanza. Tukifanya hivyo ndiyo tutafanya kiwanja cha Mwanza kitakuwa cha kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda pia kuweka mifumo ya kisasa ya taa, ambayo tunaenda kuweka *AGN* na *instrument landing system* ambayo itafanya siku yoyote ya Mwanza mchana, usiku kama kuna mvua, kama kuna ukungu, ndege inaweza kutua pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kujenga maeneo kwa ajili ya maegesho ya magari ambayo yatakuwa na uwezo wa kuhudumia magari mengi. Haya yote tunayafanya kwa sababu tunataka Uwanja wa Ndege wa Mwanza uwe uwanja wa ndege wa kimataifa, kwa sababu kule kuna biashara kubwa, kuna maendeleo makubwa na kule ndiyo kanda ya biashara ya kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtazamo huo tumeamua sasa kama nilivyosema utekelezaji wa mradi huo utafanywa kwa ubia kati ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii. Ni mradi mkubwa, mradi ambao utaleta mabadiliko makubwa sana kwenye Uwanja wa Ndege wa Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi Mwanza itaendelea kuwa lango kuu la biashara na usafirishaji wa Kanda ya Ziwa, hakuna wasiwasi lazima kupatikane jengo kubwa la abiria, pia Serengeti itabaki na itachukua nafasi yake kuwa lango kuu la

utalii wa kimataifa. Tunasema viwanja hivi havishindani, vinashirikiana. Kwa vile tunaenda kuvijenga vyote kwa wakati mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba baada ya kueleza hayo machache kuhusu Uwanja wa Ndege wa Serengeti pamoja na Mwanza, sasa ninaomba nianze kujibu hoja za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la Serikali ianze kutekeleza ahadi mpya kwa watumiaji wa bandari nchini (ada mpya kwa watumiaji wa bandari nchini) kuanzia tarehe Mosi Julai, mwaka huu. Kuongeza ada za bandari siyo adhabu kwa wananchi wala wafanyabiashara, bali ni hatua ya kimkakati ya kuimarisha uchumi wa Taifa na kuongeza uwezo wa nchi yetu kiushindani, kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato yatakayotokana na ada hizo yatasaidia kuboresha miundombinu ya bandari, kuongeza kina cha maji, kununua vifaa vya kisasa vya upakuaji na upakiaji wa mizigo, pamoja na kupunguza ucheleweshaji wa huduma katika Bandari ya Dar es Salaam na bandari nyingine. Bandari yenye ufanisi mkubwa huongeza biashara, huleta wawekezaji na kuongeza ajira kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la ada linaenda sambamba na ongezeko la utoaji wa huduma. Tunakwenda kuongeza ada, lakini vilevile tutaongeza huduma kwenye bandari zetu. Haiwezekani tukawa na bandari za kisasa zenye ushindani mkubwa huku tukabaki na viwango vya zamani vya mapato. Mataifa mengi duniani hufanya maboresho ya kimifumo kwa kuhakikisha Sekta ya Bandari inajiendesha kwa tija na kujitegemea kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii inalenga kulinda maslahi mapana ya Taifa letu. Bandari ni lango kuu la uchumi wetu, hivyo mapato yake yanapaswa kuchangia maendeleo ya reli, barabara na huduma nyingine muhimu zinazowanufaisha Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo tunapaswa kuhakikisha kuwa, ongezeko hilo halileti mzigo mkubwa kwa wananchi wa kawaida kupitia kupanda kwa gharama za bidhaa. Ni muhimu kuweka wazi, usimamizi madhubuti wa mapato pamoja na maboresho yanayoonekana ili wadau wanaotoa fedha yao waweze kupata thamani ya fedha yao kwenye bandari zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na *TPA* ilianza kutekeleza ada mpya bandari za mwambao wa Hindi kuanzia tarehe 8 Machi hadi kufikia mwezi Mei mwaka huu utekelezaji huo unaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa ada ya uendelezaji wa miundombinu mipya ya bandari, aidha kutokana na mapokeo tofauti ya ada ya uendelezaji miundombinu mipya ya bandari, miongoni mwa wadau na wateja wa bandari *TPA,* mnamo tarehe 9 Machi iliahirisha kuanza kutumika kwa ada hiyo hadi tarehe Mosi Julai, mwaka huu ili kutoa muda zaidi kwa wateja na wadau kujipanga na kujiandaa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili inasema Serikali ihakikishe inatekeleza kwa kasi maboresho ya miundombinu ya bandari ili kuhakikisha kuwa kasi ya ufanisi wa bandari inawiana na maendelezo hayo. Majibu ya hoja hiyo ni kwamba Wizara kwa kushirikiana na *TPA* imeandaa mpango mkakati wa miaka mitano, ambao unaanzia mwaka wa fedha 2026/2027 hadi mwaka wa fedha 2030/2031. Mpango huo umeainisha miradi mbalimbali ya kimkakati na ya kipaumbele itakayotekelezwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo kwa lengo la kuimarisha sekta ya uchukuzi na usafirishaji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi hiyo unatarajiwa kuongeza uwezo wa bandari nchini kutoka tani 30,000,000 za sasa hadi kufikia tani 62,000,000 ifikapo mwaka wa fedha 2030/2031. Hii itaendelea kuimarisha Tanzania kama lango kuu la biashara na usafirishaji katika ukanda wetu wa Afrika Mashariki na kati. Sambamba na kuongeza mapato ya Serikali, kuchochea ukuaji wa uchumi, kuvutia uwekezaji na kufungua fursa zaidi kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya tatu, Wizara na *TPA* ziendelee kukutana na wadau na watumiaji wa bandari mara kwa mara kwa ajili ya kutoa elimu kuhusu umuhimu wa ada hiyo. Majibu ya hoja hiyo, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Bandari Tanzania imeendelea na itaendelea kutekeleza programu maalum ya utoaji elimu kwa wadau kuhusu ada ya uendelezaji wa miundombinu mipya ya bandari. Lengo ni kuhakikisha wadau wanapata uelewa wa kina kuhusu umuhimu, madhumuni na manufaa ya utekelezaji wa ada hiyo kwa uchumi wa Taifa na maendeleo ya sekta ya usafiri na usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, programu hiyo inahusisha mikutano ya mashauriano na wateja pamoja na wadau mbalimbali wa sekta ya bandari, uchapishaji wa makala maalum katika vyombo vya habari pamoja na matumizi ya mitandao ya kijamii ili kufikisha elimu kwa umma kwa uwazi na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa programu hiyo ulianza tarehe 17 Machi, mwaka huu ambapo Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari ilikutana na wadau walio chini ya Tanzania *Private Sector Federation* linalojumuisha sekta mbalimbali za uzalishaji biashara na usafirishaji wakiwemo wazalishaji wa bidhaa za viwandani na wasafirishaji wa mizigo ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao hicho cha mashauriano Serikali, imeendelea kusikiliza maoni, ushauri na mapendekezo ya wadau mbalimbali kwa nia njema ya kuboresha zaidi mfumo wa utekelezaji wa ada ya uendelezaji wa miundombinu mipya ya bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni hayo yamewezesha kufanyika kwa maboresho muhimu yatakayohakikisha utekelezaji wa ada hiyo unakuwa rafiki zaidi, wenye tija kwa wadau na unaendana na mazingira halisi ya biashara na ushindani wa kikanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine iliyozungumzwa ni msongamano katika Bandari ya Dar es Salaam. Ili kuhakikisha bandari inaendelea kutoa huduma kwa ufanisi, ushindani na

viwango vinavyokidhi mahitaji yanayoongezeka, Serikali inaendelea kutekeleza hatua mbalimbali za kimkakati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye hotuba yangu hatua ya mwanzo ambayo tunaifanya ni kukamilisha ujenzi wa reli ya kisasa ya *SGR* inayoingia moja kwa moja bandarini, ambapo utekelezaji wake umefikia 99.7%, na majaribio ya usafirishaji wa mizigo yameanza hivi sasa. Sambamba na hilo, *TRC* inajenga eneo maalum *(loading platform)* na kupakulia mizigo kwenye treni hiyo kwa ajili ya kuondoa msongamano kwenye Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TRC* inategemea kupeleka treni ya *SGR* ambayo itakuwa na uwezo wa kubeba mabehewa 50 kwa wakati mmoja ambayo itakuwa na uwezo wa kuchukua kontena 100 kwa wakati mmoja. Reli hiyo ya *SGR* itafanya safari 10 kwa siku. Maana yake ni kwamba, itaweza kutoa angalau kontena 1,000 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Dar es Salaam tunavyoongea, kwa siku Bandari ya Dar es Salaam inatoa kontena 3,600. Tukiweza kutoa kontena 1,000, maana yake ni kwamba tumeondoa 50% ya mizigo yote ya makasha katika Bandari ya Dar es Salaam. Tunaamini tukifanya hivyo tutapunguza msongamano kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua nyingine tunayoifanya ni mfumo wa ratiba wa magari *(Truck Appointment System)*. Madereva wanapangiwa muda maalum wa kuingia bandarini ili kuepuka magari mengi kwa wakati mmoja ndani ya bandari. Hatua nyingine tunayoifanya, ambayo tunazungumza na Waziri wa Ujenzi, tunataka kuweka njia maalum ya malori ambayo itaweza kusaidia kupunguza msongamano hasa wakati wa usiku ambapo *traffic* katika Jiji la Dar es Salaam imepungua kwa asilimia kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo tunalifanya ni kuendelea na upanuzi wa eneo la Kurasini lenye ukubwa wa

mita za mraba 220,000 kwa ajili ya kuhudumia makasha 700,000 kwa mwaka. Awamu ya kwanza ya mradi huu inatarajiwa kukamilika mwezi Juni mwaka huu na awamu ya pili itakamilika mwezi Julai mwakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mkakati mwingine wa kuondoa msongamano kwenye Bandari ya Dar es Salaam kwa kujenga kituo cha kisasa cha mizigo katika Stesheni ya *SGR* ya Morogoro chenye ukubwa wa mita za mraba 68,000 na uwezo wa kuhudumia makasha 600 kwa siku kwa ajili ya kuhudumia mizigo inayosafirishwa Mikoa ya Iringa, Mbeya, Ruvuma na nchi za jirani. Tunaamini hii itapunguza sana msongamano kwenye Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Mradi wa Reli ya Kisasa ya *SGR* katika kipande cha tatu, tumekuja na mpango maalum, ambapo tunatarajia kujenga *ICD* kubwa pale Tabora kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Tabora. Tayari zipo zaidi ya hekari elfu moja zimetengwa kwa ajili ya kujenga kituo hicho cha kimkakati. Kituo hicho kitahudumia shehena za mizigo zinazoingia na kutoka katika Mikoa ya Tabora, Kigoma, Katavi pamoja na Nchi jirani za Burundi na DRC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati yote hii tunaifanya kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunaondoa msongamano kwenye Bandari ya Dar es Salaam ili Bandari ya Dar es Salaam iweze kufanya zaidi. *TRC* kwa kushirikiana na Serikali pia ina mpango wa kujenga vituo vingine vya mizigo katika maeneo ya Isaka Mkoani Shinyanga, Fela Mkoani Mwanza na Katoshi Mkoani Kigoma. Vituo hivyo vitasaidia kuhudumia shehena za mizigo kwa mikoa husika na maeneo ya jirani pamoja na Nchi za DRC, Burundi, Uganda na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala kuhusu sekta ndogo ya anga, kwamba, Serikali ifanye tathmini kuhusu *ATCL* kuanzisha safari za ndege kutoka Dodoma kwenda mikoa mingine moja kwa moja bila kupitia Dar es Salaam ili kukidhi mahitaji ya wananchi wanaohitaji huduma hiyo. Safari za ndege kuanzia Dodoma kwenda katika viwanja vingine vya ndani ya nchi vinatarajiwa kuanza mwaka wa fedha 2026/2027 baada ya *ATCL*

kuongeza ndege ndogo nne za aina ya *Dash 8-Q400*. Ndege hizo zitaongeza uwezo wa utoaji wa huduma ya usafiri wa anga ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala ambalo limezungumzwa kuhusu kasi ya ujenzi wa reli ya *SGR*. Serikali kupitia *TRC* imeendelea kuwasimamia wakandarasi wote wa Mradi wa *SGR* kwa vipande vyote kwa karibu kwa lengo la kuhakikisha Miradi ya Ujenzi wa Reli ya Kisasa ya *SGR* inatekelezwa na kukamilika kwa mujibu wa mikataba iliyosainiwa, sambamba na kuzingatia viwango vya ubora vinavyotakiwa ili kuwawezesha wananchi wetu kunufaika na huduma bora, salama na ya uhakika ya usafiri wa reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kimkakati kuhakikisha utekelezaji wa miradi hiyo unaendana kwa kasi inayokusudiwa. Kwa hivyo, mkandarasi mkuu wa kipande cha tatu (Yapi Merkezi) kutoka Makutupora mpaka Tabora na kipande cha nne, Tabora mpaka Isaka ameendelea kusisitizwa kuongeza kasi ya utekelezaji wa kazi ili kuhakikisha malengo yaliyowekwa yanafikiwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kwamba kasi ya utekelezaji inaongezeka katika vipande hivyo na vinakamilika ndani ya muda uliopangwa, Serikali ilimwelekeza mkandarasi mkuu (Yapi Merkezi) kushirikiana na wakandarasi wazabuni wengine yaani *subcontractors* kuwapatia baadhi ya maeneo ya kazi ili kuongeza nguvu ya utekelezaji. Hatua hiyo tayari imeanza kuzaa matokeo chanya kwa vipande vya Makutupora-Tabora na Tabora-Isaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa ujenzi wa vipande hivyo viwili ulikuwa ukikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo fedha za ujenzi kwa kipindi kirefu, hali iliyosababisha kasi ya utekelezaji kuwa ndogo kuliko ilivyotarajiwa. Hata hivyo, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tayari imechukua hatua madhubuti ya kupata suluhisho

la kudumu la changamoto hiyo kwa kuhakikisha upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanikiwa, kama nilivyosema asubuhi, kupata mkopo wa masharti nafuu wa thamani ya dola za Kimarekani USD Billion1.227 ambayo ni sawa na shilingi trilioni 3.32, fedha ambazo zitawezesha kuongeza kasi ya ujenzi na kuhakikisha vipande hivyo vinakamilika kwa wakati kwa manufaa ya wananchi na maendeleo ya uchumi wa Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ninaomba u-*wind up*.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala, lakini masuala yote yaliyobakia, tutayajibu kwa maandishi na tutaweza kuyaleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa, ninaomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono. Waheshimiwa ninaomba tukae.

Ninaomba niwatambue wageni waliopo ndani ya ukumbi. Tuna wageni watatu wa Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila. Hawa ni watumishi kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (*LATRA*). Karibuni sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Kamati ya Matumizi.

*Hapa Spika (Mhe. Mussa Azzan Zungu) Alikalia kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Mheshimiwa Waziri Mkuu karibu, kwa kweli tuliku-*miss*, karibu sana.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yako ijielekeze kwenye Kitabu cha Pili, Matumizi ya Kawaida. Kwenye kishkwambi ukurasa wa 577, Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi.

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*…………..….Sh. 3,102,844,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Kifungu hiki kina mshahara wa Waziri na nina takribani watu wengi. Nitaanza na Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninaomba nipate ufafanuzi kutoka kwa Serikali. Ili uweze kupata leseni ya usafirishaji Mamlaka ya Usimamizi wa Usafiri wa Nchi Kavu *(LATRA)* inahitaji viambatanisho kadhaa ikiwemo leseni ya udereva. Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na usumbufu mkubwa sana wa namna ya kupata leseni za udereva hasa kwa wale wanaohuisha leseni ambazo zimekwisha muda wake. Hivyo jambo hili limekuwa likiathiri sana mtiririko wa utoaji wa mizigo katika bandari kwa sababu madereva wanalazimika kuingia

mafunzoni kwa siku 14, lakini pia wanalipishwa zaidi ya shilingi 300,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo kupata cheti baada ya hayo mafunzo ni zaidi ya mwezi mmoja, kwa hiyo tunakuwa na zaidi ya miezi miwili tunakosa idadi kadhaa ya madereva ambao wamepata mafunzo; kiasi kwamba sasa inasababisha msongamano wa mzigo katika Bandari ya Dar es Salaam kwa sababu malori mengi yanakosa madereva.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nipate ufafanuzi wa Serikali. Tumeboresha bandari, mizigo inaingia kwa wingi, lakini huku wenyewe tunajipiga chenga kwa kuanzisha vitu ambavyo vinazorotesha *easy of business*. Ninaomba nipate ufafanuzi. Kama sitaridhika na maelezo ya Serikali nitaomba Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono ili tuweze kujadili jambo hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi tunakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Mbunge, kwamba ni hoja muhimu madereva wanahitaji kutazamwa kwa jicho la kipekee kutokana na mchango mkubwa wanaoutoa katika usafirishaji. Serikali kwa kutambua hilo yapo mengi ambayo imeendelea kuyafanya ili kuhakikisha kwamba mazingira yao yanakuwa ni mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa kuweka hoja hii ya kwamba wapate mafunzo upya ipo. Hivi karibuni utakubaliana na mimi kwamba kulikuwa na changamoto kubwa sana ya ajali barabarani, hivyo Serikali ilianzisha utaratibu wa kuhakikisha kwamba inawahakiki. Mara baada ya kuwa wamepita kwenye hatua hizo wakithibitishwa wale ambao walikuwa na vyeti walikuwa wanaweza ku-*renew* kama kawaida; lakini wale ambao hawakuwa na vyeti walikuwa wanatakiwa wa-*submit* vyeti au wasome tena waweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, hoja hii tumeshauriana na wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Ndani; tunaipokea kama

Serikali, tukaichakate na kutafuta namna bora ya kupunguza pengine usumbufu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi acha wakaichakate halafu ninadhani tutakapojadili Wizara ya Mambo ya Ndani tutaijadili kwa kina.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Ninataka nipate ufafanuzi kuhusiana na suala la ndege ya abiria kutokea Mwanza kuja Dodoma. Nilikuwa mmoja wa waanzilishi kuipanda ile ndege na ilifanya vizuri kwa wingi wa abiria ukilinganisha na baadhi ya *route* nyingine ambazo ndege zetu zinaenda; lakini ghafla ilitolewa ile ndege na baadaye tuliambiwa kuna baadhi ya ndege zimeharibika, kwa hiyo wameamua kupunguza *route*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa tunaona ndege zote zinatembea; na sisi kwa *lake zone* tupo wengi tunalazimika kutoka hapa kwenda Dar es Salaam kwenda Mwanza na kurudi zaidi ya 3,000,000 *trip* moja kwenda na kurudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kupata ufafanuzi, ni lini ndege yetu inarudi? Nisiporidhika nitashika shilingi ili Waheshimiwa Wabunge wa Kanda ya Ziwa na Waheshimiwa Wabunge wengine watusaidie kupata ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu suala la Mheshimiwa Musukuma kama ifuatavyo: Tunajua kwamba *route* hiyo ya Dodoma *to* Mwanza ni *route* muhimu na ilikuwa inatoa unafuu mkubwa kwa wananchi wa Mwanza. Kwa vile sasa tuna uwezo, tutairejesha *route* hiyo mara moja. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kwa kuwa maneno yanaumba na Bunge bado lipo na sisi tupo tunaisubiri hiyo, tutaanzisha *route* mara moja kwa sababu na sisi tutakuwa tunaisubiri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaomba ufafanuzi wa kutosha juu ya ukamilishaji wa jengo la abiria ili kuwa hadhi ya kiwanja cha kimataifa au uwanja wa Mwanza. Kama sitapata maelezo ya kutosha nitachukua shilingi ya mshahara wa Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi tunakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Mbunge. Mwanza ni kitovu cha biashara, Kanda ya Ziwa. Tunakubaliana na Mheshimiwa Mbunge juu ya umuhimu wa Uwanja wa Ndege wa Mwanza na kwa kulitambua hilo Serikali ilikwishaanza kufanya maandalizi mbalimbali ya kuufanya kuwa wa kimataifa ikiwa ni pamoja na kujenga jengo la abiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mchakato unaendelea lile jengo la abiria na baada ya kutazama upya tukabaini kwamba lisingeweza kukidhi viwango vinavyohitajika kwa uwanja wa kimataifa wenye hadhi kama ya Mwanza. Hivyo basi tumerudi Serikalini na kuanza kufanya tathmini upya. Moja, maamuzi yamefanyika uwanja huo, jengo hilo litajengwa lakini si lile lililokuwepo kwa sababu lilikuwa ni dogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge atuachie shilingi. Tumekwishaanza kufanya taratibu za kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza kujenga jengo hilo lenye hadhi na litakaloendana na Uwanja wa Kimataifa wa Mwanza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiswaga.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kila mwaka bajeti hutengwa na utekelezaji wake unakuwa kinyume, ninaomba nitoe hoja ili Waheshimiwa Wabunge tujadili jambo hili muhimu la kitaifa.

**MWENYEKITI:** Hoja yako imekubaliwa, tumalize sasa.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Endelea tu.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa uwanja huu ambao tunatarajia uwe wa kimataifa ni uwanja muhimu sana kwa nchi; ndege ambazo zinatua kwa siku *ATCL* ni nne na ndege nyingine ni zaidi ya tatu, kwa hiyo jumla ni ndege saba. Hata hivyo, uwanja huu hata leo ukitafuta tiketi ya kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza zimejaa, kwa hiyo ni uwanja muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kwa sababu faida kubwa inapatikana Mwanza, tunaomba *commitment* ya Serikali kwamba sasa huu uwanja utakamilika ndani ya muda gani? Kwa sababu shilingi 6,000,000,000 ambazo zimetengwa tunaona haziwezi kusukuma huu uwanja. Kwa hiyo tunaomba *commitment* ya Serikali, ni muda gani uwanja huu utakamilika ili tuache kuwa tunazungumza zungumza humu tukuze uchumi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Matiko…., Mheshimiwa Ado.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaunga mkono hoja, lakini Mwalimu Nyerere alituusia; kupanga ni kuchagua. Tunapaswa kuchagua pale Mwanza tunachokitaka ni maboresho au ujenzi na upanuzi timilifu wa kuufanya uwe na hadhi ya kimataifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lugha iliyotumika kwenye hotuba ni lugha ya kwamba ukitazama lugha ya Serengeti (na mimi ninaunga mkono ujenzi wa uwanja wa kimataifa wa Serengeti, *no*

*problem),* lugha ipo *clear* kabisa, ni ujenzi wa Uwanja wa Kimataifa wa Serengeti. Lugha hiyo ni tofauti kila pale Mwanza inapotajwa, ni maboresho ya Uwanja wa Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaonesha kwamba, Serikali bado haina *clear plan* na nia ya dhati ya ujenzi wa Uwanja wa Kimataifa wa Mwanza. Kwa hiyo, ninakubaliana na hoja ya kwamba, tunataka *clear commitment* ni lini Mwanza watapata uwanja wa kimataifa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kuniona. Kwa kweli ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kiswaga na utulinde kwa sababu sisi tumeshika mshahara wa Waziri, sasa ninaona Naibu Waziri anatuingilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tuungane na wenzangu wote kwamba, hapa hatumkomoi mtu ila tunajaribu kuzungumza. Tuna miaka 15 humu ndani na kaka yangu Mheshimiwa Profesa Mbarawa hata mwaka jana ilikuwa hivyo hivyo. Kwenye lile Bunge lililoisha mwishoni, alituambia hivyo hivyo kwamba nini nini, tukaenda tukafungua mkataba wa shilingi 33,000,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo wa shilingi 33,000,000,000 umeshindikana kwamba wameweka vigezo vikubwa, akaondoka kwa sababu ya mkataba, leo shilingi 6,000,000,000; hii haiwezekani. Kwa hiyo, tunahitaji Mheshimiwa Profesa Mbarawa kipaumbele chake kwenye bajeti yake, atuambie ni lini unaanza na unakamilika basi sisi tutaachia shilingi wala hatuna matatizo na shilingi ya Mheshimiwa. Ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ulega.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa na taadhima, ninaomba Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Mwanza na majirani wamwamini Profesa Mbarawa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwanja wa Mwanza umekuwa ukifanyiwa mambo kadhaa. Hapo mwanzo Serikali iliwahi kujaribu kuuboresha ili kuhakikisha kwamba, minofu ya samaki inapita pale, jitihada kubwa zilifanywa na nina hakika zinaendelea kufanywa. Ni kutokana na lile lile la uaminifu wa Serikali na inapoahidi inatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimshawishi Mheshimiwa Boniventura Kiswaga kwamba, tumwache *Professor* na shilingi yake atakwenda kufanya. Kwa hakika ule Uwanja wa Mwanza hapo mwanzo, hata ile *fence* anayoiona haikuwepo na kihistoria iliwahi kushuka ndege pale, ikapata ajali kwa kumgonga mnyama pori nguruwe. Waheshimiwa Wabunge wa Mwanza wanajua, Serikali ilipokea, ikafanya jitihada, ikatengeneza na leo tunashukuru Mungu kwamba hilo halipo…*(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ninawaomba kwamba, waiachie Serikali shilingi yake, ili kusudi ikatekeleze ikiwa ni pamoja na kuliboresha hilo na lile la *airport* Igombe mpaka Kayanza kule kwenda kutengeneza ile barabara inayoungana na huu Uwanja mkubwa muhimu wa Mwanza ambayo itakwenda kuunganisha mpaka na Magu, watu wanaotoka upande ule wote waweze kupata huduma iliyo bora katika uwanja wetu wa Mwanza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja ambayo imetolewa na Mheshimiwa Kiswaga, Mbunge wa Magu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalitambua jambo hilo ambalo Mheshimiwa Mbunge ameliweka mezani na niungane na Mheshimiwa Waziri wa Sekta pamoja na timu yake, ikiwepo hoja ambazo zimetolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali tunatambua umuhimu wa Uwanja wa Ndege wa Mwanza na zipo jitihada ambazo zimekuwa zikifanyika kuhakikisha kwamba Uwanja wa Ndege unaojengwa Mwanza uendane na hadhi kwamba Mwanza ni *hub* ya uchumi wa Kanda ya Ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya hatua ambazo zimekuwa zikichukuliwa ni pamoja na kuangalia namna ya kuongeza *runway* ili iweze kukidhi ndege zote kubwa kutua pale. Katika hilo kumekuwepo na jitihada za kutafuta eneo zaidi ambapo kumekuwepo na mazungumzo ya hapa na pale yanayohusiana na kuongeza eneo ili kuweza kupata ukubwa wa eneo…

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa kwa mujibu wa kanuni ninaongeza muda mpaka tumalize shughuli yetu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja iliyoletwa ambayo inahusiana na upande wa jengo, nimepata fursa ya kufanya ziara Mwanza na nikakaa na Wabunge wa Mwanza, nikakaa pia na viongozi wa Serikali wa Mwanza. Ni kweli hiki ambacho Mheshimiwa Waziri amekisema, jengo lililokuwa linatazamiwa kujengwa awali halikuwa linaendana na hadhi inayotakiwa kujengwa, ikihusisha hata kuongeza urefu na upana wa Uwanja wa Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipi ambacho kimekuja kukubalika ndani ya Serikali? Imekuja kukubalika kwamba lijengwe jengo ambalo hatutataka kulibomoa tena baada ya muda mfupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwanja wa Mwanza, sina maana ya kubeza viwanja vingine, lakini huwezi ukajenga Uwanja wa Mwanza jengo lake likalingana na Uwanja wa Ndege wa Singida au Uwanja wa Ndege wa Dodoma huu uliopo wa sasa, ukiacha ule wa Msalato ama Uwanja wa Ndege wa Iringa wa zamani. Linatakiwa jengo ambalo litakuwa na *standard* ya viwanja vya kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii ni hoja ambayo tulikubaliana. Kwa kuwa sasa bajeti imeandaliwa, nimeongea na Mheshimiwa Waziri amenihakikishia kwamba hata lile linalotokea kwa Uwanja wa Serengeti siyo mbadala wa Uwanja wa Mwanza. Ule kule utajengwa kwa *PPP* ukihusisha sekta binafsi, lakini *commitment* ya Serikali ya kujenga uwanja wa ndege wa kimataifa wenye hadhi ya viwanja vya ndege vya kimataifa na kufanya Mwanza kuwa *hub* ya shughuli za kiuchumi hasa zile zinazohusisha viwanja vya ndege ile iko pale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *commitment* niliyowaachia Waheshimiwa Wabunge wa Mwanza ni kwamba tutakuwa na kikao cha pamoja ili tuwe na uelewa wa pamoja na baada ya hapo waiachie Serikali kutekeleza yale ambayo yamepangwa. Kwa hiyo, nimeitisha kile kikao Ijumaa ambapo Wabunge wa Mwanza wote watakuwepo, Serikali ya mkoa itakuwepo, Wizara ya Fedha watakuwepo, Wizara ya Uchukuzi watakuwepo pamoja na Wizara ya Ujenzi ili tuweze kumaliza haya yote ambayo yalikuwa yanaleta mkwamo na baada ya hapo Serikali tuendelee na utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Waheshimiwa Wabunge waridhie hili, tutajadiliana kuondoa yale yanayoleta mikwamo katika kikao hicho cha Ijumaa ili tuweze kuiachia Serikali iendelee na hatua ambazo zitafuatia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kiswaga.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kauli hiyo ya Serikali ya kukutana na Wabunge, niombe Wabunge wa Kanda tuachie shilingi ya Mheshimiwa Waziri ili mazungumzo yaendelee Ijumaa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Festo Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze Serikali kwa kazi ambayo inafanya kwenye ujenzi wa viwanja nchini. Tunafahamu Sera ya Serikali kuhakikisha kila mkoa

unakuwa na uwanja wa ndege na sisi watu wa Mkoa wa Njombe tumekuwa na uhitaji wa uwanja wa ndege kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitoa ahadi mbalimbali za viongozi, kwenye rai na kwenye majibu hapa ya kuoneshwa kwamba wanaweza kujenga Uwanja wa Njombe. Moja kati ya majibu ambayo Serikali imekuwa ikitoa ni kwamba kuna majadiliano yanaendelea. Kwa hiyo, ninatamani *commitment* ya Serikali…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sanga, hoja yako haiendani na sera, *specific* umetaja eneo lako. Kwa hiyo, kaa chini.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza kwa sera.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, kaa chini.

Mheshimiwa Aeshi.

**MHE. AESHI K. HILALY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi. Ninamwomba Waziri, sikumsikia katika majibu yake kuhusiana na lini sasa tutaanza ujenzi wa kujenga meli mpya ndani ya *Lake* Tanganyika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aeshi, tunataka masuala ya sera, unapogusa eneo lako hau-*qualify*, kaa chini. *(Makofi/Kicheko)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi**

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*................Sh.925,894,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*……………..Sh.1,491,976,000
Kifungu 1004 – *Government Communication Unit*……………………………….…………..Sh.417,459,000

Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*……………………………….……..Sh.757,063,000
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*……………….………Sh.579,003,000
Kifungu 1007 – *Legal Services Unit*………………..............Sh.659,449,000
Kifungu 1008 – *Information and Communication Technology Unit*……………….……....Sh.673,635,000
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*..........Sh.780,498,000

Kifungu 2005 – *Transport Infrastructure Division*…………………..……..….......Sh.1,430,928,000
Kifungu 2006 – *Transport Services Division*…….….Sh.113,952,874,000
Kifungu 2007 – *Air Transport Accidents Investigation Unit*……………….……….Sh.223,316,000
Kifungu 5002 – *Transport Safety and Environment Division*…………………….……..….Sh.1,046,297,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi**

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*…………Sh.263,943,076,000
Kifungu 2005 – *Transport Infrastructure Division*…………………….….Sh.1,962,718,533,000
Kifungu 2006 – *Transport Services Division*….......Sh.520,035,237,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imekamilisha shughuli zake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Mtoa hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 126(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Agosti la Mwaka 2025, ninaomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zake. Ninaomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

**SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

Sasa, nitawahoji kuhusiana na hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Walioafiki wameshinda. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Nichukue nafasi hii Mheshimiwa Waziri nikupongeze sana wewe na timu yako pamoja na wataalam wa *TPA* na *management* yote kwa kazi nzuri ambayo mnaifanya. Imeonesha dhahiri uwekezaji uliofanywa na Serikali kwenye bandari yetu una tija kubwa sana.

Bandari yetu kwa sasa hivi imeelemewa na mizigo pamoja na meli. Lazima kuwe na *affirmative action* na *strategies* za kuboresha na barabara. Reli yetu hii ya *SGR* itakapofika 2030 sasa hivi *capacity* yake ni 25 *million tons*. Mizigo ambayo itategemewa 2030 ni *almost* tani 62,000,000. *(Makofi)*

Kwa hiyo, bila Barabara bora ya Tanga – Handeni - Singida – Tabora na Dar es Salaam – Morogoro – Dodoma lazima Serikali (na Mheshimiwa Waziri Mkuu uko hapa) muwe na mkakati maalum. Kontena hizi 110,000 ukiziweka barabarani ni kilometa 640. Kilometa 640 ni Dar es Salaam *probably* mpaka Tabora au labda karibu na Mwanza. Msongamano utakuwa mkubwa kama barabara zetu siyo za kisasa. *(Makofi)*

Lazima tuwe na mkakati maalum wa barabara, viwanja vya ndege, bandari na *SGR* ili tuwe na malengo. Kama bandari yetu hatujaboresha *the dream* ya Dira ya 2050 itakuwa haipatikani. Hapo ndiyo kwenye pesa za kusaidia Taifa letu. *(Makofi)*

Kutokana na uzuri na maboresho wanayofanya wenyewe, ningefikiri hata sasa hivi Serikali ifikirie, *authority* kama hii ya *TPA* iwe na uhuru, iwe na *autonomy*. *TPA Hybrid Public Authority* ni chombo cha umma, lakini kinajiendesha na *market* (masoko) yanavyokwenda ili waweze kuwa na ufanisi zaidi na Watanzania wenyewe wanaweza kufanya. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nishukuru sana na nikushukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuweka vizuri suala la Uwanja wa Ndege wa Mwanza. Uwanja huu ni *strategic* sio kibiashara tu, hata kwenye mambo ya ulinzi. Tulipovamiwa na Idd Amin ndiyo uwanja uliotumika kujikomboa. Kama watu hamjui, ndiyo ulitumika kuikomboa Tanzania na Mutukula kurudi nchini Tanzania. Kwa hiyo, ni muhimu sana kwenye biashara, lakini vilevile, una *rapid response* chini ya kufanya kazi ya kiulinzi pale inapohitajika. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ninashukuru sana. Bahati mbaya tai yangu haionekani hapa.

Ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi. *(Makofi/Kicheko)*

*(Saa 1.56 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 14 Mei, 2026 Saa Tatu Asubuhi)*

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA